# UCHANGANUZI WA KISEMANTIKI-LEKSIA WA MANENO TEULE YA KISWAHILI YALIYOTUMIKA KATIKA NYIMBO TEULE ZILIZOIMBWA NA NONINI NA JUACALI

**MAROLYNE JERUJAEL MOSES**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KAMA SEHEMU YA KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**SHULE YA SANAA NA SAYANSI JAMII**

**CHUO KIKUU CHA MASENO**

**©2019**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kama mahitaji ya shahada katika chuo kingine chochote.

......................................................... TAREHE............................

**MAROLYNE JERUJAEL MOSES**

**MA/FA/00022/2015**

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo kikuu cha Maseno, kwa idhini yetu kama wasimamizi.

............................................................................ TAREHE...........................

**DAKTARI BEVERLYN ASIKO**
**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**
**CHUO KIKUU CHA MASENO**

............................................................................ TAREHE...........................

**DAKTARI DEBORAH AMUKOWA**
**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**
**CHUO KIKUU CHA MASENO**

## SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati ninamtolea Mwenyezi Mungu kwa kunikirimia na kunifikisha umbali huu. Shukrani ziwaendee Dkt. Beverlyne Asiko na Dkt. Deborah Amukowa waliokuwa wasimamizi katika kazi hii. Hamkuchoka kuisoma kazi yangu, mkanipa ushauri na kunitaalamisha kwa weledi wenu. Mlinishugulikia kwa dhati na kunitia moyo wa kuendelea hivyo nashukuru. Asanteni kwa kuwa dira na kielelezo kwa wasomi limbukeni kama mimi.

Nawashukuru Wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika kwa kunifaa kila nilipohitaji mchango na ushirikiano wenu. Asanteni kwa kunifundisha na kunielekeza kiusomi. Aidha shukrani zangu zimwendee David Kaleka ambaye kazi yake ilinipa mwanya uliozua mada ya utafiti. Namshukuru mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Kandaria, Bwana Martin Mito ambaye ni msimamizi wangu kazini kwa kunitia moyo na kunitakia heri.

Namshukuru Dkt. Yakub Adams kwa kunichagiza kujibwaga na kuogelea katika shumbi hii ambayo sikujua kina chake. Ulinihimiza mara kwa mara ukanizindua nilipopayapaya kando na kunitia ujasiri maishani. Nathamini mno ushauri wake tangu mada ya tasnifu hii ilipojengwa. Sitasahau asilani ulivyonikongoja na kunitanabahisha kumakinikia kazi hii.

Kwa vitoto vyangu vichanga, Fadhili na Kibali wanaonilaki kwa shangwe kila mara ninapowasili nyumbani baada ya panda shuka za masomo na kusisimua nafsi yangu. Ukamilifu wa maisha yangu unafungamana na nafsi zenu. Kipande cha moyo mnaochojikita kitadumu daima. Kwa mume wangu mpendwa Dkt. Jared Mbete mbali na stahamala wako, ulinihimiza kwa dhati na kunikumbusha kwamba kila aotaye ana uwezo wa kujukumikia utimiaji wa ndoto zake.

Japo ni muhali kumtaja kila mtu, yeyote aliyechangia urutubishaji wa kazi hii, mchango wenu utathaminiwa daima.

## TABARUKU

**Kwa dhati ya dhamiri, wazazi wangu Moses na Saline Oduor**

*Tangu azali, meonesha azali*

*Nijitie makali, mpukutikie dhalili,*

*Almuradi ya mustakabali, niumbulike ugiligili,*

*Nyie majabali iso kalili, utashi wa stahamili*

*Nyie amana aali, Jalali akupevusheni jamali.*

## IKISIRI

Tafiti za awali zinasawiri kuwa wasanii huibua maumbo ya sanaa dhahania ambayo aghalabu hueleweka kwa hadhira kwa namna mbalimbali. Inajulikana kuwa wasanii hutumia maneno ya kawaida yanayotumiwa kuwasiliana kila siku na hata kuzua maana nyingine katika jaribio la mawasiliano. Kuelewa maneno ya nyimbo kama umbo lolote la sanaa, kwa kiasi kikubwa hutegemea jinsi maneno hayo ya nyimbo yalivyotumiwa kuwasilisha maana kusudiwa na namna ambavyo maneno hayo yaliyotumika yanavyofasiriwa na hadhira. Kuelewa maana za maneno yaliyotumiwa na wasanii huenda kukawa changamoto kwa wasikilizaji hasa katika muziki wa kizazi kipya nchini Kenya. Hivyo, inawezekana kuwa kadiri lugha inavyozidi kutumika katika nyimbo, ndivyo maana za maneno mengine zinavyoweza kupanuka na kuiathiri lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hii, maana hizi zaidi zinaweza kusababisha kuvurugika kwa mawasiliano. Utafiti huu ulichanganua kisemantiki-leksia maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo za kizazi kipya nchini Kenya zilizoimbwa na Nonini naJuacali. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa: Kubainisha maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za Nonini na Juacali yenye maana tofauti na maana za kawaida na kueleza maana zao, Kujadili athari ya upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za Nonini na Juacali kwa lugha ya Kiswahili na Kutathmini utata katika mawasiliano kutokana na upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule zilizoimbwa na Nonini na Juacali. Nadharia ya maana kimatumizi ya Ludwig Wittgenstein iliyokuzwa na Ken Turner (2011) ndiyo iliyotumika kuchanganua data iliyokusanywa. Kwa mujibu wa nadharia hii; maana ya maneno hupatikana katika matumizi yake. Pili, maana ya neno inatokana na muktadha wa matumizi ya neno lenyewe. Tatu, neno halimaanishi kitu kimoja katika kila matumizi yake. Hivyo, maana ya neno iangaliwe kwa kuzingatia muktadha wa neno na jinsi neno hilo lilivyotumika. Utafiti huu uliwashirikisha watafitiwa wakuu 16 ambao ni walimu wa lugha na isimu katika chuo kikuu cha Maseno, wanafunzi wanachama 180 wa chama cha Chama cha Kiswahili cha Maseno (CHAKIMA) na nyimbo 66 za wasanii Nonini na Juacali. Nyimbo 5 zilizoimbwa na Nonini na Juacali zilisampulishwa kimakusudi huku mbinu ya usampulishaji usioratibika ikitumika kuwapata washiriki 27 kutoka CHAKIMA waliojadiliana katika makundi na watafitiwa wakuu 6 waliohojiwa. Data ilikusanywa kwa kutumia usaili, majadiliano kimakundi na udondozi. Uwasilishaji wa data ulihusisha utambuzi na ufasiri huku matokeo ya utafiti yakiwasilishwa kwa maelezo na katika jedwali. Utafiti ulibainisha kuwa maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo yalizua maana nyongeza tena tofauti na maana za kikamusi. Upanuzi wa maana ulibainika na kuonekana kuiathiri lugha ya Kiswahili kwa kukuza msamiati na lugha kwa jumla, kuivuruga kimatumizi, maenezi na maendeleo ya lugha pamoja na kusababisha utata katika mawasiliano. Utafiti huu unatarajiwa kuchangia maarifa kwa kutazama lugha ya Kiswahili katika mwanga wa maana kimatumizi hususan katika muktadha wa nyimbo za kizazi kipya na maarifa ya makuzi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili.

## ABSTRACT

Previous studies indicate that artists generally create abstract art forms that are mostly not comprehensible to the audience. Artists normally use commonplace lexicon in novel ways in their bid to communicate with their audiences. Comprehending song lyrics, like any other art form, largely depends on how the lyrics are used in conveying the intended meaning and how the audience interprete the words. Chances of intended meaning being achieved in the lyrical diction used by individual artists may cause comprehension challenges, for instance, to the audiences of Kenya's hip hop music. Hence, there's a possibility that as language use in songs develops, some words expand in meaning and subsequently affect the Swahili language. Therefore, meanings of the swahili words in Kenyan hip-hop music can possibly cause communication breakdown to the music listeners. This study therefore undertook a lexico-semantic analysis of Kiswahili words in Kenya's present generation music by Nonini and Juacali. This study's objectives were: to identify Swahili words that seemed to have different meanings and analyze their meanings as used in the songs, evaluate the perceptual effect of the semantic broadening on Kiswahili and establishing ambiguity in communication from the expanded meaning of the selected Swahili words used in the songs. Ludwig Wittgenstein's theory of meaning as use, a theoretical framework that was further developed by Ken Turner (2011) was used to analyze the data collected.This study's population comprised 16 key informants who are teachers of language from the departments of linguistics and Kiswahili in Maseno University, 180 members of CHAKIMA and 66 songs sung by Nonini and Juacali. 5 songs were purposively sampled while 27 discussants were simple randomly sampled from CHAKIMA for focus group discussions and 6 key informants for interviews. Data was collected using interviews, extraction and focus group discussions. Data analysis was qualitative involving identification, codification and interpretation of patterns, themes and a table. The findings indicate that there are more meanings of the Swahili words as used in the songs which were different from the dictionary meanings hence evidencing semantic expansion. Meaning expansion grows and develops the Swahili language but also interfering with its use, spread, direction and sustainability. There was ambiguity in communication emanating from the new meanings of the words as used in the songs. This study is expected to contribute to knowledge by looking at Swahili language in the context of present generation songs and subsequent vocabulary development with regard to meaning, growth and maintenance of language comprehension will be enhanced.

## YALIOMO

UNGAMO ........................................................................................................ ii
SHUKRANI........................................................................................................ iii
TABARUKU ........................................................................................................ iv
IKISIRI ........................................................................................................v
ABSTRACT ........................................................................................................ vi
YALIOMO…………………………………………………………………………Vii

**SURA YA KWANZA: MISINGI YA UTAFITI**..........................................................1
1.0 Utangulizi ..........................................................................................1
1.1 Usuli wa utafiti ....................................................................................1
1.1.1 Lugha katika jamii ...............................................................................1
1.1.2 Maana kimatumizi katika muktadha..........................................................3
1.1.3 Utata katika mawasiliano......................................................................7
1.1.4 Usuli na Maendeleo ya Nyimbo za Kizazi Kipya ...........................................11
1.2 Swala la Utafiti ...................................................................................17
1.3 Maswali ya Utafiti ................................................................................18
1.4 Madhumuni ya Utafiti............................................................................19
1.5 Umuhimu wa utafiti ..............................................................................19
1.6 Upeo wa Utafiti....................................................................................20
1.7 Misingi ya Kinadharia ............................................................................20
1.8 Hitimisho ..........................................................................................25
**SURA YA PILI MAPITIO YA MAANDISHI:**..........................................................26
2.0 Utangulizi ..........................................................................................26
2.2 Dhana ya maana...................................................................................26
2.3 Maana za maneno kimatumizi na muktadha ..................................................28

2.3 Mabadiliko na Upanuzi wa Maana ........................................................................ 33
2.4 Utata na mawasiliano ........................................................................ 38
2.4 Hitimisho ........................................................................ 41
**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI** ........................................................................ 42
3.0 Utangulizi ........................................................................ 42
3.1 Muundo wa Utafiti ........................................................................ 42
3.2 Eneo la Utafiti ........................................................................ 43
3.3 Kundi Lengwa ........................................................................ 43
3.4 Usampulishajina Sampuli ........................................................................ 44
3.5 Njia na Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........................................................................ 46
3.5.1 Unukuzi ........................................................................ 47
3.5.2 Usaili ........................................................................ 48
3.5.3 Majadiliano Kimakundi ........................................................................ 48
3.6 Ufaafu na Utegemezi wa Vifaa vya Kukusanya Data ........................................................................ 49
3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ........................................................................ 50
3.8 Maadili Katika Utafiti ........................................................................ 50
3.9 Hitimisho ........................................................................ 51
**SURA YA NNE: MATOKEO NA MJADALA** ........................................................................ 52
4.0 Utangulizi ........................................................................ 52
4.1 Maana za maneno katika nyimbo teule ........................................................................ 52
4.1.1 Muktadha wa Starehe na sherehe ........................................................................ 60
4.1.1.1 Neno Katika ........................................................................ 60
4.1.1.2 Neno Ngoma ........................................................................ 63
4.1.1.3 Neno Poa ........................................................................ 64
4.1.2 Muktadha wa Pesa na shughuli ya kutafuta pesa ........................................................................ 66
4.1.2.1 Neno Rarukia ........................................................................ 66
4.1.2.2 Neno pigwa ........................................................................ 68

4.1.3 Muktadha wa Mapenzi na ngono....................................................................................70
4.1.3.1 Neno Nyundo..........................................................................................................70
4.1.4 Muktadha wa Mahusiano..........................................................................................84
4.1.4.1 Neno Mbuyu/ buda ..................................................................................................84
4.1.4.2 Nahau Rushia mkono...............................................................................................86
4.1.4.3 Neno kibao...............................................................................................................88
4.1.4.4 Neno damu...............................................................................................................89
4.1.4.5 Neno pepea ..............................................................................................................92
4.1.4.6 Neno kaa ..................................................................................................................93
4.1.4.7 Neno bamba .............................................................................................................93
4.1.4.8 Neno kuchanuka ......................................................................................................95
4.1.4.9 Neno shika ...............................................................................................................96
4.1.4.10 Neno roga...............................................................................................................96
4.1.4.11 Neno wika...............................................................................................................98
4.1.4.12 Neno shona ............................................................................................................98
4.1.5 Miktadha ya Ulevi na uhalifu ..................................................................................101
4.1.5.1 Neno gonga.............................................................................................................101
4.1.5.2 Neno chota..............................................................................................................102
4.1.5.3 Neno vitu ...............................................................................................................103
4.2 Upanuzi wa maana na athari yake katika lugha ya Kiswahili ...............................................105
4.3 Utata katika mawasiliano kutokana na upanuzi wa maana ...................................................133
4.4 Hitimisho .................................................................................................................145
**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**............................146
5.0 Utangulizi ...............................................................................................................146
5.1 Muhtasari ................................................................................................................147
5.1.1 Maana za maneno katika nyimbo teule ..................................................................147
5.1.2 Upanuzi wa maana na athari yake kwa lugha ya kiswahili ...............................................148

5.1.3 Utata katika mawasiliano kutokana na maana zaidi ....... 149
5.2 Hitimisho ....... 150
5.3 Mapendekezo ....... 152
5.4 Mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye ....... 153
**MAREJELEO ....... 154**
**VIAMBATISHO ....... 163**

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia mambo ya kimsingi ambayo yanajenga usuli wa utafiti huu. Vipengele muhimu vya utangulizi kama vile: usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti pamoja na misingi ya kinadharia vimeshughulikiwa.

## 1.1 Usuli wa utafiti

Huu ni utafiti unaojikita katika maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo za kizazi kipya hasa zilizoimbwa na wasanii Nonini na Juacali nchini Kenya. Sehemu hii inaangazia lugha inavyotumiwa katika jamii, maana inavyozuliwa kutokana na matumizi katika muktadha maalum na utata katika mawasiliano.

### 1.1.1 Lugha katika jamii

Lugha ni chombo muhimu sana katika maisha yetu kwani hutusaidia katika mawasiliano na utangamano. Kulingana na Whorf (1956), lugha huzipatia mawazo na hisia sura, na hivyo kubainisha mtazamo halisi wa mtu. Sapir (1921) anasema kwamba, wanadamu wanatawaliwa na lugha mahususi inayoishia kuwa chombo cha kujieleza. Lugha ndio chombo cha kupitisha maana na uamilifu wa lugha hudhihirishwa na maana inavyosimbwa

katika maneno. Umuhimu huu wa lugha ndio unaozua ule msukumo wa kuichunguza kisayansi kila kuchao.

Chukwu (2002) anasema ni lazima kuwe na mawasiliano kwa sababu watu hawana budi kutangamana katika jamii.Matumizi ya lugha katika mawasiliano hubeba ujumbe au huwasilisha maana. Tukio lolote la mawasiliano huelekezwa na uteuzi wa lugha hutegemea vigezo kama hafla, lengo, hadhira na ujumbe kusudiwa. Vigezo hivi hufanyiza muktadha ambao kulingana na Walhstorm (1992) ni muhimu. Kwake, mawasiliano ni mchakato wa uwasilishaji wa habari kwa kusudi la kuishawishi hadhira, unaozingatia muktadha kwa kiwango cha juu. Fribsy (1957) pia anabainisha kusudi la kipengele cha mawasiliano hususan lugha anaposema kuwa, kinachozuliwa na mtu huelezwa kwa kusudi fulani. Kwa misingi hii dhima ya kimawasiliano ya maneno na mafanikio yao katika mawasiliano ilichunguzwa.

Kulingana na Taiwo (2001), matumizi ya lugha ni amali ya jamii, kwa hiyo ipo haja ya kuonyesha jinsi lugha yenyewe inavyohusiana na jamii ya watumizi wake na jinsi maana inavyozuliwa katika tangamano za lugha za kila siku. Lugha hutumiwa popote palipo na watumizi wake na utangamano upo. Watu hutangamana katika shughuli mbalimbali kama vile biashara, michezo, mahojiano au hata sanaa na burudaniamabpo wanatumialugha kwa namna anuwai.Taiwo (2001) anachukulia kwamba watu huchagua kimakusudi na kwa upekee, maneno yanayoweza kupitisha maana na hivyo ujumbe kwa njia bora zaidi kutoka kwa mifumo inayofanyiza lugha. Akichangia suala la maana Massamba (1987) anasema

kuwa uibuaji wa maana ya maneno unaweza kutokana na mazoea ya matumizi yake kwa njia fulani kando na maendeleo pamoja na mabadiliko yanayotukia maishani.

Ipara na Maina (2008) wakinukuliwa na Odawo (2015) alipotafitia uhamishaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda, wanaeleza kwamba lugha katika upekee wake huweza kukosa kukidhi mahitaji ya watumizi wake katika nyanja za kimawasiliano. Kutokana na hali hii, wawili hawa wanadai kuwa, watu hujitokeza na namna mbalimbali za kuitumia lugha ile moja. Odawo (2015) anaunga mkono wazo hili kwa kusema kwamba matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali hutofautiana na tofauti hizo ndizo zinazoibainisha lugha kimatumizi. Aidha katika hali ya kujitosheleza kimatumizi maana huibuka na hivyo kuonyesha kwamba maneno katika lugha yatatumiwa kwa vyovyote vile kufanikisha mawasiliano. Upekee wa matumizi ya lugha hususan maneno ya Kiswahili unaohusisha uibuaji wa maana katika nyimbo teule za kizazi kipya ndicho kiini cha utafiti huu.

### 1.1.2 Maana kimatumizi katika muktadha

Mawasiliano faafu huzingatia maana. Kusambaratika kwa mawasiliano kunakosababisha kutoelewana hudhihirika pale kitendo tarajiwa kinapokosa kufanyika na hivyo kusudi la mawasiliano kutotimizwa. Kwa mujibu wa Short na Leech (1981), lugha ni pana hivi kwamba inaruhusu uzalishaji wa maana zaidi ya ile ya kawaida. Snowball (2011) anaendeleza wazo hili anaposema kwamba maneno yanaweza kuwa na maana nyingi. Hivyo basi, maana inayokusudiwa na mtu mmoja sio kwa hakika maana inayopokelewa na wengine kwani maneno yanaweza kueleweka kwa njia nyingi tu.

Gamble na Gamble (2013) wanajadili kwamba kutowasiliana hutokea pale ambapo watu wawili wanadhani wanaelewana kumbe wamekosa maana inayokusudiwa na kila mmoja wao. Vilevile, watu wanapotoa maana zinazotofautiana za neno au kirai kimoja mawasiliano huhitilafiwa. Kinachodhihirika hapa ni kwamba, maneno yanayomaanisha kitu fulani kwa mtu mmoja na kingine tofauti kwa mwingine yana uwezekano mkubwa wa kusababisha matatizo ya kimawasiliano. Hili linadhihirishwa na Khachula (2013) anayefafanua kwamba maneno yanapotumika kwa muda mrefu huweza kupata maana nyingine kando na zile asilia. Khachula (2013) anasema kwamba maneno yaliyobadilika kimaana huzua semi zilizo tata na kupelekea kutofaulu kwa mawasiliano katika wazungumzaji wa lugha.

Maana husimbwa jinsi ambavyo maneno yametumiwa katika muktadha fulani. Sinclair (2014) anafafanua kwamba maneno kiasilia ni vyombo visivyotegemea kutengwa na muktadha wa matumizi yao. Khachula (2013) anasema kwamba wazungumzaji hutumia maneno katika lugha kwa njia tofauti ili kufaa katika muktadha wa matumizi ya maneno hayo. Hivyo basi, maana za maneno hubadilika kutegemea muktadha ambamo maneno hayo yametumika. Neno ‘waka’ kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu toleo la tatu ya Oxford (2013) ni neno linalorejelea kutoa mwangaza, kuanza kufanya kazi kwa mashine au kuungua. Katika muktadha mwingine zungumzi neno hili pia linarejelea ‘kulewa’. Hii ndio sababuHartman (1983) anasema kwamba lugha iko katika muktadha fulani hivyo maana hueleweka kwa misingi ya muktadha husika. Mawazo haya yanaibua haja ya kuangalia maana ya maneno kimatumizi kwa misingi kwamba maana za maneno hutofautiana kwa misingi ya muktadha wa matumizi.

Odawo (2015) anaeleza kwamba maana ya lugha inachunguzwa kulingana na muktadha wa matumizi yake na hivyo lugha hueleweka katika muktadha wake. Muktadha huu kwa mujibu wa Werth (1999) ni mazingira kamilifu ambamo neno fulani linatumika. Kulingana na King'ei (2010) muktadha ni ile hali inayotawala na kuelekeza matumizi ya lugha inayozungumzwa kwa mfano mahali, wakati, hadhira, kusudio la mnenaji na kadhalika.Muktadha huelekeza ujenzi wa maana na huja kwanza. Muktadha unatekeleza dhima kuu katika ujenzi wa maana. Odebunmi (2006) akinukuliwa na Ajayi-Osuolale (2017) anasisitiza kwamba muktadha ni uti wa mgongo wa maana ya neno na ni vigumu kuendelea kutafuta maana bila kuzingatia muktadha wa matumizi ya maneno fulani. Hivyo basi, bila ujuzi wa muktadha ufasiri wa maana hautakuwa faafu. Firth (1935) anasema kwamba maana kamilifu ya neno huwa ya kimuktadha na hamna utafiti wa maana pasipokuwa na muktadha ulio kamilifu unaoweza kutiliwa maanani. Kimsingi lugha inapotafitiwa muktadha hutangulia kuelekeza kuzuliwa kwa maana kwani muktadha huiathiri maana ya neno.

Lugha ina dhima kuu katika mawanda mbalimbali, mojawapo ni sanaa. Kwa mujibu wa Jilala (2012), sanaa inarejelea matumizi yaliyokuzwa na madhubuti ya lugha kupitisha maana kwa kina mara moja. Sanaa hubainika kwa njia mbalimbali mojawapo ikiwa ni nyimbo. Hivyo, nyimbo ni kati ya vibainishi vya sanaa vinavyotumia lugha kama kiungo muhimu. Kwa kuwa nyimbo zina mvuto kwa watu wengi katika jamii, lugha katika wimbo wowote ule huweza kuwa na athari kubwa ya kiisimu kwa jumla. Gekau (1993) anashikilia kwamba nyimbo ni kioo cha mambo yalivyo katika sehemu tofauti za ulimwengu na yanayoimbwa ni yale yanayotokea wala hayaimbwi bila kuwepo.

Nyimbo asemavyo Ajayi-Osuolale (2017) ni zana ya nguvu ya kijamii iliyo mikononi mwa wanajamii. Kulingana na Sawhney (2013) kila mara maneno katika nyimbo ni njia maarufu ya kuufikia ulimwengu na kustawisha mawasiliano kwani nyimbo hutekeleza dhima ya uwasilishaji kwa njia nyingi. Nketiah (1974) anasema kwamba matini za nyimbo zinatiwa msukumo na umuhimu wa nyimbo hizo kama njia ya mawasiliano, chombo cha maelezo yanayosawiri tajriba za kibinafsi na kijamii. Hivyo kulingana na Nketiah (1974), hii ndiyo sababu inayowafanya watunzi wa kisasa kutunga nyimbo kwa kutumia lugha wanayomudu ili kudumisha mahitaji ya kimaana. Kulingana na mtazamo huu basi, kila neno katika wimbo lina ujumbe unaoelekezewa msikilizaji. Aidha, ujumbe huu unaelekezwa kwa kusudi la kuzua mtazamo kwa msikilizaji.

Lugha inachukuliwa kuwa kifaa kinachotumiwa na wasanii wa nyimbo kueleza dhana na hisia zao. Hivyo basi, ina dhima kuu katika kufanya nyimbo ziamilike kwa wasikilizaji. Hata hivyo anavyosema Koech (2013), lugha ilivyotumiwa katika nyimbo huweza kusababisha kuvurugika kwa mawasiliano kwa hadhira kutokana na jinsi ambavyo mwimbaji ametumia lugha kwa upekee unaohitaji ufasiri fulani ili kufikia maana iliyokusudiwa. Lugha inavyotumika inaweza kuzuia mchakato wa kupata maana iliyokusudiwa hasa ikiwa mfasiri anatokea nje ya utamaduni ule wa mwasilishaji wa ujumbe. Isitoshe mmoja wa wasikilizaji wa nyimboanafasiri maana za maneno yaliyotumiwa katika nyimbo kwa namna inayoweza kutofautiana na mwenzake.

### 1.1.3 Utata katika mawasiliano

Uings (2008) anafafanua utata kama hali ya kuwepo kwa maana zaidi ya moja. Ruby (1962) anachukulia utata kuwa matumizi ya neno moja kuwasilisha zaidi ya maana moja. Wazo hili linaungwa mkono na Hurtford & Heasely (1982) wanaosema kwamba maneno huwa tata ikiwa yana maana zaidi ya moja. Keysar (2007) anasema kwamba utata upo kila mahali na wakati kwa sababu kila neno lina maana zaidi ya moja linaloweza kutokana na usemi wa kawaida. Hivyo kwake, msikilizaji anaweza kukanganywa akose kuelewa kile ambacho mzungumzaji anasema na kuhitilafisha mawasiliano miongoni mwao. Kwa misingi hii ni wazi kwamba utata hutokea pale ambapo neno moja lina maana zaidi ya moja na hivyo huegemea muktadha.

Kulingana na Reuster- Jahn (2007), nyimbo huwa katika mstari wa mbele wa uvumbuzi wa lugha na maenezi ya maneno yenye maana kupita ya kawaida. Maneno hayo huweza kuundwa upya na waimbaji au maana mpya kupewa maneno yaliyo ya kawaida. Reuster-Jahn (2007) anaongeza kwamba maneno ya Kiswahili hupewa maana zilizochepuka katika muktadha wa nyimbo teule. Mawazo haya yanaonyesha kwamba ubunifu wa muziki unachangia kuzuliwa kwa maneno na maana zaidi. Kwa kuchukulia kwamba nyimbo huwavutia watu wengi katika jamii, ni wazi kuwa lugha katika nyimbo hizi inaathiri jamii pakubwa. Ni katika mtazamo huu ndipo utafiti huu ulihitaji kuelekeza makini yake katika maneno yanayotumika na yanavyotumika katika nyimbo hasa za kizazi kipya katika misingi kwamba, nyimbo za kizazi kipya zinasawiri lugha inavyotumika katika enzi za sasa.

Kirai ‘semantiki leksia’ ni dhana inayojumuisha istilahi ‘semantiki’ na ‘leksia’. Kulingana na Lyons (1992), kuna mazoea ya kuchukulia kwamba vipengele vya kileksia ni maneno pekee. Hata hivyo, mtaalamu huyu anabainisha kwamba vipengele vya leksia vinazidi maneno kwani kuna virai pia. Hivyo utafiti huu utachukua mtazamo wa isitilahi ‘leksia’ kurejelea maneno pekee. Lyons (1992), anafafanua semantiki kuwa ni utafiti wa maana. Aidha, Dockrell na Messer (1999) wanaeleza semantiki kuwa ni maana ya maneno na semi. Kulingana na wataalamu hawa, semantiki basi inahusisha maana za maneno zinazoweza kubadilika kutegemea muundo na muktadha wa kimahali na kiwakati. Utafiti huu kwa kuzingatia mitazamo hii ulichukulia semantiki leksia kuwa maana ya maneno katika miktadha ya matumizi yao.

Boomhower (2005) anadai kuwa lugha inapokua maana za maneno yake huweza kubadilika wakati mwingine na kuiathiri lugha yenyewe. Lugha hiyo yaweza kusalia hai, ikarekebika na hata kukua zaidi. Hoja hii iliungwa mkono na Katamba (1994) anaposema kwamba maana inaweza kuhama, kuongezeka au hata kufifia. Mabadiliko ya maana kwa hivyo yanaashiria kwamba neno linaweza kuwa na maana nyingi. Kwa mfano neno ‘fyeka’ kulingana na Kamusi ya Kiswahili sanifu toleo la tatu ya TUKI (2013) ni kukata miti au nyasi ziwe fupi vilevile kumwangamiza adui. Sasa hivi neno hili pia linarejelea kujamiiana hasa na watu katika uraibu. Neno ‘mtoto’ kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu toleo la tatu ya TUKI (2013) linarejelea kiumbe anayezaliwa na mtu au mnyama lakini katika miktadha mingine kama vile ya kimapenzi neno hili linarejelea binti mrembo.

Kulingana na Boomhower (2005), maneno yaliyopata maana zaidi huenea haraka na hutumiwa mara nyingi kuliko matumizi yao asilia na hivyo kupata nafasi katika jamii. Mtazamo huu unaungwa mkono na McCridle (2011) anayesema kwamba kadiri lugha inavyokua ndivyo maana za maneno zinavyopotea na wakati mwingine maneno hayo kuchukuliwa kuwa kongwe. Anazidi kusema kuwa jinsi maana nyingine za manenozinavyofifia katika matumizi ndivyo maananyingine zinavyozuliwa na hivyo kuchangia katika mapinduzi ya lugha. Masuala ya mabadiliko ya maana yanajengwa zaidi na Suguitan (2005) anayehoji kwamba maana ya neno huamuliwa na watumizi wa neno lenyewe. Hivyo ni dhahiri kwamba maneno yanaweza kueleweka kwa njia nyingi sana.

Kulingana na Fromkin na Rodman (1978) neno hupanuka kimaana linapomaanisha kila kitu kilichokuwa kikimaanisha na kuzidisha maana nyingine.hivyo basi neno linapopanuka kimaana , neno hilo huwa limeongezewa vitajwa na kujumuisha vitajwa vingine. Ullman (1970) naye anafafanua kwamba maneno huweza kupewa maana moja bunifu au zaidi bila ya maana asilia kupotea. Aidha, Anusu (2015) anaunga mkono hoja hii anaposema kuwa ile maana asilia na ya pili zinaishi upande upande bora tu pasiwepo na ukinzano.Kwa misingi hii, neno lenye maana thabiti kiasi hupanuliwa ukingoni na kujumuisha mawanda ambayo kwa hakika yanapatikana nje ya maana yake kamili inayoishia kuwasilishwa na wasemaji.

Sehemu za miji huwa na watu wengi wenye asili tofauti na wakaazi hao huwa na uwezo wa kuzungumza lugha zaidi ya moja kama anavyothibitisha Mojela (2000). Kwa sababu hii, lugha huzuka katika jaribio la kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wanajamii hawa.

Lugha hii kimsingi anavyosema Reuster-Jahn (2006) hubainishwa kwa kule kuchipuka kwake kutoka kwa lugha sanifu ya Kiswahili. Sifa hii kuu inadhihirishwa na maneno yake maalum ambayo daima yanaibuka upya kimaana. Gathigi (2012) anaendeleza mawazo haya anapofafanua kwamba lugha hutukia pale ambapo kinachosemwa kina maana na kinaeleweka kwa watumizi wake mahususi katika jamii. Kulingana na Gathigi (2012), kuchepuka kutoka kwa umbo sanifu linalochukuliwa kuwa kawaida kunazua upote wenye nguvu kati ya hadhira kusudiwa.

Kulingana na King'ei & Kobia (2007), wasanii wengi hasa vijana hutumia lugha ya usanii kuwasilisha maudhui kutokana na uwezo wao kuwafikia vijana wengi kwa mvuto wa hali ya juu. Muziki katika jamii ni maktaba inayothibitisha lugha inavyotumika katika jamii hiyo, waimbaji huweza kueneza lugha yenyewe kwa sababu aghalabu hao hutangamana na vijana na kuimba kwa kutumia lugha inayoeleweka na mashabiki wao. Hili laweza kuchukuliwa kuwa mapinduzi ya lugha kwani lugha inayotumika kwenye usanii huonekana kuififisha maana za maneno za kawaida na kuzua maana nyingine mpya.

Dunbar (1996) anasema kuwa lugha haina ushindani katika uwezo wake wa kupitisha habari lakini viwango vya mawasiliano vinapopanda hadi kiwango cha kijamii, lugha inategemea muziki ili kupitisha ujumbe unaokusudiwa.Mara nyingi masuala yanayowaathiri vijana wanaochukuliwa kutengwa huelekezwa katika maneno elezi yanayoimbwa na hivyo kuwapa vijana nguvu na sauti. Hili linadhihirishwa na Rheuster-Jahn (2007) anaposema kwamba vijana baada ya kutelekezwa katika jamii hutumia muziki kama jukwaa la kuzungumzia hali

zao za maisha na matamanio yao kusikizwa katika jamii. Pia, kulingana na Turner (2017) akiwanukuu Lynch na Kryzyeki (1998), muziki wa kizazi kipya ni simulizi na sauti za mitaani. Hivyo basikupitia kwa lugha katika nyimbo hizo zinazotumika kama vishawishi, kioo cha mawazo na kitambulisho cha kijamii kinachotia hisia za upeke, maneno yaliyotumika huweza kuibua maana zaidi ya kawaida. Katika mitazamo hii, utafiti huu ulinuia kuangalia maana inayowasilishwa kwa maneno ya Kiswahili katika mwanga wa muziki wa kizazi kipya.

### 1.1.4 Usuli na Maendeleo ya Nyimbo za Kizazi Kipya

Okumu (1998) anasema kwamba, nyimbo za kizazi kipya zinazopendwa na watu wengi hapa Kenya zimeendelea kukua kadiri historia ya kijamii ya nchi inavyokua. Kukua huku kumewezeshwa kuongezeka kwa idadi ya watu na hiyo jamii kupanuka. Kulingana naye, kuwepo kwa huduma za utangazaji nchini Kenya kumechangia pakubwa maendeleo ya muziki pendwa wa Kenya. Kabla na baada ya uhuru, nyimbo zilikuwa zinatungwa katika lugha zinazochukuliwa kuwa sanifu. Nyimbo zilikuwa zinatungwa kwa kutumia lugha za kiasili kama vile Kikuyu, Kiluo, Kinandi, Kiluhyia, Kikamba, Kilingala pale Wazaire walipofika Kenya na hata katika lugha ya Kiarabu. Hata hivyo, Kaleka (2008) anashadidi kuwa kwa muda mrefu tangu Kenya kupata uhuru mnamo 1963, nyimbo zilizotawala masikizi ya wakenya zilitungwa na kuwasilishwa kwa lugha zinazochukuliwa kuwa kadiri nazo ni Kiingereza, Kiswahili na lugha za wenyeji. Hata hivyo, kuanzishwa kwa idhaa za redio ‘FM’ katika miaka ya tisini kuliibua utunzi wa nyimbo hasa miongoni mwa vijana ambao wengi walitoka katika mitaa ya mjini Nairobi. Hapo ndipo safu nzima na mpya ya mashabiki ilipoibuka kutokana na maneno ya nyimbo hizi za watunzi.

Jean (2012) anasema kwamba katika miaka ya tisini, mtindo mpya ulitangulizwa Kenya kupitia kwa kanda za video, radio na runinga. Mtindo huu wenye sifa ya kufokafoka ulitambulika na wanamuziki wakaanza kutunga nyimbo katika mtindo wenyewe. Asemavyo Shisiali (2014) hapa nchini Kenya nyimbo hizi zinaaminika kutokea sehemu za mashariki mjini Nairobi hasa katika mtaa wa Dandora. Japo Hiigino (2009) akinukuliwa na Shisiali (2014) anasema kwamba waimbaji wa nyimbo hizi wanajihusisha na hali tambuzi ya mihemko yaani 'hiphop' ya California nchini Marekani.

Kuanzia pale, nyimbo za kizazi kipya zimeonekana kuonyesha matumizi kwa kiasi kikubwa ya lugha inayotumiwa miongoni mwa wanajamii mijini. Nyimbo hizi kwa sababu ya kuenea na kutawala usikizi wa Kenya zimeishia kuwa pendwa. Samper (2004) anathibitisha hili anapohoji kuwa nyimbo katika mtindo wa kufokafoka zimevuma katika masikizi ya hadhira Kenya katika siku za hivi karibuni. Kwake yeye, kilichoanza kama mwigo wa mtindo wa kimarekani katika vilabu na mashindano humu nchini kimenawiri na kuwa umbo linalobainisha utamaduni wa Kenya. Inavyotumika katika muziki huu wa kizazi kipya, utafiti huu unaona umuhimu wa kuchunguza lugha inavyotumika kupitisha ujumbe katika maneno ya nyimbo zinazowalenga na hivyo kushabikiwa na vijana.

Nyimbo za kizazi kipya zinachukuliwa kuwa mojawapo ya kipengele cha ule utamaduni wa 'hiphop'ambao ni aina ya ushairi, usimuliaji au usemaji unaopangwa vina kwa kufuata mdundo wa ala za muziki ambao ulikwisha rekodiwa awali. Kulingana na Neloon (2005) akinukuliwa na Shisiali (2014), hizi ni nyimbo zenye mahadhi ya mtindo wa fokafoka

uliotokea Marekani katika miaka ya 1970 miongoni ma jamii ya Waafrika wamerakani waliokuwa wafanyikazi katika jiji la New York. Nyimbo hizi alivyosema Orido mwandishi wa habari za burudani akinukuliwa na Nyaga (2016) zinahusishwa na vijana. Wazo hili linaungwa mkono na Shisiali (2014) anayesema kwamba lugha inayotumika katika nyimbo hizi ni lugha ambayo vijana Wakenya wanapenda kujihusisha nayo.

Nyimbo hizi zilizozuliwa kutoka kwa mtindo wa fokafoka hapa Kenya, kwa mujibu wa Gathigi (2012) zilikuzwa sana kutokana na kupanuliwa kwa kulegeza masharti ya vyombo vya habari. Upanuzi huu ndio ulileta idhaa za 'FM' zilizopatikana mno mjini mwanzoni. Idhaa hizi ziko hewani mchana na usiku kucha huku zikipeperusha kwa kiwango kikubwa burudani pamoja na maelezo machache ya kuelimisha. Aidha,idhaa hizi zilipozinduliwa wasikilizaji wengi wa walikuwa watu wenye umri chini ya miaka thelathini na tano. Gathigi (2012) anazidi kufafanua kwamba idhaa hizi zinazopatikana mijini huwalenga vijana na hivyo nyimbo za burudani zinazochezwa zinanuiwa kuwashughulikia mashabiki. Aidha anashadidia kwamba nyimbo hizo pendwa zinachukuliwa kuwa za mjini kwani waimbaji ni wakaazi wa mijini. Matumizi ya lugha katika nyimbo hizi kwa mujibu wa Gathigi (2012) yanakubaliana na usemi wa mtaani.

Nyimbo za kizazi kipya zinahusishwa na mtindo wa fokafoka zilizotungwa kwa kutumia kilugha cha Kiswahili zungumzi na hivyo kuchukuliwa kuwa nyimbo za mjini. Kulingana na Githiora (2002) nyimbo hizi zilihusishwa na wasanii hasa Kalamashaka na Hubert Nakitare (Nonini). Aidha Nyambura (2006) anauhusisha usuli wa nyimbo hizi na kikundi cha

Kalamashaka anaposema kwamba katika mwaka wa 1996 mandhari ya muziki Kenya yalibadilishwa na kikundi cha wasanii cha Kalamashaka kilipoibuka na wimbo 'Tafsiri Hii' ulioimbwa kwa Kiswahili cha mtaani. Ngunjiri (2006) anachangia suala hili kwa kusema kwamba hakuna aliyedhania kwamba nyimbo hizi zingevuma kabla ya Kalamashaka kuimba wimbo wa 'Tafsiri Hii'. Nyimbo hizi ziliendelea kupendwa na kuvuma hivyo majina ya kujitambulisha pia yakawa yanaibuliwa. Majina haya ni kama vile *Boomba, Kapuka* na hata *Genge*.

Kulingana na Wasike (2011), katika miaka ya 2002-2003 nyimbo hizi zilipata masikizi ya mara kwa mara kwenye idhaa za redio baada ya kuandaliwa na kituo cha kurekodi muziki cha Calif Records iliyokuwa chini ya usimamizi wa Clement Rapudo. Kulingana na Kaleka (2008), mnamo mwaka wa 2000 msanii Nonini aliibua istilahi *genge* na kuipigia debe kurejelea muziki huo wa kizazi kipya uliotia fora mijini hapa nchini Kenya. Kampeni hii hata hivyo haikufua dafu kwani nyimbo zilizorekodiwa kwenye kituo cha Calif Records ambacho kilikuwa ni kituo kikuu katika unakili na utayarishaji wa nyimbo hizi, ndizo ziliishia kurejelewa kwa neno hili *genge*. Hivyo basi,hamna istilahi maalum inayoweza kutumiwa kurejelea muziki huu wa kizazi kipya.

Kwa mujibu wa Josiah (2005) akinukuliwa na Kaleka (2008), nyimbo hizi zilitungwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili inayotumiwa mtaani. Anasema kuwa mtindo huu wa kuimba unachukuliwa kuwa aina ya muziki wa kisasa wa *fokafoka* yenye mianzo yake mjini Nairobi nchini Kenya inayojumuisha mitindo mingine kama vile ya kitamaduni na densi katika

kumbi za burudani. Githiora (2002) pia anashadidia kuwa kilugha cha Sheng kimetumika kwa kiwango kikubwa katika nyimbo hizi za kizazi kipya na hivyo kuishia kupanua matumizi ya maneno katika miktadha ya nyimbo hizo kutokana na masikizi ya nyimbo zenyewe.

Utafiti huu ulielekezwa na misingi kwamba katika nyimbo hizi za kizazi kipya kuna maneno ya Kiswahili yaliyotumika kuwasilisha maana zaidi ya ile ya kawaida. Lugha ya Kiswahili inayotumika katika nyimbo hizi ni ile zungumzi na ya mitaani isiyozingatia kanuni za sarufi. Nyimbo za kizazi kipya za Kenya zinahusishwa na Kiswahili kinachotumiwa mtaani na maana inazuliwa na hadhira.Hivyo, maana ya neno lilivyotumiwa katika nyimbo hizi hutegemea wasikilizaji wanavyofasiri dhana inayowasilishwa na neno. Ni katika mtazamo huu ndipo utafiti huu ulihitaji kuchunguza matumizi ya lugha hususan maneno ya Kiswahili na hivyo nafasi ya lugha katika nyimbo hizi za kizazi kipya zinazojivunia usikilizaji mkubwa.

Nyimbo za kizazi kipya anavyoshadidia Kaleka (2008) zimeenezwa zaidi na wasanii Hubert Nakitare (Nonini) na mwenzake Paul Nunda (Juacali). Wazo hili linaungwa mkono na Adol (2016) anayeshikilia kuwa wasanii hawa kwa nyimbo zao waliipa Kenya utambulisho kimuziki hasa katika miaka ya tisini na ile ya awali ya milenia. Mchango wao unadhihirishwa na tuzo mbalimbali walizopokea kwa sababu ya nyimbo zao na hata masikizi ya nyimbo zao yanayoonekana kuwapiku wasanii wengine. Aidha wameishia kuitwa ‘baba’ na ‘mfalme’ wa *genge* mtawalia. Kwa misingi hii utafiti huu ulijikita zaidi

katika nyimbo zilizoimbwa na wasanii hawa wawili. Wasanii wengine walioendeleza mtindo huu wa muziki ni pamoja na Flexx, Jimw@t, Pilipili, marehemu E-Sir, Gidigidi Majimaji miongoni mwa wengine hasa katika miaka ya 2000-2012.

Nyimbo za kizazi kipya zinazopendwa Kenya ni za aina nyingi. Nyimbo hizi kwa mujibu wa Chachage (2002) hubainisha matumizi ya maneno yanayoibuka kila siku ambayo yanaonekana kuwalenga hasa vijana na ndio wanaelewa maneno hayo. Hivyo, maneno ya nyimbo yamekuwa njia inayoshabikiwa ya kuifikia jamii na kustawisha mawasiliano. Uelewa huu ndio uliozua hitaji la kuchunguza matumizi ya maneno ya Kiswahili katika nyimbo hizi na hivyo hadhi ya lugha ya Kiswahili katika nyimbo hizi ambazo kimsingi zinachukuliwa kutungwa kwa lugha yenye mtindo maalum.

Nyimbo hutekeleza dhima kuu katika maisha ya mwanadamu ya kila siku bila shaka kwa sababu ya mvuto wake masikioni. Rivera na Benardo (2018) wanasema kwamba katika enzi za sasa nyimbo pia ni njia ya kuwasiliana iliyoenea sana na kuaminika kwa kote. Wanaendeleza wazo hili kwa kusema kwamba hata wale ambao masikizi yao ya nyimbo ni nadra hupata nyimbo zenyewe kwenye vipindi vya redio na runinga vinavyotumia lahani zinazovutia ili kutangaza bidhaa na huduma mbalimbali. Nguvu za nyimbo katika kutumbuiza na kuathiri watu zinazifanya nyimbo kuwa sehemu muhimu katika jamii na eneo pevu la tafiti jarabati. Hata hivyo kungali kuna mwanya wa kuchunguza maana kwenye nyimbo, inayofunuliwa kupitia kwa mtazamo wa kiisimu. Utafiti wetu kwa hivyo

ulitathmini mahusiano ya muziki na lugha kwa kuchunguza kisemantiki leksia nyimbo za kizazi kipya zilizoimbwa na Juacali na Nonini.

Tafiti za awali zimebainisha nafasi na uamilifu wa nyimbo katika jamii. Kuhusiana na lugha katika nyimbo, tafiti nyingi zimejikita kwenye mbinu na maudhui na jinsi yalivyosawiriwa. Hivyo dhima na uamilifu wa nyimbo pendwa katika jamii kwa kiasi kikubwa imetafitiwa. Aidha, kazi hizi zinahusu dhima na mahusiano ya muziki wa kizazi kipya na vijana katika jamii. Miongoni mwa tafiti hizi ni pamoja na zile za Nyairo & Ogude (2003, 2005, 2007) ambapo wamechunguza uamilifu wa nyimbo za kizazi kipya na dhima zao katika miktadha ya kijamii kama vile kisiasa. Isitoshe, mahusiano ya nyimbo hizi za *genge* na kilugha cha sheng' yametafitiwa na baadhi ya wasomi kama vile Attyang' (2002) alipoangazia kuzuka kwa Sheng', Ogone (2004) aliyetafitia matumizi ya sheng' katika usafiri na Kaleka (2005) aliyechunguza matumizi ya kilugha cha sheng' katika muziki wa kizazi kipya Kenya. Kutokana na tafiti hizi, maana zaidi yanayotokana na matumizi ya maneno ya Kiswahili katika nyimbo hizi ndio kiini cha utafiti huu.

**1.2 Swala la Utafiti**

Nyimbo huchangia kukua kwa lugha ambayo pia ni kifaa cha mwingiliano na hata mawasiliano. Inatarajiwa kuwa lugha yoyote inayotumiwa inaibuka kutokana na akiba ya msamiati ili kutoa maana kutegemea ujumbe na muktadha. Maana kutokana na matumizi ya maneno inaweza kuhusisha mawanda mapana ya kisemantiki. Hivyo basi, kuna nafasi ya kuibua maana mpya au hata kupanua maana za maneno hayo. Msamiati hukuzwa ili

kufanikisha mawasiliano mwafaka miongoni mwa wanajamiilugha husika. Mawasiliano kwa kuzingatia maana hutegemea muktadha.Hata hivyo, inabainika kwamba katika nyimbo za kizazi kipya kuna uwezekano wa matumizi ya maneno yanayowasilisha maana tofauti na ya kawaida kutegemea fasili za hadhira. Maana katika misingi hii japo katika muktadha mmoja yanaweza kutofautiana miongoni mwa wasikilizaji wa nyimbo hizo. Hivyo basi, utafiti huu ulishughulikia maana za maneno teuleya Kiswahili katika muktadha wa nyimbo teule, athari ya upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili na utata katika mawasialiano kwa mujibu wa matumizi ya maneno teule katika nyimbo za kizazi kipya za Nonini na Juacali.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

i. Je, maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za Nonini na Juacali yenye maana tofauti na maana za kawaida ni yepi na yametumiwa kuwasilisha maana zipi?

ii. Upanuzi wa maana ya maneno ya lugha ya Kiswahili katika nyimbo teule za Nonini na Juacali unaiathiri vipi lugha ya Kiswahili?

iii. Je, ni utata upi unaotokana na upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili yalivyotumika katika nyimbo teule zilizoimbwa na Nonini na Juacali kimawasiliano?

### 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza kisemantiki-leksia maneno ya Kiswahili katika nyimbo pendwa za kizazi kipya hapa Kenya. Ili kutimiza lengo hili madhumuni mahsusi yafuatayo yalishughulikiwa:

i. Kuchanganua maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za Nonini na Juacali yenye maana tofauti na maana za kawaida katika muktadha wa nyimbo teule.

ii. Kujadili athari ya upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za Nonini na Juacali kwa lugha ya Kiswahili.

iii. Kutathmini utata katika mawasiliano kutokana na upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili yalivyotumika katika nyimbo teule zilizoimbwa na Nonini na Juacali.

### 1.5 Umuhimu wa utafiti

Utafiti huu kwa misingi kwamba maana inatokana na muktadha, uliazimia kuonyesha jinsi ambavyo maana inafanyizwa katika muktadha wa matumizi ya maneno. Aidha, kutokana na uwezekano wa maana kufanyizwa katika muktadha maalum ambamo neno limetumiwa kutegemea anavyofasiri mpokezi wa ujumbe,utafiti uliazimia kuonyesha maana kimatumizi inavyozuliwa na watu tofauti katika muktadha mmoja hususan wa nyimbo za kizazi kipya.

Mtazamo hasi wa nyimbo hizi kwa sababu ya vipengele vya kileksia vinavyosawiri lugha isiyo na tasfida umekuwepo. hivyo basi, kuna msukumo kwa misingi hii kuitathmini lugha ya Kiswahili katika nyimbo za kizazi kipya nchini Kenya. Utafiti huu ulinuia kuchangia katika kutoa mwanga kwa kutazama mustakabali wa lugha ya Kiswahili katika muktadha wa

nyimbo za kizazi kipya hapa Kenya kando na makuzi ya msamiati wa Kiswahili kwa kuzingatia maana. Utafiti huu hususan uliangazia maneno ya Kiswahili katika muziki huu na namna maana inavyopanuliwa katika muktadha wa nyimbo hizi. Utafiti huu ulitarajia kustawisha tafiti nyingine zinazohusiana na semantiki. Zaidi ya haya, utafiti huu ulidhamiria kuchangia katika kuboresha nadharia za kiisimu zinazojikita katika maana na matumizi ya maneno hasa nadharia za semantiki.

## 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti ulikuwa na upeo maalum ili kuyatekeleza madhumuni yaliyowekwa. Utafiti huu ulijikita katika lugha ya Kiswahili kwa kutazama nyimbo za kizazi kipya Kenya zilizoimbwa na Juacali na Nonini kwa kutilia maanani maneno ya lugha ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule za wasanii hao. Kulingana na Obbo (2006), uimbaji wa kizazi kipya unashuhudiwa katika eneo nzima la Afrika Mashariki. Hii ni kwa sababu maneno yasiyokuwa ya Kiswahili pia hudhihirika katika usanii wao. Mihimili ya nadharia ya maana kimatumizi ilishughulikia upanuzi wa maana za maneno na athari zake katika lugha ya Kiswahili. Isitoshe, utafiti huu ulijishughulisha na utata katika mawasiliano unaoweza kutokana na upanuzi wa maana zinazotokana na matumizi ya maneno katika muktadha wa nyimbo teule.

## 1.7 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya maana kimatumizi iliyoasisiwa na Wittgenstein (1963) na kuendelezwa na Turner (2011). Wittgenstein (1963) anachukulia maana kuwa maelezo ya wazo anapojadili kwamba fasili ya dhana akilini inategemea lugha kwa hiyo

hapana tatizo la fikra au dhana kutowakilishwa. Hivyo, lugha inaweza kueleza dhana waziwazi. Lugha kulingana naye ni njia ya kujihusisha kwa ulimwengu na jinsi ulimwengu huo ulivyosawiriwa katika mfumo wa ishara. Hoja hii inathibitisha kwamba lugha ni njia ya kueleza kinachotolewa katika ulimwengu huo. Mawazo ya Wittgenstein yanajengwa zaidi na Turner (2011) anayesema kwamba maana ya usemi wowote ni jambo la matumizi yake miongoni mwa watumiaji wake.

Wittgenstein (1963) anashikilia kuwa maana inatokana na matumizi yake hivyo maana ya neno ni matumizi yake katika lugha linamotumiwa neno hilo. Aidha anahimili kuwa maneno yana maana katika matumizi yanayotofautiana kutegemea miktadha. Wittgenstein anasema kwamba matumizi mbalimbali ya maneno hayawezi kusimilishwa kwani ni tofauti kabisa. Matumizi haya mbalimbali ndiyo yanatoa maana hizi tofautitofauti kwa maneno.Kwa misingi hii matumizi pekee ndiyo yanayoyapa maneno maana. Turner (2011) pia anasema maana ya neno ni jinsi neno hilo lilivyotumiwa na wazungumzaji wa jamii husika. Mawazo haya yaliungwa mkono na Suguitan (2005) aliyesema kwamba, kamusi haiamui maana ya neno bali watumizi wa neno lenyewe ndio huamua maana kutokana na jinsi wanavyolitumia neno lenyewe. Anasema kuwa maneno ambayo ni sehemu ya lugha tawala yaweza kutumika kiistiari na kupelekea kupatikana kwa maana kuu au mantiki iliyo tofauti na asili yao.

Turner (2011) anayakuza mawazo ya Wittgenstein (1963) anaposema kwamba mazingatio faafu ya maana ya neno ni matumizi yake. Chukulio hili pia ni la Flofman (1997) kwamba maana ya neno ni njia zote ambazo kwazo neno hilo laweza kutumika. Yeye anapendekeza ya kwamba sehemu ya kimuundo ya maana ya neno kimsingi ni vipengele tengwa vya

matumizi vinavyopatikana katika njia zozote ambazo neno lenyewe laweza kutumika. Aidha anaelekeza kwamba katika utamaduni wowote ule kunapohitajika, majina ya vitendo mbalimbali na maneno ya kawaida yanayokaribia kimaana hutumika ifaavyo. Kutokana na wazo hili, Flofman (1997) anasema kuwa katika tendo lolote mahususi lililowekewa mipaka basi neno laweza kutumika kwa njia tofauti na ile ya kawaida na hivyo kusemekana kuwa na maana tofauti. Kwa hivyo njia iliyo maarufu kwenye isimu ni ile ya kuchukulia maana ya neno kuwa ni uwezekano wa matumizi yake katika mawasiliano.

Mtazamo wa Ritchter (2006) unachangia mawazo haya ya maana kimatumizi anaposema kwamba maana ya neno inaweza kuhusisha mambo mengi ambayo ni pamoja na makusudio yanayorejelewa kwa neno, ikiwa neno lenyewe ni la kutumika, uainishaji wake kisarufi na iwapo ina wimbo linaashiria athari fulani. Anaendelea kusema kuwa, ili kujua haya yote au kufikia vigezo hivi ndiko kujua matumizi. Kimsingi kujua matumizi ni kujua maana. Nadharia ya maana kimatumizi pia ilipata kunawiri katika chukulio la Baldwin (2007) kuwa maana ya neno huchunguzwa kwa upekee kwa kutaka kujua ni kwa nini neno fulani lina maana hiyo na jinsi maana hiyo inavyowasilishwa na hata panapotokea fasiri mbalimbali za maana za maneno. Kuligana na Baldwin (2007) dhana ya maana ya neno itaangaziwa kwa misingi ya matumizi na uwasilishaji wa ujumbe kwa mpokezi wa ujumbe unapowasilishwa na neno lililotumika, lilipotumika na lilivyotumika.

Wittgenstein (1963) anashadidia kuwa neno halimaanishi kitu kimoja katika kila matumizi yake. Matumizi kulingana na kanuni maalum ndiyo yanaweza kuwajibikia mawasiliano kwa sababu lugha ni njia ya mawasiliano. Katika utendaji, anashikilia kuwa maneno yana maana

iwapo tu yanaweza kutumika kutekeleza mambo. Neno linahusishwa na maana yake kanuni mahsusi ya matumizi yake yanapowekwa bayana. Maneno hupata maana kutoka kwa matumizi. Hata hivyo, wanachomaanisha watumizi wa maneno hakisalii sawa kila wakati maneno haya yanapotumiwa. Turner (2011) anaukuza mtazamo huu anapochukulia kwamba maana yoyote ile inapatikana katika nguvu ya ukweli kwamba inazingatiwa kwa namna fulani na wazungumzaji katika jamii fulani.

Kulingana na Wittgenstein (1963), mara nyingi japo si kila mara neno "maana" linapotumiwa linaweza kuchukuliwa kuwa maana ya neno si chochote zaidi ya matumizi yake. Anachukulia maana ya neno kuwa jambo la kile kinachofanywa na lugha. Hivyo maana ya neno ni matumizi yake katika lugha. Anaendelea kufafanua kwamba kujua maana ya neno kunahusisha kinachorejelewa na neno hilo, ikiwa neno lenyewe ni la kutumika mtaani, aina ya neno lenyewe na ikiwa neno hilo linawasilisha dhana nyingine. Kwa mujibu wa Wittgenstein (1963), maana haitegemei tu kinachosemwa bali pia muktadha. Hivyo maana hutolewa na mazingira. Kwa misingi hii, kila mtumizi wa neno fulani anaweza kumaanisha kitu tofauti kwa kuwa na hisia tofauti na mawasiliano yakawa magumu au hata kutowezekana kabisa.

Turner (2011) anakisia kwamba maana yoyote ile ya neno ipo kwa misingi ya chukulio la wazungumzaji wanaotumia neno hilo. Aidha, anavyochukulia mtu kuwa neno fulani linamaanisha kitu fulani huweza kuwa tofauti na anavyochukulia mtu mwingine kuwa maana ya neno lilo hilo moja. Kulingana naye, neno linaweza kuwa maana zaidi ya moja ila

kwa mujibu wa watumiaji wake. Makisio haya ndiyo yanaifanya nadharia ya maana kimatumizi kuzingatiwa hasa katika kuzua maana za maneno kutokana na muktadha wa matumizi ya maneno hayo. Hivyo, maana kimatumizi ilivyoasisiwa na Wittgenstein (1963) ilipata kuendelezwa inavyodhihirika katika mtazamo wa Turner (2011) katika uchanganuzi wa maana za maneno kimatumizi.

Msisitizo wa nadharia ya maana kimatumizi upo katika maana ya neno au kisemo kilichotumika katika muktadha maalumu. Kwa mujibu wa nadharia, muktadha unachukuliwa kuwawa kijamii,usemi na kiisimu.Muktadha wa kijamii unabainishwa katika hali ambapo maneno fulani yana maana katika jamii fulani ambapo pana dhana inayoashiriwa kwa maneno hayo lakini hayana maana katika jamii nyingine ambapo dhana hiyo haipo. Kwa mfano neno ngariba lina maana katika jamii inayojihusisha na ukeketaji ila katika jamii ambazo hazina utamaduni huu neno hili halina maana.Muktadha wa usemi nao huongoza uteuzi na matumizi ya maneno mbalimbali huku muktadha wa kiisimu ukibainishwa kwa maana ya neno katika sentensi kutegemea mazingira ya kiisimu ambamo neno hilo limetumika. Hivyo basi ni wazi kwamba nadharia hii inahalalisha tabia ya mabadiliko ya maana kutokana na muktadha na kuifanya maana iwe mali ya watumizi wa neno katika muktadha fulani kutegemea fasiri mbalimbali.

Kijumla, nadharia ya maana kimatumizi ina mihimili kuwa: maana ya maneno hupatikana katika matumizi yake. Pili, maana ya neno inatokana na muktadha wa matumizi ya neno lenyewe. Tatu, neno halimaanishi kitu kimoja katika kila matumizi yake. Hivyo, maana ya neno iangaliwe kwa kuzingatia muktadha wa neno na jinsi neno hilo lilivyotumika. Utafiti

huu uliongozwa na nadharia hii katika kubainisha maana ya maneno hasa kwa kujikita katika muktadha wa nyimbo teule. Maana za maneno teule kwa mujibu wa nadharia zilibainishwa kutokana na matumizi yao katika muktadha wa nyimbo teule. Kwa mfano neno lililotambuliwa kuwa na maana nyongeza lilibainishwa kwa kuzingatia mhimili wa nadharia kwamba maana ya neno ni matumizi yake. Matumizi zaidi ya maneno ya Kiswahili yaliweza kuonyesha upanuzi wa maana za maneno haya ambayo yana maana zao za kimsingi zilizoorodheshwa katika kamusi za Kiswahili.

Utafiti huu ulichanganua maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule za kizazi kipya katika mtazamo wa semantiki leksia ambao kulingana na Baldwin (2007) inahusu utambuzi wa maneno na uwasilishaji wa maana zao. Mtazamo huu unaasisi utoaji wa maana mahsusi na kamilifu ya maneno katika lugha. Mtazamo wa semantiki-leksia unatarajiwa kuvumbua jinsi maana yenye uwezo wa kuzidi maana ya kawaida inavyofikiwa kupitia kwa ubunifu na uelezi na kuishia kuiathiri lugha ya Kiswahili.

## 1.8 Hitimisho

Sura hii imewasilisha usuli wa utafiti kwa kuangazia lugha, maana na utata katika mawasiliano. Aidha suala la utafiti, maswali, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti pamoja na misingi ya kinadharia imewasilishwa hapa. Hata hivyo, masuala yote yaliyoibuka katika sura hii yanahitaji ufahamu na uelewa zaidi. Hivyo sura inayofuata inaangazia uhakiki wa maandishi mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu.

## SURA YA PILI

## MAPITIO YA MAANDISHI

### 2.0 Utangulizi

Maandishi yaliyopitiwa yalidhihirisha kuwa maana inaweza kuibuka kutokana na matumizi yake katika muktadha fulani. Kuzuka kwa maana zaidi ya zile za kawaida huweza kuiathiri lugha kwa namna fulani. Mojawapo ya athari hizo huwa ni makuzi ya lugha anavyothibitisha Anttila (1972) anaposema kwamba vitu vyote duniani hukua na vivyo hivyo lugha. Sura hii imegawanywa katika sehemu tatu za kimsingi ili kuangazia maandishi yanayohusika na mada hii ya utafiti. Sura hii inaangazia: dhana ya maana, mabadiliko na upanuzi wa maana pamoja na utata wa maana ya maneno unavyoathiri mawasiliano.

### 2.2 Dhana ya maana

Ili kufanikwa katika utafiti wa maana ni sharti kinachorejelewa kama 'maana' kieleweke. Ullman(1957) anasema kuwa maana ya maana ni mojawapo ya dhana zenye changamoto kutokana na machukulio mbalimbali kutoka kwa wataalamu ambao ni pamoja na wanafalsafa, wanasaikolojia na wanaisimu. Hili linadhihirisha kwamba kuna utata katika maana ya maana. Hivyo basi, kutokana na wingi wa mitazamo ya dhana hii ya maana, taratibu za kuitathmini maana ziliibuka.

Ogden na Richards (1923), Crystal (1987), Habwe na Karanja (2007) na Matinde (2012)wanakubaliana kuwa, neno 'maana' lina fahiwa nyingi kwani linaweza kudokeza sababu, kusudi, ishara, urejeleo, maelekezo, ufafanuzi, kufaa na ukweli.

Wittgenstein (1963) alichukulia maana kuwa maelezo ya wazo aliposema kwamba fasili ya dhana akilini inategemea lugha kwa hiyo hapana tatizo la fikra au dhana kutowakilishwa. Chomsky (1973) alifaulu kuonyesha kwamba maana ya maneno au vipengele vya kileksia hutegemea matumizi yao aliposanya mifano ya lugha. Utafiti wake ulidhihirisha kwamba vipengele vya kileksia vinahitaji kutathminiwa kwa makini ili kuleta maana. Utafiti huu ulizingatia dhihirisho hili kwa kujishughulisha na vipengele vya kileksia.

Kulingana na Leech (1977) na Kurniawan (2016) maana ni dhana zinazoweza kuhamishwa kutoka akilini mwa mzungumzaji mpaka akilini mwa msikilizaji kwa kuzijumuisha dhana hizo kama umbo moja la lugha. Kimsingi maana inarejelea namna zote ambazo lugha imefungamanishwa na ulimwengu. Vilevile, maana hutoka kwa lugha. Mitazamo hii ya Adedimeji (2006), Leech (1977) na Kurniawan (2016) ilitoa uelewa wa maana uliounufaisha utafiti wetu ambao ulichukulia maana kuwa kipengele muhimu cha lugha tena chenye uwezo wa kutathminiwa kurejelea matumizi na kusudi.

Lyons (1992) anaeleza kwamba kumekuwa na mjadala miongoni mwa wanafalsafa kuhusu kinachochukuliwa kuwa maana bila kufanikiwa kupata majibu toshelezi. Hii ni kwa sababu maana ina dhana mbili zinazotatiza: uwepo na mfanano. Hivyo, anachukulia maana kuwa dhana zinazoweza kuhamishwa kutoka akilini mwa wazungumzaji hadi akilini mwa wasikilizaji jinsi zilivyo katika umbo la lugha moja hadi nyingine. Maelezo haya ya Lyons (1992) yanaikita maana katika vigezo vya kusema na kusikiliza.

Kwa mujibu wa mitazamo hii maana ilichukuliwa kama kitu ambacho hakijatengamaa, kilicho tepetepe ama telezi kwani hakiwezi kushikika, kinateleza. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba wanaisimu walichukulia maana kuwa kitu muhimu katika mawasiliano.Aidha,maana inapokuwa tepetepe, mawasiliano huwa si kamili na hakika mawasiliano bila maana si kitu. Hii ni kwa sababu,maana ni muhimu sana katika mawasiliano kwani kuna kuwa na kitu ambacho mzungumzaji amekusudia kukisema ila anayepokea ujumbe pia ana uwezo wa kufanyiza maana ambayo huenda ikawa tofauti na ile iliyokusudiwa na msemaji.

### 2.3 Maana za maneno kimatumizi na muktadha

Lyons (1968) anasema kwamba maana na uamilifu wa neno hutokana na matumizi ya neno lenyewe. Hivyo, maana ya neno inatokana na uwezo wa neno lenyewe kutumika katika mawasiliano. Mtazamo huu unachukulia kwamba lugha ni kifaa cha kutekeleza majukumu mbalimbali kinachobadilika kulingana na mahitaji ya wanaoitumia. Kwa misingi hii, lugha inavyotumiwa wakati mwingine kwa kazi isiyo yake ya kawaida, maana ya neno inaweza kubadilika kulingana na matumizi tofauti. Ni mtazamo huu ndio uliegemewa katika kuchunguza maana za maneno ya Kiswahili katika muktadha wa nyimbo teule za kizazi kipya.

Falk (1973) katika kuchangia suala la maana anasema kuwa maana za maneno yanapotumiwa popote pale huangazia kusudi la mwasilishaji na mpokezi wa ujumbe. Aidha, katika kuangazia maana katika muktadha anachukulia kwamba wakati mwingine kanuni za

matumizi ya semi zinaweza kubadilika kutegemea mazingira ya matumizi yao. Hivyo maana hutokana na matarajio ya wale wanaoshiriki katika mawasiliano. Maoni haya yaliufaa utafiti huu uliozingatia namna lugha hususan maneno ya Kiswahili yanavyotumiwa kuwasilisha ujumbe kati ya waimbaji na hadhira. Utafiti huo uliegemea zaidi pragmatiki ila utafiti huu wa kisemantiki ulijikita katika maana ya maneno yanavyotumiwa katika muktadha wa nyimbo.

Brown na Yule (1983) wanachukulia maana kuwa kauli inayoweza kuchambuliwa kwa kuzingatia uzito inavyoibuliwa. Kwa hivyo wanaotumia lugha wakati mwingine humaanisha zaidi ya yale yanayosemwa hasa kutegemea miktadha tofauti. Kulingana nao neno linaweza kutumiwa kwa maana ya kimsingi au ya kawaida. Chukulio lao ni kwamba matumizi ya neno yanaifuma dhana inayorejelewa na neno hilo. Kwa kuwa utafiti huu ulihusu maana inavyoibuliwa katika miktadha ya nyimbo, utafiti wa Brown na Yule (1983) uliufaidi utafiti huu kwani kwa kuzingatia mawazo haya utafiti uliegemea vipengele vya maana, muktadha na matumizi ya maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za Nonini na Juacali. Utafiti ulinuia kutazama jinsi maana inavyoibuliwa katika muktadha wa nyimbo teule za Nonini na Juacali.

Jackendoff (1990) anaendeleza mchango wake kuhusu suala la maana kwa kutoa mitazamo mitatu ya maana ambayo yaweza kuchukuliwa kuwa viwango vya semantiki. Viwango hivi ni pamoja na semantiki leksia inayojikita katika maana ya maneno, semantiki maumbo

inayohusisha maumbo ya sentensi ambamo maana hujumuika kuunda maana ya sentensi au semi. Kiwango kingine ni pragmatiki au usemi ambamo maana hujumuika na ukweli kuhusu muktadha mbalimbali ili kuunda maana ya matini au usemi. Maelezo haya ya Jackendoff (1990) yaliufaa utafiti wetu kwani yalibainisha lengo la utafiti wetu. Utafiti ulikuwa wa kisemantiki leksia kwani ulijikita katika maana ya maneno ya Kiswahili yenye maana tofauti na maana za kawaida katika nyimbo teule za kizazi kipya hasa zilizoimbwa na Juacali na Nonini.

Wendell (1992) anasisitiza muhimu wa kuchunguza lugha kulingana na muktadha na matumizi yake. Hili ni katika jaribio la kufafanua jinsi mawasiliano yanavyotukia na uwezo wa mawasiliano kutukia katika matumizi ya lugha. Mtazamo wake ni kwamba maneno yanavyotumiwa kuwasilisha maana yanazua masuala yanayouzunguka mchakato mzima wa mawasiliano. Yeye anachukulia kwamba uamilifu wa lugha hukamilika ndani ya matumizi yake katika muktadha maalumu. Chukulio hili liliufaa utafiti huu uliobainisha maana zinazotokana na matumizi ya maneno ya lugha ya Kiswahili katika nyimbo teule za kizazi kipya.

Norwich (1998) anasema kwamba neno hukubalika katika lugha kutokana na matumizi yake hivi kwamba neno humaanisha kazi ya neno lenyewe katika mawasiliano. Chukulio hili linayaangalia maneno katika lugha kama vifaa vinavyojukumika kwa namna mbalimbali y**e**nye uwezo wa kubadilika kulingana na mahitaji ya watumiaji wao. Hivyo basi, kama vifaa vinavyotumiwa wakati mwingine kufanyia kazi isiyo yao ya kawaida, maana ya maneno

huweza kubadilika kulingana na matumizi tofauti. Mtazamo huu unaoonyesha mahusiano ya maana na matumizi, uliufaa utafiti huu ambao ulijishughulisha na maana zilizodhihirika za maneno yaliyotumiwa katika nyimbo teule za Nonini na Juacali.

Taiwo (2001) anachukulia kwamba matumizi ya lugha ni tendo la kijamii hivyo kuna hitaji la kubainisha jinsi lugha inavyohusiana na jamii na jinsi maana zinavyozuliwa katika maingiliano ya lugha kila siku. Anazidi kusema kwamba watu huchagua maneno yanayoeleza vyema zaidi maana wanazojaribu kuwasilisha kutoka kwa taratibu za lugha. Lengo haswa ni kuonyesha jambo au dhana inayoweza kutajwa inavyomaanisha. Mtazamo wa Taiwo (2001) unakikuza kipengele cha matumizi katika mchakato wa kufanyiza maana na kuunga mkono maana inayozuliwa kutokana na matumizi ambayo ndiyo kiini cha utafiti huu. Utafiti huu ulizingatia mtazamo wa Taiwo (2001) katika kuchanganua maneno katika muktadha wa nyimbo ambamo maneno yenyewe yametumika.

Maelezo mengine yaliyo muhimu kuhusiana na maana ya maneno ni yale yanayoibuliwa Farquharson (2004) aliyeutafitia muziki pendwa wa kisasa wa Jamaika unavyochangia Krioli inayotumika nchini humo. Kwake yeye, muziki huo ulipelekea kukua kwa Krioli ya Jamaika kwa kuzua maneno mapya, ufasiri mpya wa maneno yaliyokuweko awali au upanuzi wa kisemantiki wa maneno ambayo tayari yapo katika hazina ya msamiati wa lugha hiyo. Anaishia kupendekeza utafiti wa kisemantiki leksia wa muziki huo. Moja kati ya malengo yake ni kutazama michakato ya uundaji wa maneno, kupiga darubini mawanda ya kisemantiki ya vipengele vya kileksia katika muziki huo wa ‘dance hall’. Utaratibu wa

utafiti wake uliufaa utafiti huu ambao ulichanganua maneno ya Kiswahili katika nyimbo za kizazi kipya hususan za Nonini na Juacali.

Mwihaki (2004) anaangazia pia suala la maana kimatumizi kwa kurejelea lugha ya Kiswahili. Amejikita katika uainishaji wa maana akisisitiza kwamba uelewa wa aina za maana unaweza kurutubisha mawasiliano kwa kutumia maneno na hivyo lugha yoyote ile. Mtazamo huu wa maana kimatumizi ni nguzo ya utafiti huu ambao pia unajikita katika maana inayozuliwa kutoka kwa matumizi ya maneno katika lugha ya Kiswahili kwa namna isiyo ya kawaida. Kwa mujibu wa Mwihaki (2004), uainishaji wa maana una thamani katika jaribio la kueleza dhana na upeo wa maana. Hivyo, utafiti huu ulitofautiana na wake kwa mkondo uliochukuliwa wa kutazama maana kimatumizi, bila uainishaji wa maana hiyo iliyozuka kutoka kwa matumizi ya maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za kizazi kipya.

Kurnawian (2016) anarutubisha mtazamo wa maana katika ufasiri wa maana shirikishi ya maneno katika wimbo. Kulingana naye maana ni dhana zinazoweza kutoka akilini mwa mzungumzaji mpaka akilini mwa msikilizaji. Hivyo, kujumuishwa kwa dhana hizo kama umbo moja la lugha kunadhihirisha kwamba maana irejelee namna zote ambazo lugha imefungamanishwa na ulimwengu. Kwa mujibu wa Kurnawian (2016) maana inatoka kwa lugha. Utafiti wa sasa ulizingatia mtazamo huu lakini ukaangazia namna ambavyo maana inafanyizwa kutokana na matumizi ya maneno katika muktadha wa nyimbo. Kimsingi, maana pasipo uainishaji wowote ndio uliangaziwa japo kwa kujikita katika maneno ya nyimbo.

Kwa mujibu wa Chibueze, Ordu na Omoghie (2017) maana ndiyo zana ya lugha. Bila maana hamna lugha na kimsingi umuhimu wa lugha ni kule kuzua au kupitisha maana. Kwa hivyo, utafiti huu ulipambanua maana zilizozuka katika usanii wa kizazi kipya hususan nyimbo teule zilizoimbwa na wasanii Juacali na Nonini.

### 2.3 Mabadiliko na Upanuzi wa Maana

Mabadiliko pia huweza kutokea kwa kutumia rasilimali iliyopo ya manenokatika lugha yenyewe. Wakati neno linapopanuliwa kimaana na kuwakilisha dhanapana zaidi kuliko lilivyokuwalikiwakilisha awali, mabadiliko husemekana kutokeakatika neno hilo kwani limepata dhima mpya katika jukumu lake la kimsingi la kuwakiashiria cha dhana.Massamba (2004) anafafanua hali hii kwa kusema ni upanuzi wamaana ya neno hivi kwamba neno hilo linaweza kuingizadhana nyingine zinazokaribiana na ilemaana ya awali k.m *kichwa* (cha mwanadamu) lakini pianeno lililo na maana yakiongozi au sehemu ya mbele ya gari.

Bloomfield (1933) alizungumzia mabadiliko katika maana kwa kutaja ufinyu na upanuzi na maana miongoni mwa aina nyingine ya mabadiliko yanayoweza kutokea katika maana. Mtaalamu huyu aliendeleza mtazamo mwake kwamba mabadiliko katika maana ya neno fulani huyaathiri mahusiano ya neno lenyewe na maneno mengine. Kutokana na kazi yake Bloomfield (1933), utafiti huu uliyagusia mabadiliko ya maana yanayoithiri lugha ya Kiswahili kwa kulenga kipengele cha wingi wa maana unaojitokeza katika njia mbalimbali, kupitia usanii wa nyimbo.

Mchango mwingine unaohusiana na mabadiliko katika maana hususan wingi wa maana ni ule wa Ullman (1957) ambaye alishikilia kwamba mabadiliko ya maana ya neno yanaathiri

namna ambavyo neno hilo linahusiana na mengine. Katika kazi yake, anatofautisha namna na athari za mabadiliko katika maana ya maneno. Utafiti huu hata hivyo ulitathmini mawazo haya kwa kuonyesha wingi wa maana na athari ya maana nyingi kwa lugha nzima ya Kiswahili kwa mujibu wa nyimbo teule za wasanii Juacali na Nonini.

Blank (1998) alichangia kipengele cha mabadiliko katika maana alipozungumzia kani zinazosababisha mabadiliko katika maana katika lugha. Aliibua dhana ya muktadha anaposema kwamba mabadiliko katika maana yanaweza kusababishwa na matumizi ya maneno hayo katika mazingira fulani. Kulingana naye, maneno huweza kutoa maana zaidi na tofauti kutegemea muktadha wa matumizi yao. Aliyaendeleza mawazo haya kwa kusema kwamba maneno huweza kutumiwa katika miktadha kuwasilisha maana tofauti anazotaka kuwasilisha mzungumzaji. Utafiti huu hata hivyo ulichunguza maana tofauti anazoweza kupata msikilizaji ambaye pia ni mpokezi wa maana katika nyimbo teule. Utafiti huu ulijikita katika muktadha wa nyimbo ili kueleza maana zaidi zinazotokana na matumizi ya maneno ya Kiswahili yanapotumika katika nyimbo za kizazi kipya.

Fromkin (2003) anachangia suala la mabadiliko katika maana anaposema kwamba neno linalotumiwa kuashiria dhana fulani linaweza kubadilika kwa kupanuka. Hili basi linakuwa tukio la upanuzi wa maana zaidi ya ilivyomaanisha awali. Hivyo utafiti huu katika nguzo za Fromkin (2003) ulionyesha maana inavyotokana na matumizi ya maneno katika nyimbo za kizazi kipya.

Nyairo (2005) anachangia suala la ufasiri wa maana katika muziki wa kizazi kipya. Ananakili matini yenye maneno katika nyimbo na miktadha ya nyimbo hizi kwa mtazamo

wa kuchanganua maana na usimulizi katika nyimbo hizi. Nyairo (2005) kimsingi anajikita katika kutazama uteuzi wa lugha unavyochangia mapokezi ya hadhira na wazungumzaji wa lugha hiyo. Aidha anachunguza zaidi mahusiano baina ya muziki wa kizazi kipya na siasa. Mawazo ya Nyairo (2005) yaliendelezwa katika utafiti huu ambapo maana kimatumizi inabainishwa inavyochangia maendelezi ya lugha hasa ya Kiswahili kupitia nyimbo za kizazi kipya. Utafiti huu hata hivyo ulijikita katika maana zaidi zilizo tofauti na maana zilizozuliwa na wapokezi wa nyimbo teule za kizazi kipya hapa nchini Kenya.

Maxilom (2008) alitafitia mabadiliko ya maana ya maneno katika lugha ya Cebuano kwa kutumia mitazamo ya Crowley (1997) na Campell (1998) ya kuainisha maana na kuzua istiari kama moja kati ya yale mabadiliko ya maana yanayoweza kutukia. Aidha kulingana naye, upanuzi wa maana aghalabu hutokea katika lugha zungumzi. Maxilom (2008) anafafanua mabadiliko ya maana kuwa kubadilika kwa dhana zilizokuwa zinahusishwa na neno fulani pamoja. Kulingana nao, mabadiliko ya maana yanaweza kuziathiri maana za maneno yenyewe kwa kuchukua maana mpya. Kwa kuzingatia maelezo haya, utafiti ulijihusisha na mabadiliko ya maana. Hata hivyo, utafiti huu uliangazia mabadiliko yanayotokana na upanuzi wa maana na kujadili athari ya upanuzi wa maana kwa lugha ya Kiswahili.

Washington (2010) anaendeleza usawiri wa maana hasa inavyobadilika katika mtazamo wa Kiingereza kinachozungumzwa na Wamarekani weusi. Kulingana naye uchunguzi wa maana huzua maneno yenye maana mpya zinazokubalika katika jamii inayotumia na

inavyotumia maneno haya. Aidha maana huchangia mabadiliko katika lugha. Katika kazi yake, anadhihirisha kwamba maana kimatumizi yanahusisha maumbo ya lugha na muktadha wa kijamii. Utafiti huu uliendelea kuangalia maana ya maneno katika muktadha wa nyimbo na maana zinazoibuka katika nyimbo hizo zinavyoiathiri lugha ya Kiswahili.

Wambugu (2010) anachanganua mabadiliko ya maana katika maneno ya lugha ya Kikuyu japo kwa kutumia nadharia ya vitendo. Anatilia mkazo aina mbalimbali za mabadiliko katika maana na uainishaji wa mabadiliko hayo ya maana kando na kuondoa utata wa kimaana wa maneno yaliyopata maana zaidi ya zile za kawaida. Maana za maneno ya Kiswahili katika muktadha wa nyimbo za kizazi kipya zilichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya maana kimatumizi. Hivyo basi, utafiti huu ulichukua mwelekeo wa kisemantiki tofauti na utafiti wa Wambugu (2010) uliojikita katika pragmatiki. Aidha utafiti ulijikita katika maana kimatumizi katika muktadha kwa kuangazia wapokezi wa nyimbo teule za kizazi kipya.

Chukwuma (2012) katika mtazamo wa kimuziki anasawiri maana kama dhana inayoathiriwa na mambo tofauti tofauti. Kulingana naye ufasiri wa maana huegemea masuala mengi yanayosababisha kuzuka kwa maana tofauti na ile iliyokusudiwa. Utafiti huu unakubaliana naye kwamba, ni muhimu maneno hasa ya nyimbo yachunguzwe katika mwanga wa maana ambapo kiasi cha mtiririko wa lugha na jinsi lugha hiyo ilivyotumiwa kuwasilisha ujumbe kusudiwa inavyofaa. Utafiti huu hata hivyo ulijikita katika suala la maana kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ya maneno katika nyimbo.

Khachula (2013) vilevile anaangazia aina mbalimbali za mabadiliko katika maana katika lugha ya Lumarama, sababu za mabadiliko hayo na athari ya mabadiliko haya kwa lugha ya Lumarama. Kulingana naye, mabadiliko haya katika maana yanachangiwa na mwingiliano wa lugha ya Lumarama na lugha nyingine pamoja na ujio wa sayansi na teknolojia. Aidha anathibitisha kuwa mabadiliko ya maana katika maneno yanapelekea utata hasa wakati wa mawasiliano. Khachula (2013) anatumia misingi ya pragmatiki-leksia na utafiti wake uliufaa utafiti huu ambao pia ulijishughulisha na maana inayoibuka katika maneno ya Kiswahili hasa yanavyotumika katika nyimbo za kizazi kipya. Kwa misingi ya makisio ya Khachula (2013) utafiti huu uliangalia lugha ya Kiswahili katika mwanga wa matumizi yake katika mawasiliano kupitia kwa nyimbo.

Katika mtazamo wa maana kimatumizi, Odawo (2015) anadokeza kwamba lugha ni kifaa cha kutekeleza majukumu mbalimbali na kama chombo kinachobadilika kutegemea mahitaji ya watumizi wake. Hivyo kama kifaa kinavyotumika wakati mwingine kwa kazi isiyo yake ya kawaida, maana za maneno pia zinaweza kubadilika kutegemea matumizi tofauti. Kimsingi, Odawo (2015) anaangazia uwezekano wa mabadiliko ya maana katika lugha. Mitazamo hii iliufaa utafiti huu uliobainisha maneno teule ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo za kizazi kipya yanayobadilika kwa kupata maana zaidi yaani kupanuka kwa maana. Katika utafiti huu upanuzi wa maana na athari yake kwa lugha ya Kiswahili uliangaziwa ikizingatiwa kwamba ni muhimu kuelewa ni vipi kupanuka maana kunavyochangia katika lugha.

Kijumla, masuala yanayochangia mabadiliko na upanuzi wa maanani pamoja na: muktadha, mahusiano ya maneno, mtindo unaozua istiari,maumbo ya lugha pamoja na maingiliano lugha kando na sayansi na teknolojia. Upanuzi wamaana

**2.4 Utata na mawasiliano**

Mawasiliano yanajengwa kwa misingi ya maelewano kati ya mzungumzaji na msikilizaji. Mawasiliano yanachukuliwa kufanikiwa ikiwa mwasilishaji na mpokezi wa ujumbe wana fasiri moja ya maana iliyokusudiwa. Hata hivyo anavyosema Chapman (1989) kuna uwezekano wa kuuvuruga mchakato huu pale ambapo panazuka maana zaidi ya moja. Mwasilishaji wa ujumbe hasa msanii hutumia lugha kwa njia tofauti na yale ya kawaida yanayomwezesha kumshangaza mpokezi wa ujumbe wake na kuibua taswira yenye nguvu zaidi akilini mwake. Mtazamo huu wa Chapman (1989) uliupa utafiti huu mwanga wa utata na misingi ya kutukia kwa utata. Katika uelewa huu, utafiti huu ulibainisha utata unaotokana na maneno kuwa zaidi ya moja na uwezekano wa mawasiliano kwa maneno haya kuvuruga mawasiliano.

Mchango mwingine kuhusiana na suala la utata ni ule wa Bucaria (2004) aliyetafitia utata wa kimaana na kimuundo katika mada cheshi. Bucharia anajikita katika utata lakini kwa mtazamo chanya wa kuchangia kuleta ucheshi. Utafiti wa Bucaria ulitathmini fenomena ya lugha inayopelekea utata wa maana ambao huishia kusababisha ucheshi. Aidha mwingiliano wa utata wa maana ya maneno na ule wa kimuundo ulitathminiwa na utafiti ukaonyesha maana mbalimbali zinazozuka katika fasiri kwa misingi ya miundo ya maneno. Utafiti wa

Bucari (2004) uliufaa utafiti huu kwa kuupa mtazamo wa wingi wa maana unavyozua ule uwezekano wa kuvuruga maana inavyofasiriwa.

Mchango mwingine katika suala la utata ni ule wa Tambunan (2009) aliyechunguza utata wa maneno na kimuundo katika bango la *Your letters of the Jarkarta Post*. Katika utafiti wake alitumia nadharia ya Ullman (1977) ya utata kuonyesha maneno yaliyoleta utata na jinsi yalivyoleta utata hasa katika muundo wa semi na sentensi katika makala hayo ya *'The Jakarta Post'*.Alifaulu kuonyesha jinsi ambavyo utata wa kimuundo ulivyotawala kwani wasomaji walitatanishwa na maneno fulani yaliyokuwa na maana zaidi yalivyotumiwa pia kwa kiwango kikubwa katika muktadha huo hivyo kuvuruga mawasiliano pale wasomaji walipokosa maana kusudiwa.Utafiti huu ulizingatia mtazamo wa utata katika maneno na maana zaidi zinazoibuka katika nyimbo teule za kizazi kipya.

Kinanti (2014) alitathmini utata wa kileksia na kimuundo ulio katika mada za Gazeti la 'Suara Merdeka'. Utafiti wake ulionyesha ugumu wa kufasiri maana hasa kwa wasomaji wa gazeti hilo. Kutokana na utafiti huo utata wa maana hasa ya maneno yanachangia zaidi kuvurugika kwa mawasiliano kwani wasomaji wengi wanakosa kuelewa maana iliyokusudiwa katika matumizi ya maneno yaliyotumiwa kama anwani. Utafiti wa Kinanti ulichangia kudhihirisha utata wa maana ya maneno unavyovuruga mawasiliano katika usomaji wa gazeti. Utafiti huu pia ulitathmini utata wa maana lakini kwa kujikita katika maneno hususan ya Kiswahili yalivyotumika nyimbo teule za kizazi kipya. Aidha utata unavyosababishwa na wingi maana ulibainika katika utafiti huu.

Khoshkhabar na Iraji (2015) walionyesha utata wa kijamii katika magazeti ya Iran kwa kutumia magazeti kwa mtazamo wa maana. Utafiti wao ulifaulu kuonyesha jinsi ambavyo uzingativu wa muktadha katika ufasiri wa maana na uakifishaji faafu unavyoweza kusaidia kuondoa utata. Utafiti wao ulieleza kuwa utata wa muundo unaweza kupatikana katika muktadha wa vyombo vya habari vya Iran na hivyo kubainisha mchango wa muktadha katika mchakato wa kufanyiza maana. Kama utafiti wa Khoshkhabar na Iraji (2015) ulivyojikita katika utata wa maana unaotokana na maneno katika muktadha maalum ndivyo utafiti huu pia ulijishughulisha na suala la utata wa maana unaoibuka kutokana muktadha wa muziki wa kizazi kipya. Utafiti ulitathmini hali ya kuwepo kwa utata wa kimaana katika mawasiliano kutokana na maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule.

Miller, Kluver, Thebault-spieker, Tervan na Hecht (2017) wanatathmini ufasiri wa ishara za emoji na uwezekano wa kuvurugika kwa mawasiliano. Utafiti wao ulifaulu kuonyesha matumizi ya zile ishara za emoji zilizoongeza utata kwani ulibainisha maana zinavyozuliwa kutoka kwa ishara za emoji na mahusiano baina ya maana na muktadha. Aidha walijaribu kuonyesha utaratibu wa kufasiri maana za ishara za emoji na uwezekano wa kuvurugika kwa mawasiliano. Utafiti huu hata hivyo, ulijikita katika maneno japo ulifaidi zaidi kutokana na utafiti wa Miller na wengine (2017) kwa kuchukua mtazamo wa wingi maana kuonyesha utata na namna mawasiliano yanavyoweza kuvurugika.

## 2.4 Hitimisho

Sura hii imehakiki maandishi mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu mada hii. Michango ya kazi awali zinazohusiana na mada imejadiliwa na nafasi iliyonuiwa kuchangiwa katika usomi pia imebainishwa. Katika juhudi za kuweka wazi uchanganuzi imebidi kutalii masuala ya maana na mabadiliko yake pamoja na athari inayotarajiwa katika lugha. Aidha dhana ya utata wa maana na mawasiliano zimeangaziwa. Yaliyojadiliwa hapa yachukuliwe kama kiungo cha kufungamanisha uatangulizi na hatimaye uchanganuzi wa kazi hii.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii itataarifu jinsi utafiti huu ulivyofanywa. Muundo wa utafiti, eneo la utafiti, waliolengwa katika utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji data na hata mchakato wa kukusanya data umeangaziwa. Aidha jinsi ya kuwasilisha na kuchanganua data iliyokusanywa, tathmini ya ufaafu na utegemezi wa vifaa vya kukusanya data na maadili katika utafiti huu yameangaziwa katika sura hii.

## 3.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo elezi. Kwa mujibu wa Saravanavel (1992), kimsingi muundo elezi ni uchunguzi unaohusishwa pakubwa na makisio ya kisasa na dhahania ya undani wa utafiti wenyewe. Muundo elezi ulisaidia kuchambua na kueleza data iliyokusanywa. Data ya utafiti huu ilikuwa ya kithamano na fafanuzi kwani matokeo yalikuwa ithibati ya kuwepo kwa upanuzi wa maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule za kizazi kipya. Kulingana na Salinger na Shohamy (1990), utafiti elezi hutumiwa kustawisha uwepo wa tukio la kiasili linalohusiana na makuzi yake na kuichakata kwa kueleza dhahiri data iliyokusanywa. Kupitia maelezo ya data, utafiti uliweza kuonyesha jinsi upanuzi wa maana unavyoiathiri lugha ya Kiswahili. Aidha, utafiti uliweza kueleza uwezekano wa kuvurugika kwa mawasiliano kunakosababishwa na utata unaotokana na kuwepo kwa maana zaidi za maneno ya Kiswahili yaliyotumiwa katika nyimbo teule.

### 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa kisemantiki hususan semantiki-leksia ambapo maneno ya nyimbo hizi teule ndizo zilizoangaziwa katika tathmini ya maana kimatumizi katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu uliwahusisha washiriki kutoka katika bewa kuu la Chuo kikuu cha Maseno. Eneo hili lilitarajiwa kutosheleza mahitaji ya utafiti kwa mujibu wa malengo yake kwani kuna vijana wenye asili mbalimbali kijamii wanaoshabikia nyimbo hizi za kizazi kipya. Chuoni humo mna wanafunzi wanaotoka sehemu mbalimbali nchini na walimu wa Kiswahili waliotumiwa kama watafitiwa wakuu. Utafiti huu ulilenga nyimbo za kizazi kipya.

### 3.3 Kundi Lengwa

Utafiti huu ulilenga nyimbo 66 za kizazi kipya zilizozuliwa katika muda wa miaka ya 2000-2016 za Nonini na Jua Cali (www.softkenya.co.ke). Kuna wasanii wengi wanaoimba nyimbo hizi za kizazi kipya hapa Kenya kwa mujibu wa Nakhone na Musungu (2014). Wasanii hawa ni pamoja na Nonini, Juacali, Mejja, PiliPili, P-Unit, Flexx, Jimw@t, Longombas, Nameless, na marehemu E-sir ambaye ameendelea kushinda tuzo hata baada ya kifo chake. Utafiti huu hata hivyo ulichunguza nyimbo za wasanii Nonini na Jua Cali katika misingi kwamba wasanii hawa wanachukuliwa kuwa watangulizi wa muziki wa kizazi kipya Kenya, wamesalia kuimba nyimbo hizi, tuzo kadhaa walizoshinda nchini na kimataifa kando na idadi kubwa ya nyimbo walizoimba (www.capitalfm.co.ke). Washiriki katika utafiti huu walipatikana kutoka kwa wanafunzi wa chuo kikuu cha Maseno, bewa kuu ambao walikuwa ni wanachama wa chama cha Kiswahili chuo kikuu cha Maseno (CHAKIMA). Kundi hili la

wanafunzi lina wanachama takriban 180 wanaoweza kufikika na wanaojishughulisha na masuala ya lugha ya Kiswahili. Utafiti huu pia uliwahusisha wataalamu wa lugha na isimu kutoka katika idara za lugha na isimu katika chuo kikuu cha Maseno ambao ni 16 (9 wa Kiswahili na 7 wa Kiingereza) wa Chuo Kikuu cha Maseno (maseno.ac.ke). Hawa ndio waliokuwa waarifu wakuu katika utafiti huu.

**3.4 Usampulishajina Sampuli**

Usampulishaji kulingana na Saravanavel (1992) ni mchakato wa kuteua sehemu ya jamii ya utafiti. Hata hivyo Sankoff (1980) anaonya kwamba usampulishaji unafaa kuhusishwa kwa karibu na madhumuni ya utafiti wenyewe. Utafiti huu ulisampulisha nyimbo za Nonini na Jua cali ambao ni miongoni mwa wanamuziki wanaoimba nyimbo za kizazi kipya Kenya. Sampuli wakilishi ya nyimbo iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa kimaksudi. Kwa mujibu wa Mwanje (2001), Kombo na Tromp (2006), usampulishaji wa kimakusudi huzingatia, huangalia na kuchuja data ili kupata sampuli yenye sifa zinazohitajika. Aidha wanavyofafanua, Gall, Borg na Gall (1996) usampulishaji wa kimakusudi ni usampulishaji ambapo uteuzi unafanywa kuegemea maamuzi ya kibinafsi kwa minajili ya uelewa wa kina wa kile kinachotafitiwa. Mbinu hii ilitarajiwa kumwezesha mtafiti kujikita tu katika nyimbo ambazo zilikuwa zinatarajiwa kuwa na maelezo yaliyohitajika ili kufikia madhumuni ya utafiti huu. Mtafiti alihusisha nyimbo zilizokuwa na maneno mengi ya Kiswahili yanayobeba maudhui. Nyimbo zilizoteuliwa ni zile zilizovuma kiasi kwamba ziliweza kutambuliwa moja kwa moja hata na washiriki katika makundi ya majadiliano. Kwa misingi hii jumla ya nyimbo5 yaani 2 za Jua Cali na 3 zilizoimbwa na Nonini zilihusishwa kwa kusampulishwa kimakusudi katika utafiti huu.

Mulusa (1990) anasema kuwa sampuli ndogo zaidi ni ile ya washiriki thelathini walioteuliwa kibahatishi. Gay (1996) anaunga mkono hoja hii kwa kusema kuwa katika tafiti nyingine wataalamu huchukulia mwongozo wa jumla kuwa washiriki thelathini. Kwa misingi hii, utafiti huu uliazimia kuwashirikisha wanafunzi 30 kutoka katika chama cha Kiswahili cha chuo kikuu cha Maseno (CHAKIMA) katika chuo kikuu cha Maseno. Kutokana na mazungumzo ya awali na wanafunzi hawa, kundi hili lilionekana kuwa na wanafunzi ambao ni wasikilizaji wa nyimbo hizi za kizazi kipya au wanafikiwa na muziki huu. Isitoshe idadi kubwa ya wanachama hawa ni wanafunzi wa Kiswahili na hivyo wenye kuvutiwa zaidi na masuala ya lugha ya Kiswahili. Hivyo mtafiti aliandaa vijikaratasi 30 vilivyonakiliwa 'ndio' na vingine 'la' alivyowasilisha kwa wanachama wa CHAKIMA katika mojawapo ya mikutano iliyofanyika chuoni Maseno mwaka wa 2018.Hii ni baada ya kuwaarifu kuhusu utafiti huu. Kwa kutumia njia hii washiriki thelathini walipatikana ila 27 ndio walipofika katika vikao majadiliano na hivyo kushirikishwa katika majadiliano katika makundi.

Waarifu wakuu katika utafiti huu walikuwa wataalamu 6 wa kimawasiliano ambao ni wahadhiri wa lugha na isimu kutoka katika idara za lugha na isimu katika chuo kikuu cha Maseno ambao waliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji kiratibu. Ili kupata sampuli ya wasailiwa hawa wakuu mtafiti alizingatia orodha ya majina ya wahadhiri wa idara ya Lugha na Isimu pamoja na ile ya Kiswahili na lugha nyinginezo za Kiafrika. Mtafiti alihesabu majina na kuteua la tatu hivyo kuishia kupata majina sita. Msailiwa wa sita alikuwa ni mwenye jina la kumi na sita.

### 3.5 Njia na Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Kasomo (2006) anasema kwamba ili utafiti uwezekane na ufanikiwe sharti mtafiti atumie mbinu na vifaa faafu. Yeye anachukulia kwamba kifaa kinachofaa hurahisisha kukusanya habari inayohitajika. Data katika utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili, mijadala ya vikundi lengwa pamoja na unukuzi. Utafiti huu ulishirikisha uthibitishwaji katika ukusanyaji wa data. Oslen (2004) anafafanua uthibitishwaji kama kuchanganya njia za ukusanyaji data au data yenyewe ili kupata mitazamo mbalimbali inayoangaza mada husika. Altrichter, Posch na Somekh (1996) wanaeleza uthibitishwaji kuwa ni njia ya kupata picha inayosawiri hali ilivyo kwa usawa na utondoti. Utafiti huu ulitumia usaili na majadiliano kimakundi baada ya kudondoa maneno yaliyochukuliwa kuwa yanahusiana na utafiti kutoka kwa maneno ya nyimbo teule, ili kupata maelezo kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti wenyewe. Katika makundi, maana za maneno ya Kiswahili yaliyochukuliwa kuwa na maana tofauti na zile za kawaida yalibainishwa na kudondolewa kutoka kwa maneno ya nyimbo teule. Maneno hayo teule yalielezwa na matumizi ya maana hizi zaidi katika mawasiliano yakajadiliwa. Usaili nao ulitoa uelewa wa mtazamo unaoibuka kutokana na upanuzi wa maana na athari yake kwa lugha ya Kiswahili kando na kuthibitisha utata wa kimaana katika maneno husika ya Kiswahili, hivyo uwezekano wa kuvurugika kwa mawasiliano.

Kulingana na Cohen na Manion (1986), katika sayansi za jamii, uthibitishwaji hujaribu kufafanua kikamilifu ukwasi na uchangamano wa hulka ya mwanadamu kwa kuichunguza kutoka kwa zaidi ya mtazamo mmoja. Katika utafiti wa kithamano kama huu, uthibitishwaji uliongeza kusadikika, uhalali na ukamilifu wa matokeo na hivyo kutoa picha tondoti. Utafiti

ulijikita katika lugha ya Kiswahili ambapo maneno ya Kiswahili yaliyokwisha kubainishwa, yalichanganuliwa yalivyotumiwa katika nyimbo teule za kizazi kipya na maana zao hasa katika muktadha wa nyimbo hizo teule. Aidha, mitazamo kuhusiana na maana katika muktadha wa nyimbo hizi teule ilibainishwa na kuelezwa baada ya mahojiano. Data zote zilikusanywa, zikahakikiwa, zikachambuliwa, na hatimaye kutolewa maelezo ya kina kwa kuongozwa na nadharia ya maana kimatumizi iliyoendelezwa na Turner (2011).

Vifaa vilivyotumiwa kukusanya data katika utafiti huu ni kicheza CD, kinasa sauti, kalamu na kitabu cha kunukulia. Baada ya kupata sampuli ya nyimbo, nyimbo teule zilisikizwa na kunakiliwa kisha maneno ya Kiswahili yakadondolewa kutoka kwa nakala za nyimbo hizo teule. Hii ndiyo data iliyotumiwa kuandaa maswali yaliyojadiliwa katika makundi baada ya washiriki kuwekewa na kusikiza nyimbo hizo teule. Mbinu za ukusanyaji wa data zinafafanuliwa kama zifuatazo:

### 3.5.1 Unukuzi

Nyimbo 5; 3 za Nonini na 2 za Juacali ziliteuliwa na kutumiwa katika utafiti huu. Kwa misingi ya maana, maneno ya Kiswahili hasa yaliyowasilisha maana zisizo za kawaida katika muktadha wa nyimbo teule yalibainishwa. Washiriki waliokuwa wakijadiliana katika makundi waliyabainisha maneno ya Kiswahili yenye dhima ya kubeba ujumbe au maana kutoka kwa nyimbo teule. Baada ya kunakili maneno haya ya kiswahili, hasa ikizingatiwa kwamba washiriki hawa walikuwa ni wanafunzi wa Kiswahili katika chuo kikuu hivyo

wenye ujuzi kuhusiana na maneno katika lugha ya Kiswahili, maana za maneno hayo kama yalivyotumika katika nyimbo teule zikatolewa katika majadiliano hayo.

### 3.5.2 Usaili

Katika utafiti huu waarifu wakuu walikuwa ni wataalamu wa mawasiliano na lugha. Utafiti huu uliwashirikisha waarifu wakuu 6. Wataalamu hawa walihojiwa ana kwa ana katika ofisi zao na kupata mtazamo wao kuhusiana na tukio la upanuzi wa maana, ukubalifu wa maana zile zaidi pamoja na matumizi ya maneno haya katika mawasiliano ya kila siku katika jamii, athari za upanuzi wa maana kwa lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa sanaa ya kisasa hususan nyimbo za kizazi kipya za Kenya. Dodoso iliyotumika kuwahoji wataalamu wa lugha na mawasiliano kutoka idara za lugha na mawasiliano katika chuo kikuu cha Maseno ilikamilisha shughuli ya kukusanya data ili kuridhia matakwa ya madhumuni ya utafiti. Ili kuzuia kupotea kwa maelezo, yaliyosemwa yote yalirekodiwa kwa idhini ya wahojiwa kwa kutumia kinasa sauti.

### 3.5.3 Majadiliano Kimakundi

Haya ni majadiliano yenye mpangilio maalum yanayohusisha kati ya washiriki kuhusu suala fulani. Katika makundi 5 yenye watu 6 kwa kila kikundi, majadiliano yaliyochukua kadiri ya masaa mawili yaliyofanyika chuoni Maseno kwa siku tatu tofauti. Nyimbo zilizoteuliwa kutumiwa katika utafiti huu zilichezwa kisha maneno ya Kiswahili yaliyochukuliwa kuwa na maana tofauti na maana za kawaida, yalibainishwa, yakadondolewa na kunakiliwa na washiriki wenyewe. Maana za maneno haya zilielezwa na washiriki wenyewe katika

majadiliano hayo. Katika makundi haya pia upanuzi wa maana ulibainishwa pamoja na athari ya upanuzi huo wa maana kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo majadiliano haya yalikuwa muhimu katika kujibu maswali ya utafiti huu ya kwanza na pili. Waliohusishwa na majadiliano hayo ni wanafunzi wanaosomea Kiswahili katika chuo kikuu tena ni wanachama wa CHAKIMA wa chuo kikuu cha Maseno. Hivyo, tajriba yao ya lugha ya kiswahili iliunufaisha utafiti kwani kama wapenzi na watetezi wa lugha ya Kiswahili,mitazamo yao kuhusiana na lugha ya Kiswahili katika enzi ilijitokeza wazi hasa kwa kuzingatia nyimbo za kizazi kipya. Makundi hayo ya majadiliano yalitimiza madhumuni ya kwanza na pili kwa mujibu wa maswali waliyojikita kwayo. Yaliyojadiliwa katika makundi haya yalinukuliwa na kurekodiwa kwa kutumia kinasa sauti, kalamu na karatasi.

### 3.6 Ufaafu na Utegemezi wa Vifaa vya Kukusanya Data

Ili kutathmini ufaafu na utegemezi wa vifaa vya kukusanya data mtafiti alifanya utafiti majaribio katika bewa la mjini Kisumu la chuo kikuu cha Maseno kwa kutumia sampuli jaribio. Majaribio haya yalifanywa kwa mujibu wa Gay (2009) kwa kuzingatia maadili na vigezo vyote vinavyonuiwa kuzingatiwa katika utafiti wenyewe. Ili kuhakikisha uhalali wa vifaa vya utafiti, mtafiti alihakikisha kuwa vifaa vyenyewe vinaoana na malengo ya utafiti akisaidiwa na wasimamizi wake. Hii ni kwa misingi ya Grinuel (1993) anayesema kwamba vifaa vya utafiti hufanyiwa majaribio ili kusaidia kupunguza makosa yanayoweza kutokea katika matumizi ya vifaa vya utafiti. Majaribio haya yaliwasihirikisha wanafunzi wa miaka ya kwanza na pili wa Kiingereza.Mtafiti alipata fursa ya kuijaribu rekoda na kuboresha maswali ya majadiliano. Aidha mtafiti aligundua kuwa maneno ya nyimbo yaliyoandikwa

yalihitajika kwa washiriki ili waweze kusoma na kuchanganua maneno yaliyokuwa yakiangaziwa katika utafiti huu.

### 3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Kwa mujibu wa Selinger and Sohamy (1989), uchanganuzi wa data ulihusisha kupekua, kuratibu, kufanya muhtasari na usanisi wa data ili kufikia matokeo na maoni yaliyotokana na kuzingatia suala zima. Uchanganuzi wa data ulihitaji uainishaji wa vipengele changamano katika sehemu nyepesi na pia kuleta pamoja katika mipango mipya kwa kusudi la ufasiri. Uchanganuzi wa kithamano ulihusisha hasa uchanganuzi wa kimaudhui. Kutokana na uchanganuzi wa aina hii, data iliyokusanywa iliwekwa katika maudhui faafu kulingana na madhumuni ya utafiti. Data ilichambuliwa na kuwasilishwa kimaelezo na pia kwa kutumia jedwali lenye kufafanua maana za maneno. Data iliyokusanywa baada ya kupangwa ilichanganuliwa kithamano kurejelea mihimili ya nadharia ya maana kimatumizi kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti.

### 3.8 Maadili Katika Utafiti

Mathooko (2007) anafafanua maadili kama kaida zinazoelekeza tabia za watu katika mahusiano yao ya kila siku na wenzao. Katika utafiti, maadili ni uwajibikaji na uelekevu kitabia kuhusiana na haki za washiriki wa utafiti, nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo ya utafiti wenyewe kwa uadilifu ili kuifaidi jamii. Kibali cha kufanya utafiti huu kiliombwa kutoka kwa kamati ya maadili ya chuo kikuu cha Maseno (MUERC). Hivyo mtafiti alipata barua iliyomwidhinisha kukusanya data kutoka kwa washiriki. Mtafiti

pia aliwasihi washiriki kufanya hivyo kwa hiari kwani kwa mujibu wa Schutt (2006) ni muhimu kuhakikisha kwamba washiriki wa utafiti wanashiriki kwa kujitolea. Zaidi ya hayo, mtafiti alizingatia usiri wakati wa kukusanya data hivi kwamba hakuna ambaye angejua chanzo cha data wala utambulisho wa washiriki. Haki miliki ya waandishi wa makala na wasanii waliotunga na kuimba nyimbo teule zilihifadhiwa. Lugha faafu ilitumiwa katika utafiti huu na mapendekezo ya tafiti zaidi yalitolewa bila kudunisha juhudi zilizofanywa awali kuhusiana na swala la utafiti. Habari zilizopatikana zilitumika kwa minajili ya utafiti tu na usiri kuhusu utambulisho wa watafitiwa ulidumishwa.

### 3.9 Hitimisho

Sura hii imebainisha jinsi utafiti huu ulivyofanywa, waliolengwa, uteuzi wa walengwa hao, mbinu zilizotumika kukusanya data pamoja na maadili yaliyozingatiwa katika utafiti huu. Vilevile tathmini ya ufaafu na utegemezi wa vifaa vya kukusanya imefanyika kwa mujibu wa malengo ya utafiti.

## SURA YA NNE

## MATOKEO NA MJADALA

### 4.0 Utangulizi

Kombo na Tromp (2006) wanafafanua uwasilishaji wa data kama namna ya kupanga data ili ziweze kueleweka vizuri, na uchambuzi wa data ni kuangalia kwa undani data zilizopangwa na kuzitolea hitimisho. Babbie (1999) naye anachukulia uchambuzi wa data kuwa kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo inamwezesha kukamilisha malengo ya utafiti husika. Best (1981) anasema kwamba sura hii ndiyo moyo wa ripoti ya utafiti. Katika sura hii data iliyokusanywa imechanganuliwa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti ambayo yalikuwa ni: kuchanganua maana za maneno ya Kiswahili yalivyozua maana zaidi ya kawaida katika nyimbo teule zilizoimbwa na Juacali na Nonini, kutathmini athari ya upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule zilizoimbwa na Juacali na Nonini kwa lugha ya Kiswahili, pamoja na kuthibitisha utata wa kimaana katika mawasiliano kutokana na maneno ya Kiswahili yalivyotumika katika nyimbo teule zilizoimbwa na Nonini na JuaCali. Maelezo na fasiri ya data yamefanywa kwa kuweka maudhui na maneno sisisi ya nyimbo teule na kutumia mihimili ya nadharia ya maana kimatumizi na maandishi yanayohuisana na mada.

### 4.1 Maana za maneno katika nyimbo teule

Utafiti ulibainisha maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za Juacali na Nonini yenye maana tofauti na maana za kawaida na kueleza maana zao. Nyimbo tano zilizoteuliwa ni; Mabeshte damu, Nyundo zilizoimbwa na Juacali, Kiasi na Manzi wa Nairobi na Nonini

zilizoimbwa na Nonini na We kamu ulioimbwa na Nonini kwa kumshirikisha Juacali. Kutokana na usemi wa watafitiwa mbalimbali, ilidhihirika kuwa muktadha ni muhimu katika kubainisha maana ya maneno. Katika mahojiano, wasailiwa walizungumzia nafasi ya muktadha katika mchakato wa kuzua maana za maneno:

**Msailiwa wa kwanza**

> Wajua semantiki hasa pragmatiki maana ni muktadha ushaona?Neno hupewa maana na muktadha.La sivyo wajua  maneno haya hayana maana.Hupewa maana na miktadha ,miktadha mbalimbali kwa neno moja litakuwa na maana hivi katika muktadha huu neno lilelile litakuwa na maana tofauti katika muktadha tofauti ushaona?Ukisema kwamba mtu huyu ni mchafu kiwanjani.Huu ni muktadha wa kiwanjani,michezoni,ule uchafu si sio kwamba kapakwa tope ahaha ni tofauti.Mtu anaweza akawa mchafu kwamba matendo yake si mazuri siyo,katika muktadha ambapo tunazungumzia tabia,muktadha uwe ni tabia.Muktadha ni mchezo kwa hivyo mtu mchafu ni kwamba yeye ni hodari sana katika ule mchezo. Hivyo, muktadha ndio hutupa maana ya neno.Maneno yenyewe kama yalivyo hayana maana.

Msailiwa anabaini kuwa maana ya neno hutolewa na muktadha anaposema *Neno hupewa maana na muktadha*. Kwa mujibu wa msailiwa huyu, maana inafanyizwa kutoka kwa muktadha na hivyo kuna uwezekano wa neno moja kuwa na maana nyingi tu kwa kuzingatia muktadha. Maneno huchukuliwa kuwasilisha dhana fulani katika muktadha ambamo maneno hayo yanatumiwa. Maana tofauti za maneno zinaibuka katika hali ambapo neno limetumiwa katika muktadha moja likawasilisha dhana fulani katika muktadha huo, kisha neno lili hili likatumika katika muktadha mwingine na kuwasilisha dhana nyingine tofauti. Hivyo maana inazuka kutegemea matumizi ya maneno katika miktadha mbalimbali. Anashadidia wazo hili kwa kutoa mfano anaposema *Ukisema kwamba mtu huyu ni mchafu kiwanjani .Huu ni muktadha wa kiwanjani,michezoni ,ule uchafu si sio kwamba kapakwa tope ahaha ni tofauti.Mtu anaweza akawa mchafu kwamba matendo yake si mazuri*

*siyo,katika muktadha ambao tunazungumzia tabia,muktadha uwe ni tabia.Muktadha ni mchezo kwa hivyo mtu mchafu ni kwamba yeye ni hodari sana katika ule mchezo* Mawazo ya msailiwa yanaoana na Sinclair (2014) anayefafanua kwamba maneno kiasilia ni vyombo vya muktadha visivyotegemea kutengwa na muktadha wa matumizi yao. Aidha kwa mujibu wa Turner (2011), anavyochukulia mtu kuwa neno fulani linamaanisha kitu fulani huweza kuwa tofauti na anavyochukulia mtu kuwa maana ya neno lilo hilo moja. Kulingana naye, neno linaweza kuwa maana zaidi ya moja ila kwa mujibu wa watumiaji wake. Hivyo maana husimbwa jinsi ambavyo maneno yametumiwa katika muktadha fulani.

**Msailiwa wa pili**

> Msingi wa kuelewa kazi yoyote iwe nyimbo au shairi ni muktadha basi kuelewa mazingira hayo ambayo mtunzi amezingatia itakuwa ni vigumu sana. Kuna baadhi ya nyimbo ambazo zimeimbwa na ikawa vigumu kwa watu wasikilizaji kupata maana kwa sababu ukikosa kupata muktadha wa wimbo basi itakuwa vigumu wewe kuelewa yanayozungumziwa. Ama unaweza kupata maneno ukakosa kupata kusudio la mtunzi katika utunzi wa wimbo wake.

Msailiwa huyu anachukulia pia kuwa maana inategemea muktadha wa matumizi. Kwa mujibu wake maana ni kipengele muhimu katika mawasiliano katika sanaa, inapozingatiwa tungo zinazoimbwa na kukaririwa. Aidha ameangazia mchango wa muktadha katika uvurugaji wa mawasiliano. Kulingana naye, maana inajikita katika muktadha wa matumizi na ujumbe unavyomfikia mpokezi wa ujumbe hasa katika nyimbo inategemea uelewa alio nao wa muktadha wa matumizi ya maneno. Msailiwa huyu anathibitisha maoni ya Hartman (1983) anayesema kwamba lugha iko katika muktadha fulani hivyo maana hueleweka kwa misingi ya muktadha husika. Hivyo, kwa kuzingatia Wittgenstein (1963) anayesema maana ya neno ni jambo la kinachofanywa na lugha, maana ya neno ni matumizi yake katika lugha.

Chukulio kwamba kujua maana ya neno kunahusisha kinachorejelewa na neno hilo, ikiwa neno lenyewe ni la kutumika mtaani, aina ya neno lenyewe na ikiwa neno hilo linawasilisha dhana nyingine limepata ustawi.

**Msailiwa wa tatu**

> Muktadha huwa na nafasi. Muktadha ulipo hapa ni wa mazungumzo ya vijana ambao wazee hawapati. Mawasiliano hapa yamefanikishwa miongoni mwa vijana na kuwatenga wazee. Katika nyimbo hizi walengwa ambao ni vijana wanapata ujumbe kwani nyimbo inajikita katika miktadha yao.

Mawazo haya yanaendelea kukuza nafasi ya muktadha katika kuzua maana ya maneno na hivyo kupitisha ujumbe katika jamii. Ikizingatiwa kwamba wanajamii huwa katika viwango tofauti tofauti, kuna uwezekano wa wanajamii kutopata maana moja iliyokusudiwa na mwasilishaji wa ujumbe hasa katika nyimbo. Hii ni kwa misingi kwamba makundi mbalimbali katika jamii hutumia lugha moja kuwasilisha yanayowahusu yanayoweza kutofautiana na kundi jingine katika jamii hiyo moja. Msailiwa huyu anathibitisha kauli ya Wittgenstein (1963) kwamba maana haitegemei tu kinachosemwa bali pia muktadha. Aidha anakubaliana na Khachula (2013) anayesema kwamba wazungumzaji hutumia maneno katika lugha kwa njia tofauti ili kufaa katika muktadha wa matumizi ya maneno hayo. Hivyo, dhima ya muktadha katika suala la maana haiwezi kamwe kuepukika. Mchakato wa kufanyiza maana unategemea pakubwa kipengele cha muktadha.

**Msailiwa wa nne**

> Muktadha ni muhimu sana kwa sababu kikawaida maneno haya yanapotumiwa katika mazungumzo ya kawaida hamna fasiri nyingine ya ziada. Lakini hapa katika sajili ya muziki hasa unapozingatia hawa ni vijana wenzao. Utapata kwamba muktadha wa kufasiri maneno haya ni muhimu sana kwa sababu kikawaida hayawezi kutumika tu hivyohivyo. itabidi ujiweke katika muktadha wa kiburudani, muktadha wa kimawasiliano kwa hali ya kufundisha na pia kutumia mambo yanyofanyika katika jamii kupitia nyimbo hizo kwa hivyo muktadha huo ni muhimu sana katika fasiri hizo.

Msailiwa hapa anatoa mtazamo kwamba kuna fasiri kadiri inayojulikana ya maneno katika jamii. Japo, matumizi katika mazingira mbalimbali yanachangia kuwepo kwa maana nyingine tofauti na zile za kawaida katika jamii. Maoni yake yanaoana na Khachula (2013) anayesema kwamba wazungumzaji hutumia maneno katika lugha kwa njia tofauti ili kufaa katika muktadha wa matumizi ya maneno hayo. Kwa mujibu wa msailiwa huyu muktadha inabidi izingatiwe maana inapofasiriwa ilivyowasilishwa katika matumizi ya maneno. Aidha, kulingana na msailiwa huyu maana ya kawaida ni ile iliyozuliwa kutoka kwa matumizi ya neno ambayo yamekubalika miongoni mwa wanajamii hao. Hivyo, anathibitisha kauli ya Turner (2011) kwamba maana yoyote ile inapatikana katika nguvu ya ukweli kwamba inazingatiwa kwa namna fulani na wazungumzaji katika jamii fulani.

**Msailiwa wa tano**

> Muktadha ni jambo muhimu katika kutoa maana ya maneno na unapoangalia ile taaluma ya semantiki. Maana inaweza kuangaliwa kwa jinsi tofauti tofauti. Kuna ile maana ya kileksia na kimuktadha. Wale wanaotumia hiyo lugha na pia neno husika wataangalia huu muktadha; nikitumia neno hili basi maana itakuwa hii. Maana hii itakuwa tofauti pia wakielekea katika muktadha mwingine tofauti. Kimsingi hao vijana wanaoimba nyimbo hizi za kizazi kipya unajua kulingana na umri wao bado

> wana mazoea ya kuzungumzia masuala ya kimapenzi n.k kwa hivyo unaweza kuchukua ule muktadha wa hali, naweza kusema ni hali yao ya maisha katika kiwango kulingana na umri wao.

Maoni ya msailiwa kwamba *muktadha ni jambo muhimu katika kutoa maana ya maneno* yanasisitiza nafasi inayotwaliwa na muktadha katika mchakato wa kufanyiza maana. Mtazamo huu unaangaziwa pia na Ajayi-Osuolale (2017) anayesisitiza kwamba muktadha ni uti wa mgongo wa maana ya neno na pasipo kuzingatia muktadha ambamo neno fulani limetumika ni vigumu kuendelea kutafuta maana. Hivyo, inathibitika hapa kwamba bila ujuzi wa muktadha ufasiri wa maana hautakuwa faafu. Msailiwa anadokeza kwamba maana za maneno zinapatikana katika muktadha na pia hutofautiana kulingana na matumizi tofauti katika miktadha mbalimbali. Kwa mujibu wa msailiwa huyu, suala la maana linategemea matumizi na muktadha. Aidha lugha inaangaliwa kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ya maneno yake. Hivyo basi, wingi wa maana unaibuka kutokana na matumizi tofauti ya maneno katika miktadha mbalimbali. Chukulio hili linajengwa na Turner (2011) anayesema kuwa maana ya neno ni jinsi neno hilo lilivyotumiwa na wazungumzaji wa jamii husika.

> **Msailiwa wa sita**
>
> Muktadha ni kila kitu hususan katika mchakato wa kufanyiza maana hasa pale ambapo maana halisi ya neno hilo hulijui; tunategemea muktadha ili kufahamu maana. Hata hivyo muktadha pia huweza kupanua maana ya neno kutegemea maeneo kimuktadha unayolenga. Muktadha unaweza kuwa kitu kipana na ndio maana wakati mwingine kunazuka maana tofauti za neno moja.

Kipengele cha muktadha kulingana na msailiwa huyu kimezidi kukuzwa juu ya vyote vinavyozingatiwa katika kufanyiza maana anaposema *Muktadha ni kila kitu*. Msailiwa anakubaliana na Firth (1935) aliyesema kwamba maana kamilifu ya neno huwa ya kimuktadha na hamna utafiti wa maana pasipokuwa na muktadha ulio kamilifu unaoweza kutiliwa maanani. Msailiwa anathibitisha kwamba katika uchunguzi wowote wa lugha, muktadha hutangulia kuelekeza kuzuliwa kwa maana kwani muktadha huiathiri maana ya neno. Muktadha anavyochukulia msailiwa huyu unatumiwa kukisia maana ya neno fulani. Kwa mujibu wa msailiwa, muktadha unaweza kuwa tofauti kutegemea maeneo mbalimbali ambamo jamii inayotumia lugha hiyo inapatikana. Muktadha unaishia kurejelea vipengele vingi vinavyozua pia maana tofauti. Aidha anaangazia muktadha unavyosababisha upanuzi wa maana anaposema *muktadha pia huweza kupanua maana ya neno kutegemea maeneo kimuktadha unayolenga*. Kulingana naye maneno yanavyotumiwa katika miktadha mbalimbali yanazua maana zaidi na kuonyesha upanuzi wa kile kinachochukuliwa kuwa maana.

Maoni ya wasailiwa hawa kuhusu nafasi ya muktadha katika kufanyiza maana yanadhihirisha kuwa maana yoyote inapoibuliwa katika jamii ambamo neno linatumiwa inategemea mazingira ya matumizi. Msailiwa wa kwanza anasema *neno hupewa maana na muktadha* na kukubaliana kikauli na msailiwa wa sita aliyesema *muktadha ni kila kitu.* Maana husimbwa jinsi ambavyo maneno yametumiwa katika muktadha fulani. Sinclair (2014) anafafanua kwamba maneno kiasilia ni vyombo vya muktadha. Hivyo wanavyosema msailiwa wa pili kwamba *msingi wa kuelewa kazi yoyote ile ni nyimbo au shairi ni muktadha* na wa tano, *muktadha ni jambo muhimu katika kutoa maana ya maneno* ni dhihirisho kwamba muktadha ni kiungo muhimu katika mchakato wa kufanyiza maana.

Wasailiwa hawa walisisitiza umuhimu wa muktadha, maana inapofanyizwa. Maoni yao ni kwamba muktadha huelekeza ujenzi wa maana hivyo kuja kwanza. Machukulio ya wasailiwa haya yanaoana na maoni ya Odedunmi (2006) akinukuliwa na Ajayi- Osulale (2017) kwamba muktadha ni uti wa mgongo wa maana ya neno na ni vigumu kuendelea kutafuta maana bila kuzingatia muktadha wa matumizi ya neno fulani. Umuhimu wa muktadha uliegemewa katika mhimili wa nadharia ya maana kimatumizi kwamba maana ya neno inatokana na muktadha wa matumizi ya neno lenyewe.

Kulingana na Wittgenstein (1963), maana ya neno ni matumizi yake katika lugha. Kulingana naye maana inategemea muktadha. Kwa hiyo, maana hutolewa na mazingira ambamo neno hilo limetumika. Mhimili wa nadharia kwamba maana ya neno ni matumizi yake inaungwa mkono na Suguitan (2005) anayeshikilia kuwa kamusi haiamui maana ya neno bali wanaotumia neno lenyewe. Anasema kuwa maneno ambayo ni sehemu ya lugha tawala yaweza kutumika kiistiari na kupelekea kupatikana kwa maana kuu au mantiki iliyo tofauti na asili yao. Mwihaki (2004) anachangia mawazo haya kwa kusema kwamba maana kimatumizi inarejelea maana ya mwasilishaji hususan kusudio la mwasilishaji au athari tarajiwa. Kulingana naye mtazamo huu wa maana unahalalishwa katika misingi ya lugha kuwa azimifu. Hivyo, tunapozungumza tunakusudia kupata matokeo mahsusi. Matumizi ya lugha kwa misingi hii, inarejelea uteuzi wa maneno katika mazingira faafu ya kimawasiliano na muktadha.

Katika uelewa huu, maana za maneno teule ya Kiswahili katika nyimbo teule zilitolewa zilivyotumiwa katika mazingira ya nyimbo teule. Katika majadialiano kimakundi washiriki walibainisha maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za Juacali na Nonini ambayo kulingana nao yalikuwa na maana tofauti na zile za kawaida zinazotumika kila siku. Kisha, maana za maneno ya Kiswahili yalivyotumika katika nyimbo teule zilibainishwa. Kwa kigezo cha maana katika muktadha wa nyimbo teule, maneno haya yaliwekwa katika miktadha mbalimbali na kuchanganuliwa kimaana ifuatavyo:

### 4.1.1 Muktadha wa Starehe na sherehe

#### 4.1.1.1 Neno Katika

Neno *katika* lilipatikana katika nyimbo kadhaa:

**Wimbo We kamu (Nonini na Juacali)**

kuna food poa hapa napika na usivae jeans imekushika,
juu ya meza leo lazima **utakatika**,
bila kiti utafanya cheza kwa speaker! na leo usikuje peke yako
kuja na beshte zako.

**Wimbo wa Kiasi (Nonini)**

Na zote ziko poa ka mchele imeekewa mnazi ama imegusiwa kiasii
Ka hii ngoma inakubambababasi si u**katike**
na ka inakushika si uongeze sauti tenje kiasii

**Wimbo Manzi wa Nairobi (Nonini)**
Machali leo hamtalala, machali leo hamtalala,
Ka we ni manzi wa nairobi amka uanze **kukatika**

Washiriki walitoa maoni yao kuhusu neno hili kama ifuatavyo:

**Mshiriki B (kundi la tano)**: *Kukatika* ni kucheza. Maana halisi japo ni kutenga kwa kisu au pia kihusishi kwenye sentensi. Wimboni humu ni kunengua tu.

**Mshiriki B (kundi la tatu)**: *kukatika* si ni kucheza tu yaani kufurahia wimbo.

**Mshiriki C (kundi la tatu)**: kweli ku*katika* ni kudensi yaani kusonga kwa sehemu fulani za mwili mtu anaposikiliza wimbo.

**Mshiriki C (kundi la nne)**: neno *katika* humaanisha kucheza au kuvunjika kwa kitu kulingana nami lakini wimboni humu ina maana tofauti na kucheza wenzangu, kwangu neno hili linamaanisha kuumizwa ama kusikia raha ya kilele wakati wa ngono.

**Mshiriki D (kundi la nne)**: mimi naona inamaanisha kutosheka na ngono.

Washiriki walitoa maana ya neno *katika* kama kucheza au kunengua. Mshiriki B (kundi la tano) anaposema *maana halisi japo ni kutenga kwa kisu au pia kihusishi kwenye sentensi* anaonyesha uwepo wa maana inayochukuliwa kuwa halisi yaani ya kikamusi. Hivyo, anagundua kwamba maana ya neno hili katika muktadha wa wimbo teule ni tofauti na ile maana ya kawaida.Mshiriki B (kundi la tatu) anawasilisha dhana nyingine ya *kufurahia wimbo*. Kulingana naye maana hii ni zaidi ya kitendo cha kunengua viungo vya mwili tu. Dhana hii inaonyesha hali ya upanuzi wa maana kwa neno *Katika*.Mshiriki C (kundi la nne) amewasilisha maana za; *kuvunjika kwa kitu*, *kuumizwa* na *raha ya kilele wakati wa ngono*.Kwa mujibu wa fasiri hizi, hali ya upanuzi wa maana inadhihirika kwani neno hili moja limezua maana nyingi katika muktadha wa nyimbo teule. Mshiriki D katika kundi la nne anaposema neno *katika* linamaanisha *kutosheka na ngono* anazidi kuzua fasiri tofauti ya neno hili. Washiriki C na D katika kundi la nne walizua maana katika mtazamo wa mahusiano ya kingono. Maana hizi za neno katika zinadhihirisha tofauti za kimtazamo zinavyochangia maana japo kwa kuzingatia matumizi ya neno hili katika nyimbo teule.

Kuzua maana ya neno hilo kwa mujibu wa matumizi katika muktadha wa nyimbo teule kunadhihirisha pia uwezekano wa kuwepo kwa maana nyingi tu kutokana na matumizi.

Neno *katika* lilivyotumika katika nyimbo teule za Juacali na Nonini ni bayana kuwa lina maana zaidi ya zile zilizo katika kamusi za Kiswahili. Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014), neno *Katika* ni kihusishi kinacholeta dhana ya kitu ndani ya kitu au mahali, kipindi fulani cha wakati, kutengeka kwa kitu fulani na kusababisha kuwepo na vipande au sehemu ya kitu hicho. Turner (2011) anasisitiza kwamba maana ya neno ni matumizi yake. Kwa hivyo maana zaidi za neno *katika* zilizotolewa na washiriki katika majadialiano yao zinaweza kuchukuliwa kuwa maana za maneno haya ikizingatiwa kwamba kuna dhana inayosudiwa na matumizi ya neno hilo katika nyimbo hizo imfikie mpokezi wa nyimbo teule ambamo neno *katika* limetumika. Mwihaki (2004) anasema kwamba maana kimatumizi inarejelea maana ya mwasilishaji hususan kusudio la mwasilishaji au athari tarajiwa. Kwa misingi hii neno *katika* limepata ongezeko la maana zinazosawiriwa na neno lenyewe hususan katika muktadha wa nyimbo teule za kizazi kipya. Maana hizi kutokana na kujulikana na kuzingatiwa kimatumizi zinadhihirisha mabadiliko kwa kiasi fulani katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu neno hili la Kiswahili lina maana yake asilia.

#### 4.1.1.2 Neno Ngoma

Neno *ngoma* lilipatikana pia katika baadhi ya nyimbo;

**Wimbo Kiasi (Nonini)**

> Na zote ziko poa ka mchele imeekewa mnazi ama imegusiwa kiasii. Ka hii **ngoma** inakubambabasi si ukatike na ka inakushika si uongeze sauti tenje kiasii. Walikua wanafikiria nimeacha **ngoma** sababu nimepotea **ngoma** ni mingi **ngoma** si...kiasii

**Wimbo Manzi wa Nairobi (Nonini)**

> Si-ta-choka na kuwapatia manzi wa Nairobi sifa, hii **ngoma** inaeza enda one-hour kabla haijaisha. Kuna manzi mpoa ni ugonjwa huaga ameshikishwa'

**Wimbo We kamu (Nonini na Juacali)**

> Nimekuwa kwa keja tu nikipika nikikushughulika. **Ngoma** yako wee kamu si unaiskia vile iko poa, jako yako na trao kila kitu toa, kuna siri yoyote unaezalike kuniambia toboa.

Kutokana na nyimbo hizi, neno *ngoma* linaelezwa na washiriki kama ifuatavyo:

**Mshiriki C (kundi la 5)**: ngoma ni muziki tu ama kando na ile ala; maana ya kawaida.

**Mshiriki A (kundi la 5)**: kwangu mimi ngoma ni wimbo.

**Mshiriki E (kundi la 3)**: *ngoma* hapa ni wimbo tu

**Mshiriki A (kundi la 4)**: katika muktadha huu *ngoma* haimaanishi muziki hata.

**Mshiriki B (kundi la 4)**: ngoma inamaanisha kitu spesheli.

Washiriki C na A (kundi la 5),A (kundi la 4) na E (kundi la 3), walizua maana ya wimbo huku mshiriki B (kundi la 4) akirejelea kitu spesheli. Mshiriki huyu alichukulia neno *ngoma* kuwa na maana fiche kwani hajataja kitu hicho spesheli ni nini haswa ila inaweza

kuchukuliwa kuwa kitu hicho spesheli kinajulikana miongoni mwa wanaolitumia neno hilo. Neno *ngoma* kama tu neno *katika* kutokana na matumizi yake katika nyimbo teule, maana nyingine zinazoibuka ni zaidi ya maana ya kawaida. Maana ya kawaida kulingana na Paul (1920) akinukuliwa na Geerearts (2009) ni ile ya kamusi. Hivyo, maana hizi katika muktadha wa starehe na sherehe katika nyimbo teule zinachukuliwa kuwa faafu kwa mujibu wa mazingira ya matumizi yao. Kulingana na Kamusi ya Kiswahili sanifu toleo la tatu,TUKI(2014), neno *ngoma* linarejelea ala ya muziki au mchezo wa kufuata mdundo wa kimuziki. Katika nyimbo hizi neno hili pia linamaanisha wimbo na kando na kitu kinachochukuliwa cha thamani cha kupeanwa kwa mgeni aliyemtembelea mwenyeji wake.

#### 4.1.1.3 Neno Poa

Neno hili limetumika katika nyimbo teule.

> **Wimbo Manzi wa nairobi (Nonini)**
>
> Nyuma ukimcheki maze amebeba zote, Nikisimama na yeye, tunatoshana, Tuki**poa** down ni mrefu tena sana, Nashindwa nikimpata hizo mizigo nitaezana
>
> **Wimbo We kamu (Nonini na Juacali)**
>
> Ngoma yako wee kamu si unaiskia vile iko **poa** .... ushaiguzwa mahali ukaskia ku-kohoa leo mi na we au sio **poa poa...**...kuna food **poa** nhapa napika na usivae jeans imekushika, ju ya meza leo lazima utakatika
>
> **Wimbo Mabeshte damu (Juacali)**
>
> Noma hapa ah-ah msinivute hivo naamka, naamka naenda, naenda pekee yangu
> niacheni niende tu sawa, sawa, sawa OK **poa** ‘

Washiriki walitoa maelezo ya neno *poa* ifuatavyo:

**Mshiriki A (kundi la nne)**: kitu *poa* ni kitu kizuri, iko sawa au inapendeza

**Mshiriki B (kundi la tatu)**: *Poa* nayo inamaanisha kitu kizuri japo tusisahau kwamba neno hili linaweza pia kumaanisha kutulia tu kando na maana ya kawaida ya kitu kilichofanyika kuwa baridi.

**Mshiriki A (kundi la tatu)**: ndio, poa ni nzuri tu.

Kwa mujibu wa washiriki neno *poa* lilimaanisha uzuri, hali ya kupendeza kwa kitu na anavyosema mshiriki B (kundi la tatu), *kutulia tu.* Mshiriki huyu vilevile alitoa maana inayopatikana kwenye kamusi aliposema *kuwa baridi* na kudhihirisha maana kimatumizi na ile ya kikamusi. Aidha anadhihirisha uelewa wake wa uwezekano wa kuzua maana kwa kuzingatia muktadha wa matumizi. Maana za neno *poa* zilizoibuka katika nyimbo hizi teule ni zile maana zinazoweza kutolewa kwa neno wakati mwingine kwa kurejelea jinsi neno hilo lilivyotumiwa katika nyimbo hizi mbalimbali na hivyo kuoana na ule mtazamo wa Paul (1920) katika Geeraerts (2010). Wazo hili linaendelezwa na Butchavarov (1960) anayesema kwamba maana ya neno hutokana na matumizi yake. Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014), neno *poa* lina maana ya kupungua joto au uchungu na kukaa kimya bila wasiwasi. Katika nyimbo hizi neno *poa* linaleta dhana ya sifa ya uzuri na pia kuketi mahali kwa jumla bila kudhihirisha umahususi wowote. Neno *poa* katika misingi hii linaonekana kupata maana zaidi kando na zile zilizoorodheshwa kwenye kamusi na hivyo kudhihirisha upanuzi wa kimaana.

Kulingana na muktadha ulioibuliwa katika nyimbo teule za starehe na sherehe kwa mujibu wa matumizi ya maneno haya ni bayana kwamba maneno *poa, katika* na *ngoma* yanawasilisha dhana tofauti na ile ya kimsingi iliyo kwenye kamusi. Muktadha huelekeza unatekeleza dhima kuu katika ujenzi wa maana. Hili linathibitishwa na Wittgenstein (1963) anaposema maana ya neno inatokana na muktadha wa matumizi ya neno lenyewe. Nafasi ya muktadha katika mchakato wa kufanyiza maana imesisitizwa na watafitiwa wakuu katika utafiti huu. Kwa mfano; msailiwa wa kwanza alisema, *"maana ni muktadha ushaona? Neno hupewa maana na muktadha. La sivyo wajua maneno haya hayanamaana.*" Kutokana na maoni haya ni bayana kwamba mchakato wa kufanyiza maana unategemea muktadha. Hivyo maneno yalivyotumika katika nyimbo yana uwezo wa kuibua maana zaidi kulingana na muktadha wa matumizi yao katika nyimbo hizi teule.

### 4.1.2 Muktadha wa Pesa na shughuli ya kutafuta pesa

#### 4.1.2.1 Neno Rarukia

**Wimbo wa Kiasi (Nonini)**

Maisha yangu tamu siku inani**rarukia** mbaya lakini nimeamua kuitulizakiasii
Kabla pombe iniue itabidi nimeiwacha kabisa ama nianze kuikunywa kiasii 'kiasi'

Kutokana na maoni ya washiriki, maana ya 'rarukia' ni:

**Mshiriki A**: Neno *kurarukia* kwa kweli maana yake si sawa na ile ya kawaida tunayojua. Naona dhana ya kinaya hapa. kwamba mambo yamepita kiasi.

**Mshiriki B**: *kuraruka* yenye tunajua ni kutawanyisha kwa hivyo msanii ni kama anasema maisha yake ni matamu lakini siku haienendi vizuri, anamaanisha kuwa anaona siku imemwanzia vibaya lakini maisha yake ya kila siku huwa sawa.kwa hivyo kurarukia hapa
kwamaanisha tu siku haimwendei vizuri wala hahisi salama na jinsi siku ilivyomwanzia.

Mshiriki A anaposema *maana yake si sawa na ile ya kawaida tunayojua* anabainisha kuwa anafahamu kuwa neno *rarukia* lina maana asilia yaani ya kikamusi. Kwa mujibu wa mshiriki huyu neno hili lina maana ya *mambo yamepita kiasi* kulingana na jinsi lilivyotumiwa katika wimbo teule wa Kiasi. Mshiriki A anaonyesha uelewa wa maana inavyozuliwa katika matumizi hususan katika muktadha wa wimbo teule na uwepo wa wingi maana. Mshiriki B anathibitisha maoni ya A anaposema *kuraruka yenye tunajua ni kutawanyisha,* neno rarukia lina maana iliyoorodheshwa katika kamusi. Hivyo maana zinazotokana na matumizi katika wimbo teule ni mpya kwani maana yake mshiriki B ya kinyume cha matarajio ya uzuri yanathibitisha anavyosema mshiriki A kwamba *Naona dhana ya kinaya hapa.* Maana hiyo mpya ya neno *rarukia* ni tofauti na ile iliyoorodheshwa katika kamusi na hivyo kujulikana kiasi cha kuchukuliwa kuwa ya kawaida.

Neno *rarukia* kutokana na maelezo wa washiriki kwa mujibu wa matumizi yake katika wimbo lina maana ya mambo au pengine shughuli kupita kiwango cha kawaida, mambo kuharibika au kuenda kinyume na matarajio. Ni bayana kuwa washiriki walikuwa na uelewa kwamba neno hili lina maana yake inayochukuliwa kuwa ya kawaida na ya kimsingi.Kwa kuzingatia vigezo vya Lujan (2010), kwamba maana ya kimsingi ya neno ni ile iliyoorodheshwa katika kamusi na yaweza kurejelewa moja kwa moja kabla ya kuzingatia mengine. Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu, TUKI (2014), neno rarukia limenyambuliwa kutoka kwa kitenzi raruka chenye maana ya kuchanika kwa kitu na kuwa vipande vipande. Kwa hivyo, katika mtazamo wa Turner (2011) kwamba maana ya maneno hupatikana katika matumizi yake na maana ya neno inatokana na muktadha wa matumizi ya neno lenyewe, maana ya neno *rarukia* imechukuliwa na matumizi yake katika nyimbo teule. Neno hili vilevile linaonekana limepanuka kimaana.

#### 4.1.2.2 Neno pigwa

**Wimbo wa Mabeshte damu (Juacali)**

> ...jioni saa kumi najianika kwa jua baadaye cell tunaosha na maji ya mvua, kazi hapa nime**pigwa** sumuni mbili...

Neno ‘pigwa’ kwa mujibu wa washiriki;

> **Mshiriki A (kundi la kwanza)**: kupigwa kunakozungumziwa hapa ni kama kulipwa ama kupewa ama niaje.
>
> **Mshiriki B (kundi la kwanza)**: Ndio, hata mimi naona hivyo. Ukisema mtu ame*pigwa* kitu ni kama kumaanisha amepewa yaani.

Neno *pigwa* katika wimbo wa Mabeshte damu limezuliwa maana za *kulipwa* na *kupewa* na mshiriki A(kundi la kwanza) huku mshiriki B katika kundi lilohilo alitoa dhana ya kupewa na hivyo kukubaliana na mwenzake. Kwa mujibu wa washiriki hawa neno pigwa lina maana na kupewa na kupokea malipo fulani. Maana hizi ni mpya na zinatokana na matumizi katika wimbo teule hazijulikani kumaanisha vile katika mazungumzo ya kawaida.

Falk (1973) anasema kuwa maana za maneno yanapotumiwa popote pale huangazia kusudi la mwasilishaji na mpokezi wa ujumbe. Hivyo maana hutokana na matarajio ya wale wanaoshiriki katika mawasiliano. Maoni haya yalizipa msingi maana za maneno zinazoibuka katika nyimbo teule. Neno *pigwa* linatokana na neno piga ambalo kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu,TUKI (2014) kimsingi ni kitendo cha kukutanisha vitu kwa nguvu. Katika nyimbo teule neno pigwa linawasilisha dhana zaidi za pokea kitu kama malipo hivi. Kwa mujibu wa nadharia ya maana kimatumizi maneno hupata maana kutoka kwa matumizi. Hivyo, neno *pigwa* limepata maana kutokana na matumizi yake katika wimbo teule uliibua maana zaidi ya ile ya kikamusi.

Mazingira ya pesa na shughuli za kutafuta pesa yanaibuliwa katika nyimbo teule za ‘Mabeshte damu’ na ‘Kiasi’ kwa maneno haya mawili; rarukia na pigwa. Maana za maneno haya za kimsingi au halisi kwa mujibu wa Lujan (2010) ni tofauti na zile zilizoukiliwa na matumizi ya maneno haya katika nyimbo teule. Maana hizi zaidi zinaweza kuchukuliwa kuwa faafu kutokana na muktadha wa matumizi yao katika nyimbo hizo teule.

Ukubalifu kulingana na Paul (1920) akinukuliwa na Geerearts (2009) kwamba, kuna maana nyingine iliyo kwa washiriki katika mawasiliano na hutengewa maneno ikitarajiwa kwamba itatambuliwa, unathibitishwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu maneno haya; *pigwa* na *rarukia* yamepata maana zaidi katika muktadha wa nyimbo teule zinazoweza kuthibitishwa na matumizi ya maneno yenyewe. Maana hizi zaidi zinaonyesha upanuzi wa maana unaothibitishwa na Turner (2011) anaposhadidia kuwa neno halimaanishi kitu kimoja katika kila matumizi yake. Mtazamo huu unahimili muktadha katika kuzua maana mbalimbali kama anavyosema msailiwa wa nne, *“Muktadha ni muhimu sana kwa sababu kikawaida maneno haya yanapotumiwa katika mazungumzo ya kawaida hamna fasiri nyingine ya ziada.”* Hivi ni kumaanisha kwamba maana zaidi zinapozuka, hali huwa ni kutokana na muktadha wa matumizi ya maneno ambayo kwa kawaida yanawasilisha dhana nyingine. Uwepo wa maana zaidi kunadhihirika tu katika uelewa kuwa maneno haya yana maana zinazochukuliwa kuwa asilia yaani zilizoorodheshwa kwenye kamusi na kukubalika kimatumizi miongoni mwa wanajamii ambamo maneno hayo yanatumika.

### 4.1.3 Muktadha wa Mapenzi na ngono

Ochichi (2013) anasema kuwa maneno katika lugha hupata maana mpya yanapotumika katika mazungumzo kutokana na ukweli kwamba lugha sio kitu kinachosimama. Vilevile maneno yanayosawiri mapenzi na ngono yana maana inayochukuliwa kuwa ya kawaida kwa mujibu wa Paul (1920) akinukuliwa na Geerearts (2009). Hata hivyo maneno haya yanaonekana kuzua maana nyingine yalivyotumika katika nyimbo teule.Katika muktadha huu neno 'nyundo' lilishughulikiwa.

#### 4.1.3.1 Neno Nyundo

Neno hili lilipatikana limetumika katika nyimbo teule:

> **Wimbo wa Nyundo (Juacali)**
>
> Nashindwa jo nizame wapi, **nyundo** yangu sasa itauwa wapi
> Usiwache endelea cheza nalo, mpaka iseme jina zote unazo....
>
> **Wimbo wa We kamu (Nonini na Juacali)**
>
> *****pia nimenunua (sabu yako tu) mpaka tenje nikaomba (we we we we kamu)
> Tape za **nyundo** ninazo (sabu yako tu), sa fanya hivi (we we we we kamu) remix '

Washiriki katika makundi ya majadiliano walieleza kuhusu neno 'nyundo' ifuatavyo:

> **Mshiriki A (kundi la nne)**: *nyundo* katika wimbo huu ni ngono.
>
> **Mshiriki F (kundi la nne)**: kwa kweli nilivyosoma maneno ya wimbo huu, nakubaliana na mwenzangu hapa kwamba nyundo ni ngono.
>
> **Mshiriki A (kundi la nne)**: mimi ninachukulia neno hili kumaanisha mchakato mzima wa ngono.
>
> **Mshiriki A (kundi la pili)**: wimbo huu ni wa mapenzi kwa hivyo muktadha wote ni wa mapenzi. neno *nyundo* hapa linamaanisha sehemu ya mwili hasa wa mwanaume katika hali ya ngono.

> **Mshiriki B (kundi la pili)**: msanii ametumia maneno kuleta maana zinazoelekezwa kwa lile tendo la mapenzi. Kwa hiyo nyundo hapa lina maana ya sehemu nyeti ya mwanaume ikiwa tayari katika kushiriki ngono.

Neno *nyundo* limetumiwa katika nyimbo mbili teule na kuonekana kuzua maana zaidi. Washiriki A na F katika kundi la nne wanakubaliana kwamba neno hili lina maana ya *ngono* ila mshiriki A anaeleza zaidi chukulio lake lilivyo kwamba *neno hili kumaanisha mchakato mzima wa ngono.* Hali hii inaonyeshauwiano wa kimtazamo unaozua maana hii. Katika wimbo wa nyundo neno *nyundo* lina maana zaidi ambapo mshiriki A katika kundi la pili anasema *sehemu ya mwili hasa wa mwanaume katika hali ya ngono* na kuungwa mkono na mshiriki B katika kundi lilo hilo anayesema sehemu nyeti ya mwanaume ikiwa tayari katika kushiriki ngono. Dhana ya ngono imepanuliwa sio kwa kuangazia tu mchakato bali pia kiungo cha mwili kinachohusishwa na mchakato huo.

Katika muktadha wa nyimbo hizi teule *nyundo* ni neno linalowasilisha dhana ya ngono. Kuna machukulio ya neno hili kuwa mchakato mzima wa ngono na jingine kuwa neno hili linarejelea sehemu ya siri ya mwanaume katika shughuli nzima ya ngono. Kwa vyovyote vile kilicho bayana hapa ni kwamba maana hizi zaidi zimeibuliwa katika muktadha wa nyimbo kutokana na matumizi yao. Hivi kwa mujibu wa nadharia ya Witgenstein (1963), maana ya neno nyundo limepatikana katika matumizi yake katika nyimbo teule. Pili, maana ya neno hili limetokana na muktadha wa matumizi ya neno lenyewe. Haidhuru kwamba neno *nyundo* kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) ni kifaa cha kugongomelea katika shughuli kama vile ujenzi na useremala.

Kando na nyundo maneno mengine yanayowasilisha dhana ya viungo vya mwili vinavyohusishwa katika mchakato wa ngono ni pamoja na kiti, kabati, kitanda, msumeno na msumari kama tunavyoona katika nyimbo zifuatazo:

**Wimbo wa Nyundo (Juacali)**

hapa job kuna nyundo moja itadunga wapi na **msumari** ni moja itaingia wapi
tulia nipe **msumeno**, nigware vifiti na ikiezekana nikutengenezee hiyo **kiti**
lakini **kabati** yako ni kubwa sana, ilalishe hivi iipige randa na sandpaper
ni kitu ya maana kusugua **kitanda** ya mtu mmoja staki, wall unit ni nzito kusongesha

**Wimbo wa Manzi wa nairobi (Nonini)**

Nikisimama na yeye, tunatoshana, Tukipoadown ni mrefu, tena sana Nashindwa nikimpata hizo **mizigo** nitaezana, Usiniulize mzigo gani, wajua wacha kujifanyaaa

Kutokana na muktadha wa wimbo huu maana ya maneno za maneno haya yalitolewa maana kwa maelezo katika kundi la washiriki waliokuwa wakijadiliana ifuatavyo:

**Mshiriki B (kundi la pili)**: Halafu *msumari* na *msumeno* ni maneno yanayoashiria sehemu za siri za kike na kiume mtawalia wakati wa ngono.

**Mshiriki F (kundi la pili)**: nakubaliana na mwenzangu kwa sababu hata *kiti* na *kabati* ni maneno yaliyotumiwa kumaanisha sehemu nyeti ya msichana.

**Mshiriki B (kundi la pili)**: naunga mkono yaliyosemwa na mwenzangu japo neno *kabati* kwangu linamaanisha makalio ya msichana nikizingatia wimbo husika.

**Mshiriki A (kundi la tatu)**: ...halafu mizigo hapa ni makalio yaani sehemu ya nyuma ya msichana.

**Mshiriki C (kundi la tatu)**: Kwa hilo neno *mizigo* mimi naona inamaanisha mambo yanayomhusu au mkao wa jumla wa anayezungumzia.

Maneno *msumari, msumeno, kiti* na *kabati* yanarejelea viungo vya mwili vinavyohusishwa moja kwa moja katika mchakato wa ngono kwa mujibu wa washiriki hawa wanapozingatia

matumizi ya maneno haya katika wimbo wa nyundo. Mshiriki A anasema maneno msumari na msumeno yanarejelea *sehemu za siri ya kike na kiume mtawalia.* Kwa mujibu wa mshiriki huyu kuna umahususi wa maana katika mazingira yanayoimbwa katika wimbo ambamo tendo la ngono linatendeka. Mshiriki F (kundi la pili) ana uchukulio sawa na mwenzake anaposema *nakubaliana na mwenzangu* na hivyo kuonyesha jinsi ambavyo maana hizi zaidi zinavyozuliwa kutokana na matumizi ya maneno ya lugha. Mshiriki F vilevile anatoa maana za maneno kiti na kabati kama *sehemu nyeti ya msichana*. Mahusiano ya kimaana yanatukia katika hali ambapo maneno yanachukuliwa kuwasilisha dhana moja. Maneno msumeno, kiti na kabati katika muktadha wa wimbo wa Nyundo kwa mujibu wa washiriki yana maana ya sehemu ya siri ya mwanamke. Neno mizigo vilevile limezuliwa maana zaidi ya ile maana inayojulikana na washiriki. Mshiriki A kundi la tatu anachukulia neno hili kumaanisha *makalio* ilhali mshiriki C (kundi la tatu) anasema *neno mizigo mimi naona inamaanisha mambo yanayomhusu au mkao wa jumla wa anayezungumzia*. Washiriki A na C wanathibitisha jinsi ambavyo mitazamo katika muktadha wa matumizi inachangia katika kufanyiza maana.

Fafanuzi za maana walizotoa washiriki walipokuwa wakijadiliana katika kundi hili la pili, ziliashiria kwamba kama wasemavyo Brown na Yule (1983) maneno huweza kutumiwa kwa maana ya kimsingi au ya kawaida. Kulingana nao maneno yanapotumiwa huzifuma dhana zinazorejelewa na maneno yenyewe. Kwa misingi hii, maneno *kiti, kabati, kitanda, na msumari* yanaibua dhana ya sehemu za siri za kike huku *msumeno* ukirejelea sehemu nyeti ya mwanaume. Mizigo kulingana na washiriki ni makalio au sehemu ya nyuma ya mwanamke. Maneno haya yanaashiria viungo vya mwili vinavyohusishwa katika ngono.

Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014): *kiti* na *kabati* ni vifaa vya kukalia na kuhifadhia vitu mtawalia huku msumeno ukiwa kifaa cha ufundi hasa wa mbao. *Msumari* pia ni kifaa cha kiseremala ilhali *Mizigo* ni kitu kizito au jambo lililo gumu. Kwa mihimili ya nadharia ya maana kimatumizi kwamba; maana ya maneno hupatikana katika matumizi yake na maana za maneno zinatokana na muktadha wa matumizi ya maneno yenyewe, maana za maneno *kiti, kabati, mizigo, kitanda, na msumari* ziliangaliwa kwa kuzingatia muktadha wa wimbo teule na jinsi maneno hayo yalivyotumika.

Njogu na wenzake (2006), wanasema kuwa neno linalotumiwa katika muktadha mmoja huweza kupanuliwa ili litumike katika muktadha mwingine. Kulingana nao, neno hilo linaweza kutoa maana tofauti na ile inayojulikana na kuzoeleka. Wazo hili limethibitishwa na matumizi ya maneno *kiti, kabati, kitanda, na msumari* katika wimbo teule yaliyoibua maana zilizo tofauti na maana zinazojulikana na kuchukuliwa kuwa za kawaida. Katika misingi hii pia ni wazi kwamba kuna uwezekano wa mahusiano ya kimaana kama vile usawe; hali ya kuwepo kwa maneno yenye maana sawa na utawe; hali ya neno kuwa na maana zaidi. Hivyo, kwa mujibu wa matokeo haya maana kimatumizi inaweza kusababisha usawe na utawe.

Matendo katika mchakato wa ngono yaliashiriwa na maneno pamoja na semi hizi: *nizame/zamisha, rusha, dunga, itauwa, kusugua kitanda, piga randa, tulia, atanipigia magoti nimbariki na chinjia*. Muktadha wa ngono ulisawiriwa na maneno pamoja na semi hizi yalivyotumiwa katika nyimbo teule:

**Wimbo wa Nyundo (Juacali)**

Nashindwa jo **nizame** wapi, nyundoyangu sasa **itauwa** wapi
Usiwache endelea **cheza** nalo, mpaka iseme jina zote unazo
.... Sijui jo nianze kusema vipi, wacha tu niseme uko fiti
Kwanza vile umesimama mtoto, unafanya **nashikwa na joto...**
.... hiyo mwili yako ikisonga kidogo, nyundo yangu **inaruka** kidogo
come ubonge nayo, **inazusha** lakini chunga inaeza **rusha**,
hapa job kuna nyundo moja ita**dunga** wapi na msumari ni moja itaingia wapi
...lakini kabatiyako ni kubwa sana, ilalishe hivi **iipige randa** na sandpaper
ni kitu ya maana **kusugua kitanda** ya mtu mmoja staki....

**Wimbo wa We kamu(Nonini na Juacali)**

Juacali ushai**chota mtoto** kwa haga, (jua cali) aa sijaichota mtoto wowote kwa haga lakini nakuambia jo, hiyo ndiyo nimepanga! (hii kiti) achana nazo ikifika **atanipigia magoti nimbariki** na juala staki mtaani kuwe na mazishi! Kwa hivyo we kamu.... Bora leo uniachie tu **nizame** vimbichi, bora leo uniachie nikushike hivi, nikupeleke juu mpaka utapike skumawiki.... juu ya meza leo lazima **utakatika**.... baby boy lazima **ataruka** (we we we we kamu)

**Wimbo wa Kiasi (Nonini)**

...Pia naskia raha unaeza **chinjia** manzi siku hizi ata ka ni mzee wako kiasii
....... Lazima nijue ka ta**zamisha** yote ama taiekelea kiasii ‘kiasi’

Katika majadiliano kimakundi maana za maneno haya yalitolewa ifuatavyo:

**Mshiriki C**: ... ku*cheza* hapa kunamaanisha lile tendo la ngono. *nizame* inamaanisha hajui aanze wapi yaani hajui sehemu ya kuhusisha kwanza katika mchakato mzima wa ngono.

**Mshiriki D**: neno hili katika wimbo huu unaweza pia kumaanisha kwamba hajui mahali ambapo nyundo itaingizwa, sehemu hasa palipo wazi.

**Mshiriki E**: katika wimbo maana ni ya ndani labda ina maana sawa na kufanya kwenyewe; kuingia kwa mwanaume sijui kama ninaeleweka.

**Mshiriki F**: neno hili kwangu linamaanisha kuweka mahali.

**Mshiriki A**: kulingana nami neno ita*uwa* linawasilisha dhana ya kuleta athari kwa nani hasa tukizingatia wimbo huu.

**Mshiriki B**: mimi naona *uwa* pia inaweza kumaanisha kiwango cha juu cha juu cha kitu fulani kufurahisha.

**Mshiriki C**: *kuzusha* nayo ni kuzungumza kwa hasira ama ukali.

**Mshiriki E**: lakini hapa katika wimbo kuzusha inamaanisha kulalamika au kusisimkwa kwa sehemu nyeti tayari kwa tendo la mapenzi.

**Mshiriki D**: tukizungumzia neno *rusha* kwangu inarejelea hali ya kilele cha ngono kwa mwanaume.

**Mshiriki F**: ku*dunga* kando na maana ya kawaida katika wimbo inamaanisha kule kuvaa nguo ukapendeza.

**Mshiriki E**: kudunga kwangu inamaanisha kutiwa mimba

**Mshiriki C**: kulingana na wimbo huu neno hili kwangu naona linamaanisha ile hali ya ngono.

**Mshiriki A**: kulingana nami *kushikwa na joto* ni kule kuwa tayari kwa tendo la ndoa. kuwa na uchu yaani kusisimka.

**Mshiriki C**: kwa misingi kwamba taswira inayochorwa katika wimbo huu ni ya ngono, naona maneno mengi hapa yanarejelea tu hiyo shughuli alivyosema mwenzangu kwa sababu hata *kupiga randa* na *kusugua kitanda* ni semi zinazomaaanisha tu hali ya kufanya ngono.Kwa kweli maneno haya ya kawaida yanaonekana yametumika kitaashira labda kuficha yanayoendelea na pengine kushabikiwa pasipofaa yaani na kikundi cha watu katika jamii ambao haitarajiwi wawe wanajihusisha na mambo haya hasa tunapozingatia maadili ya jamii kwa jumla.

Kundi la nne

**Mshiriki A**: Kuna *kuchota mtoto* hapa ambako kuna maana fiche. Kuchota kunamaanisha kitu tofauti na kitendo cha kawaida tunachojua. Katika wimbo huu nafikiri neno hili linaleta dhana ya kumteka mtu kihisia hasa kimapenzi.

**Mshiriki C**: mimi ninatofautiana na mwenzangu kidogo kwa sababu kuzingatia wimbo neno hili linaweza tu kumaanisha kumsisimua mtu na kumtayarisha kwa ajili ya tendo la ndoa labda kwa kumshika.

**Mshiriki B**: kumchota mtu wenzangu mimi nafikiria ni kumpapasa mtu na anayezungumziwa hapa ni binti mrembo.

**Mshiriki D**: mimi naona tu kumbusu msichana ukimchangamsha kwa ajili ya shughuli ya kufanya mapenzi.

**Mshiriki A**: *Atanipigia magoti nimbariki* wah! Huyu msichana leo atakipatapata.Ni kama leo ni leo katika hali ya ngono.

**Mshiriki B**: yaani inamaanisha atakuwa tayari kwa tendo la ndoa na kwamba ataonyesha ile hamu moja kwa moja.

**Mshiriki C**: usemi huu unarejelea ile hali ya kuonyesha raha na kutosheka kuhusiana na lile tendo la kujamiiana.

**Mshiriki E**: huyu msanii anajaribu tu kusema kwamba yule msichana atahisi vizuri sana na kumradhi waendelee katika tendo la mapenzi.

**Mshiriki A**: *kuzama* nako ni ile tu hali ya ngono. Katika wimbo huu taswira ni ya ngono tu.

**Mshiriki B**: mtu anaweza pia kusema nizame akawa anamaanisha astarehe na afurahie.

**Mshiriki C**: lakini wimboni humu ina maana tofauti na kucheza wenzangu, kwangu neno hili linamaanisha kuumizwa ama kusikia raha wakati wa ngono

**Mshiriki D**: mimi naona inamaanisha kutosheka na ngono.

**Mshiriki E**: *kuruka* katika wimbo huu pia ina maana fiche ambayo ni kule kusisimuka kwa uume kwa ajili ya ngono.

**Mshiriki B**: neno hili; kuruka katika wimbo huu pia unaweza kumaanisha kutungwa mimba.

**Mshiriki D**: kuruka hapa pia inaweza kumaanisha kuwepo kwa mimba yaani kupachikwa mimba katika muktadha wa wimbo huu.

Kundi la tano

**Mshiriki A**: tuna neno hapa *zamisha*, kwa maoni yangu neno hili linarejelea kuwa ndani ndani kabisa ya mahusiano.

**Mshiriki F**: mimi kwa upande wangu ninaona neno hili linamanisha kushiriki ngono kisha neno *chinjia* kwa maoni yangu ni kumtongoza msichana.

**Mshiriki B**: yeah nakubaliana na mwenzangu ila napenda kueleza kwamba si kumtongoza tu bali kufaulu kumfanya akubali kuwa na mahusiano nawe.

Maneno haya teule ya Kiswahili yaliyotumiwa katika nyimbo teule yalikuwa yanadhihirisha kwamba msanii hutumia lugha kwa njia tofauti na ile sanifu inayotumika katika mawasiliano ya kila siku. Sababu yake ya kutumia lugha vile ni kuweza kuzua kisichotarajiwa na kuibua taswira akilini mwa wasikilizaji. Maana za maneno na semi zilizoibuka katika nyimbo hizo teule zinaonekana kukubalika kwa msingi kwamba maana huweza pia kufasiriwa kwa kuhusisha muktadha wa matumizi ya maneno kama asemavyo Geerearts (2009). Maana hizi akimnukuu Paul (1920) Geerearts (2009) anaeleza kuwa hupatikana kwa washiriki na huelekezewa maneno kwa matarajio kwamba yatatambulika kama maana.

Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014) neno ku*chota* ni kuchukua sehemu ya vyowevu kama maji kutoka mahali fulani au kutaka kujua mawazo ya mtu kwa njia ya ujanja. Neno hili hata hivyo lilizua maana tofauti na ile iliyoorodheshwa kwenye kamusi. Katika wimbo wa ‘We kamu’ neno hili kwa mujibu wa Mshiriki A lina maana fiche na anathibitisha wazo lake anaposema *kuchota kunamaanisha kitu tofauti na kitendo cha kawaida tunachojua*. Anaishia kuchukulia kwamba kwa kuzingatia matumizi ya

neno katika wimbo teule neno hilo lina maana ya *kumteka mtu kihisia hasa kimapenzi*. Mshiriki C naye anatoa kauli yake anaposema *kumsisimua mtu na kumtayarisha kwa ajili ya tendo la ndoa labda kwa kumshika.* Mshiriki B anasema dhana inayowasilishwa kwa neno kuchota ni *kumpapasa mtu na anayezungumziwa hapa ni binti mrembo* huku Mshiriki D akisema *kumbusu msichana ukimchangamsha kwa ajili ya shughuli ya kufanya mapenzi*. Kauli hizi zinasawiri uelewa wa muktadha na mitazamo inayozuliwa na hivyo maana zinazohusiana kwa karibu. Dhana ya matayarisho kwa ajili ya kitendo cha kujamiiana yanayoarifiwa kwa vitendo vya kupapasa, kubusu, kusisimua, kuchangamsha na kuteka. Hivyo maana zilizoibuliwa zinakaribiana japo katika uelewa wa mazingira ya matumizi ya neno hili.

Neno 'nizame' kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014) hutokana na kitenzi zama linalomaanisha kuingia ndani ya maji na kwenda chini vilevile kutoweka. Kwa mujibu wa washiriki neno hili lilizuliwa maana toafuti.Mshiriki C alisema *hajui aanze wapi yaani hajui sehemu ya kuhusisha kwanza katika mchakato mzima wa ngono,* wazo lililoungwa mkono na Mshiriki D aliyechukulia neno hilo kumaanisha *hajui mahali ambapo nyundo itaingizwa, sehemu hasa palipo wazi.* Mshiriki E alionyesha jinsi lugha inavyotumiwa kwa namna tofauti na hivyo kuibua maana tofauti katika muktadha huo mmoja aliposema *katika wimbo maana ni ya ndani labda ina maana sawa na kufanya kwenyewe*. Mshiriki huyu katika jaribio la kufafanua zaidi alisema *kuingia kwa mwanaume sijui kama ninaeleweka.* Chukulio la Mshiriki F nalo lilikuwa *kuweka mahali.* Maana inayozuka kutokana na maelezo ya washiriki hawa ni kitendo cha kujamiiana ambapo mojawapo ya viungo vya mwili husika kutiwa mahali ndani pasipodhihirika. Aidha kwa

mujibu wa mshiriki E, neno linaweza kuwasilisha maana inayokusudiwa hadhira fulani na si kila mtu anayepokea ujumbe huo. Maneno yanapoonekana kuwa na maana ya ndani hudhihirishwa wingi maana.

Katika kundi la nne neno kuzama lilizua maana mbalimbali. Mshiriki A alisema *ile tu hali ya ngono.*Katika wimbo huu taswira ni ya ngono tu mshiriki D akasema *kutosheka na ngono*, huku Mshiriki B akisema *astarehe na afurahie*. Mshiriki C alisisitiza kuzingatiwa kwa muktadha wa wimbo teule aliposema *wimboni humu ina maana tofauti na kucheza wenzangu, kwangu neno hili linamaanisha kuumizwa ama kusikia raha wakati wa ngono.* Kwa misingi ya muktadha alivyosistiza Mshiriki C, maana zilizozuliwa zilioana na mazingira ya ngono. Neno kuzama kikamusi ina maana tofauti tena isiyo na mahusiano yoyote na maana zinazoibuka kwa mujibu wa matumizi katika nyimbo teule. Kwa kweli maana kimatumizi inavyodhihirika hapa inaonyesha kwamba kutokana na jinsi neno lilivyotumiwa. Maana yoyote kando na ya kawaida inayojulikana inaweza kutukia.

Neno*chinjia* linatokana na neno chinja ambalo kulingana na kamusi ni kukata shingo hasa kwa wanyama, kumwua mtu kwa ukatili, kupunguza udongo wakati wa ufinyanzi au kupunja katika biashara labda kwa kuuza kwa bei ya juu. Katika muktadha wa wimbo teule neno chinjia lilichukuliwa kuwasilisha dhana tofauti na ile ya kawaida inayofahamika miongoni mwa wazungumzaji watumizi wa neno hili.Mshiriki F alichukulia neno hilo kumaanisha *kumtongoza msichana.* Mshiriki B alikubaliana na mwenzake ila akaongezea kusema *si kumtongoza tu bali kufaulu kumfanya akubali kuwa na mahusiano nawe.* Neno

chinjia kwa mujibu wa maelezo kutokana na matumizi yake katika wimbo teule lina maana ya kujaribu na kufanikiwa katika tendo la kumvutia na kumshawishi mwanadada kukubali kuwa katika mahusiano ya kimapenzi na yule anayelifanya ombi lile. Hivyo, katika uelewa wa mazingira ambamo neno limetumika neno chinjia linamaanisha kutongoza.

Usemi *atanipigia magoti nimbariki* una maana ya kuweka magoti na kutakiwa heri. Katika muktadha wa wimbo teule;Mshiriki A alionyesha mshangao wa ujumbe anaopata kutoka kwa usemi huu aliposema *wah! Huyu msichana leo atakipatapata*. Alionyesha hali ya tahadhari kwamba kungekuwa na tofauti katika tendo la kujamiiana kati ya wahusika aliposema *ni kama leo ni leo katika hali ya ngono.* Mshiriki huyu anachukulia kwamba usemi ule unawasilisha dhana ya hali tofauti na hali ya kawaida ya tendo la kujamiiana. Hivyo, ulinganisho kudhihirika katika usemi huu ulivyotumiwa katika wimbo. Katika mazungumzo ya kawaida maneno haya hayarejelei dhana yoyote fiche.Mshiriki B anasema *inamaanisha atakuwa tayari kwa tendo la ndoa na kwamba ataonyesha ile hamu moja kwa moja* na hivyo kuwasilishwa maana ya utayari wa kushiriki ngono tofauti na mwenzake A. Mshiriki C naye anasema usemi huu *unarejelea ile hali ya kuonyesha raha na kutosheka kuhusiana na lile tendo la kujamiiana huku* Mshiriki E akichangia kwa kusema *huyu msanii anajaribu tu kusema kwamba yule msichana atahisi vizuri sana na kumradhi waendelee katika tendo la mapenzi.* Ufafanuzi wa washiriki wa maana ya usemi 'atanipigia magoti nimbariki' unaoonyesha mazingira yanavyozuliwa katika wimbo teule ni wa tendo la ndoa kwani maelezo yao yanaelekezwa kurejelea hali hii. Mtazamo huu hata hivyo unachanganuliwa kwa fafanuzi tofauti za maana; kuwa tayari, kuonyesha kufurahia na hamu ya kujihusisha katika tendo la kujamiiana na mwenzake.

*Kusugua kitanda* na *kupiga randa* ni shuguli za kawaida za ufundi wa mbao kwa mujibu wa maana kikamusi na katika mazungumzo ya kila siku. Maneno haya hata hivyo yanawasilisha dhana tofauti na inavyofahamika katika hali ya kawaida.Mshiriki C katika fafanuzi yake aliangazia picha inayochorwa akilini mwa msikilizaji wa wimbo na ujumbe unapowasilishwa na maneno hayo. Kulingana naye suala linaloangaziwa katika wimbo ni ngono na hivyo maana za maneno yalivyotumiwa katika wimbo wenyewe zinaweza tu kukisiwa kurejelea ngono. Hivyo anawasilisha maana za kusugua kitanda na kupiga randa kuwa semi zinazomaaanisha tu hali ya kufanya ngono Anaposema *maneno haya ya kawaida yanaonekana yametumika kitaashira labda kuficha yanayoendelea* anasisitiza suala la mpokezi aliyekusudiwa na maana anayokusudia anayewasilisha ujumbe. Aidha, anaangazia dhima ya mawasiliano katika kupitisha maadili katika jamii anapozungumzia *kikundi cha watu katika jamii ambacho haitarajiwi wawe wanajihusisha na mambo haya hasa tunapozingatia maadili ya jamii kwa jumla*. Kwa mujibu wa mshiriki huyu maana inayopokelewa kwa kutumia neno linalochukuliwa kuwa la kawaida huenda imekusudiwa kuwafikia tu wachache katika jamii ambayo wakati huo wamelifanyizia maana tofauti.

Hivyo ni wazi kwamba maneno ya Kiswahili yalivyotumika katika nyimbo teule zilizoimbwa na JuaCali na Nonini yana maana zaidi kulingana miktadha mbalimbali inayozuliwa na nyimbo hizi tofauti. Miktadha tofauti tofauti ni muhimu ili kuzua maana mbalimbali. Ullman (1994) akinukuliwa na Mambo (2009) anasema kwamba maneno yanatumiwa katika miktadha mbalimbali na wazungumzaji tofauti tofauti wanaoweza kuzua maana mbalimbali ambazo wangependa maneno hayo yawasilishe. Kulingana naye, maneno yanaweza kuzuliwa maana kwa njia rahisi kwa sababu ya mnyambuliko, maneno yakapata

maana zaidi pasi kupoteza zile asilia. Maoni haya yanastahiki katika tathmini ya sababu na jinsi maneno yanavyopata maana mpya. Maana zaidi ya maneno zinatokana na alichokusudia anayetumia neno hilo katika muktadha fulani.

Wittgenstein (1963) anasema kwamba matumizi mbalimbali ya maneno hayawezi kusimilishwa kwani tofauti kabisa. Matumizi haya mbalimbali ndiyo yanatoa maana hizi tofautitofauti kwa maneno. Kulingana na Turner (2011), kujua neno ni kujua matumizi yake. Hivyo, maana ya neno inatokana na uwezo wa neno lenyewe kutumika katika mawasiliano. Maana zinaibuka kutoka kwa matumizi yao katika muktadha wa nyimbo teule na kuwasilisha dhana zilizo tofauti na zile za kawaida kuonyesha uamilifu wa maneno kwa mujibu wa Lyons (1968) anayesema kwamba maana na uamilifu wa neno hutokana na matumizi ya neno lenyewe. Hivyo matumizi ya maneno haya teule katika nyimbo za kizazi kipya zinasawiri uamilifu wa maneno katika kuwasilisha dhana inayokusudiwa na mwasilishaji wa ujumbe wowote ule. Aidha mahusiano ya matumizi, muktadha na maana inavyozuliwa yanadhihirika hivi kwamba kuna muoano ambapo bila vipengele vya matumizi na muktadha maana haitaweza kuzuliwa. Msailiwa wa kwanza anaujenga mtazamo huu anaposema *wakisha kujua neno limetumiwa katika miktadha gani kwa misingi gani wanaweza kunyumbua maana.* Hivyo inaweza kuchukuliwa kwamba maana ya neno inatokana na matumizi ya neno hilo katika muktadha fulani.

### 4.1.4 Muktadha wa Mahusiano

Dhana ya mahusiano yalisawiriwa katika nyimbo teule zilizoimbwa na Nonini na Juacali kwa usemi rushia mkono pamoja na maneno; mbuyu, buda, zusha, anakaa, kibao, damu, mbaya, na poa.

#### 4.1.4.1 Neno Mbuyu/ buda

Neno lilisawiri mahusiano ya kibinadamu kama tunavyoona katika nyimbo zifuatazo:

> **Wimbo wa Mabeshte damu (Juacali)**
>
> .... unakumbuka ule mama ulicheki ule **buda** asikuwai kuseti kwa makarao .... salimia madha salimia **mbuyu**, kila mtu, au sio, baadaye, tuonane jo eh ‘

> **Wimbo wa We kamu (Nonini)**
>
> ...Sema unaenda laibo staki noma na **buda**ko, anajua si ni mabeshte leo ni poa

Maneno haya katika muktadha wa wimbo huu teule yaliibua maana zifuatazo:

> **Mshiriki C**: Kwa maoni yangu *buda* ni baba tu.
>
> **Mshiriki E**: Mbuyu nayo ni aina ya mti lakini katika huu wimbo ni ile tu maana ya sheng’ yaani baba au mwanamume mzazi.

Maneno haya mawili; *buda* na *mbuyu* yanawasilisha dhana moja wanavyosema washiriki C na E. Maneno *buda* na *mbuyu* yanaonekana kutumiwa kurejeleamzazi wa kiume au

mwanamume mwenye umri unaomzidi mzungumzaji. Ochichi (2013) anasema kwamba maneno katika lugha hupata maana zaidi yanapotumika kimuktadha. Maneno haya yalivyotumika katika nyimbo hizi ni bayana yaliibua maana tofauti za zile za kawaida au kikamusi kwani kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014): *Buda* ni mwanaume mzee aliyezeeka, kibogoyo au ndovu asiye na pembe ilhali *Mbuyu* ni aina ya mti. Neno *buda* lina mahusiano kimaana kwani katika nyimbo teule linarejelea mwanaume ambaye anaweza akawa mzazi wa mzungumzaji au mzungumziwa vilevile mwanaume yeyote yule. Hivi maana hizi zote zaonekana kukubalika na kuthibitisha maoni yake Norwich (1998) anayedokeza kwamba neno hukubalika katika lugha kutokana na matumizi yake hivi kwamba neno humaanisha kazi ya neno lenyewe katika mawasiliano. Mtazamo huu vilevile kuoana na wa Turner (2011) anayechukulia kwamba maana ya neno ni matumizi yake katika lugha linamotumiwa neno hilo. Neno *mbuyu* kwa upande mwingine linavyoibua maana ya ziada linathibitisha maoni ya Lyons (1968) kwamba maana na uamilifu wa neno hutokana na matumizi yake. Hii ni kwa sababu neno hili limetumika katika wimbo teule na kuwasilisha ujumbe kwa wapokezi waliotoa fasiri yao kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ya neno lenyewe. Maana ya kikamusi ya neno mbuyu ni tofauti na ile iliyozuliwa katika wimbo teule na hivyo kuzua dhana ya upanuzi anavyodhihirisha mshiriki E anaposema *Mbuyu nayo ni aina ya mti.* Mshiriki E anadhihirisha kuwa kuna maana mpya ya neno mbuyu anaposema, *lakini katika huu wimbo ni ile tu maana yaani baba au mwanamume mzazi.* Ni wazi kwamba kuna ufahamu wa maana asilia ya maneno haya kando na ile maana zaidi inayozuliwa katika wimbo teule.

#### 4.1.4.2 Nahau Rushia mkono

Nahau hii ilipatikana imetumiwa katika wimbo wa 'Mabeshte damu' japo neno *rusha* lilikuwa limetumika katika muktadha mwingine pia katika nyimbo nyingine teule.

**Wimbo wa Mabeshte damu (Juacali)**

wee ni mtu wangu kama ndugu siwezi **kurushia mkono** hata hii life ikiwa sugu
usiwai skia story za hawa mafala najua vile inatubamba wanaskilia machungu

Nahau 'rushia mkono' ilifafanuliwa na washiriki ifuatavyo:'

**Mshiriki D**: Wacha mimi nizungumzie *kurushia mkono* kwa kusema kwamba huu ni usemi ambao unaonekana kuwa fiche. Maana hapa ni kusaliti ama kumwacha mtu anapohitaji zaidi.

**Mshiriki E**: Kulingana nami kurushia mkono ni kumtelekeza mtu labda anapokuhitaji zaidi.

Nahau hii inaleta dhana ya usaliti au kumsahau mtu. Ijapo, muundo wake kwa kuzingatia neno kuu kuwa kitenzi *rusha*, kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014), unawasilisha dhana tofauti kama vile ya kutupa kitu hewani au kukataa kulipa deni. Maana kimuktadha au kimatumizi inavyobainika kuwa tofauti na maana halisi yaani ile ya kamusi ni dhihirisho kuwa maana inaweza kusimbwa jinsi ambavyo maneno yametumiwa katika muktadha fulani. Wazo hili linaoana na Sinclair (2014) anayefafanua kwamba maneno kiasilia ni vyombo vya muktadha visivyojitegemea kutengwa na muktadha wa matumizi yao. Turner (2011) anahimili kwamba maana ya maneno hupatikana katika matumizi kutokana na matumizi ya maneno yenyewe katika mazingira fulani.

Katika mahusiano, kuna ukadiriaji na katika nyimbo hizi vilevile ukadiriaji ulisawiriwa kwa misingi ya utangamano na matendo yanayoandamana na mahusiano katika jamii. Kwa hivyo, maneno yafuatayo yalionekana kutekelekeza dhima ya ukadiriaji; mbaya, kibao, damu na poa. Maneno yalitumika ifuatavyo:

**Wimbo wa Mabeshte damu (Juacali)**

Beste tuko pamoja tangu siku za kusota ma-shorty **kibao** tuliwachota,
mtaa yako ni yangu, shida zako ni zangu 'tazidi kuwa hivi mabeste
**damu** hata ka ulidandiwangwa jamu anajua haikuwa noma yako

**Wimbo wa We kamu (Nonini na Juacali)**

Juala nimenunua **kibao** (sabu yako tu) mabeshte nimewafukuza wakaenda kwao (sabu yako tu) ‘

**Wimbo wa Kiasi (Nonini)**

Maisha yangu tamu siku inanirarukia **mbaya** lakini nimeamua kuituliza kiasii

Kuhusu neno ‘mbaya’ washiriki walisema:

**Mshiriki D (kundi la tano)**: mbaya ni kivumishi chenye maana ya kitu kisichopendeza.

**Mshiriki A (kundi la tano)**: mbaya ni neno la Kiswahili linalorejelea kisicho kizuri lakini katika muktadha wa wimbo neno ‘mbaya’ limebadilishwa maana na kurejelea kitu kizuri.

**Mshiriki E (kundi la tano)**: Mimi nilitaka kusema ‘mbaya’ bado ni kivumishi ila hapa inamaanisha mtu anafurahia kitu kiasi cha kutoweza kueleza. Neno hili linaleta dhana chanya tofauti na ile ya kawaida ambayo inajulikana.

Mshiriki A (kundi la tano) alibainisha fasiri ya kawaida ya maana ya neno mbaya aliposema *mbaya ni neno la Kiswahili linalorejelea kisicho kizuri*. Alithibitisha kwamba kila neno hasa

katika lugha ya Kiswahili ina maana inayofahamika na kila mtu anayetumia lugha hii kuwasiliana. Neno mbaya ilivyotumiwa katika wimbo teule imezuliwa maana nyingine. Kwa mujibu wa mshiriki huyu, neno hili lina maana ya *kitu kizuri*.Mshiriki D (kundi la tano) analiainisha neno anaposema *mbaya ni kivumishi chenye maana ya kitu kisichopendeza*. Kwa mujibu wa mshiriki huyu, neno hili halina maana nyingine fauka ya jinsi ilivyotumika katika wimbo teule. Mshiriki E (kundi la tano) anathibitisha uainishaji uliofanywa na mwenzake kwa kusema *bado ni kivumishi* ila sasa anaishia kuzua maana kwa mujibu wa matumizi katika wimbo teule anapoeleza *mtu anafurahia kitu kiasi cha kutoweza kueleza*. Hivyo, anasawiri kiwango cha juu cha kufurahia kitu au jambo fulani. Aidha, anabainisha dhana ya kiwango katika mkondo chanya tofauti na maana ya kawaida ambayo ni uasi anaposema *Neno hili linaleta dhana chanya tofauti na ile ya kawaida ambayo inajulikana.*

#### 4.1.4.3 Neno kibao

Neno ‘kibao’ lilitolewa maelezo na washiriki ifaavyo:

> **Mshiriki C (kundi la nne)**: *kibao* tulishasema ni wingiila tu napenda kuongezea kwamba kibao kwa maana ya kawaida huwa nomino lakini hapa katika muktadha wa wimbo neno hili limegeuka na kuwa kivumishi kinapoleta dhana ya wingi.

> **Mshiriki A (kundi la kwanza)**: Kulingana nami neno kama *kibao* huwa ni nomino katika lugha sanifu lakini katika wimbo huu neno kibao linaleta dhana ya wingi au kupita kiasi.

Neno ‘kibao’ kulingana na Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) ni kifaa cha kuandikia kwa chaki au kalamu, kukalia, mpigo wa mkono kwenye uso au muziki. Katika nyimbo teule neno hili hata hivyo lina maana nyingine wanavyofafanua washiriki katika majadiliano. Kwa mujibu wa Mshiriki C (kundi la nne) neno kibao linamaanisha

wingi. Hata hivyo anatoa uelewa zaidi wa neno lilivyotumiwa katika nyimbo anaposema *kibao kwa maana ya kawaida huwa nomino lakini hapa katika muktadha wa wimbo neno hili limegeuka na kuwa kivumishi kinapoleta dhana ya wingi.* Mwenzake, mshiriki A (kundi la kwanza) alikuwa ashazungumzia neno kibao aliposema *ni nomino katika lugha sanifu lakini katika wimbo huu neno kibao linaleta dhana ya wingi au kupita kiasi.* Hivyo neno kibao katika nyimbo teule linawasilisha dhana ya wingi na hata kutekeleza dhima ya kivumishi japo ni nomino kiasilia.

#### 4.1.4.4 Neno damu

Neno 'damu' lilifafanuliwa ifuatavyo:

> **Mshiriki D (kundi la kwanza)**: *Damu* katika wimbo huu kwangu naona maana kidogo imebadilika kwa sababu hapa kuna uhusiano unaozungumziwa hapa kwa hiyo ina maana ya udhati au undani kwa kiwango fulani.
>
> **Mshiriki C (kundi la kwanza)**: Yeah ni hivyo. Na ujue sasa hapa *damu* ni kivumishi sasa hata si nomino tena kwa sababu inaeleza ubeshte.
>
> **Mshiriki B**: *Damu* kulingana na mimi ni kumaanisha urafiki wa dhati au wa toka nitoke

Mshiriki B (kundi la kwanza) alichukulia neno 'damu' kumaanisha *urafiki wa dhati au wa toka nitoke* kwa mujibu wa jinsi neno lilivyotumika katika wimbo teule. Mshiriki D (kundi la kwanza) anaeleza anavyofasiri maana ya neno damu kwa kusema *naona maana kidogo imebadilika kwa sababu hapa kuna uhusiano unaozungumziwa hapa kwa hiyo ina maana ya udhati au undani kwa kiwango fulani.* Ina maana kwamba kwa mtazamo wake neno damu linawasilisha dhana ya ukina wa mahusiano yanayozungumziwa katika wimbo wa

‘Mabeshte damu’.Mshiriki C (kundi la kwanza) anapochangia anamuunga mkono mwenzake na kusema *Yeah ni hivyo*. Anazidi kueleza dhima iliyotekelezwa na neno damu katika wimbo kwa kusema *hapa damu ni kivumishi sasa hata si nomino tena kwa sababu inaeleza ubeshte.*

Maneno *mbaya, kibao, damu* na *poa* yameonekana kuleta dhana ya kiwango au kiasi kutokana na majibu ya washiriki hawa na kusawiri muktadha wa ukadiriaji. Maneno haya kiasilia yanatekeleza dhima ambayo ni tofauti na hizi zilizoibuka katika muktadha wa nyimbo teule. Kwa mfano mshiriki D (kundi la kwanza) anaposema *Damu katika wimbo huu kwangu naona maana kidogo imebadilika,* anathibitisha kuwa maana inayozuliwa na neno damu katika nyimbo teule si sawa na ile maana inayojulikana. Mshiriki C (kundi la kwanza) anazidi kujenga wazo anaposema *ujue sasa hapa damu ni kivumishi sasa hata si nomino tena kwa sababu inaeleza ubeshte.*

Asim na Asim (2012) wakinukuliwa na Hasan (2015) wanasema kwamba watumiaji wa lugha wana mamlaka ya kuzua na kuamua maana za maneno ya lugha hiyo. Hili linadhihirika tunapotathmini maneno kibao, damu, poa na mbaya yalivyotumiwa hasa katika nyimbo teule. Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014) *kibao* ni kifaa cha kuandikia kwa chaki au kalamu, kukalia, mpigo wa mkono kwenye uso au muziki. Katika nyimbo hizi hata hivyo neno hili lilipata maana ya wingi. Pia ni nomino kwa kawaida lakini katika muktadha wa nyimbo hizi neno hili ni kivumishi kinachoashiria wingi. Pia kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) *Mbaya* ni kivumishi kinachorejelea kitu kisichopendeza au kinachodhuru. Hata hivyo, katika wimbo huu neno

hili linarejelea kufurahia kitu kiasi cha kutoweza kueleza yaani kitu kupendeza sana. Japo kimesalia kivumishi neno hili katika muktadha wa wimbo unaleta dhana chanya tofauti na ile ya kawaida iliyo hasi. Aidha, Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014) inaeleza maana ya *Damu* kuwa ni nomino yenye maana ya majimaji mekundu yanayozunguka mwilini ila katika wimbo 'mabeshte damu'neno hili ni kivumishi kinachoashiria kiwango cha juu cha urafiki.

Maneno *kibao, mbaya, poa* na *damu* yalivyotumiwa katika nyimbo teule yanadhihirisha kwamba maneno huwasilisha maana kutegemea mazingira yalimotumiwa. Kwa mujibu wa Douglas (2004) akinukuliwa na Yeibo na Akerele (2015), ili kuwasilisha maana ya kipekee kunaweza kuondoka kwa matumizi ya kawaida ya maneno. Kwa misingi hii, maneno *kibao, mbaya, poa* na *damu* ilivyotumika imewasilisha maana zinazoweza kuchukuliwa kuwa za kipekee kwani maneno haya yana maana za kawaida.

Katika mahusiano, kuna kutangamana baina ya wanajamii na hivyo kuzuka kwa mitazamo mbalimbali. Maneno; ameng'ara, ameshona, kupepea, wamechanuka, nwaika, anakaa, bamba, shika na roga. Maneno haya yalivyotumiwa katika nyimbo teule yaliibua maana zaidi.

#### 4.1.4.5 Neno pepea

**Wimbo wa Mabeshte damu (Juacali)**

> tutazidi kuwa pamoja hivi hata kama hatuna ganji tutazidi **kupepea** na hii life bila wasi wasi mtoi wako ni msoo saa hii ana**kaa** tu kama wewe, najua huko ni kuzii beste

Neno 'pepea' lilifafanuliwa na washiriki ifuatavyo:

> **Mshiriki A**: Hii *kupepea* ndio sijui ni kuwa maarufu nkidhani.
>
> **Mshiriki C**: Ndio nakubaliana na huyu rafiki yangu lakini hapa kwa kupepea mimi nafikiria ni kufanikiwa ama tu kupanda ngazi ya maisha.
>
> **Mshiriki B**: Lakini si kupepea pia inaweza kuwa tu hivyo. Yaani kung'ara hivi. Ama pia mimi naona inaweza kusonga tu mbele labda kutoka mahali pamoja hadi pengine labda viwango hivi.

Mshiriki A anachukulia neno 'kupepea' kumaanisha kujulikana na wengi. Mshiriki C anakubaliana naye anaposema *ndio nakubaliana na huyu rafiki yangu* ila anaendeleza mchango wake kutokana na mtazamo na kusema ni *kufanikiwa ama tu kupanda ngazi ya maisha.* Kulingana na mshiriki huyu neno kupepea limepata maana mpya hasa muktadha wa matumizi yake unapozingatiwa. Mshiriki B hata hivyo anachukulia neno hili kutobadilika kimaana pasi kuzingatia matumizi ya neno katika wimbo. Yeye anakisia maana kuwa *kung'ara hivi* na kueleza zaidi anaposema *kusonga tu mbele labda kutoka mahali pamoja hadi pengine labda viwango hivi.* Kwa misingi ya maelezo ya washiriki hawa inabainika kwamba si kila mmoja anayetambua maana mpya iliyo tofauti na ile ya kawaida hata kwa mujibu wa jinsi neno lilivyotumika katika muktadha fulani. Aidha, kuna uwezekano kwamba wanapotoa maelezo huwa wanafanyiza maana mpya bila wao kutambaa kwamba wanafanyiza maana mpya na tofauti na machukulio yao ya kawaida ya maana ya neno husika. *Kupepea* nayo kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014)ni

kupuliza labda kifaa, kuivisha matunda kwa kuyafukia shimoni kuliko na joto au pia kudhoofika. Hivyo maana katika wimbo teule ni mpya na inathibitisha upanuzi wa maana.

#### 4.1.4.6 Neno kaa

**Wimbo wa Mabeshte damu (Juacali)**

tutazidi kuwa pamoja hivi hata kama hatuna ganji tutazidi **kupepea** na hii life bila wasi wasi mtoi wako ni msoo saa hii ana**kaa** tu kama wewe, najua huko ni kuzii beste

**Mshiriki C**: Katika wimbo neno kaa kwa maoni yangu ni kufanana juu anamzungumzia mwanawe rafiki yake.

Neno ‘kaa’ limepata maana nyingine kwa mujibu wa mshiriki C kutokana na jinsi ilivyotumika katika wimbo teule. Mshiriki huyu anazungumzia dhana ya kufanana ilhali katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014) *Kaa* ni neno lenye maana nyingi ambazo ni pamoja na kipande cheusi cha kuni, mnyama wa majini, kitenzi kinachorejelea kitendo cha kuweka makalio mahali fulani kama kitini hivi, kuwa na maskani mahali, kuwa mahali kwa muda fulani, kutumika kwa muda mrefu na kupendeza. Hivyo, neno ‘kaa’ kwa mujibu wa maana mpya kutokana na matumizi yake katika wimbo wa mabeshte damu, limepanuka kimaana.

#### 4.1.4.7 Neno bamba

**Wimbo wa Mabeshte damu (Juacali)**

usiwai skia story za hawa mafala najua vile inatu**bamba** wanaskilia machungu

**Wimbo wa Kiasi (Nonini)**

Ka hii ngoma inaku**bamba** basi si ukatike na ka inakushika si uongeze sauti tenje kiasii...
Naskia raha wasee wamechanuka siku hizi ngoma mbaya haziskizwi ata kiasii

Neno ‘bamba’ lilielezwa na washiriki ifuatavyo:

> **Mshiriki E**: Kulingana nami kurushia mkono ni kumtelekeza mtu labda anapokuhitaji zaidi. Halafu *bamba* mimi naona ni kufurahisha tu ila maana yake sanifu ni tofauti sana.

> **Mshiriki C**: Mimi ninafikiri maneno hayo yana maana kwamba msanii amezidiwa. Anaingiwa sana na wimbo wenyewe unaoibua hisia kutokana na maneno na labda mapigo yake. Kimsingi anafurahia wimbo.

Mshiriki E anathibitisha kwamba neno linaweza kupata maana nyingine kutokana na matumizi yake katika muktadha huo anaposema neno bamba lina maana ya *kufurahisha tu*. Pia anabainisha kuwa neno lina maana asilia anayochukulia kuwa sanifu yaani iliyopata ukubalifu katika jamii hata kuorodheshwa katika kamusi anaposema *ila maana yake sanifu ni tofauti sana.* Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) neno *bamba* ni nomino linalorejelea bati au kitu chembamba chenye makali au kundi la watu, aidha neno hili linaweza kutumika kama kitenzi chenye kuleta dhana ya kumshika mtu kwa nguvu na kuzuia au kuziba mahali. Hata hivyo, kwa mujibu wa washiriki huyu maana zaidi ya neno hili iliyopatikana katika matumizi yake wimboni ni tofauti na hivyo kudhihirisha kwamba idadi ya maana hizi imeongezeka.

#### 4.1.4.8 Neno kuchanuka

**Wimbo wa Kiasi (Nonini)**

Ka hii ngoma inakubambabasi si ukatike na ka inakushika si uongeze sauti tenje kiasii...
Naskia raha wasee wame**chanuka** siku hizi ngoma mbaya haziskizwi ata kiasii

Neno ‘kuchanuka’ lilijadiliwa na washiriki ifuatavyo:

**Mshiriki E**: *kuchanuka* ni kupevuka kimawazo ama tunaweza kusema kwamba kule kupata ujuzi ambao mwanzo haukuwepo.

**Mshiriki D**: mimi naona kuchanuka hapa ni kule ambako watu wana uwezo wa kuchagua yaani wana uelewa fulani unaowaongoza kufanya mambo ambao haukuwepo awali.

Neno kuchanuka limepata maana zaidi kwa mujibu wa washiriki E na D. Mshiriki E anasema ni *kupevuka kimawazo* huku mwenzake ambaye ni D akizidisha mawazo hayo kwa kusema ni *kule ambako watu wana uwezo wa kuchagua yaani wana uelewa fulani unaowaongoza kufanya mambo ambao haukuwepo awali.* Maelezo haya yanasawiri mabadiliko katika kiwango cha fikra kuhusu suala fulani. Hivyo neno kuchanuka linahusishwa na mitazamo inayoonekana kuongezeka ikilinganishwa na hali ilivyokuwa hapo awali. *Chanuka* ni kitenzi kinachoashiria kufumbuka kwa maua au kufumua kitu kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014). Hivyo, neno hili kiasilia husawiri kutoa ila katika wimbo teule dhana nyingine tofauti ya kuzinduka kimawazo ndiyo inayokisiwa kutokana na matumizi ya neno katika wimbo.

#### 4.1.4.9 Neno shika

**Wimbo wa Kiasi (Nonini)**

Ka hii ngoma inakubambababasi si ukatike na ka inaku**shika** si uongeze sauti tenje kiasii...
Naskia raha wasee wamechanukasiku hizi ngoma mbaya haziskizwi ata kiasii

Neno hili lilielezwa na washiriki ifuatavyo:

**Mshiriki B**: Halafu ku*shika* ni kule kufurahishwa au kuburudika kutokana na wimbo

**Mshiriki A**: nakubaliana naye.

Kwa mujibu wa washiriki hawa, maana ya kupata furaha au burudani kutokana na kitu fulani ndiyo inayozuliwa. Maana hii ni tofauti na ile asilia yaani iliyoorodheshwa kwenye kamusi. Aidha, ni maana inayofanyizwa kwa kuzingatia jinsi neno lilivyotumiwa katika wimbo teule.

#### 4.1.4.10 Neno roga

**Wimbo wa Manzi wa Nairobi (Nonini)**

Na naongea from experience niliacha moja juzi, Mluhya kumunduyo manzi ame**shona** bana... wacha ikae ka ni huyo ni na**wika** hapana, Nime**rogwa** na ninazidi **kuroga** juu ya vile **wananiroga**, Au vipi jua kali (mmh mmh)

Kulingana na washiriki hawa Neno ‘roga’ linaashiria:

**Mshiriki E**: .... halafu roga ni kuimba tu kunakofurahisha yaani kuimba vizuri.

**Mshiriki C**: Kwani *roga* ina maana tofauti hapa?

**Mshiriki A**: Ndio.kama katika sentensi hii roga inamaanisha tu kuburudisha sana yaani kufurahisha kabisa.

**Mshiriki D**: Nakubaliana na mwenzangu; roga hapa hasa katika wimbo huu na hata mazungumzo ya kawaida inamaanisha kutekwa makini na kitu kinachofurahisha.

Mshiriki C anavyouliza ikiwa neno roga lina maana tofauti katika muktadha wa wimbo, inathibitisha kwamba wapokezi wa ujumbe unapowasilishwa katika wimbo huu wana fasiri tofauti za dhana zinazowasilishwa na maneno ya nyimbo. Kulingana naye, maneno yana maana asilia na ukubalifu wa maana unapatikana katika utambuzi wake miongoni mwa watumizi wa maneno katika lugha.Mshiriki E anatoa maana ya neno ‘roga’ kama *kuimba tu kunakofurahisha yaani kuimba vizuri* huku mshiriki C akizungumzia *kuburudisha yaani kufurahisha kabisa.* Mshiriki D vile vile anakubaliana na wenzake E na C wanathibitisha namna ambavyo maana inafanyizwa kwa matumizi anapozungumzia maana ya neno hili katika muktadha mwingine ulio tofauti na wimbo. Anasema *hata mazungumzo ya kawaida inamaanisha kutekwa makini na kitu kinachofurahisha.* Kwa mujibu wa mshiriki huyu, maana nyingi huweza kutokana na matumizi ya maneno katika muktadha wa matumizi yao.

#### 4.1.4.11 Neno wika

**Wimbo wa Manzi wa Nairobi (Nonini)**

> Na naongea from experience niliacha moja juzi, Mluhya kumunduyo manzi ameshona bana... wacha ikae ka ni huyo ni na**wika** hapana, Nimerogwa na ninazidi kuroga juu ya vile wananiroga, Au vipi jua kali (mmh mmh) '

Neno 'wika' lilifafanuliwa na washiriki ifuatavyo:

> **Mshiriki C**: *kuwika* nayo ni kukataa na kuonyesha pingamizi kwa jambo fulani.
>
> **Mshiriki E**: kulingana na mimi kuwika ni kuzungumza kwa nguvu.

Washiriki C na E wanatoa maana za neno kuwika; *kukataa na kuonyesha pingamizi kwa jambo fulani* na *kuzungumza kwa nguvu* mtawalia. Maana hizi kwa kweli ni tofauti na maana asilia ya neno kuwika. *Kuwika* kulingana na kamusi ni kulia kama jogoo au kutawala. Hivyo, neno hili lilivyotumika linasawiri dhana ya mazungumzo yanayofanywa ila fasiri za kiwango cha sauti ya juu au kauli kutetewa vikali, inakisiwa kutokana na muktadha katika wimbo teule ambamo neno kuwika limetumika.

#### 4.1.4.12 Neno shona

**Wimbo wa Manzi wa Nairobi (Nonini)**

> Na naongea from experience niliacha moja juzi, Mluhya kumunduyo manzi ame**shona** bana... wacha ikae ka ni huyo ni nawika hapana, Nimerogwa na ninazidi kuroga juu ya vile wananiroga, Au vipi jua kali (mmh mmh)

Neno shona lilifafanuliwa na washiriki hawa ifuatavyo:

**Mshiriki B**: Ukisema mtu *ameshona* ni kumaanisha tu yeye ni mnene lakini wakati mwingine inaweza pia kuwa inamaanisha kushiba au wingi wa kitu.

**Mshiriki A**: kushona ni kunenepa.

**Mshiriki D**: ndio ni hivyo. Kushona enyewe ni kuwa mkubwa kimaumbile.

Dhana za unene, kushiba, wingi wa kitu, kunenepa au maoni ya kitasfida kama ya mshiriki D ya *kuwa mkubwa kimaumbile* yote yanazua mtazamo kuhusu mkao wa jumla wa mtu anayezungumziwa katika wimbo. Kitenzi shona kwa kawaida humaanisha kuwekwa pamoja kwa vitu kwa kutumia sindano na uzi. Kitenzi shona katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) lenye maana ya kuupisha uzi kwa kusudi labda la kuunganisha. Katika muktadha wa matumizi ya neno hili limepata maana zaidi. Maana inayowasilishwa inatokana na mtazamo unaozuliwa katika wimbo teule.

Kutokana na majadiliano na maana za maneno haya teule yaliibuka ambayo ni zaidi ya zile maana za kawaida. Kulingana na Paul (1920) akinukuliwa na Geerearts (2009), maana ya kawaida ni le ya kamusi huku maana inayoibuka kutokana namatumizi ya maneno katika mazingira fulani ilichukuliwa kuwa maana japo kimuktadha. Kwa misingi hii ni bayana kwamba maneno *ameng'ara, ameshona, kupepa, wamechanuka, nawika, anakaa, bamba, shika na roga* yameibua kimuktadha kulingana na matumizi yao katika nyimbo teule.

Kuna tofauti katika maana za maneno haya teule ya Kiswahili yalivyotumika katika wimbo na yanavyoamaanisha katika kamusi. Maana hizi zilizoibuka kutoka kwa nyimbo teule zinatoka kwa wasikilizaji ambao pia huenda ni wapokezi wa nyimbo hizo teule. Ina maana kwamba maana kimatumizi asemavyo Munawwaroh (2008), inategemea maneno ya nyimbo yalivyotumika na kusudi linalotarajiwa kupokelewa na msikilizaji. Tathmini ya matumizi ya maneno haya pamoja na maana ibuka inathibitisha misingi ya nadharia ya Wittgenstein (1963) kwamba maana ya maneno hupatikana katika matumizi yao. Pili, maana ya neno inatokana na muktadha wa matumizi ya neno lenyewe. Aidha, kuwepo kwa maana za ziada za maneno mengine kama yalivyotathminiwa hapa kunathibitisha upanuzi wa maana kwa maneno haya teule ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule zilizoimbwa na Nonini na Juacali.

Maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule za kizazi kipya zilizoimbwa na Nonini na Juacali, yana maana asilia zilizoorodheshwa katika kamusi za Kiswahili. Hata hivyo yanaonekana yakiibua maana zaidi na kuchukuliwa kuwa yamepanuka kimaana. Upanuzi wa maana unachangiwa pia na muktadha unaokuzwa na kusudi la yule anayepitisha ujumbe. Kwa mujibu wa Falk (1973), maana za maneno yanapotumiwa popote pale huangazia kusudi la mwasilishaji na mpokezi wa ujumbe. Hivyo maana hutokana na matarajio ya wale wanaoshiriki katika mawasiliano. Kwa mfano neno damu kwa kawaida ni nomino ila katika muktadha wa wimbo ‘Mabeshte Damu’ neno hili linawasilisha dhana ya udhati na undani wa mahusiano. Kiasilia neno hili ni jina la kitu ila lilivyotumiwa katika wimbo teule wapokezi wanapata dhana ya ukadiriaji wa mahusiano. Dhihirisho la wazo hili katika utafiti huu ni maana zaidi zinazosawiri mahusiano katika nyimbo teule kwa kuzua

mitazamo na ukadiriaji unaozuka kutokana na utangamano unaonekana katika nyimbo jinsi maneno teule ya Kiswahili yalivyotumiwa.

Kulingana na Turner (2011) matumizi mbalimbali ndiyo yanatoa maana hizi tofautitofauti kwa maneno. Hivyo maneno haya yalivyozua jumbe za mahusiano katika matumizi yao kwenye nyimbo teule, maana zaidi zimeibuka kwani kuna uelewa kwamba maana zao za kikamusi zipo. Kwa misingi kwamba maana inatokana na matumizi maneno yanavyotumiwa na yanapotumiwa popote pale kwa vyovyote yanaweza kuzua maana nyingi. Aidha kuna mahusiano ya kiutegemezi kati ya vipengele vya matumizi na muktadha katika mchakato wa kufanyiza maana unaoishia kupanua maana ambayo tayari ipo.

### 4.1.5 Miktadha ya Ulevi na uhalifu

Katika muktadha huu kuna maneno haya: gonga, chota na vitu.

#### 4.1.5.1 Neno gonga

**Wimbo wa Mabeshte damu**

ebu kwanza **gonga** glass wajue vile hapa damu ni nzito kuliko maji mabeshte damu
Beste tuko pamoja tangu siku za kusota ma-shorty kibao tuliwachota

**Mshiriki A**: Halafu ku*gonga* kwa wimbo huu ni kunywa. Unaona kuna mambo ya glasi kwa hivyo ni kunywa tu pombe.

**Mshiriki B**: Nakubaliana na mwenzangu

Washiriki walikubaliana kuhusu maana ya neno gonga waliyopata kutoka wimboni humo. Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) inafafanua *Kugonga kitu* ni kukikutanisha ama kukipiganisha kitu na kingine. Neno gonga limepewa maana ya kunywa katika wimbo huu tofauti na maana katika kamusi na hivyo kuthibitisha jinsi ambavyo maana inatokana na matumizi ya maneno katika miktadha mablimbali. Aidha tofauti katika maana za neno hili moja inazua pia ule uwezekano wa kutopata ujumbe uliokusudiwa kwani maana anayokusudia mtunzi hasa wa nyimbo huenda isiwe waliyozua.

#### 4.1.5.2 Neno chota

**Wimbo wa Mabeshte damu (Juacali)**

ebu kwanza gongaglass wajue vile hapa damu ni nzito kuliko maji mabeshte damu
Beste tuko pamoja tangu siku za kusota ma-shorty kibao tuliwa**chota**,

Neno hili ‘chota’ lilifafanuliwa na washiriki ifuatavyo:

**Mshiriki A**: Halafu kuchota sasa hapa mimi ninafikiri ni kule kumlaghai mtu au kumlaghai mtu au kumnyang’anya.

**Mshiriki B**: kuchotakwangu naona ina maana ya kumwomba mtu ngono ama labda kumteka mtu kwa njia fulani.

Neno ‘chota’ lilizuliwa maana tofauti kwa mujibu wa washiriki hawa japo katika uelewa wa muktadha katika wimbo teule.Mshiriki A alichukulia neno chota kumaanisha *kumlaghai mtu au kumlaghai mtu au kumnyang’anya*. Mshiriki B kwa upande mwingine alizua maana ya *kumwomba mtu ngono ama labda kumteka mtu kwanjia fulani*. Dhana za ulaghai, unyang’anyi, utekaji na ngono ndizo zinazoibuliwa hapa kwa kuzingatia muktadha wa

matumizi kwenye wimbo teule. Baadhi ya dhana hizi ni tofauti mno na dhana asilia inayowasilishwa na neno hili. *Kuchota* kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014) ni kuchukua sehemu ya vyowevu kama maji kutoka mahali fulani au kutaka kujua mawazo ya mtu kwa njia ya ujanja. Hivyo, dhana ya ulaghai pekee ndiyo inayokaribiana na maana asilia. Ni kukaribiana huku ndiko kunakodhihirisha kwamba maana kimatumizi husababisha mahusiano ya kimaana ambako neno moja linaweza kukaribiana kimaana na jingine au hata kuchukuliwa kufanana.

#### 4.1.5.3 Neno vitu

**Wimbo wa Kiasi**

Na najua tapata kiswahili yangu ni mambo yote hapa hakuna cha lugha kiasii
Afta hio tunakuta **vitu** kuta vitu mchana tunatulia kiasii

Neno ‘vitu’ lilifafanuliwa na washiriki ifuatavyo:

**Mshiriki B**: *vitu* sasa hapa ni pombe ama; mimi nafikiria hivyo

**Mshiriki E**: kwangu vitu inarejelea maumbile ya binti fulani.

**Mshiriki A**: vitu mimi inanichanganya juu sijui kama ni pesa, ngono au vileo. Lakini nafikiri maana zote hizi ni za neno vitu inalingana tu na mazingira.

Mshiriki B anachukulia neno vitu kumaanisha pombe. Mshiriki E hata hivyo anatofautiana naye na kusema *kwangu vitu inarejelea maumbile ya binti fulani*. Mshiriki A naye anazua dhana zaidi anaposema pesa. Kulingana naye neno hili linaweza kuwasilisha dhana nyingi kwa mujibu wa mazingira ambamo neno lenyewe limetumika. Neno vitu lilivyozua maana zaidi tena inaonyesha umuhimu wa uelewa wa muktadha wa matumizi ya neno. Muktadha

wa matumizi ulivyodhihirishwa na maana zaidi za neno vitu ni kiungo muhimu sana kwani chukulio la maana linaweza kutofautiana moja na jingine ila tunapojikita katika muktadha basi maana huenda ikawa mahususi na hivyo finyu.

Kutokana na majadiliano kwenye makundi kuhusu maneno haya yalivyotumiwa katika nyimbo teule maana zaidi zilizuliwa kutegemea matumizi ya maneno hayo katika nyimbo teule. Kwa kutegemea matazamo wa Turner (2011) kwamba maana inatokana na matumizi yake hivyo maana ya neno ni matumizi yake katika lugha linamotumiwa neno hilo, maana hizi zaidi zinaonyesha upanuzi wa maana za maneno ambayo yana maana asilia zilizoorodheshwa katika kamusi za Kiswahili.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014) inafafanua neno v*itu*kama neno la kawaida linaloweza kurejelea chochote kinachoweza kuonekana, kushikika, kuhisika, kusikika na kuonjeka. Aidha ni pesa au mali ila katika nyimbo teule neno hili pia linaashiria pombe, maumbile ya binti fulani, ngono au vileo. *Kuchota* kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) ni kuchukua sehemu ya vyowevu kama maji kutoka mahali fulani au kutaka kujua mawazo ya mtu kwa njia ya ujanja. Neno chota lina maana zifuatazo kulingana na muktadha wa wimbo ’mabeshte damu’ ni kule kumlaghai mtu au kumnyang’anya, kumwomba mtu ngono ama labda kumteka mtu kwa njia fulani. Aidha, Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014) inafafanua kitenzi *gonga* kama kukikutanisha ama kukipiganisha kitu na kingine lakini katika nyimbo hizi ni kule kunywa pombe au pia kusherehekea. Maana hizi tofauti na zile zilizo kwenye kamusi inavyodhihirika zilizuliwa kutokana na muktadha wa matumizi ya maneno haya katika

nyimbo teule. Hivyo nadharia ya maana kimatumizi imepata ithibati katika mtazamo wa suala la maana. Vilevile maana ya neno haiwezi kuchukuliwa kuwa ni moja tu kwani uwezekano wa kuzuliwa kwa maana nyingine kwa kutegemea muktadha na matumizi katika mchakato wa mawasiliano.

**4.2 Upanuzi wa maana na athari yake katika lugha ya Kiswahili**

Utafiti huu ulitathmini upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za kizazi kipya na athari ya upanuzi huo kwa lugha ya Kiswahili. Maneno ya Kiswahili yaliweza kudhihirisha maana pana zaidi ya maana za kawaida kwa mujibu wa matokeo. Baadhi ya maneno hayo yaliwasilishwa kwa njia ya jedwali ifuatavyo:

| **Neno** | **Maana kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014):** | **Maana iliyozuliwa kutoka kwa nyimbo** | **Muktadha wa tukio la neno** |
|---|---|---|---|
| Kibao | kifaa cha kuandikia kwa chaki au kalamu, kukalia, mpigo wa mkono kwenye uso au muziki. | (Kivumishi) dhana ya wingi, | Beste tuko pamoja tangu siku za kusota ma-shorty kibao tuliwachota. |
| Chota | kuchukua sehemu ya vyowevu kama maji kutoka mahali Fulani au kutaka kujua mawazo ya mtu kwa njia ya ujanja | kumlaghai mtu au kumnyang’anya, kumwomba mtu ngono, labda kumteka mtu kwa njia Fulani, kumteka mtu kihisia hasa kimapenzi. | Beste tuko pamoja tangu siku za kusota ma-shorty kibao tuliwachota. (Mabeshte damu)<br>Juacali |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ushaichota mtoto kwa haga.(We kamu) |
| Buda | mwanaume mzee aliyezeeka, kibogoyo au ndovu asiye na pembe. | mzazi wa kiume au mwanamume mwenye umri unaomzidi mzungumzaji | unakumbuka ule mama ulicheki ule buda asikuwai kuseti kwa makarao. (wimbo wa'Mabeshte damu'.) |
| Rusha mkono | kutupa kitu hewani au kukataa kulipa deni. | kuacha, kusaliti, kusahau. | wee ni mtu wangu kama ndugu siwezi kurushia mkono hata hii life ikiwa sugu. (wimbo wa 'Mabeshte damu.') |
| Bamba | ni nomino inayorejelea bati, kitu chembamba na chenye ubapa, sehemu ya upanga ulio na makali. pia ni kitenzi kinachomaanisha kumkamata mtu kwa nguvu, kuzuia au kuziba mahali, | kuburudika au kufurahia kitu fulani. | najua vile inatubamba wanaskilia machungu (wimbo wa Mabeshte damu.') |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| Gonga | kukikutanisha ama kukipiganisha kitu na kingine | kunywa pombe au pia kusherehekea. | ebu kwanza gonga glass wajue vile hapa damu ni nzito kuliko maji. (wimbo wa Mabeshte damu.') |
| Kupepea | kupuliza labda kifaa, kuivisha matunda kwa kuyafukia shimoni kuliko na joto au pia kudhoofika. | kufanikiwa, kubobea, kuvuma, kuendelea, kuwika, kung'aa na kutambaa. | tutazidi kuwa pamoja hivi hata kama hatuna ganji tutazidi kupepea na hii life bila wasi wasi (wimbo wa Mabeshte damu.') |
| Damu | nomino yenye maana ya majimaji mekundu yanayozunguka mwilini | kivumishi kinachoashiria kiwango cha juu cha urafiki. | 'tazidi kuwa hivi mabeste... damu hata ka ulidandiwang wa (wimbo wa Mabeshte damu.') |
| Kaa | kipande cheusi cha kuni, mnyama wa majini, kitenzi kinachorejelea kitendo cha kuweka makalio mahali Fulani kama kitini hivi, kuwa na | kufanana na kitu. | mtoi wako ni msoo saa hii anakaa tu kama wewe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | maskani mahali, kuwa mahali kwa muda Fulani, kutumika kwa muda mrefu na kupendeza. | | (wimbo wa Mabeshte damu.’) |
| Pigwa | | kulipwa. | kazi hapa kibao nimepigwa sumuni mbili, |
| Mbuyu | aina ya mti | mzazi wa kiume, mwanaume yeyote aliyemzidi mzungumzaji umri. | salimia matha salimia mbuyu |
| Nyundo | kifaa cha kugongomelea katika shughuli kama vile ujenzi na useremala | uume, sehemu ya siri ya kaka na pia mchakato mzima wa ngono. | Nashindwa jo nizame wapi, nyundo yangu sasa itauwa wapi (Nyundo)<br><br>Tape za nyundo ninazo (sabu yako tu), sa fanya hivi (we we we we kamu). (We kamu) |
| Nizame | kutokana na kitenzi zama linamaanisha kuingia ndani ya maji na kwenda chini vilevile kutoweka. | nistarehe, nifanye tendo la ngono; tendo la mapenzi la kuingiza kibofu kwenye uke. | Nashindwa jo nizame wapi, nyundo yangu sasa itauwa wapi (Nyundo) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| Itauwa | Ondoa uhai wa kitu au mtu | Kupendeza mno, kufurahisha sana. | nyundo yangu sasa itauwa wapi (Nyundo) |
| Rusha | kutupa kitu hewani au kukataa kulipa deni | kucheza densi, kuumiza, kuweza kutungwa mimba, mwaga manii, kuacha, kusaliti, kusahau. | inazusha lakini chunga inaeza rusha (Nyundo). |
| Dunga | Choma kwa kitu chenye ncha, kapu lenye mfuniko, uchawi ua sihiri. | Kukutanisha sehemu nyeti wakati wa ngono, kuvalia vizuri, kufurahishwa, kusisimuliwa kimapenzi. | hapa job kuna nyundo moja itadunga wapi (Nyundo). |
| Msumari | Kipande chembamba cha chumba chenye ncha kichwani kinachopigiliwa kwenye mbao, vyuma au ukutani, mwiba wa mdudunaotumia kudungia. | uume wa mtu, sehemu nyeti ya mwanaume. | na msumari ni moja itaingia wapi (Nyundo). |
| Msumeno | Kifaa chenye meno ya kukekereza kinachotumiwa na seremalakupasulia au kukatia mbao au mti. | sehemu nyeti ya msichana, uke. | tulia nipe msumeno, (Nyundo). |
| Kabati | Aina ya sanduku la wima lililotengenezwa kwa mabo, chuma au bati kwa kuhifadhia vitu. | uke, sehemu ya siri ya mwanadada, makalio, mwili mzima wa mwanamke. | lakini kabati yako ni kubwa sana (wimbo wa ‘Nyundo’). |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Piga randa | Kusawazisha mbao. | Kupapasa mtu katika hali ya ngono, mchakato wa ngono. kumsisimua mtu kingono | ilalishe hivi iipige randa na sandpaper (wimbo wa ‘Nyundo’) |
| Kusugua kitanda | Kusugua ni kupitisha kitu juu ya kingine kwa kurudiarudia kwa nguvu ili kuondoa alam au uchafu. kitanda ni kifaa cha kulalia, hivyo huu usemi ambao kimsingi unamaanisha kusafisha kitanda. | Tendo la kimapenzi, ngono. | kusugua kitanda ya mtu mmoja staki, (wimbo wa ‘Nyundo’) |
| Katika | Ndani ya, mahali fulani, kipindi Fulani cha wakati au shughuli Fulani pia kitu Fulani kupitishwa kwenye makali. | umizwa, sakata densi, sikia utamu, cheza kwa kunengua, kuwa na hisia ya kutosheka, shiriki ngono. | Ka we ni manzi wa Nairobi amka uwanza kukatika (wimbo wa ‘Manzi wa Nairobi)<br><br>juu ya meza leo lazima utakatika (wimbo wa ‘We kamu’) |
| Imemkaza | Inatokana na neno kaza lenye maana ya funga imara, shika kwa nguvu, tumia nguvu au tembea haraka. | Kuonekana kufinywa katika vazi Fulani, kuhisi shinikizo la kitu, kubanwa kwenye nguo. | Hiyo jeans imemkaza itamkazia kufika huko. (wimbo wa ‘Manzi wa Nairobi) |
| Itamkazia | Kitenzi kazia kina maana ya kutia msisitizo. | Amezuliwa kwa namna Fulani, kuna kizuizi. | Hiyo jeans imemkaza itamkazia kufika huko. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | (wimbo wa 'Manzi wa Nairobi) |
| Ameshona | Kutokana na neno shona lenye maana ya kupitisha uzi katika vitu lainikama vile nguo kwa kutumia kitu ili kuviunganisha. | Yeye ni mnene, ana mwili mkubwa. | Mluhya kumunduyo manzi ameshona bana (wimbo wa 'Manzi wa Nairobi) |
| Nawika | Kutokana na neno wika lenye maana ya kulia kama jogoo au tawala. | kukataa na kuonyesha pingamizi kwa jambo Fulani na pia kuzungumza kwa nguvu kwa wengine. | Wacha ikae ka ni huyo mi nawika hapana (wimbo wa 'Manzi wa Nairobi) |
| Mizigo | Vitu vizito vilivyobebwa, jambo linalotatiza au lililo gumu kukabiliana nalo. | Makalio, umbo la mwanamke. | Nashindwa nikimpata hizo mizigo nitaezana (wimbo wa 'Manzi wa Nairobi) |
| Ngoma | Ala ya muziki, mchezo wa kufuata mdundo, kufanya jambo lisilo na faida. | nyimbo, muziki, ngono. | Hii ngoma inaeza enda one-hour kabla haijaisha (wimbo wa 'Manzi wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Nairobi') <br><br> Ngoma yako wee kamu si unaiskia (wimbo wa 'We kamu') |
| Nimerogwa | Kutokana na neno roga lenye maana ya dhuru kwa uchawi. | kuimba tu kunakofurahisha yaani kuimba vizuri. | Nimerogwa na ninazidi kuroga juu ya vile wananiroga (wimbo wa 'Manzi wa Nairobi) |
| Dondoa | Okota kitu kimojakimoja kama vile punji au wadudu walio mwilini, kariri au nukuu shehemu ya maandishi au mazungumzo ya mtu mwingine. | kushuka kutoka kwa gari, kumwonyesha mtu mahali fulani. <br><br> kumfanya mtu asahau. <br><br> kumtoa mtu labda mahali. | ambia ule concodi atakudondoa kwetu hapo nje (wimbo wa 'We kamu) |
| Mtoto | Kiumbe anayezaliwa na mtu na mnyama, mtu mwenye umri mdogo, kitu kidogo kinachopachikwa kwenye kitu kingine au kidoa cheupe kinachochomea ndani ya jicho la mtu. | msichana mrembo | Kwanza vile umesimama mtoto (wimbo wa 'Nyundo) <br><br> Juacali ushaichota mtoto kwa haga (wimbo wa We Kamu) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Atanipigia magoti nimbariki | Kuweka magoti chini kama wakati wa kuabudu au kama ishara ya unyenyekevu, kusalimu amri, kuomba masamaha. Kubariki ni kutoa baraka, kuwa kiasi cha kutosha. Hivyo maana ya usemi huu kimsingi kuweka magoti (sehemu ya mwili) ili kupokea heri njema. | atakubali, ataomba msamaha, atajiachilia, atajisalimisha, atakubali kushiriki ngono, atajisahau, atakosa uwezo wa kukataa chochote kitakachotendeka. | achana nazo ikifika atanipigia magoti nimbariki na juala staki mtaani kuwe na mazishi! Kwa hivyo we kamu (wimbo wa We Kamu) |
| Tulia | Kuwa katika hali ya utulivu. | keti bila kufanya chochote, kutoshiriki ngono, kutokunywa pombe, kupunguza | tulia nikafungue mlango kuna mzungu anangoja, ana moto jo ananiambia anataka kuto to toka. (wimbo wa We Kamu)<br><br>Maisha yangu tamu siku inanirarukia mbaya lakini nimeamua kuituliza, kiasi... (wimbo wa kiasi) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| Ataruka | Kitenzi ruka kina maana ya toka chini kwenda juu, toka mahali kumoja hadi kwinginekwa kutumia mabawa au chombo, pita juu ya kitu bila kukikanyaga, kata kukubali jambo ambalo unalifahamu au kuwa fupi kuliko ilivyokuwa mwanzo. | atamdunga mimba | baby boy lazima ataruka we we we we kamu (wimbo wa We Kamu) |
| Mbaya | kivumishi kinachorejelea kitu kisichopendeza au kinachodhuru | Isiyo na kifani. | Genge jo inanibamba **mbaya**, yani hii mziki yani (kiasi) |
| Inanibamba mbaya | Bamba ni nomino inayorejelea bati, kitu chembamba na chenye ubapa, sehemu ya upanga ulio na makali. pia ni kitenzi kinachomaanisha kumkamata mtu kwa nguvu au kuziba mahali.<br><br>Mbaya ni neno linalotokana na kivumishi baya chenye maana yakuchukiza, chenye hitilafu, kudhuru au hasara. | inanifurahisha sana | Genge jo **inanibamba mbaya**, yani hii mziki yani (kiasi) |
| Siku inanirarukia mbaya | Kuraruka ni kuchanika kwa kitu kama vile karatasi na kuwa vipandevipande. | siku kuharibika au kukumbwa na tatizo Fulani | Maisha yangu tamu **siku inanirarukia mbaya** (we kamu) |
| Zitoke | Linatokana na neno toka linalorejelea kianzio cha kitu, kitendo cha kuondoka mahali na kwenda | kuachana na kitu, wapate burudani pamoja | Chukua chali yako chukua manzi yako mweke karibu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kwingine. | | **zitoke** nae 'kiasi'. |
| Wakiiva | Kuiva ni kuwa mbivu, kupevuka, kupikika na kuwa tayari kuliwa, kuwa tayari kwa jambo lililokuwa linaandalliwa. Pia ni shemu ya nahau yenye maana ya kuona uchungu au haya. | kuwa katika upeo wa kufanya kitu kama kusoma au hata ngono | Juzi gari ya mafuta ikaanguka si waliangalia watu **wakiiva** (Kiasi) |
| Wanaungua | Kutokana na kitenzi ungua chenye maana ya kuteketea kwa moto. | Kuteketea. | Kumetulia ama watu **wanaungua** ama watu wanaiva hivi (Kiasi) |
| Wamechanuka | Kutokana na kitenzi chanuka chenye maana yakufumuka kwa kilichochanwa au kufumbuka kwa maua. | kitenzi kupevuka kimawazo Aidha ni kule ambako watu wana uwezo wa kuchagua yaani wana uelewa Fulani unaowaongoza kufanya mambo ambao haukuwepo awali. | Naskia raha wasee **wamechanuka** siku hizi ngoma mbaya haisikizwi ata (kiasi) |
| Chinjia | Kutokana na kitenzi chinja chenye maana ya kukata shingo hasa wa mnyama, kuua mtu kwa ukatili, kupunguza udongo wa chu gu kinachofinyangwa au pia kupunja katika biashara kwa kuuza ghali. | shughuli nzima ya kumhusisha binti fulani ngono au kumwomba binti Fulani awe na mahusiano ya kimapenzi na mzungumzaji. | Pia naskia raha unaeza chijia manzi siku hizi ata ka ni mzee wako...(kiasi) |
| Tunakuta vitu | Kuta ni kuona mtu au kitu ufikapo mahali Fulani. Kitu ni chochote kinachoweza kushikika, kuonekana, kuhisika, kusikika au kuonekana. kitu pia ni neno linalotumiwa kumaanisha mali au fedha. | tunafanya tendo la kimapenzi vitu hapa ni pombe, maumbile ya binti fulani au ngono | After hio tunakuta vitu kuta vitu mchana tunatulia(kiasi) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| Ameshiba | Kutosheka na chakula baada ya kukila; kukokosa nafasi tumboni baada ya kula au kunywa. | Kutosheka kingono, amenenepa | Msafi resize yake ameshiba kiplani (wimbo wa Manzi wa nairobi) |
| Poa | Pungua joto, kaa kimya bila wasiwasi. | inayopendeza, nzuri, sawa, kuketi mahali. | anajua si ni mabeshte leo ni poa (mabeshte damu)<br><br>Ngoma yako wee kamu si unaiskia vile iko poa (we kamu)<br><br>Tukipoa down ni mrefu, tena sana (Manzi wa nairobi) |

Katika utafiti huu maneno ya Kiswahili yaliyobainika kuwa na maana mpya ilivyowasilishwa katika jedwali yalithibitisha upanuzi wa maana. Maana kutokana na matumizi ya maneno hayo katika nyimbo teule zilionekana kuwa tofauti na maana za kikamusi kama zilivyoorodheshwa katika jedwali. Kulingana na Hasan (2015), upanuzi wa maana hudhihirika pale neno moja linalorejelea maana zaidi ya yale yaliyorejelewa na neno hili hapo awali. Maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule yalionyesha upanuzi wa maana

kwani maneno haya yana maana zao za kimsingi zilizoorodheshwa katika kamusi za Kiswahili. Wittgenstein (1963) anajadili kwamba fasili ya dhana akilini inategemea lugha kwa hiyo hapana tatizo la fikra au dhana kutowakilishwa. Lugha kulingana naye ni njia ya kujihusisha kwa ulimwengu huo unasawiriwa. Hoja hii inathibitisha kwamba lugha ni njia ya kueleza kinachotolewa katika ulimwengu huo. Maneno kama vipashio vya lugha yanaweza kutumika kuwasilisha ujumbe hivyo maana mbalimbali kutegemea muktadha wao wa matumizi.

Katika utafiti huu, upanuzi wa maana ulidhihirishwa na maana zilizotolewa na washiriki kuwa tofauti na maana za maneno haya teule ya Kiswahili zinazopatikana katika kamusi ambazo pia zinachukuliwa kuwa za kawaida. Maana hizi zaidi zinaweza kuchukuliwa kuwa zilifanyizwa kwa misingi ya mtazamo wa Turner (2011) kwamba neno halimaanishi kitu kimoja katika kila matumizi yake. Matumizi kulingana na kanuni maalum ndiyo yanaweza kuwajibikia mawasiliano kwa sababu lugha ni njia ya mawasiliano. Isitoshe, baadhi ya maneno yaliibua maana tofautitofauti kutokana na matumizi yao katika nyimbo teule zaidi ya moja.

Kwa mfano,katika wimbo ‘mabeshte damu’ neno *kibao* maana yake kulingana na mshiriki A katika kundi la kwanza alisema, *“Kulingana nami neno kama kibao huwa ni nomino katika lugha sanifu lakini katika wimbo huu neno kibao linaleta dhana ya wingi au kupita kiasi.”* Neno kibao lina maana asilia yaani maana ya kikamusi; kifaa cha kuandikia kwa chaki au kalamu, kukalia, mpigo wa mkono kwenye uso au muziki. Kutokana na maana

iliyopatikana katika muktadha wa wimbo ni wazi kwamba inachukuliwa kuwa maana zaidi kwa misingi kwamba neno kibao limetumika kuwasilisha dhana ambayo nje ya muktadha huo wa nyimbo haipatikani vile kimaana. Neno ‘kibao’ linathibitika kupanuka kimaana na kuoana na mtazamo wa Mumbua (2009) akimnukuu Lyle (1998) anayeeleza kwamba upanuzi maana hutokea pale ambapo maana za maneno zimepanuka ili kutumika katika miktadha mingi ya mawasiliano kuliko ilivyokuwa ikitumika hapoawali. Hivi ni kusema kwamba matumizi ya neno hupanuka katika muktadha wa mawasiliano.

Neno *damu* ambayo kulingana na matumizi yake katika wimbo ‘Mabeshte damu’ washiriki katika majadiliano kimakundi walisema;

> **Mshiriki D**: Damu katika wimbo huu kwangu naona maana kidogo imebadilika kwa sababu hapa kuna uhusiano unaozungumziwa hapa kwa hiyo ina maana ya udhati au undani kwa kiwango fulani.
>
> **Mshiriki C**: Yeah ni hivyo. Na ujue sasa hapa damu ni kivumishi sasa hata si nomino tena kwa sababu inaeleza ubeshte.
>
> **Mshiriki B**: Damu kulingana na mimi ni kumaanisha urafiki wa dhati au wa toka nitoke.

Neno ‘damu’ kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) ni nomino yenye maana ya majimaji mekundu yanayozunguka mwilini ila katika wimbo mabeshte damu. Neno hili limepata maana zaidi na dhima kisarufi katika sentensi ambapo neno lenyewe linatoa habari zaidi kuhusiana na urafiki unaozungumziwa katika wimbo wenyewe. Hili linadhihirishwa na Mshiriki C anayesema *ni kivumishi* kinachotekeleza jukumu la kuzungumzia undani wa urafiki anavyoendeleza mawazo kwa kusema *urafiki wa dhati au*

*wa toka nitoke.* Hali hii inaoana na maelezo ya Njogu, Mwihaki, na Buliba (2006) wanaodai kuwa neno linalotumiwa katika muktadha mmoja huweza kupanuliwa ili litumike katika muktadha mwingine. Hivi kusema kwamba neno hilo huweza kutoa maana tofauti na ile inayojulikana au kuzoeleka.

Maneno haya yaliibua maana zaidi kulingana na matumizi yao katika nyimbo teule. Maana hizi ziliibuka kutokana na mitazamo ya washiriki katika makundi ya majadiliano kurejelea wimbo mmoja baada ya nyingine. Khachula (2013) anasema kwamba wazungumzaji hutumia maneno katika lugha kwa njia tofauti ili kustahiki katika muktadha husika. Hii ina maana kuwa maneno hubadilisha maana kutegemea muktadha ambamo maneno hayo yametumika. Maneno haya ya Kiswahili yalivyotumika katika nyimbo teule za Juacali na Nonini yana maana zaidi ya zile zilizo katika kamusi za Kiswahili. Hali hii ilidhihirisha kuwa maneno hupata maana zao kutokana na matumizi yao katika mazingira fulani. Hivyo, uwepo wa maana inayochukuliwa kuwa zaidi unategemea pia upanuzi wa mazingira. Hivi kwamba, ikiwa neno fulani linamaanisha kitu fulani na kingine katika mazingira mengine basi upanuzi wa maana unachangiwa pia na upanuzi wa matumizi unaoweza tu kudhihirishwa na kuwepo kwa mazingira mengine ambamo pia neno lilo hilo moja laweza kutumiwa likazua maana nyingine.

Kwa mujibu wa nadharia ya maana kimatumizi maneno yanaweza kupata maana zinazohitilafiana na maana katika kamusi, ikizingatiwa kwamba maana za maneno hutoka kwa watumizi wa maneno yenyewe. Mawazo haya yanaungwa mkono na Suguitan (2005)

anayechukulia kuwa maana ya maneno zinapambanuliwa na watumizi wa lugha ambamo maneno hayo yanatumika na sio kamusi. Hivyo maana kimatumizi kimsingi ni maana kimuktadha.

Utafiti huu ulitathmini athari ya upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule za Nonini na Juacali. Hali ya lugha ya Kiswahili ilidhihirishwa kutokana na upanuzi wa maana ulioshuhudiwa katika maneno teule ya Kiswahili yalivyotumika katika nyimbo teule zilizoimbwa na Nonini na Juacali. Katika mahojiano na watafitiwa wakuu maoni yafuatayo yaliibuka washiriki hawa walipoulizwa maoni yao kuhusiana na jinsi upanuzi wa maana katika nyimbo hizi teule unavyoathiri lugha ya kiswahili:

> Msailiwa 1
>
> "Kiswahili kama Kiswahili na kama lugha lazima kiwe na uwezo wa kustahimili mapigo ya namna hii. La sivyo haitakuwa lugha. Itaporomoka iwe si lugha tena na tunajua lugha zilizokufa. Kama lugha haina uwezo wa kustahimili mapigo na mitindo ya kawaida katika maisha na katika matumizi yake eeh itakuwa ni lugha hafifu. Na mimi najua kwamba Kiswahili ni lugha ambayo ina nguvu, inaweza kustahimili, itakuwa tu inajimudu katika uwepo wake kama lugha inayotumiwa na watu wengi."

Msailiwa wa kwanza anasisitiza anaposema *Kiswahili kama Kiswahili na kama lugha lazima kiwe na uwezo wa kustahimili mapigo ya namna hii. La sivyo haitakuwa lugha* kwamba hili ni pito la kimsingi katika uhai wa lugha na ni bainisho la Kiswahili kuwa lugha.

Msailiwa huyu wa kwanza ana mtazamo kwamba kuzuka kwa maana zaidi kunaiathiri kwa njia chanya lugha ya Kiswahili na kuifanya kuwa na hadhi katika jamii. Kulingana naye lugha inapata uhai kutokana na upanuzi wa maana za maneno unaotokana na matumizi ya maneno katika miktadha mbalimbali. Kwa mfano; neno *Kibao* kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) ni kifaa cha kuandikia kwa chaki au kalamu, kukalia, mpigo wa mkono kwenye uso au muziki. Katika nyimbo hizi hata hivyo neno hili lilipata maana ya wingi. Neno kibao pia ni nomino kwa kawaida lakini katika muktadha wa nyimbo hizi neno hili ni kivumishi kinachoshiria wingi. Hivyo, neno kibao lilipata maana zaidi za ile halisi ya kikamusi. Aidha, matumizi ya lugha yanayozua maana zaidi ndiyo yanayoikuza lugha. Maoni haya yanaoana na Boomhower (2005) anayedai kuwa lugha inapokua maana za maneno yake huweza kubadilika wakati mwingine na kuiathiri lugha yenyewe.

Msailiwa 2

Nyimbo hizi zinaiathiri lugha ya Kiswahili kwa sababu huvurugika maana sanifu za maneno. Tuna maana za maneno tunazojua ni sanifu ama mantiki. Tunapata kwamba neno ambalo tuseme limeandikwa katika kamusi sasa wao watavuruga neno hilo hadi neno lenyewe liwe lina maana ambayo haikuwepo hapa awali. Sasa utapata hata wanafunzi wenyewe ambao wamekulia katika kizazi cha kisasa huwa hawapati maana hizi asilia hasa katika mtihani. Wanatumia maana zile katika muktadha wa kimuziki.

Msailiwa alitambua kuwepo kwa maana zaidi za maneno hasa katika muktadha wa nyimbo teule aliposema *tuna maana za maneno tunazojua ni sanifu ama mantiki*. Kwa mujibu wa msailiwa huyu maana mpya zinazozuliwa katika matumizi ya maneno haya ya Kiswahili hasa kwenye nyimbo zinaivuruga lugha hasa maana inapozingatiwa. Anazidi kusema kwamba somo la Kiswahili linahitilafiwa na maana hizi mpya zilizozuliwa katika miktadha kama hii ya nyimbo. Msailiwa anaposema, *hata wanafunzi wenyewe ambao wamekulia katika kizazi cha kisasa huwa hawapati maana hizi asilia hasa katika mtihani,* anachukulia kwamba maneno yalivyotumiwa katika nyimbo teule na kuzua maana mpya yanawakanganya wanafunzi katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kwa mfano *Kuchota* kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) ni kuchukua sehemu ya vyowevu kama maji kutoka mahali fulani au kutaka kujua mawazo ya mtu kwa njia ya ujanja. Neno chota lina maana zifuatazo kulingana na muktadha wa wimbo 'mabeste damu' ni kule kumlaghai mtu au kumnyang'anya, kumwomba mtu ngono ama labda kumteka mtu kwa njia fulani. Katika wimbo 'We kamu' neno hili lina maana; kumteka mtu kihisia hasa kimapenzi au kumwomba mtu ngono. Neno hili liliwasilisha dhana za uasi na kuzua mtazamo hasi kwa misingi kwamba matarajio ya wanajamii kuhusiana na maadili yanahitilafiwa inapokisiwa kwamba mahusiano ya kihalifu na ngono yanatukuzwa. Hivyo, upanuzi wa maana unaiathiri lugha ya Kiswahili kwani inavuruga usanifu wake.

Msailiwa 3

"Natumai kwamba kuchipuka kwa maana hizi kutokana na neno moja maana yake kuvurugika inafanya maenezi ya Kiswahili yanatingwa na maendeleo ya Kiswahili yanatingwa tunapata sasa Kiswahili kinakuwa ovyo tu, watu wanatumia lugha viovyo hawanuii maana kusudiwa na wale watunzi wa kamusi ambayo ndio

> inayochukuliwa kuwa asilia. Sasa neno limevurugwa hata hujui maana halisi ni ipi. Kiswahili basi kitaishia kuwa lugha ya watu ovyo ambao hawajajipanga, hapa panakuwa hata na utata katika upangaji wa lugha, maenezi yake na maendeleo yake.”

Msailiwa huyu anachukulia kwamba matumizi ya lugha ya Kiswahili yanayozua maana zaidi yanaleta utata na hivyo kuvuruga mawasiliano hivi kwamba maana iliyokusudiwa isiwe imezuliwa. Kwa mfano *Mtoto* kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014) ni kiumbe kilichozaliwa hasa na mtu au mnyama, mtu mwenye umri mdogo au kitu kidogo kilichopachikwa kwa kingine kilicho kikubwa. Katika nyimbo hizi mtoto ni msichana aliye mrembo. Neno ‘mtoto’ lilipata maana zaidi ya ile ya kawaida inayojulikana hata katika mazungumzo. Msailiwa anaposema *sasa neno limevurugwa hata hujui maana halisi ni ipi*. Anamaanisha kwamba maana hizi zote za neno hili zikitumika pasipo kuzingatia miktadha, mawasiliano kwa kutumia maneno hayo yatavurugika na hivyo kuthibitisha maoni ya msailiwa huyu wa tatu.

Kulingana naye hitilafu katika mawasiliano inayotokana na hali ambapo neno lina maana nyingi kiasi cha maana iliyokusudiwa kutomfikia anayewasilishiwa ujumbe, ndio inayoifanya lugha hususan ya Kiswahili kusawiriwa kwa njia hasi. Mtazamo hasi kwa mujibu wa msailiwa huyu unaosababishwa na utata wa maana ndio unaishusha hadhi lugha ya Kiswahili. Maoni haya yanaoana na Sapir (1921) anayeonyesha nafasi ya lugha kimatumizi anaposema kwamba, wanadamu wanatawaliwa na lugha mahususi inayoishia kuwa chombo cha kujieleza. Hii ina maana kuwa lugha ilivyo chombo cha kupitisha maana, uamilifu wake hudhihirishwa na maana inavyosimbwa katika maneno.

Msailiwa 4

> "Tunavyojua ni kwamba lugha haijikiti katika kamusi kwamba maneno ya kamusi ndio yenye maana pekee yake katika matumizi. Tunapozingatia zaidi matumizi ya lugha jinsi watu wanavyotumia lugha katika jamii ndipo tunapoelekeza kipengele cha maana. Kwa hivyo unakuta kwamba baadhi ya maneno yaliyotumika na yakubalike kwa urahisi basi yataingizwa katika msamiati unaotumika na watu kwa kawaida. Watu huibua maana za maneno kulingana na jinsi yanavyotumika. Kwa hivyo utakuta kwamba mchango wa muziki huu wa kisasa ni ule wa kupanua maana asilia ya maneno katika lugha. Hata hivyo, kuna athari kwamba msamiati huu ibuka unaweza pia kutatanisha matumizi sahili ya Kiswahili kiasi cha kupata upotovu wa maana na wale wanaojifunza hasa wakiwa ni wale vijana chipukizi, wanaweza kuwa na mwelekeo tofauti wa maana ya maneno."

Msailiwa huyu anasema kwamba maana haiangaziwi kuegemea kamusi bali kwa kuzingatia namna ambavyo neno limetumika. Kwa mfano neno *Mbaya* kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) ni kivumishi kinachorejelea kitu kisichopendeza au kinachodhuru. Hata hivyo katika wimbo huu neno hili linarejelea kufurahia kitu kiasi cha kutoweza kueleza yaani kitu kupendeza sana. Japo kimesalia kivumishi neno hili katika muktadha wa wimbo unaleta dhana chanya tofauti na ile ya kawaida iliyo hasi. Hivyo neno hili lina maana zaidi ya ile iliyowasilishwa katika kamusi. Mfano huu unadhihirisha maoni ya msailiwa kwamba *tunapozingatia zaidi matumizi ya lugha jinsi watu wanavyotumia lugha katika jamii ndipo tunapoelekeza kipengele cha maana.*

Msailiwa huyu wa nne ameyakuza matumizi katika kufikia maana na kuchukulia kwamba maana katika lugha inaelekezwa na matumizi ya maneno katika lugha kuashiria dhana mbalimbali zinazowasilishwa jamii ilivyokubaliana katika matumizi ya neno hilo. Kwa

mujibu wa msailiwa huyu matumizi ya maneno katika nyimbo hizi teule yanayoibuka maana mpya yanachangia upanuzi wa maana ambao kwa maoni yake yanavuruga taratibu za maana na hivyo makuzi ya lugha. Aidha anaona lugha ya Kiswahili inayumbishwa kunapotokea utata wa kukisia maana ya neno fulani. Maoni haya yanathibitisha chukulio la Keysar (2007) anayesema kwamba utata upo kila mahali na wakati kwa sababu kila neno lina maana zaidi ya moja linaloweza kutokana na usemi wa kawaida. Hivyo kwake, msikilizaji anaweza kukanganywa akose kuelewa kile ambacho mzungumzaji anasema na kuhitilafisha mawasiliano miongoni mwao.

> Msailiwa 5
>
> "Lugha yoyote ile hukua na Kiswahili ni lugha changa sana na utakuta kwamba lugha ya muziki ina upekee wake. Lugha hii kama kuboronga sarufi na usanifu wa lugha lakini kimatumizi hasa kwa lengo la kuwasiliana ni muhimu sana maanake ni lugha nzito. Utakuta kwamba msamiati ambao unatumika katika muziki huu ni msamiati wenye picha pana zaidi ya yale yanayozungumziwa. Kwa mfano nyundo ni kifaa cha ujenzi tu lakini mpigo ule wa nyundo na zile ishara zinazoandamana na matumizi ya nyundo unapozipanua kitaashira na kuzielekeza katika tendo la kimapenzi utapata ule mpigo wa hali ya juu zaidi ukilinganisha na jinsi msanii atakavyozungumzia kwa kawaida mambo ya kimapenzi n.k. Kwa hivyo unakuta kwamba msamiati ule ni msamiati unaotumia…ninasema ni tamathali ya hali ya juu ya usemi. Ni msamiati wenye ishara kubwa na hujenga taswira/picha pana zaidi inayoweza kumpanulia na kumpa mtu maana halisi maana kimatumizi jinsi maneno hayo yanavyotumika."

Chukulio la msailiwa huyu ni kwamba makuzi ya lugha ya Kiswahili yanahimizwa japo matumizi ya lugha kwenye nyimbo katika ukiukaji wa kanuni za kawaida, yanahakikisha ujumbe umewafikia waliokusudiwa. Kwa mujibu wa msailiwa huyu anaposema *msamiati*

*wenye ishara kubwa na hujenga taswira/picha pana zaidi inayoweza kumpanulia na kumpa mtu maana halisi maana kimatumizi jinsi maneno hayo yanavyotumika*, maneno yanavyotumiwa katika nyimbo hizi yanazua maana mpya kando na maana za kawaida. Yaani maneno haya yanaashiria dhana zaidi ya zile asilia na maana kuishia kupanuka. Kulingana naye basi, maana inaweza kuzuliwa kutoka kwa matumizi ya maneno katika muktadha fulani. Kwa mfano,maana halisi za neno *Ua* kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu TUKI (2014) ni sehemu ya mmea, mzunguko wa boma, au kitenzi kinachorejelea kuondoa uhai. Katika nyimbo hizi hata hivyo, neno hili linarejelea kitendo cha kupendeza, kufurahisha au kuibua zile hisia za kingono. Katika misingi hii msailiwa huyu anaashiria kuwa lugha inakua kutokana na kupanuka kwa maana kunakothibitishwa katika nyimbo teule ambako maneno yanayowasilisha dhana zaidi ya kawaida yametumika. Mtazamo huu unathibitishwa na Short na Leech (1981) wanavyosema kuwa, lugha ni pana kiasi cha kuruhusu uzalishaji wa maana zaidi ya ile ya kawaida.

> Msailiwa 6
>
> “Ninafikiri lugha ya Kiswahili inakua kwa vyovyote vile. Huenda ni maendeleo …. Huenda maneno mengine yana maana zaidi zilizozuliwa upya. Kwa hiyo, neno linaweza kuwa na maana tofauti na ile asilia. Wakati huohuo huenda kuna athari mbaya kwa sababu wanaojifunza lugha hii ya Kiswahili huenda wakachanganyikiwa kuhusiana na maana ya maneno na tunapata mtu anaweza kutaka kutumia neno lakini akaishia kutumia neno vibaya bila kujua analitumia hilo neno vibaya kwa kukosa kujua maana. Hii ni kwa sababu huenda neno hilo lina maana nyingine tofauti katika nyimbo hizi za kizazi kipya. Kwa hiyo tuna vipengele hivi viwili kwamba lugha huenda ikawa na wakati huohuo ikawa hatarini hasa upande wa wanafunzi wachanga wa lugha hii.”

Msailiwa huyu kama wengine anakubaliana na wenzake kwamba upanuzi wa maana unakuza lugha ila kulingana naye kuzuliwa kwa maana mpya za maneno kunasababisha utata kutokana na jinsi neno lilivyotumika kwani maana inayokusudiwa huenda isimfikie mpokezi wa ujumbe hasa katika nyimbo hizi za kizazi kipya. Kwa mfano neno *Roga* kikamusi ni kitenzi chenye dhana ya kudhuru kwa uchawi lakini katika nyimbo hizi neno hili lilimaanisha pendeza, furahisha, maliza yaani teka makini ya mtu kwa mujibu wa washiriki. Matumizi ya neno hili hasa kwa kuzingatia pia kuwepo kwa maana mpya za neno hili yanaweza kuzua utata pale ambapo maana aliyokusudia mzungumzaji kuwa tofauti na ile maana anayofahamu mpokezi wa neno hili moja. Anaposema *lugha huenda ikawa na wakati huohuo ikawa hatarini hasa upande wa wanafunzi wachanga wa lugha hii*, mtazamo wake ni kwamba, japo lugha inakuzwa kwa maana zaidi, lugha hiyo vilevile yaweza kuwa hatarini uwepo kutokana na utata unaozuliwa na matumizi tofauti tofauti ya maneno fulani.

Watafitiwa wakuu waliokuwa wataalamu wa lugha wametoa mitazamo mbalimbali kuangazia suala la upanuzi wa maana na athari yake kwa lugha ya Kiswahili.Wasailiwa hawa wote wanakubaliana kwamba lugha ya Kiswahili inaathiriwa kunapozuka maana zaidi na athari yenyewe ni kuwili. Kulingana na wasailiwa hawa, lugha ya Kiswahili inaonekana ikikua na kunawiri zaidi katika misingi kwamba upanuzi wa maana unapelekea kupandisha kiwango cha matumizi ya lugha kwa jumla ikizingatiwa kwamba lugha asemavyo Adedimeji (2006) akinukuliwa na Chibueze na wezake (2017) kwamba injini ya lugha ni maana na kwa hakika kiini cha lugha ni kuzua au kuwasilisha maana.

Msailiwa wa pili alisema, *“kwangu naona maana hizi yanachangia ujenzi wa msamiati wa lugha.”* Chukulio hili chanya pia linatokana na mtazamo kwamba japo upanuzi wa maana unaonekana kuitikisa lugha, lugha yenyewe inapata nguvu alivyosema msailiwa wa kwanza kwamba*,” Wakati mwingine unapoona kwamba lugha ni kama inapotoka eeh sasa ndio nguvu zake zinatokea pale kwenye kupotoka huko. Ikitoka kule ikija huku inapewa nguvu zaidi.”*

Kwa misingi hii inaweza kuchukuliwa kwamba lugha ya Kiswahili itaishia kupata nguvu kujengeka na kunawiri kuliko swali. Kimsingi, ilidhihirika kwamba lugha inakua kutokana na upanuzi wa maana za maneno na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Ikizingatiwa kwamba nyimbo ni njia muhimu ya jamii kupata ujumbe kupitia kwa wasanii, jinsi lugha ilivyotumiwa itachangia ufasiri wa maana. Boomhower (2005) anadai kuwa lugha inapokua maana za maneno yake huweza kubadilika wakati mwingine na kuiathiri lugha yenyewe. Lugha hiyo yaweza kusalia hai, ikarekebika na hata kukua zaidi. Turner (2011) anathibitisha hili anapohimili kwamba neno halimaanishi kitu kimoja katika kila mazingira ambapo neno hilo limetumiwa. Matumizi kulingana na kanuni maalum ndiyo yanaweza kuwajibikia mawasiliano kwa sababu lugha ni njia ya mawasiliano.

Mkondo mwingine kando na makuzi ya msamiati ni ule unaohusu uwasilishaji wa ujumbe na kueleweka kwa kusudi la ujumbe wenyewe hasa na walionuiwa kuupokea ujumbe ule kwa mujibu msailiwa wa tano; *“kimatumizi hasa kwa lengo la kuwasiliana ni muhimu sana maanake ni lugha nzito. Utakuta kwamba msamiati ambao unatumika katika muziki huu ni*

*msamiati wenye picha pana zaidi ya yale yanayozungumziwa."* Kutokana na maoni haya, athari ya upanuzi wa maana kwa lugha ya Kiswahili inaangaziwa katika kipengele cha matumizi ya maneno na maana inavyoibuka kutegemea matumizi katika nyimbo za kizazi kipya. Norwich (1998) anasema kwamba neno humaanisha tu kazi yake katika matumizi ya ujumbe. Hivyo, lugha ni kifaa cha kutekeleza majukumu mbalimbali na kinachobadilika kutegemea mahitaji ya watumizi wake. Kulingana na Taiwo (2001), lugha ni tukio la kijamii. Kauli hii ina maana kuwa watu huchagua maneno yanayoweza kupitisha kwa njia bora maana wanayojaribu kuwasilisha.

Washiriki katika majadiliano kimakundi walichangia suala la upanuzi wa maana na athari yake kwa lugha ya Kiswahili.Baadhi yao walisema,

> **Mshiriki A**: kwangu mimi naona maneno mengine yanapotosha watu. Tuseme Watoto watakaposikia ngoma hizi yaani nyimbo hizi za Juacali, Nonini na wengine ambazo zimejaa maneno haya yenye maana zaidi kulingana na nyimbo zenyewe watakuwa wanapotoka kwa sababu wakienda kule labda ninafunza wanafunzi kuandika insha kwa mfano; utapata mwanafunzi anaandika maneno akimaaanisha vingine vilivyo tofauti na maana halisi.Tuseme kwa mfano anasema buda alinituma sokoni nikamletee vocha….Sasa unajua kama mwalimu sitaelewa amemaanisha nini kwa sababu huenda amemaanisha mzazi anapotumia neno buda lakini neno hili maana yake halisi katika lugha ya Kiswahili ni tofauti kwa hiyo itakuwa inakanganya sana mawasiliano katika Kiswahili sanifu na labda itakuwa tu inapotosha kwa jumla.

> **Mshiriki A (2)**: maana inabadilika na kuongezeka. Kuna wale labda wanaelewa sana, kuna wale labda wanapotoka. Wale ambao hawawezi tuseme kutenganisha maana za kisanii na maana sanifu. Kuna wale wanapotoka kuna wale watajua huyu amemaanisha hivi sababu ameimbia mahali hapa na amekuwa na watu hawa. Labda watajua huyu alitumia maneno haya kwa sababu fulani na pale pengine labda angetumia kivipi kwa maana nyingine.

Mshiriki A (kundi la kwanza) alisema *naona maneno mengine yanapotosha watu* huku wa A (kundi la pili) akisema *maana inabadilika na kuongezeka* kuonyesha jinsi lugha ya Kiswahili inavyoathirika maana mpya zinapochipuka kutokana na matumizi ya maneno katika muktadha wa nyimbo teule. Kutokana na maoni haya, ni wazi kwamba maana zaidi inaiathiri lugha ya Kiswahili kwa kuzua utata anavyothibitisha mshiriki anaposema *hawawezi tuseme kutenganisha maana za kisanii na maana sanifu.* Lugha ya Kiswahili inaonekana kupotoka kwa mtazamo wa mshiriki A (kundi la kwanza) kwa misingi kwamba kunaibuka maana tofauti inayochukuliwa na wengine kuwa maana za kisanii. Mtazamo huu unaoana na wa Ullman (1957) ambaye anashikilia kwamba mabadiliko ya maana ya neno yanaathiri namna ambavyo neno hilo linahusiana na mengine. Lugha huishia kubadilika kwa misingi hii kwa maana kimatumizi zinategemea muktdha ambao unaweza kuzuka popote watumiaji wa lugha walipo.

Mitazamo kuhusiana na athari kulingana na wasailiwa ilikuwa ni mseto hivi kwamba machukulio ni chanya lakini pia hasi. Kwanza, ilibainika kwamba lugha ya Kiswahili inaathirika kwa kuvurugwa na kuibua shaka kuwa huenda vizazi vijavyo na watakaojifunza lugha hii siku zijazo watatatizika hasa kwa kurejelea matumizi. Aidha pana uwezekano wa vizazi hivi kupoteza mwelekeo. Msailiwa wa sita alisema, *wanaojifunza lugha hii ya Kiswahili huenda wakachanganyikiwa kuhusiana na maana ya maneno na tunapata mtu anaweza kutaka kutumia neno lakini akaishia kutumia neno vibaya bila kujua analitumia hilo neno vibaya kwa kukosa kujua maana. Hii ni kwa sababu huenda neno hilo lina maana nyingine tofauti katika nyimbo hizi za kizazi kipya.*

Msailiwa wa pili alisema, *utapata hata wanafunzi wenyewe ambao wamekulia katika kizazi cha kisasa huwa hawapati maana hizi asilia hasa katika mtihani. Wanatumia maana zile katika muktadha wa kimuziki.*"

Huku msailiwa wa nne akisema, *Hata hivyo, kuna athari kwamba msamiati huu ibuka unaweza pia kutatanisha matumizi sahili ya Kiswahili kiasi cha kupata upotovu wa maana na wale wanaojifunza hasa wakiwa ni wale vijana chipukizi, wanaweza kuwa na mwelekeo tofauti wa maana ya maneno.*"

Pili, juhudi za maenezi na maendeleo ya Kiswahili zilikuwa zatingwa kutokana na mtazamo hasi unaoibuka kutokana na upanuzi wa maana. Msailiwa wa tatu alisema, *"Kiswahili basi kitaishia kuwa lugha ya watu ovyo ambamo hawajajipanga, hapa panakuwa hata na utata katika upangaji wa lugha, maenezi yake na maendeleo yake."*

Chukulio la tatu, ni kwamba lugha ya Kiswahili huvurugwa na kutikiswa hasa maana zaidi zinapochipuka hivi kwamba utata hauwezi kuepukika. Maoni haya yanaoana na Lyons (1979) anayeeleza kwamba maana za neno kuzidi moja ni kisababishi cha utata. Hivyo, utata huzuka kutokana na maneno kuwa na maana nyingi. Utata wa kimaana na hivyo mwelekeo wa vizazi vijavyo kulingana na baadhi ya wasailiwa wa pili na wa nne unaonekana kuangaziwa.

Msailiwa wa pili

> “Tunapata kwamba neno ambalo tuseme limeandikwa katika kamusi sasa wao watavuruga neno hilo hadi neno lenyewe liwe lina maana ambayo haikuwepo hapoawali. Sasa utapata hata wanafunzi wenyewe ambao wamekulia katika kizazi cha kisasa huwa hawapati maana hizi asilia hasa katika mtihani. Wanatumia maana zile katika muktadha wa kimuziki.”.

Msailiwa wa nne.

> “...kuna athari kwamba maana hizi ibuka zinaweza pia kutatanisha matumizi sahili ya Kiswahili kiasi cha kupata upotovu wa maana na wale wanaojifunza hasa wakiwa ni wale vijana chipukizi, wanaweza kuwa na mwelekeo tofauti wa maana ya maneno.”

Maoni haya yanaungwa mkono na Massamba (1987) anayesema kwamba maana inaweza kuibuka kutokana na mazoea ya matumizi yake kando na maendeleo au mabadiliko yanayotokea maishani. Maneno teule ya Kiswahili yakizidi kutumika yalivyotumika katika nyimbo teule zilivyoonekana katika utafiti huu, kuna uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa vurugu la lugha kwani vizazi vijavyo vinaweza kupokezwa maana hizi na hivyo lugha ya Kiswahili kuchukua mkondo mwingine kimaana ikizingatiwa kwamba maana ya neno ni matumizi yake. Utafiti huu ulithibitisha makisio ya Njogu na wenzake (2006) kwamba neno linalotumiwa katika muktadha mmmoja huweza kupanuliwa ili litumike katika muktadha mwingine. Hivi ni kusema kwamba neno hilo linaweza kutoa maana tofauti na ile inayojulikana au kuzoeleka. Hali hii ya ukengeushi wa maana inaweza kuzuia ufanisi wa mawasiliano kwani kutakuwa kumeibuka mtindo mwingine wa lugha unaoeleweka kati ya vizazi fulani katika jamii.

Halliday (1964) akinukuliwa na Kung'u (2006) anasema kwamba lugha inakua kupitia tajriba za kijamii wala si katika ombwe, na papa hapa inapata msingi, sura na ruwaza zake. Uamilifu mkubwa wa lugha ni matumizi yake kama tukio la mawasiliano baina ya watu. Aidha, tamko la lugha haliwezi kueleweka ipasavyo ila kwa kuhusishwa na muktadha. Kwa mujibu wa Wittgenstein (1963), lugha ni njia ya kujihusisha kwa ulimwengu na jinsi ulimwengu huo ulivyosawiriwa. Hivyo, lugha ni njia ya kueleza kinachotolewa katika ulimwengu huo.

Kwa kuhitimisha, ni wazi kwamba upanuzi wa maana unavyoweza kuiathiri lugha ya Kiswahili bila shaka ni jambo lianalotarajiwa na kushabikiwa ila kwa hofu ya kuvuruga lugha kwa upande mwingine.

### 4.3 Utata katika mawasiliano kutokana na upanuzi wa maana

Utafiti huu ulitathmini utata katika mawasiliano kutokana na upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili yalivyotumika katika nyimbo teule zilizoimbwa na Nonini na Juacali kwa kuonyesha jinsi ambavyo kuzuliwa kwa maana zaidi kunavyoweza kuzua utata na hatimaye kuvurugika kwa mawasiliano. Yafuatayo ni maoni ya wasailiwa kuhusiana na suala hili kwa kuzingatia tofauti katika maana kimatumizi:

**Msailiwa 1**

> Kuna uwezekano mkubwa kwamba maana inayokusudiwa na mzungumzaji unaweza kupoteana ndio maana swali lako la kwanza lilikuwa likizungumzia watu kuwa na maana tofauti za maneno fulani. Kwa hivyo inamaanisha kwamba hitilafu katika mawasiliano ipo. Kumbuka kwamba mwimbaji huenda amemaanisha upendo au mapenzi ilhali wasikilizaji wawe wanapata maana ya ufisadi. Hivyo, maana kwa hakika itapotea wakati wowote ambapo hatuna ile maana iliyokusudiwa na mzungumzaji. Ni wazi kwamba maana itapotea.

Msailiwa wa kwanza anaeleza jinsi uwepo wa maana zaidi unavyoweza kuhitilafiana na mawasiliano ambapo mpokezi wa ujumbe atashindwa kupata ujumbe ulivyokusudiwa na mwasilishaji. Kwa mfano neno *chota* kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2014) ni kuchukua sehemu ya vyowevu kama maji kutoka mahali fulani au kutaka kujua mawazo ya mtu kwa njia ujanja. Katika nyimbo teule neno chota limezua maana za kumlaghai mtu au kumnyang'anya mtu, kumwomba mtu ashiriki ngono na anayeimba, kumteka mtu kwa njia fulani kama vile kihisia hasa kimapenzi. Hivi, neno 'chota' lilivyotumika limepata maana zaidi. Sasa, iwapo mpokezi wa ujumbe ambamo neno chota limetumika anamaanisha kitu tofauti na ile maana anayokusudia kuwasilisha mzungumzaji basi mawasiliano yatakuwa yamevurugwa. Anaposema *maana kwa hakika itapotea wakati wowote ambapo hatuna ile maana iliyokusudiwa na mzungumzaji* ni dhahiri kwamba mchakato wa mawasiliano umekosa kufanikiwa. Kutokana na maoni haya ujumbe ulionuiwa kupitishwa kwa mpokezi unaweza kutomfikia mpokezi iliyokusudiwa au hata kupotea. Kulingana na msailiwa huyu ujumbe unapokosa kumfikia mpokezi ulivyokusudiwa ina maana kwamba mawasiliano yamevurugwa.

Mtazamo wa msailiwa huyu wa kwanza ni kwamba maana ni kiini cha mchakato wa mawasiliano. Maoni yake yanathibitisha anavyosema Turner (2011) kwamba maana ya neno si moja tu neno hilo linapotumiwa wala wanachomaanisha watumizi wa maneno hakisalii sawa kila wakati maneno haya yanapotumiwa. Maana zikiwa zaidi kuna uwezekano kwamba mpokezi wa ujumbe na mwasilishaji wote wana maana zao tofauti kutokana na matumizi. Tofauti hizi katika mawasiliano kutokana na maana zaidi ndiyo huchukuliwa kuwa utata.

**Msailiwa 2**

> Ni kweli kuna kuvurugika kwa mawasiliano na hali hii hutokea kwa sababu hizi nyimbo si lazima zisikizwe katika dancehall pekee. Nyimbo hizi zinaweza pia kusikizwa hata nyumbani vijana hao wanapokuwa wameketi na wazazi wao. Inaweza kuwa unasafiri ukakuta gari limebeba watu wenye umri wa makamu pekee hamna vijana. Sasa unajua nyimbo kama hizi zinapochezwa wanajaribu kusikiza wanaona neno fulani limetumika kwa njia ambayo si ile ya kawaida kwa hivyo hapa tunaona kwamba kuna kuvurugika kwa mawasiliano. Hata hivyo vijana mahali popote wakiwa nyumbani, dancehall, wanaosoma au hata wanaposafiri hizo nyimbo zinawaingia na wanaelewa kile ambacho kinamaanishwa moja kwa moja.

Huu ni mtazamo kwamba utata katika mawasiliano unasababishwa na maana zaidi ikizingatiwa kwamba wanaosikiliza nyimbo za kizazi kipya si mashabiki ambao ni vijana pekee anavyothibitisha kwa kusema *Nyimbo hizi zinaweza pia kusikizwa hata nyumbani vijana hao wanapokuwa wameketi na wazazi wao*. Hivyo maana inayopokelewa huenda isiwe ile inayokusudiwa. Kwa mujibu wa Mbatiah (2012) mawasiliano yanavurugwa na kuzuka kwa maana zaidi. Chukulio hili linathibitishwa na msailiwa huyu wa pili anayedai kwamba tofauti katika fasiri za maneno yaliyotumika katika nyimbo za kizazi kipya zinazowafikia watu wengi tu inapelekea utata kwani kinachokusudiwa huenda ikawa tofauti na kinachopokelewa kama maana. Msailiwa anasema kwamba *unajua nyimbo kama hizi zinapochezwa wanajaribu kusikiza wanaona neno fulani limetumika kwa njia ambayo si ile ya kawaida kwa hivyo hapa tunaona kwamba kuna kuvurugika kwa mawasiliano*. Nadharia ya maana kimatumizi ya inashikilia kuwa neno halimaanishi kitu kimoja katika kila matumizi yake. Matumizi kulingana na kanuni maalum ndiyo yanaweza kuwajibikia mawasiliano kwa sababu lugha ni njia ya mawasiliano. Maneno hupata maana kutoka kwa matumizi. Hata hivyo, wanachomaanisha watumizi wa maneno hakisalii sawa kila wakati

maneno haya yanapotumiwa. Kwa misingi hii kwa mujibu wa msailiwa huyu wa pili kuna mahusiano moja au zaidi ya maneno yaliyotumiwa yalivyotumiwa katika nyimbo teule na hivyo kutoa nafasi ya kuvuruga mawasiliano kati ya waimbaji na wapokezi wa ujumbe katika nyimbo.

**Msailiwa 3**

> Ni kweli  mawasiliano yanaweza kuvunjika na hata kuleta vita miongoni mwa wasikilizaji maanake kuna wakati nimemsikiza mzee fulani akihojiwa akiulizwa ,je muziki wa kisasa unaukadiria vipi? sasa yeye akawa anazungumzia mambo ya kupiga randa,kupiga nyundo  na juala.Yeye anachukulia maneno haya katika muktadha wa kawaida maanake kila mtu anajua karatasi ya kubeba bidhaa au vbitu kwenda sokoni.Sasa yeye anapoulizwa kwamba watu watumie juala ili wasipate taabu wanapobeba vitu vyao ama wanaposafiri na vitu vyao. Fasiri yake ni tofauti sana na jinsi ilivyokuwa katika wimbo ule. sasa yeyekatika muktadha wa kawaida unaweza kumpata anazungumzia mambo haya ,hali inayomweka katika aibu maanake yeye fasiri anayotoa katika muktadha huu ni tofauti na jinsi mwimbaji alivyokusudia.Kwa hivyo unakuta kwamba hali kama hizi zinaweza kuzusha aibu au vilevile zizushe mtafaruku katika mawasiliano kiasi cha watu kukuona wewe pengine ni mpumbavu unayezungumzia vitu ovyoovyo katika jamii ama huna heshima katika lugha yako.Ingawa kwenye muziki unavyoimbwa na maneno yale yanapotamkwa watu huchangamkia lakini katika mazungumzo ya kawaida yanaweza kuleta matatizo.

Msailiwa huyu anasema kwamba kuwepo kwa maana zaidi kunaweza kusababisha utata na kuhitilafisha mawasiliano miongoni mwa wapokezi wa ujumbe. Tofauti katika fasiri za maana za maneno yanazuia ujumbe uliokusudiwa kuwafikia wasikilizaji na uwezekano wa kuharibu hata kuvunja mahusiano kutokana na hali ambapo wahusika wanahitaji kuwasiliana. Maoni ya msailiwa huyu wa tatu yanaoana na mtazamo wa Miller na wenzake (2017) katika tathmini yao ya ufasiri wa ishara za emoji. Kulingana nao maana

zinavyozuliwa kutoka kwa ishara za emoji mahusiano baina ya maana na muktadha yanabainika ila wingi wa fasiri za maana za ishara zile unasababisha utata na kuvuruga mawasiliano kwa kuzitumia ishara hizo za Emoji. Vivyo hivyo, msailiwa anavyosema *Fasiri yake ni tofauti sana na jinsi ilivyokuwa katika wimbo ule,* inamaana kwamba neno la kawaida linapofasiriwa watu tofauti, kunatukia utata iwapo kila moja ana fasiri yake ya neno hilo lilivyotumika katika muktadha fulani. Turner (2011) pia anathibitisha anaposema kuwa japo maneno hupata maana kutoka kwa matumizi wanachomaanisha watumizi wa maneno hakisalii sawa kila wakati maneno haya yanapotumiwa.

**Msailiwa 4**

> Ni kweli. vijana hawa wanaishi katika maeneo tofautitofauti sasa unaweza ukapata maana ya neno katika eneo fulani ni tofauti na maana ya neno lenyewe katika eneo jingine. Watajifanya tu kwamba wamepata ujumbe ilhali fasiri yao ni tofauti kwa sababu mtindo huu wa lugha katika muziki huwa si sanifu. Watu wa eneo fulani wanazua maana yao wengine katika eneo jingine wakibuni yao. Sasa wakizua maana hivyo wanachukulia kwamba wamepata ujumbe lakini ni kieneo wala si fasiri ya jumla.

Msailiwa huyu wa nne alithibitisha tukio la utata katika mawasiliano lakini katika mwanga wa tofauti za kimaeneo. Kulingana naye kwa kuzingatia kwamba maana ipo katika matumizi anavyohimili Turner (2011) kwamba maneno hupata maana kutoka kwa matumizi, kila anayetumia maneno huwa anawasilisha dhana fulani ambayo huenda ikawa tofauti na ile ya kawaida inayojulikana. Msailiwa anasema *wanaishi katika maeneo tofautitofauti sasa unaweza ukapata maana ya neno katika eneo fulani ni tofauti na maana ya neno lenyewe katika eneo jingine.* Kwa mujibu wamsailiwa huyu, tofauti za kimaeneo zinatarajiwa kuibua fasiri tofauti za maana za neno fulani na hivyo kusababisha utata watu hawa wanaotoka

maeneo tofauti wanapotangamana na kutumia neno lilelile moja. Maoni haya yanaoana na mtazamo wa Uings (2008) anayechukulia utata kuwa hali ambapo pana maana zaidi ya moja au uwazi wa kufasiriwa kwa njia zaidi ya moja. Hivyo, utata upo kwa misingi ya fasiri tofauti kutokana na hali ya kuwa katika maeneo tofauti yenye machukulio tofauti ya maneno yanayotumiwa.

**Msailiwa 5**

> Kweli kwamba mara nyingi na sio wakati mmoja tu tuseme asilimia 30 ya watu wanaotumia maneno haya katika nyimbo hizo ndio hupata ujumbe lakini asilimia 70 ya watazamaji au wasikilizaji hupotoka yaani hawapati mantiki kabisa. Kuna watu watakaposikia neno kwa kurejelea misingi ya masomo wanaweza kulifasiri neno hilo kwa njia tofauti kabisa. Lakini kuna wale ambao labda kwa kukosa nafasi ya kwenda shule ama kiwango duni cha masomo wanaweza kupata maana tofauti basi neno moja linalotumika katika nyimbo linaweza kuzua maana nyingi tofauti tofauti.

Maoni ya msailiwa huyu wa tano kuhusiana na suala la utata katika mawasiliano yanabainisha maana zaidi inavyozuliwa kwa kuzingatia mtazamo kutokana na vigezo vinavyochangia ufasiri wa maana katika jamii ujumbe unapowasilishwa. Kwa mujibu wa Turner (2011), kila mtumizi wa neno fulani anaweza kumaanisha kitu tofauti kwa kuwa na hisia tofauti na mawasiliano yakawa magumu au hata kutowezekana kabisa. Kwa mtazamo wa msailiwa, mwasilishaji wa ujumbe hasa yule msanii hutumia lugha kwa njia tofauti na ile ya kawaida inayomwezesha mpokezi wa ujumbe wake kuibua taswira yenye nguvu zaidi akilini mwake.

**Msailiwa 6**

> Bila shaka.Kuvurugika kwa maana ni kwamba labda msikilizaji anayehusika eh si mmoja wa lile kundi- lugha ,sijui kama tunaelewana.Maanake hata tunapozungumza tuna makundi lugha mbalimbali kwa hivyo kama unasikiza muziki ambao labda ni wa umri fulani, labda msikilizaji anayehusika eh si mmoja wa lile kundi- lugha you know you are lost.So huko ndiko kuvurugika sasa kwa mawasiliano au maana kwa sababu mwimbaji anapoimba anasikizwa na watu wengi; wale ambao wapo katika kundi-lugha lake na wale ambao labda hawapo.Kwa hivyo, kuna tena labda ambaye haelewi ,lazima aulize,afunzwe au ajizoeshe.

Kulingana na msailiwa huyu wa sita utata katika mawasiliano unasababishwa na maana zaidi katika mwanga wa tofauti katika matumizi ya lugha miongoni mwa wanajamii. Kutokana na namna ambavyo neno limetumiwa kupitisha ujumbe miongoni mwa kundi fulani la wanajamii neno lenye maana ya kawaida tu linaweza kuibua maana zaidi hasa kwa walio nje ya kundi hilo na hivyo kuzua utata kutokana na fasiri tofauti za maana ya neno hilo moja. Kutokana na mhimili wa nadharia ya maana kimatumizi kwamba maana ya neno ni matumizi yake neno moja linaweza kuzua maana zaidi katika muktadha mmoja tu na hivyo. Kwa misingi hii, kila mtumizi wa neno fulani anaweza kumaanisha kitu tofauti kwa kuwa na hisia tofauti na mawasiliano yakahitilafiwa. Kwa mfano neno kama vile *kaa* lenye maana nyingi kulingana na kamusi; kipande cheusi cha kuni, mnyama wa majini, kitenzi kinachorejelea kitendo cha kuweka makalio mahali fulani kama kitini hivi, kuwa na maskani mahali, kuwa mahali kwa muda fulani, kutumika kwa muda mrefu na kupendeza. Katika muktadha wa nyimbo neno lina maana ya kufanana na kitu. Neno hili lenye maana nyingi tu linapotumiwa hata katika mazungumzo, mpokezi wa ujumbe anaweza kukosa ujumbe kwa sababu huenda maana iliyokusudiwa ni tofauti na anavyochukulia yeye. Mtazamo huu

unaoana na Tambunan (2009) aliyebainisha utata kutokana na maana zaidi ya maneno ulivyovuruga mawasiliano na kuwafanya wasomaji kushindwa kupata maana iliyokusudiwa.

Wasailiwa hawa wote walikubaliana kwamba kuna uwezekano wa mawasiliano kuvurugika kutokana na maana kusudiwa kufasiriwa vinginevyo au kupotea. Keysar (2007) anasema kwamba mawasiliano yanachukuliwa kufanikiwa ikiwa mwasilishaji wa ujumbe na mpokezi wa ujumbe huo wana uelewa au fasiri moja ya kile wanachozungumzia. Anazidi kuhoji kwamba watu wengi hudhania kuwa wamewasiliana na wenzao kwa kutumia lugha iliyoeleweka kwao bila kugundua kwamba kuna utata wa maana ya ujumbe kwa sababu wanavyofasiri wao sivyo wanavyofasiri ujumbe huo huo. Chukulio hili linaungwa mkono na Uings (2008) anayesema kwamba wahusika katika mawasiliano wanachanganyikiwa na kuna kuvurugika kwa mawasiliano ikizingatiwa kwamba maneno yanaweza kufasiriwa kwa namna zaidi ya moja. Marge (2015) anasema kuwa kutowasiliana kunazingira kutoelewana kunakotokea pale ambapo msikilizaji anafasiri ujumbe kwa njia ambayo si sawa na kile alichokusudia msemaji japo msemaji anaamini kwamba mawasiliano yamefanyika kwa kiwango fulani.Hivi,ufasiri hauoani na makusudio ya ujumbe.Utafiti huu unakubaliana na Satlin (2014) anayehoji kuwa uwezekano wa kutowasiliana na kuvurugika kwa mawasiliano unasababishwa na utata unaojikita katika uwezo wa kuwepo kwa dhana kwamba kuna miktadha mingine ya matumizi ya maneno tena kunawiri katika hali hii.

Ruby (1962) anachukulia kwamba utata ni matumizi ya neno moja kuwasilisha maana zaidi. Chukulio hili linathibitisha wazo la Wittgenstein (1963) kwamba maana ya neno ni matumizi yake katika lugha na hivyo maana kulingana na mtumizi yaweza kuwa tofauti na ile inayofahamika kwa mpokezi wa ujumbe. Tofauti katika maana kutokana na matumizi ya neno yanayochukuliwa kuwa yasiyo ya kawaida, anavyosema Mbatiah (2012) yanaweza kuvuruga mawasiliano

Hali ya utata wanavyofafanua Hurtford na Heasely (1982) kwamba maneno yanatatanisha ikiwa yana maana zaidi ya moja ilithibitishwa katika utafiti huu. Kulingana nao neno linakuwa lenye utata ikiwa lina maana zaidi ya moja. Kwa mfano neno *katika* ni kihusishi kinacholeta dhana ya kitu ndani ya kitu au mahali, kipindi fulani cha wakati, kutengeka kwa kitu fulani na kusababisha kuwepo na vipande au sehemu ya kitu hicho. Kwa mujibu wa nyimbo hizi neno 'katika' linamaanisha sakata densi au kufurahia tu nyimbo kwa kunengua sehemu za mwili, kuumizwa, sikia utamu, cheza kwa kunengua, kuwa na hisia ya kutosheka, pamoja na kushiriki ngono. Hivyo, neno *katika* inavyoonekana kuwa na maana hata zaidi kutokana na matumizi yake katika nyimbo teule linazua utata katika mawasiliano.

Mtazamo mwingine ulioibuka kuhusiana na utata na mawasiliano ni mahusiano baina ya watumizi wa lugha ni kuathirika kwa utangamano baina ya wanajamii watumizi wa lugha hususan Kiswahili. Kwa maoni ya msailiwa wa nne,*labda msikilizaji anayehusika si mmoja wa lile kundi- lugha…Kwa hivyo kuna tena labda ambaye haelewi, lazima aulize, afunzwe au ajizoeshe.* Kwa misingi kwamba lugha inavyotumika katika jamii ni tofauti kutegemea

watumizi, kunaibuka suala la kundi lugha. Maana za maneno kimatumizi huweza kuzuka zaidi na hivyo kuhitilafiana na mawasiliano hasa miongoni mwa wanajamii zungumzi walio katika makundi lugha tofauti. Hii ni kwa sababu kama asemavyo Ullman (1994), maneno yanavyotumiwa katika miktadha tofautitofauti na wazungumzaji hutofautiana katika maana wanazonuia kuwasilisha.

Washiriki katika majadiliano kimakundi walikuwa na maoni mbalimbali kuhusiana na utata katika mawasiliano katika mwanga wa athari kwa lugha ya Kiswahili:

> **Mshiriki C (kundi 2)**: neno kama buda sasa kwa Kiswahili tunajua ni mzee ambaye hana meno halafu tunapata maana ya baba. Sasa itakuwa kwamba mahali palipotolewa maelezo ya maana ya baba pia pawe na kisawe kama buda na mahala pa neno buda kulikuwa na tu na maelezo. Kimsingi si unaona upo utata.
>
> **Mshiriki B**: kabisa mawasiliano yanaweza kuvunjika yakawa hayapo.Hii ni kwa sababu tunahesabu kuwa mtu amewasiliana na mwenzake iwapo anayepokea ujumbe amemeelewa kilichomaanishwa. Sasa ikiwa yeye anapata maana nyingine ambayo si sawa na yule anayezungumza hapo tunachukulia kwamba mawasiliano hayajakamilika. maana zinazotokana na jinsi maneno yalivyotumiwa katika nyimbo hizi zitatatanisha hasa ikiwa watu ni wa umri tofauti kwa sababu kijana na mzee kwa mfano watatumia neno moja lakini wanamaanisha vitu tofauti katika mazungumzo yao hivyo hawataelewana.
>
> **Mshiriki A (kundi 1)**: kwa kweli mawasiliano yanavurugika pakubwa kutokana na maana zaidi zinazoibuka katika mazingira mbalimbali ambamo maneno yanatumiwa.Hii ni kwa sababu ya uwezekano wa watu kumaanisha vitu tofauti kwa neno moja.
>
> **Mshiriki E (kundi 1)**: kwa kweli ukitumia maana kama hii ya kuiva kwa mazingira ya wazungumzaji wa lugha walio wachanga huenda wakachukulia maana ilivyo ilhali huenda ulimaanisha kitu fiche kwa hiyo maana hizi zaidi ambazo zinaonekana pia kuwa fiche zitatumika kurejelea mazingira na kimsingi mtu ambaye atakuelewa kikamilfu unavyokusudia kama maana.

Washiriki hawa walibainisha kwa mifano jinsi utata katika mawasiliano yanavyosababishwa na kuwepo kwa maana nyingi za neno moja ambalo huenda likatumika. Kulingana nao maana anayokusudia mwasilishaji wa ujumbe ikiwa tofauti na ile maana inayopokelewa kwa mwasilishiwa basi mawasiliano yatavurugika. Aidha kuzua maana fiche kutokana na maneno yanayochukuliwa kuwasilisha dhana za kawaida kunaweza kuwakanganya wahusika katika mazungumzo ikizingatia kwamba ujumbe huenda umekusudiwa kupokelewa kwa kundi fulani la watu katika jamii. Maoni haya yanaoana na Turner (2011) kwamba neno halimaanishi kitu kimoja katika kila matumizi yake. Hivyo, wanachomaanisha watumizi wa maneno hakisalii sawa kila wakati maneno haya yanapotumiwa. Kwa misingi hii, maana tofauti zinazozuka maneno yanapotumika huweza kusababisha hitilafu katika mawasiliano kwani maana zaidi huvuruga mawasiliano pale wapokezi wanaposhindwa kupata maana kusudiwa. Maoni haya yalioana na yale ya wataalamu kubainisha maana zaidi zinavyochangia utata katika mawasiliano. Utafiti unathibitisha upanuzi wa maana unavyosababisha utata unaoishia kuvuruga mawasiliano miongoni mwa wanajamii ikizingatiwa kwamba maana ya maneno katika lugha ni matumizi ya maneno yenyewe katika muktadha wao. Utafiti ulithibitisha maoni ya Washington (2010) kwamba upanuzi wa maana za maneno huchangia kuwepo kwa maana zaidi na hivyo kuwezesha utata kuzuka miongoni mwa watumizi.

Mawasiliano yanafanikishwa pale ambapo mpokezi amepokea ujumbe jinsi alivyokusudia mzungumzaji. Chukulio hili linashadidiwa na Munawwaroh (2008) anayesema kuelewa maana ni jambo muhimu zaidi katika mawasiliano. Kama mpokezi wa ujumbe kuelewa maana za semi za wengine ni muhimu ili kuzuia kuvurugika kwa mawisiliano. Maana

kimatumizi katika misingi hii ni maana ya msemaji hususan kusudi lake au athari tarajiwa ya semi. Maana kimatumizi inategemea usemi unaofanyiza uhusiano kati ya mwasilishaji wa ujumbe, mpokezi wa ujumbe na ujumbe wenyewe na kusudi la usemi wenyewe. Ilivyothibitishwa katika utafiti huu, kuwepo kwa utata wa maana unaochangiwa na maana nyingi za neno lililotumiwa kunaweza kuhitilafiana na mawasiliano kati ya mzungumzaji na mpokezi wa ujumbe. Hii ni kwa sababu maana aliyopata mpokezi wa ujumbe siyo ile maana aliyokusudia mzungumzaji anayewasiliana na mwenzake.

Mwasilishaji wa ujumbe huathiri tendo la kufanyiza maana na ujumbe kwa kutumia lugha. Sapir Newmeyer (1988) akinukuliwa na Mambo (2009) anathibitisha wazo hili anaposema kwamba wanachoambiwa na wanachoelewa watu kina uhusiano kadirifu na ulimwengu wanaofahamu. Chochote kinachotolewa kutoka kwa ulimwengu wanaofahamu kinaweza kukosa kuelewana. Watu hufanyiza taswira ya kile wanachoambiwa na si kutoka mtazamo wa mwasilishaji wa ujumbe. Aidha, ikizingatiwa kwamba maana hupatikana katika matumizi basi ni muhali kutopata kuelewa jinsi neno fulani lilivyotumiwa na hivyo kumaizi muktadha ni muhimu mno. La sivyo kutozingatia muktadha wa matumizi ya maneno yanaweza kusababisha utata utakaovuruga mawasiliano ambayo ni kipengele muhimu cha maisha ya mwanadamu.

## 4.4 Hitimisho

Sura hii imeangazia uchanganuzi wa data iliyowasilishwa kulingana na madhumuni ya utafiti huu. Utafiti huu umebainisha maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za Juacali na Nonini yenye maana tofauti na maana za kawaida na kueleza maana za maneno hayo katika muktadha wa nyimbo teule, ukachanganua athari ya upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za Juacali na Nonini kwa lugha ya Kiswahili. Utafiti huu pia ulitathmini utata katika mawasiliano kutokana na upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule zilizoimbwa na Nonini na Juacali.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Utafiti huu ulichunguza kisemantiki-leksia maneno ya Kiswahili katika nyimbo za kizazi kipya hapa Kenya. Kwa kutumia njia za utafiti kithamano ilivyojadiliwa katika sura ya tatu data ilikusanyawa na matokeo ya utafiti kujadiliwa katika sura iliyotangulia. Hivyo, sura hii inasawiri kwa jumla utafiti huu kuzingatia matokeo yalivyoelezwa katika sura ya nne. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchanganua maana za maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule za kizazi kipya, kutathmini athari ya upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za kizazi kipya kwa lugha ya Kiswahili na kufafanua utata katika mawasiliano kutokana na upanuzi wa maana za maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule zilizoimbwa na Nonini na Juacali.

Utafiti huu uliegemezwa kwenye nadharia ya maana kimatumizi iliyoasisiwa na Wittgenstein (1963) na kuendelezwa na Turner (2011) yenye mihimili kuwa: maana ya neno hupatikana katika matumizi yake. Pili, maana ya neno inatokana na muktadha wa matumizi ya neno lenyewe. Tatu, neno halimaanishi kitu kimoja katika kila matumizi yake. Maana za maneno ya kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule za kizazi kipya zilichanganuliwa, upanuzi wa maana na athari yake kwa lugha ya Kiswahili ukatathminiwa kisha maelezo yanayothibitisha utata katika mawasiliano kutokana na uwepo wa maana zaidi za maneno teule yakatolewa kwa misingi ya nadharia hii.

Sura hii inatoa mukhtasari wa matokeo na majadiliano katika tasnifu hii pamoja na mapendekezo ya mtazamo bora wa maana za maneno, matumizi ya maneno na mawasiliano katika lugha ya Kiswahili.Ilivyobainika katika sura ya nne muhtasari wa matokeo unatokana na matokeo ya mahojiano na majadiliano kimakundi yaliyofanywa. Kufikia hapa lililo muhimu zaidi ni kusema kwamba lugha ya kiswahili haipo katika hatari yoyote katika matumizi yake ikizingatiwa kwamba kuna upanuzi wa maana unaoshuhudiwa katika matumizi ya maneno katika miktadha mbalimbali ukiwemo nyimbo za kizazi kipya. Hata hivyo kuna haja ya uangalifu ili kuzuia kuvurugika kwa mifumo ya maana katika lugha hii, suala linaloangaziwa na baadhi ya washiriki. Hii ni kwa sababu maana ilidhihirika kuwa tumizi tena yenye uzingativu wa fasiri binafsi za washiriki. Hivyo, katika muktadha mmoja maana ziliibuka tofauti. Muhtasari wa matokeo ni kulingana na madhumuni ya utafiti. Sura hii vilevile ina mahitimisho ya utafiti, na mapendekezo.

## 5.1 Muhtasari

Ufuatao ni muhtasari wa matokeo ya utafiti huu kwa mujibu wa madhumuni.

### 5.1.1 Maana za maneno katika nyimbo teule

Maneno yaliyobainishwa kuwa na maana nyongeza katika nyimbo teule na kuchanganuliwa ni: kibao, chota, buda, , bamba, gonga, kupepea,damu, pigwa, mbuyu, nyundo, kaa, nizame, itauwa, rusha, dunga, msumari, msumeno, kabati, kusuguakitanda, katika, imemkaza, itamkazia,ameshona, nawika, mizigo, ngoma, nimerogwa, dondoa, mtoto, , tulia,ataruka, mbaya,zitoke, wakiiva, wanaungua, wamechanuka, chinjia, ameshiba, poa na misemo;rusha

mkono,piga randa, atanipigia magoti nimbariki, inanibamba mbaya,siku inanirarukia mbaya, tunakuta vitu.

Uchanganuzi wa maneno ya Kiswahili katika nyimbo teule za Juacali na Nonini yenye maana tofauti na maana za kawaida uliibua mawanda ya kimuktadha ambayo ni pamoja na: starehe na sherehe, pesa na shughuli za kutafuta pesa, mapenzi na ngono, mahusiano, ulevi na uhalifu. Maana za maneno ya Kiswahili kutegemea muktadha wa nyimbo teule zilizuliwa. Maana hizi zilikuwa tofauti na maana asilia za maneno haya zilizoorodheshwa katika kamusi ya Kiswahili. Kuzuka kwa maana hizi zaidi za zile zinazojulikana kulitokana na uelewa wa muktadha wa matumizi ya maneno hayo. Hivyo ilithibitika kuwa fasili ya maana inategemea mpokezi wa ujumbe ambaye analengwa, maneno hayo yanapotumiwa popote na kwa vyovyote vile. Aidha utafiti ulionyesha kuwa kuna uwezekano wa neno kuwa na maana mbalimbali kutegemea muktadha wa matumizi yake. Umuhimu wa muktadha katika mchakato wa kufanyiza maana ulithibitishwa pia na kuonyesha kuwa fasili ya maana inategemea muktadha. Hivyo hamna maana bila muktadha. Vilevile, mawasiliano hayawezi kufanikiwa pasipo uelewa wa muktadha.

### 5.1.2 Upanuzi wa maana na athari yake kwa lugha ya kiswahili

Katika utafiti huu upanuzi wa maana ulibainishwa na uwepo wa maana zaidi ya zile zilizoorodheshwa katika kamusi ya Kiswahili sanifu. Baadhi ya maneno yaliibua maana tofautitofauti kutokana na matumizi yao katika nyimbo teule zaidi ya moja.Ongezeko la maana za maneno teule ya Kiswahili kutokana na matumizi yao katika nyimbo teule za

kizazi kipya zilionekana kuiathiri lugha ya Kiswahili na athari yenyewe kuwasilishwa katika mitazamo mbalimbali. Mitazamo hiyo ni pamoja na makuzi ya msamiati na lugha kwa jumla, kuvurugwa kwa matumizi, mwelekeo, maenezi na maendeleo ya lugha pamoja na utata katika mawasiliano wakati wa matumizi maneno na hivyo lugha kutokana na maana zaidi zilizochipuka. Mitazamo hii ilionyesha hisia mseto kuhusiana na matumizi ya maneno ya Kiswahili katika nyimbo za kizazi kipya. Upanuzi wa maana unavyoweza kuiathiri lugha ya Kiswahili bila shaka ni jambo lianalotarajiwa na kushabikiwa ila kwa hofu ya kuvuruga lugha kwa upande mwingine.

### 5.1.3 Utata katika mawasiliano kutokana na maana zaidi

Katika utafiti huu utata katika mawasiliano kutokana na upanuzi wa maana ulioshuhudiwa katika maneno teule ya Kiswahili katika nyimbo za kizazi kipya zilizoteuliwa ulidhihirika ikizingatiwa kwamba maana iliyokusudiwa huenda isimfikie mpokezi wa ujumbe katika nyimbo hizi. Tofauti katika ufasiri wa maana za maneno yaliyotumika yalivyotumika katika nyimbo teule ilihakikisha maana zaidi kuchipuka na hivyo kuzua uwezekano wa kutatiza mawasiliano.

Neno linapotumiwa linazua maana zaidi na hivyo kuibua utata ambao utatatiza mawasiliano pale maana anayokusudia mwasilishaji wa ujumbe kwa kutumia neno lenyewe inapokuwa tofauti na fasiri ya mpokezi wa ujumbe. Kuvurugwa kwa mawasiliano kulionekana kutoweza kuepukika ikizingatiwa kwamba kuna maana zaidi za maneno ya Kiswahili

zinazozuka kutokana na tofauti za kimaeneo, uwepo wa makundi-lugha katika jamii na mtazamo wa kibinafsi wa mpokezi wa ujumbe hasa katika nyimbo hizi.

**5.2 Hitimisho**

Huu ulikuwa ni utafiti wa kisemantiki leksia wa maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule za kizazi kipya zilizoimbwa na Nonini na Juacali. Kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti na kutokana na matokeo yetu tunahitimisha kwamba:

Kwa kurejelea maana katika muktadha wa nyimbo ilibainika kwamba nyimbo za kizazi kipya hapa Kenya zinawasilisha dhana mbalimbali katika jamii. Maneno ya Kiswahili yalitumika katika nyimbo hizi hurejelea dhana hizi kwa kuashiria na pia kitamathali. Kwa mujibu wa nadharia ya maana kimatumizi maneno yanaweza kupata maana zinazohitilafiana na maana katika kamusi, ikizingatiwa kwamba maana za maneno hutoka kwa watumizi wa maneno yenyewe. Mchakato wa kufanyiza maana haupo bila kuzingatia muktadha na matumizi ya maneno. Hivyo kimsingi, ufasiri wa maana unatoshelezwa na vipengele vya muktadha na matumizi. Kwa mujibu wa utafiti huu basi, maana za maneno zina maana mbalimbali kutegemea muktadha wa matumizi. Maana inakuzwa na vipengele vya muktadha na matumizi. Aidha, maneno ya lugha hususan Kiswahili yanapotumiwa kwa namna iliyo tofauti na kawaida huishia kuzua maana tofauti na ya kawaida inayojulikana na hata imenakiliwa katika kamusi. Jinsi maneno yanavyotumiwa katika nyimbo kupitisha ujumbe unategemea walengwa wa ujumbe watakavyochukulia ujumbe unaopitishwa. Hivi,

maana wanayozua huweza kuwa tofauti na ile iliyokusudiwa na hivyo kuhitilafiana na mchakato wa mawsailiano.

Upanuzi wa maana ulibainika ikizingatiwa kwamba maana ya neno haiwezi kuchukuliwa kuwa ni moja tu kwani kuna uwezekano wa kuzuliwa kwa maana nyingine kwa kutegemea muktadha na matumizi katika mchakato wa mawasiliano. Kutokana na muktadha na matumizi ya maneno maana zaidi huibuka na hivyo upanuzi wa maana kwa maneno ya lugha. Upanuzi wa maana upo kutokana na matumizi katika miktadha mablimbali. Hivyo athari ya upanuzi wa maana kwa lugha ya Kiswahili inadhihirishwa na maana zaidi zinazozuliwa maneno yanapotumiwa kwa namna tofauti na kawaida. Upanuzi wa maana za maneno huweza kukuza lugha lakini pia kuitikisa lugha hasa ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili kwa misingi hii huweza kukua iwapo maana hizi mpya zinakubalika miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili. Hata hivyo, Kiswahili kitakuwa hatarini kutokana na upanuzi wa maana ambao huweza kuwakosesha mwelekeo hasa vizazi vijavyo vya wazungumzaji na watumizi wa lugha hii hasa iwapo maana hizi zaidi hazitatiliwa maanani. Hivyo, kutokana na mitazamo mbalimbali kuhusu athari ya upanuzi wa maana, ni vyema athari hizi zifahamike hasa katika matumizi ya kugha katika siku zinazoendelea.

Utafiti huu ulifanikiwa kuonyesha jinsi ambavyo kuzuliwa kwa maana zaidi kunavyoweza kuzua utata na hatimaye kuvurugika kwa mawasiliano. Utata katika mawasiliano unasababishwa na uwepo wa maana zaidi za maneno katika lugha hasa ya Kiswahili. Maana zaidi huhitilafiana na mawasiliano. Kuelewa maana ni jambo muhimu zaidi katika

mawasiliano. Kama mpokezi wa ujumbe kuelewa maana za semi za wengine ni muhimu ili kuzuia kuvurugika kwa mawisiliano.

Maana kimatumizi katika misingi hii ni maana ya msemaji hususan kusudi lake au athari ya semi na inategemea usemi unaofanyiza uhusiano kati ya mwasilishaji wa ujumbe, mpokezi wa ujumbe na ujumbe wenyewe na kusudi la usemi wenyewe. Mwasilishaji wa ujumbe huathiri tendo la kufanyiza maana na ujumbe kwa kutumia lugha. Imebainika kuwa maneno yanatatanisha ikiwa yana maana zaidi ya moja hivi kwamba kuna matumizi ya neno moja kuwasilisha maana zaidi. Ikizingatiwa kwamba maana ya neno ni matumizi yake katika lugha maana kulingana na mtumizi yaweza kuwa tofauti na ile inayofahamika kwa mpokezi wa ujumbe. Tofauti katika maana kutokana na matumizi ya maneno yanayochukuliwa kuwa yasiyo ya kawaida yanathibitisha kuvurugwa kwa mawasiliano.

### 5.3 Mapendekezo

Kutoka kwa utafiti huu baadhi ya mapendekezo ya kuzingatia kuhusiana na suala la lugha na maana. Kwanza, ni muhimu kutambua kwamba maana kimatumizi inaweza kutofautiana hata katika muktadha mmoja. Hivyo maana itaeleweka kwa misingi ya matumizi na fasiri ya mtu binafsi. Kwa misingi hii, ni muhimu kwa wanaotunga nyimbo hizi za kizazi kipya kuwa na kuijumuisha sehemu kubwa ya jamii katika jumbe na hivyo kukadiria lugha wanayotumia hususan maneno wanayotumia na wanavyotumia.Hii ni kwa sababu wao ndio wawasilishaji wa ujumbe kwa kutumia nyimbo. Hivyo, ili kuhakikisha kwamba maana inayopokelewa ni ile iliyokusudiwa na maneno yasiwe yanazua maana nyingi na hata kuishia kuvuruga lugha.

Wasanii wanapotumia maneno ya kawaida kimatumizi katika njia tofauti kuna uwezekano wa kuwepo kwa maana zaidi. Maana hizi inabidi zikadiriwe, zikubalike na labda ziweze kuorodheshwa katika kamusi za visawe vya Kiswahili kama maana pia za maneno hayo kwa minajili ya makuzi na uendelevu wa lugha. Ila katika jaribio la kupunguza wingi wa maana, wasanii wanaweza kuhimizwa kuwa na uelewa zaidi wa suala la maana.

Umahususi wa maana ni muhimu katika mawasiliano. Hivyo, ipo haja ya kushughulikia suala la utata katika mawasiliano unaosababishwa na kuwepo kwa maana zaidi katika muktadha na matumizi ya maneno. Ikizingatiwa kwamba ujumbe unapopitishwa ni ule uliokusudiwa kuzua mtazamo kwa msikilizaji. Utata katika mawasiliano japo hauwezi kuepukika, unafaa kupunguzwa kwa kuhakikisha maneno yaliyotumika hayazui maana nyingi. Hili linapendekezwa lifanikishwe kwa kutunga nyimbo zinazowalenga wanajamii wote na si sehemu tu ya jamii.

**5.4 Mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye**

Fauka ya yanayojulikana kuhusu lugha, maana na mawasiliano utafiti zaidi unapendekezwa katika mawanda ya matumizi ya lugha katika jamii ikichukuliwa kwamba lugha ina dhima kuu katika maisha ya mwanadamu.

1. Maana za maneno ya Kiswahili yanayotumiwa katika miktadha mingine mbali na nyimbo na kupanuka kimaana yanaweza kuchunguzwa.

2. Upanuzi wa maana katika miktadha mingine mbali na nyimbo unaweza kuchunguzwa.

3. Utata katika mawasiliano unaotokana na upanuzi ulinganishwe na ule unaotakana na ufinyizi wa maana.

## MAREJELEO


Attyang, J.M. (2003). *The emergence of Sheng' in Nairobi: A socio-psychological perspective.* Unpublished PhD Dissertation. Delhi University.

Adeola, T.S. (2001). Contemporary Nigerian Popular music: A tool for National Development. *Nigerian Theatre Journal vol 6: No.1.*

Adegoke, A. (2011). Language and Identity Representation in Popular Music: *International Journal of Innovative Interdisplinary Research.Issue 1 December 2011*.

Ajayi- Osulale, T.I. (2017). A sociolinguistic study of Nigerianism in selected songs of Bukola Elemide (Asa) Papers in English and Linguistics (PEL) Vol 18, No.2.

Akuno, E.A. (1999). *A conceptual framework for research in music education within a cultural context.* Paper presented at Cultural week seminar, Kenyatta University.

Altrichter,H., Posch, P. And Somech, B. (1996) Teachers Investigate their Work: An Introduction to the Methods of Action Research. London. Routledge.

Alston, W. P. (1967) Meaning The Encyclopedia of philosophy, vol 5 Macmillan and Free press,Edwards P, Editor in Chief, (pp.233-241), imesomwa tarehe 11/04/2014 saa 22 kutoka www.sciencedirect.com/science/article.

Anusu, A.(2015).Usawazishaji Leksimu katika Kiswahili: Utafiti wa Vihiga.tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Babbie, E.R.(1999). The Basic of Social Research. Australia: Wadsworth Publishing.

Baldwin, T. (2007). *Lexical Semantics: An Introduction.*Melbourne: Melbourne University Press.

Baron, J. (1972) Semantic Components and Conceptual development, Elsevier imesomwa tarehe 11/04/201saa 22:15 kutoka www.sciencedirect.com/science/article.

Blank, A. (1998). *Historical Semantics and Cognition*. Berlin and New York: Mouton. Bloomfield, W. L. P. (1933) Language, London –New york.

Brown, G. na Yule (1983). *Discourse Analysis*.Cambridge: Cambridge University Press.

Bosire, M. (2009) What makes a Sheng' word unique? Lexical Manipulation in Mixed Languages. *Selected proceedings of 39th Annual Conference on African Linguistics and languages in Africa.*

Bucaria, C. (2004) Lexical and structural ambiguity in humourous headlines. A master's thesis at Youngstown State University.

Buliba, A., Njogu, K na Mwihaki, A. (2006) Isimu jamii kwa wanafunzi wa kiswahili. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Butchavarov, P. (1960). Philosophy. London. Cambridge University Press.

Campell,L.(1998). Historical Linguistics.An Introduction. Edinburgh University Press.

Chachage, C.S.L. (2002). *Ndani ya Bongo, utandawazi na migogoro ya Utamaduni.*Paper presented at the 10th Conference on Politics in Tanzania at Dar es salaam University.

Chapman, R. (1989). Linguistics and Literature: An introduction to Literacy Studies. London: Edward Anorld.

Chibueze, O.T., Chinyere, R.O and Omoghie, I.A. (2017).LExico-Semantic Interpretation of Pentecostal Church Posters.English Linguistic Research. Vol 6 (4). Sciedu Press.

Chukwuma,O.O (2012)Meaning and Thematic Roles in the Igbo Language. Retrieved from https://www.ajo.info>article

Crowley,T. (1997) An Introduction to Historical Linguistics.3rd Edition. New York: Oxford University Press. Leech (1981). Semantics. HandWorth.Penguin.

Chukwu, N.C.(2002). *Introduction to Philosophy in an African Perspective.*Eldoret:Zapf Chancery Research Consultants and Publishers.

Cohen, L. and Manion, L. (1986) Teachers Investigate Their Work : An Introduction to the methods of Action Research. London. Routledge.

Dockrell, M and Messer, D (1999). *Children's Language and Communication Difficulties: Understanding, Identification and Interaction*. London: Continuum.

Dunbar, R. (1996). Grooming, Gossip and the Evolution of Language. Havard University Press.

Falk, J.S. (1973). Linguistics and Language: A survey of Basic Concepts and Implication.New York: John Wiley and Sons.

Farquharson,J.(2004) Dancing to new Words :A Lexico semantic Analysis of Jamaican Dancehall Music.Website: http://www.ncl.ac.uk retreived in 2016.

Fenn, J. and Perullo, A. (2003). Language ideologies, choice and practices in East African Hip Hop. In Berger H.M and Thomas, M (Eds) *Global Popular Music: The politics and Aesthetics of Language Choice.* Missisipi: University Press of Missisippi.

Filp, H (2008) What is Semantics, What is Meaning, imesomwa tarehe 11/04/2014, saa 20:00 kutoka www.sciencedirect.com/science/article.

Flofman, T.R (1997). *Realms of Meaning: An introduction to Semantics*. New York: Longman.

Firth, J. (1935). The Technique of Semantics. Transactions of the Philosophical Society.Reprinted in Firth (1957) Papers in Linguistics. London: Oxford University Press.

Fribsy, A.W. (1957). *Teaching English Notes: Notes and comments on Teaching English Overseas.*London: Longman.

Fromkin,V.& Rodman, R (1993). An Introduction to Language (5th ed). New York: Harcourt Brace College Publishers.

Fromkin , V., Robert, R. And Nina, H. (2003). An introduction to Language. (7th Ed) Wadsworth 25 Thomson Place, Boston, Massachusetts USA.

Githioria, C. (2002) Sheng: Peer Language, Swahili or Emerging Creole? *The Journal of African cultural studies 15(2) pages 159-181.*

Geeraerts, D. (2010). Theories *of Semantics*.Oxford. Oxford University Press.

Gall, M., Borg, W. and Gall, J. (1996) *Educational Research* (6th Edition). New York.Longman Publishers.

Gathigi, G. (2012). *Inventing East Africa Hiphop: Youth and Musical Convergence in East Africa* In Falola, T and Flemming T. (Eds). Music Performance and African Identities, Routledge.

Gay, L.R. (1996) *Education Research: Competencies for Analysis and Application*. (5th Edition). New Jersey: Prentice- Hall.Inc.

Gamble, T &Gamble, M (2013) *Communication works*. (11th Edition) New York: Mc Graw Hill.

Gekau, K. (1993).'The 1980s background to the popular political songs of the early 1990s in Kenya.'In media, democratization and identity. Harare: Department of of English university of Zimbabwe.

Grinell, M.R.J.R (1993). Social Work Research and Evaluation . 4th Ed. Illinois:FE Peacock Publishers, Inc.

Habwe, J. na Karanja, P. (2007) Misingi ya Sarufi ya Kiswahili, phoenix publishers LTD, Nairobi.

Hartman, R. R. K. (1993). Lexicography: Principles and Practice. Academic Press.

Hasan, M. (2015). Semantic Change of Words entered into Another Language trough the Processof LanguageBorrowing: A case of Arabic words in Bengali.International Journal of Social Sciences. Special Issue Vol 1(1). Retrieved from http:/grdpublishing.org/PEOPLE/people.

Hurtford, J. And Heaseley,B.(1983) Semantics: A Course Book: Cambridge: Cambridge University Press.

Ipara, I. O na Maina, G (2008) Fani ya Isimujamii kwa Shule Za Sekondari. Nairobi.Oxford University Press.

Jackendoff, R (1990) *Semantic structures*, MIT Press.Cambridge M.A.

Jean N.K. (2012) The local and Global in Kenyan rap and Hip hop culture: New African music in a globalising World. Bloomington: Indiana University Press.

Jilala,H.(2012) Muziki wa HipHop na Haki za Kijamii: Dhima, Changamoto na mapendekezo. Retrieved from com.opera.mini.native.operafileo=......FDownload%2F152572-399857-2-PB

Kaleka, D. (2008) *A lexico-semantic study of Sheng' in Kenya's Popular Music*.Unpublished Masters Thesis in Maseno University.

Kasomo, D. (2006) Resarch Methods in Humanities and Education. ( Statistic, Measurement, Evaluation and Testing) Egerton, Kenya: Egerton University Press.

Katamba, F. (1994). *English Words*. London: Routledge.

Keyasar, B. (2007). Communication and Miscommunication: The Role of egocentric processes. Intercultural Pragmatics Volume 4(1).

Khachula, A. (2013). *Semantic shift in Lumarama: A lexical pragmatics Approach*.Unpublished PhD thesis. The University of Nairobi.

King'ei, K. (2010).*Misingi ya Isimujamii*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

King'ei,K na Kobia, J.(2007)Lugha kama Kitambulisho: Chanamoto ya Sheng' Nchini Kenya. Nordiac Journal of African Studies. 16(3).

Khoshkhabar, G.S.&Iraji, M. (2015). The study of Ambiguity in social context of Iranian newspapers. Article published in International journal of advanced research. Vol3.Issue 8.

Kombo, D. K na Tromp, D.L. A (2006). Proposal and Thesis Writing: An introduction. Nairobi: Pauline Publications Africa.

Koech, S.K (2013) A study on language used in selected Kipsigis songs. A lexical Pragmatic analysis. A published master's thesis. The University of Nairobi.

Kung'u, D.K. (2006). Uchambuzi wa Matini: Matumizi ya Lugha katika sajili ya ya Matatu. Unpublished Masters Thesis at Kenyatta University.

Kurniawan, D. (2017). Interpretation of the associative meaning in the lyric of Maher Zain's Selected songs. An unpublished thesis. Alauddin state Islamic university of Makassar.

Leech, G. (1977). Semantics. New York, U.S.A: Penguin.

Lilenko, V. (2013). *Word Formation and Semantic mechanisms in English internet slang and memes creation and its impact on the Russian language*. Unpublished Bachelor's thesis. Tartu University. Russia.

Lyons (1992). *Language and Linguistics: An Introduction.* Cambridge University Press.

Lyons (1977). Semantics Volume 1. New York.Cambridge University Press.

Lyons (1977). Semantics Volume 2. New York.Cambridge University Press.

Lujan, E.R. (1999). The Basics of Social Research. Australia: Wadsworth Publishing.

Mambo, T.M. (2009). A Semantic analysis of some Gikuyu Words that have acquired new meanings. Unpublished M.A Thesis. Kenyatta University.

Massamba, D. P. B (1987) The impact of politics in language development in Tanzania. Kiswahili 54,1 and 54.

Mathooko, P.M (2007). *Isimu Jamii: Misingi na Nadharia*.Nairobi, Kenya: Njiku books, Kenyatta University.

Matinde, R. S. (2012) Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia, kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu,Serengeti Education publishers (T) LTD, Mwanza.

Mbatiah, M. (2012) Deviation as a communicative strategy in Gamba la Nyoka.Swahili forum 19.

Maxilom, R.M. (2008) Semantic Change of the Selected Cebuano Words.Paper Submittedat the 22nd Pacifi Asia Conference on Language, Informtion and Computation.

Miller, H., Kluver, D., Thebault-Spieker, J., Terveen, L.&Hecht, B. (2017) Understamnding Emoji ambiguity in context: The role of text in Emoji-related miscommunication. An aticle published in Association for the advancement of artificial Intelligence journal.

Mulusa, T.(1990) Evaluation Research for Beginners: A Practical Study Guide. German Foundation for International Development.

Mugenda, O and Mugenda.A.(2003) Research Methods*: Qualitative and Quantitative Approaches.*Nairobi: ACTS.

Mumbua,J.D. (2009). Uchanganuzi wa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Unpublished masters Thesis at Kenyatta University.

Munawwaroh, M. (2008) Functional Semantic Analysis on the Language of Advertisement of well Known Electronic Products. Unpublished Thesis presented at The State Isamic University of Malang.

Mutonya, M. (2008). Vol 20. East African Culture, Language.*Journal of African Cultural Studies.* Taylor and Francis Ltd.

Mwangi, E (2004). *Masculinity and Nationalism in East African Hip Hop music*. Tydskrif viir Letterkunde, 41, 2: 5-20. Vol 12. No.2.

Mwihaki, A (2004). Meaning as use: Functional view of Semantics &Pragmatics.

Nakhone,S.and Musungu, A.(2014) The linguistc Construction of Heterosexual Masculinity in Kenyan rap music, In the International Journal of Humanities and Social Studies.Vol 2 no.7. Retrieved from www.theijhss.com USA.

Ndimele M.O (1997). *Semantics: The Frontiers of Commuinication*.Port Harcourt: University of Port Harcourt Press Limited.

Ngunjiri (February 5th 2006.) Cultural Debate: Sheng gets backing from Unlikely fans. *Sunday Nation page 12.*

Nketiah, J.H.K. (1974). *Music of Africa*. New York: W.W. Norton and Company.

Norwich, P. (1998). Meaning. London: Oxford University Press.

Nyambura, I.(2006). Kalamashaka......Who's that. In Sunday Nation Buzz Pg 3 Col 1.

Nyairo, J and J. Ogude.(2005).Popular Music, Popular politics: Unbwogabble and the idioms of Freedom in Kenyan Popular Music. African Affairs, 104 (415).

Nyairo,J. (2007). " Modify": Juacali as a metaphor for African urban ethnicities and cultures'. In Ogude, J and Nyairo, J (Eds) Urban legends, Colonial Myths: Popular Culture and Literature in East Africa. Trenton NJ: Africa World Press.

Nyairo, J. And Ogude J. (2003).Populr Music and the Negotiation of Contemporary Kenyan Identity: The exampleof Nairobi City Ensemble. Social Identities 9(3). Taylor and Francias Online.

Obbo- Onyango, C (2006) Sheng' Our most Successful Export. In Daily Nation.

Ochichi, A.K (2013) Uwazi na Umaanisho: Usimbaji maana kimazungumzo katika Ekegusii na Kiswahili.Unpublished Masters Thesis at the University of Nairobi.

Odawo, A. M. (2015). Uhamishaji maana katika sajili ya mchezo wa kandanda. Unpublished Masters Thesis at Kenyatta University.

Ogone, J.O. (2014). Framing the Urban Hustler Space and Identity Discourse in Kenyan Popular Music. *The Journal of Pan African Studies Vol 16 no.9.*

Okumu, C.C. (1998) The Development of Kenya Popular Guitar Music. A study of Kiswahili songs in Nairobi. Unpublished M.A Thesis. Kenyatta University.

Osulale-Ajayi, T.I. (2017). A sociolinguistic study of Nigerianism in selected songs of Bukola elemide (Asa). In papers in English and Linguistics. Vol 18, No.2, June 2017.

Oslen,W. (2004).Triangulation in Social Research: Qualitative and Quantitative methods can really be Mixed. Retrieved from research.apc.org

Reuster-Jahn, U. (2014) *English verses Swahili: Language choice in Bongo Flava as expression of cultural and economic changes in Tanzania.*Paper presented at Swahili Forum 21.

Reuster-jahn, U (2007) *Lets go party! Discourse and self potrayal in the Bongo Fleva song 'Mikasi'*. Paper presented at Swahili Forum 14.

Rivera V.C.J. and Bernado S.A (2018) A Lexico-semantic Analysis of Phillipine Indie Song Lyrics written in English. Journal of Language and Linguistic Studies , 14(4).

Ritcher, D.J. (2006). Ludwig Wittegenstein (1889-1951).In the Internet Encyclopedia of Philosophy.

Samper, D.A (2004) 'Africa is still our Mama': Kenyan Rappers, Youth, Identity and revitalization of Traditional Values'. *African identities 2, 1:37-57.*

Sankoff, D. (1980). Linguistic Variation.Mpodels and Methods.New-York: Academic Press.

Sapir, E. (1921). *Language:An Introduction to the study of Speech.*New York: Harcourt, Brace. Saravanavel, P. (1992). Research Methodology.Kitab Mahal, Thornhill Road, Alahabad.

Sekella, M (1995). *Kiswahili in Tanzanian Music: Kiswahili and Media*.Dar es salaam: TUKI. Dar es salaam University.

Selinger,H.W., Shohamy,E. (1990) Second Language Research Methods: Oxford University Press.

Sinclair, J. McH (2004). (Edited with R, Carter) Trust the text. Language Corpus & Discourse: London.Routledge.

Short M. N and G, Leech (1981) *Style in Fiction: A linguistic introduction to English Fictional Prose*.London and New York: Longman.

Suguitan, C (2005) *A Semantic Look at Feminine Sex and Gender Terms in Philipine Gay Lingo*.University of Phillipines.

Tambunan, A.H (2009). The analysis of lexical and structural ambiguity in Your letters of Jarkarta Post.An Unpublished thesis for university of Sumatera Utara.Medan.

Taiwo, R. (2001). Lexical semabntic semantic Relations errors in Senior Secondary School Students Writting. In Nordiac Journal of African Studies. 10(3).

TUKI (2014) Kamusi ya Kiswahili Sanifu.Toleo la Tatu.Dar es salaam. Oxford Universty Press.East Africa Ltd.

Turner (2011) Making Semantics Pragmatic. In Current Research in the Semantics/ Pragmatics Interface,Vol 24. Emerald Group Publishing Ltd.

Ugwu, E.N and Ekundayo, O.S.B. (2013). Nicknaming as a morphological and lexico-semantic process: implication for language teaching and learning. *European Scientific Journal February 2013 edition Vol.9, No. 5.*

Uings, D.J. (2008). Mind, Meaning and Miscommunication.A published masters thesis to the University of Glass glow.

Ullmann, S. (1957) *The Principles of Semantics*. Blackwell and Mott.

Ullmann, S.(1970) Semantics: An Introduction to the Science of Meaning. Oxford: Basil.

Ullmann, S.(1977) Change of Meaning. In H. Hungerford et al., English Linguistics. Illinois:Scott, Foresman and Company.

Walhstorm,J.B.(1992). Perspectives in Human Communication. USA WC BROWN.

Wambugu,W.(2010) *Semantic Shifts in Gikuyu Lexemes: A lexical Pragmatic Approach.*Unpublished M.A. thesis: University of Nairobi.

Washington (2010) Bad Words Gone Good: Semantic Re- analysis in African American English. Unpublished Masters Thesis at the Unversity of Pittsburgh.

Wasike, C (2011) Jua Cali, Genge rap Music and the anxieties of living in the glocalized city of Nairobi.*Muziki; 8:1, 18-33.*

Wendell, V.H (1992). Dictionary of Concepts in Literary Criticism and Theory. New York: Greenwood Press.

Werth, P. (1999). Text World: Representing Conceptual Space in Discourse.London: Longman.

Wittgenstein, L (1963) Pilosophical Investigations.Oxford

Whorf, B.L. ((1956) Language, Thought and Reality: Selected Writtings of Benjamin Lee Whorf, John B.carroll (Ed).MIT Press. Retrieved from www.britishcouncil.org

Yeibo, E and Akerele, C. (2015) A Lexico-semanticReading of Chimamanda Adichie's Purple Hibiscus. In the International Journal of Languages and Literature. Vol 3.No. 2.American Research Institute for Policy Development.

Link: http: dx: doi.org/ 10.1080/18125980.2011.570073
(http://wikivisually.com/wiki/Genge 25th November 2016).
(http://www.musicians4africa.com/african-music-genres/genge-music/).

(http://www.mariaboomhower.blogspot.com Thursday October 2017.

http://www.linguistic society.org >files

https://www.jstor.org/stable/25473394?seq=1#page_scan_tab_contents.

https://www.researchgate.net>publication

https: standardmedia.co.ke>story

https://www.ncbi.nlm.nih.gov>articles

erespository.uonbi.ac.ke>handle

https://buleria.unileon.es>handle

https://elr.sciedupress.com

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1

### Maswali ya dodoso (Waasailiwa wakuu)

1. Je, wasikilizaji wanatumia nini kuwawezesha kuzua maana nyingine ya maneno haya ya kawaida ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo hizi? K.m. Waka, washa, kibao)

2. Je, ni vipi kuna maana nyingine ya maneno haya ya kawaida katika nyimbo hizi, k.m rusha, kibao, chota n.k)

3. Je, unafikiri nafasi ya muktadha ni ipi katika mchakato wa kufanyiza maana katika nyimbo hizi?)

4. Je, kuna uwezekano wa kuvurgika kwa mawasiliano na kupotea kwa maana iliyokusudiwa na waimbaji katika mtazamo wa wasikilizaji wa nyimbo hizi, pamoja na kwamba kuna maana zaidi inayozuliwa kutoka kwa maneno haya ya Kiswahili yalivyotumiwa katika nyimbo teule.

5. Je, nyimbo hizi za kizazi kipya hasa za Nonini na Juacali zinaathiri vipi lugha ya Kiswahili?

6. Kwa mtazamo wako, mustakabali (hali) wa Kiswahili ni upi hasa tukizingatia maana hizi zinazochipuka hasa katika nyimbo hizi.

7. Je, Kiswahili kinapotoka maneno haya ya kawaida, yanapopata maana zaidi hasa katika nyimbo hizi teule?

**Kiambatisho 2**

**Maswali ya majadiliano kimakundi**

1.Bainisha maneno ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo hizi yanayowasilisha maana tofauti kisha ueleze maana zao katika muktadha wa nyimbo hizi.

2. Taja maana nyingine ya maneno zilizo tofauti na maana ya maneno haya katika nyimbo hizi.

3. Bainisha ikiwa maana hizi nyongeza za maneno haya zinaweza kutumika katika mazungumzo ya kila siku katika jamii.

4. Toeni maoni yenu kuhusiana na matumizi ya maneno na hivyo lugha katika nyimbo hizi teule za kizazi kipya.

5. Fafanua maana nyongeza za maneno ya Kiswahili katika nyimbo za kizazi kipya zinavyoyaathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili.

**Kiambatisho 3**

**Idhini ya kushiriki**

Kwa mshiriki,

Jina langu ni Marolyne Moses, mwanafunzi katika chuo kikuu cha Maseno. Ninafanya utafiti wenye mada; Uchanganuzi wa kisemantiki leksia wa maneno ya kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule zilizoimbwa na Juacali na Nonini, kama sehemu ya kutimiza mahitaji ya shahada yangu ya uzamili katika Kiswahili. Naomba kwa hisani uwe mmoja wa washiriki katika utafiti huu. Unaombwa kujibu maswali yote kwa kutoa maelezo yanayoashiria mtazamo wako kuhusiana na suala hili la utafiti. Maelezo uliyotoa yatawekwa siri na kutumiwa tu katika utafiti huu. Iwapo unakubali kushiriki katika utafiti huu naomba uweke sahihi.

Asante.

**Wako mwaminifu,**

**Marolyne Moses**

Sahihi ya ukubalifu wa mshiriki: ..........................................................................

**DATA**

**Kiambatisho 4**

***Wimbo 1***

**MABESTE DAMU lyrics by Jua Cali ft K-Soja**

(K-Soja)
Beste tuko pamoja tangu siku za kusota ma-shorty kibao tuliwachota,
siwezi sahau nakumbuka ukipata forty tunaikula mbao mbao
unakumbuka ule mama ulicheki ule buda asikuwai kuseti kwa makarao
wee ni mtu wangu kama ndugu siwezi kurushia mkono hata hii life ikiwa sugu
usiwai skia story za hawa mafala najua vile inatubamba wanaskilia machungu
ebu kwanza gonga glass wajue vile hapa damu ni nzito kuliko maji
tutazidi kuwa pamoja hivi hata kama hatuna ganji tutazidi kupepea na hii life bila wasi wasi
mtaa yako ni yangu, shida zako ni zangu
'tazidi kuwa hivi mabeste... damu hata ka ulidandiwangwa jamu anajua haikuwa noma *yako*
hawa mafala walikuseti lakini unajua mi ntazidi kuchungia familia yako
mtoi wako ni msoo saa hii anakaa tu kama wewe, najua huko ni kuzii beste
chunga nyuma wasikufungie ka buti ya gari, utatoka soon tutaendelea na hii maisha yetu
usijali hata kesho asubuhi ntapitia nikuletee tu mkate na mangale

Verse 2 (Jua Cali)
eh, chali yangu unacheka hii kipara yangu nini?
kesho ni public holiday naskia tutapikiwa maini au sio?
mi nashukuru kila kitu umenifanyia, mi huku ndani kimwanaume navumilia
niliariwa juzi lakini leo niko mzima lunch nimekula na sijawai shiba... hivi
kwa nini tuki-hustle mtaani bado si huitwa waizi, tumbo ni ndogo na daily inaitisha
kumbo ni ndogo na daily inaumiza, kachawa za hapa ndani ni noma
make sure ukuwe umeniletea sabuni ya kuoga, jioni saa kumi najianika kwa jua baadaye
cell tunaosha na maji ya mvua, kazi hapa kibao nimepigwa sumuni mbili,
moja ya uji na ingine ya mkate slice mbili, ile part ya fegi, niaje
make sure umecheki m-junior wangu asirande mtaani
by the way Oposh alinyakwa yuko hapa ndani mpaka saa hii amekataa kunitobolea ni noma gani
kesi inaskizwa baada ya miezi tatu, tutatoka tu ile jaji iko ni mtu wangu
nirudi mtaani tuendelee kufanya mambo

Outro (Jua Cali)
eh, oya, eh chali yangu roll call inaitwa eh, usipoitika hapa ni noma wacha niende au sio
salimia kila mtu manze, salimia wife salimia mtoi wangu sana
salimia matha salimia mbuyu, kila mtu, au sio, baadaye, tuonane jo eh,
noma hapa ah-ah msinivute hivo naamka, naamka naenda, naenda pekee yangu
niacheni niende tu sawa, sawa, sawa OK poa

***wimbo 2***

**'Nyundo 'Flexx ft. Jua Cali**

Sijui niseme…
Chorus (Flexx)
Nashindwa jo nizame wapi, nyundo yangu sasa itauwa wapi
Usiwache endelea cheza nalo, mpaka iseme jina zote unazo
Nashindwa jo nizame wapi, nyundo yangu sasa itauwa wapi
Usiwache endelea cheza nalo mpaka iseme jina zote unazo

Verse 1 (Flexx)
Sijui jo nianze kusema vipi, wacha tu niseme uko fiti
Kwanza vile umesimama mtoto, unafanya nashikwa na joto
Kwanza nikicheki hiyo kifua naskia karibu kujiua
Lips zako soft zinasema nyundo yangu lazima itasema
Chorus (Flexx)

Verse 2 (Flexx)
hizo teke zako zanikwachu, unafanya beste atupe mbachu
hiyo mwili yako ikisonga kidogo, nyundo yangu inaruka kidogo
come ubonge nayo, inazusha lakini chunga inaeza rusha,
cheza nalo nine-inch yote, sista natupa bure
ukam mara sita mara sita sijui niseme, sijui niseme

(Jua Cali)
hapa job kuna nyundo moja itadunga wapi na msumari ni moja itaingia wapi
tulia nipe msumeno, nigware vifiti na ikiezekana nikutengenezee hiyo kiti
lakini kabati yako ni kubwa sana, ilalishe hivi iipige randa na sandpaper
ni kitu ya maana kusugua kitanda ya mtu mmoja staki, wall unit ni nzito kusongesha
wee niandalie tu juu ya meza (metres ngapi), tutaipima na tape measure
nifupishe nirefushe alafu nikate, rangi ile ya blue niipake
lakini bado mpaka saa hii nashindwa nipake upande gani
usiwe na wasi wasi, wee ni mteja wangu 'taimaliza leo leo

ndio utajua kwa nini siku hizi inaitwa nyundo wa komeo
Chorus (Flexx)

***Wimbo 3***

**MANZI WA NAIROBI- NONINI**

Machali leo hamtalala, machali leo hamtalala,
Ka we ni manzi wa Nairobi amka uanze kukatika,
Machali leo hamtalala, ka we ni manzi wa nairobi amka uanze kukatika
ka we ni manzi wa nairobi amka uanze kukatika, Piga nduru, piga nduru, piga nduru usikike
Huku kwetu africa nzima, nchi zote lazima kelele itafika,
Dunia nzima hakuna manzi ka wa nairobi, Amenga'ra nguo safi kidhani jana amezitoa tope,
Kila siku namwona taoo akitembea na maringo, Hata ukimpita lazima utapindua hiyo shingo,
Kwa akili nafikiria atafunguaje hizo vifungo, Hiyo jeans imemkaza itamkazia kufika huko,
Watu wameshindwa kusema jina yangu Nonini,
Sababu nimeona mwingine ameng'ara li nini na nini,
Cheki vile anatetemeka ni kama nimekunywa chang'aa
Juwa zile vitu nimeona jana jo utashangaa
Juacali nakwambia itabidi tumeanza kuchangaa
Kama huna bima we ndio utaanza kutangatanga
Cheki yule kakakakakakaka, cheki yule kakakakaka
Ningekuwa judge mi singevaa nisivyo kawaida
Manzi wote wa nairobi wangeshinda bila shidaaaa

[Chorus:]
Hamunioni Nairobi tena nikienda kucheki movie,
Ya manzi mpoa hajavaa any ndani ya jaquzi, hata ka ni Julia Roberts
Nataka wa nairobi yule anaoganga na hiyo Roberts
Masfi resize yake ameshiba kiplani,
Msauni muatherere anaweza kumalizia ganji,
Hakuona kwa kichwa yake ameketisha sisasini
Na ka kawaida kwa mfuko aningiza profit ya hamsini
Mchukuwe manzi yoyote yule humjui,
Kama hutaki kukosana na wale wako Kitui
Lakini watu husema wanataki ya hiyo mi sijui
Kuwa ready kupelekwa mbio ama utawika you-you-uwii
Na naongea from experience niliacha moja juzi,
Mluhya kumunduyo manzi ameshona bana
Hizo miguu zake amezitumia sana,

Wacha ikae ka ni huyo mi nawika hapana
(Mjaluo) Saa umeongea, huyo ndio mambo yote,
Nyuma ukimcheki mazee amebeba zote
Nikisimama na yeye, tunatoshana,
Tukipoa down ni mrefu, tena sana
Nashindwa nikimpata hizo mizigo nitaezana,
Usiniulize mizigo gani, wajua wacha kujifanyaa
Aaaaaaaaaaa Nonini

[Chorus:]
Si-ta-choka na kuwapatia manzi wa Nairobi sifa,
Hii ngoma inaeza enda one-hour kabla haijaisha
Kuna manzi mpoa ni ugonjwa huaga ameshikishwa,

mabeshte wanaambia nonini huwa umerogwa
Nimerogwa na ninazidi kuroga juu ya vile wananiroga,
Au vipi juakali (mmmh mmh)
Nakwambia ukweli mi si muongo wala muoga,
Ukilala wasikia sauti yangu nakwambia songa
Ukikaa niko kando yako ukibuy mboga
Kwa bafu kwa bafu kwa bafu
Niko nyuma yako na kusugua mgongo tukiogaaa,
Machali leo hamtalala,
Ka we ni manzi wa Nairobi amka uwanze kukatika,
Ka we ni manzi wa nairobi amka uanze kukatika
Machali leo hamtalala, calif records, aai aai
wewe hii track ni kali Aaaii, aaaii, wewe hii track ni kali, aaaii...

***Wimbo 4***

**We kamu -Nonini ft Jua Cali**

Intro: Nonini
Calif, genge remix! Watu wa Kenya wana tabia mbaya,
Nonini ana tabia mbaya, Juacali ana tabia mbaya
Verse 1: nonini
Bado home utanipata sitatoka, hii ni remix yangu ya kwanza nahope imetoka,
Nimekuwa kwa keja tu nikipika nikikushughulika.
Ngoma yako wee kamu si unaiskia vile iko poa, jako yako na trao kila kitu toa,

kuna siri yoyote unaezalike kuniambia toboa, ushaiguzwa mahali ukaskia ku-kohoa,
leo mi na we au sio poa poa, umesahau home
ambia ule concodi atakudondoa kwetu hapo nje na gate si ya blue
kuna style mpya, ebu kwanza inua mguu juu! ntainua polepole jo sababu minashuku
shingo yako konda inaeza vunjika ka ya kuku, naikachemshwa jo na wasee wakunywe supuu
naeza tembea kwa chupa zimevunjika mguu tupu, nijifanya sugu sabu yako tu sabu yako tu!
Chorus: Nonini
Leo niko kwa keja (sabu yako tu), sitoki hapa (sabu yako tu),
kwa hivyo ukitaka wewe wekamu
Leo niko kwa keja (sabu yako tu), sitoki hapa (sabu yako tu),
kwa hivyo ukitaka wewe wekamu
Verse 2: nonini
Juacali ushaichota mtoto kwa haga (jua cali) aa sijaichota mtoto wowote kwa haga
lakini nakuambia jo, hiyo ndiyo nimepanga! Siku ka leo vile manzi yangu anakuja kunicheki,
kabla aingie keja lazma ni make sure bado inaeza steady, bado inaeza ingiza ata ka ameketi!
Kwanza zime tembe zangu za Viagra vipi? Zimeexpire ama bado ziko fiti? (ziko fiti)
zimetumiwa na mtu ama bado ziko chini ya ile kiti?
(hii kiti) achana nazo ikifika atanipigia magoti nimbariki
na juala staki mtaani kuwe na mazishi! Kwa hivyo we kamu
we kamu tuongeze raha na watu kwa nchi! Bora leo uniachie tu nizame vimbichi,
bora leo uniachie nikushike hivi, nikupeleke juu mpaka utapike skumawiki! elephant run,
ningeiskia mpaka kwa coach akule itakuwa
ibidi unashtuka nini bana hii ni remix tu! ka we ni manzi nakungoja kwa keja we kamu tu, we kamu
chorus (nonini)
Leo niko kwa keja (sabu yako tu), sitoki hapa (sabu yako tu), kwa hivyo ukitaka wewe wekamu
Leo niko kwa keja (sabu yako tu), sitoki hapa (sabu yako tu), kwa hivyo ukitaka wewe wekamu
verse 3(nonini)
kuna food poa hapa napika na usivae jeans imekushika, ju ya meza leo lazima utakatika,
bila kiti utafanya cheza kwa speaker! na leo usikuje peke yako kuja na beshte zako.
Leo nataka combi sikutaki peke yako. Usiseme unaenda wapi staki noma na masako
Sema unaenda laibo staki noma na budako, anajua si ni mabeshte leo ni poa
Nikifunga mlango tu hivi nipate ushatoa, unakumbuka ile chakula nilikuambia, haezi ngoja,
Ni tamu kwa ulimi na ukitaka unaeza onja, mdogomdogo jo hujui inaeza kunyonga
Umejaza mingi kwa mdomo utashindwa kubonga,

tulia nikafungue mlango kuna mzungu anangoja, ana moto jo ananiambia anataka kuto to toka.
(Nonini)
Nywele leo nimenyoa (sabu yako tu) pia chini nimenyoa (sabu yako tu)
Nimeoga baada ya wiki moja (sabu yako tu), baby boy lazima ataruka (we we we we kamu)
Juala nimenunua kibao (sabu yako tu) mabeshte nimewafukuza wakaenda kwao (sabu yako tu)
Bed na keja zote ni safi (sabu yako tu) pia nimefukuza gadafi (we we we we kamu)
*****pia nimenunua (sabu yako tu) mpaka tenje nikaomba (we we we we kamu)
Tape za nyundo ninazo (sabu yako tu), sa fanya hivi (we we we we kamu) remix
Endeleeni kuongea…. ha!
chorus (nonini)
Leo niko kwa keja (sabu yako tu) sitoki hapa (sabu yako tu),
kwa hivyo ukitaka wewe wekamu
Leo niko kwa keja (sabu yako tu), sitoki hapa (sabu yako tu),
kwa hivyo ukitaka wewe we kamu

***Wimbo 5:***

**KIASI**

Intro
Genge jo inanibamba mbaya Yani hii mziki yani Nikiiskia yani mi uskia sijui aje
Nika ni pige nduru KIASI Watu! mnajua niaje (NIAJE)
Kitu yoyote tawaambia leo, Mtanijibu tu KIASI

Verse 1
Maisha yangu tamu siku inanirarukia mbaya lakini nimeamua kuituliza KIASI
Kabla pombe iniue itabidi nimeiwacha kabisa ama nianze kuikunywa KIASI
Ona vile nywele zangu zimerefuka mpaka watu wananiambia zipunguze KIASI
Walikua wanafikiria nimeacha ngoma sababu nimepotea ngoma ni mingi ngoma si KIASI
Na zote ziko poa ka mchele imeekewa mnazi ama imegusiwa KIASI
Ka hii ngoma inakubamba basi si ukatike na ka inakushika si uongeze sauti tenje KIASI
Chukua chali yako chukua manzi yako mweke karibu zitoke nae KIASI
Leo ata staki utupe mkono juu me nitingishie tu kichwa yako KIASI
staki ukatike sana mpaka uvunje mguu we nisaidie tu kuimba KIASI

CHORUS:
Kiasi eh eheea imeni imeni imenibamba
(Kiasi eh eheea imeni imenibamba*3)

Verse 2
Hawa watu jana walinishika ikabidi nimewaachia yao KIASI
Beste yangu akaanza kubishana nao akanyamazishwa na ma mbao KIASI
Eeeh! chali yangu haujawai skia maneno ya hawa watu hawana huruma ata KIASI
Juzi gari ya mafuta ikaanguka si waliangalia watu wakiiva KIASI
Nyama choma kila mahali kachumbari poa lakini iongeze kitungu KIASI
Wale wameponea wapeleke hosi watatibiwa na madaktari KIASI
Hao wengine hawakuja job wanasema leo wajamaliziwa ile ganji yao KIASI
Eeeh! uspotibiwa sai utaona tu maisha yako ikikuacha KIASI
Lakini usiwe na wasiwasi itarudi tu baada ya ma dakika baada ya ma dakika KIASI
Ebu niambie hio pande ingine ni ku poa ama ni kubaya hivi KIASI
Kumetulia ama watu wanaungua ama watu wanaiva hivi KIASI
CHORUS

Verse 3
Naskia raha wasee wamechanuka siku hizi ngoma mbaya haziskizwi ata KIASI
Pia naskia raha unaeza chinjia manzi siku hizi ata ka ni mzee wako KIASI
Kabla niende kumwona lazima nipige nguo pasi nijipake mafuta KIASI
Niakikishe ngotha safi na ka si ma thao mfukoni nikue na ganji ata KIASI
Leo lazima nijue ka ananipenda sana ama labda ananichukia KIASI
Lazima nijue ka tazamisha yote ama taiekelea KIASI
Akikata naachana nae naenda kutafuta mwengine msupa tu KIASI
Na najua tapata kiswahili yangu ni mambo yote hapa hakuna cha lugha KIASI
Afta hio tunakuta vitu kuta vitu mchana tunatulia KIASI
CHORUS

***Majadiliano kimakundi***

**<u>Kundi 1</u>**

**Mtafiti**: Wimbo huu unajikita katika muktadha upi?

**Mshiriki E**: Kwa kweli wimbo huu unazungumzia marafiki wawili amabo wamekutana, mmoja yuko kizuizini nafikiri kisha mwenzake anazuru humo na wanazungumza.

**Mtafiti**: Vizuri sana sasa labda katika uelewa huo naomba tubainishe maneno ya kiswahili ambayo maana zao katika wimbo huu ni tofauti na zile tunazojua....

**Mshiriki A**: kibao na tuliwachota.

**Mshiriki B**: mimi napendekeza neno buda.

**Mshiriki C**: kuna fungu fulani hapa; kurushia mkono.

**Mshiriki D**: inatubamba.

**Mshiriki E**: kwangu naona neno gonga.

**Mshiriki F:** kuna kupepea. sijui kama ni ile ya Jaguar?

**Mshiriki G**: damu na anakaa.

**Mshiriki C**: kuna pia nimepigwa.

**Mshiriki E**: Pia mbuyu

**Mtafiti:** Eleza maana ya maneno tuliyobainisha katika muktadha wa wimbo ‘Mabeshte damu’

**Mshiriki A**: Kulingana nami neno kama *kibao* huwa ni nomino katika lugha sanifu lakini katika wimbo huu neno kibao linaleta dhana ya wingi au kupita kiasi. Halafu kuchota sasa hapa mimi ninafikiri ni kule kumlaghai mtu au kumlaghai mtu au kumnyang’anya. Buda sasa si ni baba tu.

**Mshiriki B**: Nakubaliana na mwenzangu ila *kuchota* kwangu naona ina maana ya kumwomba mtu ngono ama labda kumteka mtu kwa njia fulani.

**Mshiriki C**: Kwa maoni yangu *buda* ni baba tu. Hayo mengine kwangu ni sawa na alivyosema.

**Mshiriki D**: Wacha mimi nizungumzie *kurushia mkono* kwa kusema kwamba huu ni usemi ambao unaonekana kuwa fiche. Maana hapa ni kusaliti ama kumwacha mtu anapohitaji zaidi.

**Mshirki E**: Kulingana nami kurushia mkono ni kumtelekeza mtu labda anapokuhitaji zaidi. Halafu *bamba* mimi naona ni kufurahisha tu ili maana yake sanifu ni tofauti sana.

**Mshiriki A**: Halafu ku*gonga* kwa wimbo huu ni kunywa. Unaona kuna mambo ya glasi kwa hivyo ni kunywa tu pombe. Hii kupepea ndio sijui ni kuwa maarufu nkidhani.

**Mshiriki C**: Ndio nakubaliana na huyu rafiki yangu lakini hapa kwa *kupepea* mimi nafikiria ni kufanikiwa ama tu kupanda ngazi ya maisha.

**Mshiriki B**: Lakini si kupepea pia inaweza kuwa tu hivyo. Yaani kung'ara hivi. Ama pia mimi naona inaweza kusonga tu mbele labda kutoka mahali pamoja hadi pengine labda viwango hivi.

**Mshiriki E**: Hii *damu* nayo mimi najua ni nomino tu ya kumaanisha kilicho muhimu katika mwili wa mwanadamu yeyote ule. Mimi sioni kuna maana nyingine.

**Mshiriki D**: Damu katika wimbo huu kwangu naona maana kidogo imebadilika kwa sababu hapa kuna uhusiano uanzungumziwa hapa kwa hiyo ina maana ya udhati au undani kwa kiwango fulani.

**Mshiriki C**: Yeah ni hivyo. Na ujue sasa hapa damu ni kivumishi sasa hata si nomino tena kwa sababu inaeleza ubeshte.

**Mshiriki B**: Damu kulingana na mimi ni kumaanisha urafiki wa dhati au wa toka nitoke.

**Mshiriki A**: na hii ku*kaa* kwani ni tofauti na kuweka mwili kwa kiti?

**Mshiriki C**: Bwana angalia muktadha hapa. Katika wimbo neno kaa kwa maoni yangu ni kufanana juu anamzungumzia mwanawe rafiki yake.

**Mshiriki A**: Kibao nilishasema ni wingi lakini kupigwa kunakozungumziwa hapa ni kama kulipwa ama kupewa ama niaje.

**Mshiriki B**: Ndio, hata mimi naona hivyo. Ukisema mtu ame*pigwa* kitu ni kama kumaanisha amepewa yaani.

**Mshiriki E**: Mbuyu nayo ni aina ya mti lakini katika huu wimbo ni ile tu maana ya sheng' yaani babaau mwanamume mzazi.

2.Taja maana nyingine ya maneno zilizo tofauti na maana za maneno haya katika nyimbo hizi. Je kunazo?

**Washiriki wote**:eh ndio. bila shaka.

**Mshiriki A**: kwa mfano nyundo katika nyimbo hizi inamaanisha kibofu huku likimaanisha tendo la ndoa kando na ile kawaida tunayofahamu ambayo ni kifaa cha ujenzi.

**Mshiriki B**: nyundo katika muktadha wa nyimbo ni sehemu nyeti ya mwanaume lakini kwa kawaida ni kifaa kinachotumiwa na seremala. Katika muktadha mwingine nyundo pia ni kitu au mtu mwenye ushawishi mkubwa.

**Mshiriki C**: katika muktadha wa kawaida tunapata kwamba nyundo ni kile kifaa kinachotumiwa labda katika ujenzi lakini katika ulimwengu wa siasa pia kuna maana ya neno hilo na ni labda mwanasiasa ambaye watu wanampenda sana na wanamwamini anaweza kuwa kiongozi wao.

**Mshiriki D**: nyundo hata katika muktadha mwingine toafuti na wimbo ni neno linaloweza kuashiria mtu mwenye uwezo wa kuwafanyisha watu kitu fulani hata bila wao kutoa maoni yao na kadhalika.

3.Jadili ikiwa maana zaidi za maneno haya katika muktadha wa nyimbo hizi za kizazi kipya zinaweza kutumika katika mazungumzo ya kila siku katika jamii.

**Mshiriki A**: La. Maana hizi zinatumika miongoni mwa watu wa umri wa chini hasa vijana sababu mtu kama babu au yule aliyetuzidi kwa umri huwezi kutumia neno nyundo kumaanisha kitendo cha ngono kwake. Hatakuelewa.

**Mshiriki B**: maana hizi hutumika katika mawasiliano ya kila siku laikini kwa watu ambao wana umri wa chini.kwa sababu huu ni msimbo. Misimbo hubadilika kila wakati na watu ambao wana umri wa wa juu hawawezi kuelewa lugha hii.

**Mshiriki C**: Maneno yakitumika kulingana na umri wa watu kwa msimbo fulani kwa mfano vijana. Akitumia neno kama nyundo kwa mtu aliyemzidi umri hawataelewana juu hao wao wanajua tu maana moja ya nyundo kwamba ni kifaa cha ujenzi wala hawajui maana nyingine.

**Mshiriki D**: hapana.kwa sababu unaona maana ya kiti katika muktadha wa wimbo hasa wa nyundo ni sehemu nyeti ya msichana. Sasa hiyo inaweza tu kwa mukatdha wa vijana kwa sababu ukimweleza nyanya eti kiti pia inamaanisha sehemu ya siri ya msichana atashindwa kuelewa juu yeye ni anafahamu kiti kama kifaa cha kukalia.

**Mshiriki E**: mimi ninatofautiana kidogo na wenzangu. nafikiri zinakubalika na hata kutumika kwa wale wanaoelewana wanavyotumia maneno hayo kumaanisha dhana zaidi ya zile asilia. Wajua huwezi kuenda mahali ukafanya mazungumzo na mtu ikawa kwamba hakuelewi.kwa hiyo maana zitakubalika mradi tu kuna maelewano baina ya mzungumzaji na msikilizaji ya kile kinachozungumziwa.

4.Toeni maoni yenu kuhusiana na matumizi ya maneno na hivyo lugha katika nyimbo hizi teule za kizazi kipya.

**Mshiriki A**: mimi naona ni vibaya tu kulingana na umri. Juu sisi vijana tunaona ni sawa lakini kwa wazee ni kukosa nidhamu ama heshima.

**Mshiriki B**: si swa kwa vile kama wataalamu japo wachanga wanatuvunjia lugha.

**Mshiriki C**: Mimi naona ni sawa juu kutumia maneno haya kunafanya maneno haya yawe na adabu. Huwezi kutumia neno jinsi ilivyo katika muktadha wa kawaida lakini kwa kutumia maneno hivi kunaficha au kuleta unadhifu fulani.

**Mshiriki D**: kwa maoni yangu matumizi ya maneno haya hivi si sawa kwa sababu inafanya vijana hawa kuongea kuhusu ngono hadharani wakiwaficha wakubwa au wazazi wao na hata kujihusisha. unaweza kuta kundi la vijana limekusanyika wanazungumzia mambo kama haya na kufanya mipango ya jinsi watakavyoitekeleza mipango hiyo. Wewe au yule ambaye haelewi maana hizo zaidi hutajua wanavyosema. Pili kama wataalamu au watetezi wa Kiswahili tunapata kuwa wanatuharibia lugha kwa sababu tunataka tukieneze na kulitukuza lakini wanatumia Kiswahili vibaya.

5. Fafanua maana hizi zaidi za maneno ya Kiswahili katika nyimbo za kizazi kipya zinavyoyaathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili.

**Mshiriki A**: Maneno na hivyo maana katika nyimbo hizi zinaathiri lugha ya Kiswahili kwa sababu kwanza yanaharibu ngeli, yanabadilisha majina mengine. Pili yanafanya Kiswahili kisambaratike kwa sababu wale wadogo ambao wanakua badala ya kujua Kiswahili wanakua wakijua mtindo wa sheng’ na maana mabazo si kadiri sasa inakuwa vigumu kuwarekebisha na kuwaambia neno Fulani laina maana hii hao wakichukulia maana iliyozuka hasa katika miktadha ya nyimbo hizi kuwa ndio maana.

**Mshiriki B**: kwangu naona maana hizi Zaidi zinazozuka yanaiathiri Kiswahili hivi kwamba badala ya kuzungumza lugha sanifu mtindo wa sheng’ ndio unatawala.kwa hiyo maana sanifu inapotea. Watoto na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na wataalamu wa lugha hawawezi wakapata maana iliyo kamili kwa sababu mtindo wa sheng’. Wachanga wanakua tu wakijua Kiswahili kwa mtindo wa sheng’.

**Mshiriki C**: Kwanza zinafanya Kiswahili au maneno katika Kiswahili kupoteza zile maana zao halisi kwa hivyo tunapata kuwa jinsi ambavyo mtu ataelewa neno hilo ni tofauti na yule mwingine atakavyorejelea kwa hivyo kwa kiwango fulani maana za maneno fulani zinapotea.

**Mshiriki D**: Maneno haya kupata maana zaidi inaharibu usanifu wa Kiswahili kwa mfano nyundo kumaanisha kibofu itakuwa imepoteza usanifu wake yaani maana yake haitakuwa ile ya kawaida ambayo inajulikana.

**Mshiriki E**: Maneno haya yanazua maana nyingine mpya kando na zile za kawaida hivyo wanapotumia vile yanaonyesha tofauti na hivyo kutatanisha hasa kimaana. Hata kuhitilafiana na usanifishaji wa lugha.

**Mshiriki F**: Matumizi ya maneno haya katika nyimbo hizi yanadunisha hadhi ya Kiswahili kwa sababu mtu akisikia maneno kama haya yanavyotumika tu katika nyimbo hivyo kama wazee, wataona tu lugha hii imekuwa tu ya kuashiria mambo mabaya kama yale yanayozungumziwa.

**Kundi 2**

**Mtafiti**: naomba tutambua maneno ya kiswahili ambayo yanaonekana kumaanisha kitu tofauti na kinachojulikana kwamba ni maana zao katika wimbo huu.

Mshiriki A: kwa maoni yangu maneno mengi hapa yanaashiria visiyoweza kutajwa moja kwa moja. Mifano ninayoanzia ni neno nyundo amablo ni kichwa cha wimbo. halafu kuna kushikwa na joto ambayo ni kama nahau na neno nizame.

**Mshiriki B**: mimi naona itauwa na ubonge.

**Mshiriki C**: kulingana na ninavyoona mimi kuna maneno rusha na dunga.

**Mshiriki D**: kwangu kuna msumari na msumeno.

**Mshiriki E**: kiti na kabati.

**Mshiriki F**: mimi nimeona tu miundo ya nahau; ipige randa na kusugua kitanda.

**Mshiriki C**: kuzusha pia.

**Mshiriki A**: kuna neno mtoto pia.

**Mtafiti**: Eleza maana ya maneno hayo mliyobainisha katika muktadha wa wimbo ‘nyundo’

**Mshiriki A**: wimbo huu ni wa mapenzi kwa hivyo muktadha wote ni wa mapenzi. neno *nyundo* hapa linamaanisha sehemu ya mwili hasa wa mwanaume kaika hali ya ngono.

**Mshiriki B**: msanii ametumia maneno kuleta maana zinazoelekezwa kwa lile tendo la mapenzi.kwa hiyo nyundo hapa lina maana ya sehemu nyeti ya mwanaume ikiwa tayari katika kushiriki ngono.

**Mshiriki C**: katika wimbo nyundo inaashiria sehemu ya siri ya mwanaume yaani msanii katika wimbo huuu amaekuwa akifafanua rafikiye mwanamke alivyo. kucheza hapa kunamaanisha lile tendo la ngono. *nizame* inamaanisha hajui aanze wapi yaani hajuisehemu ya kuhusisha kwanza katika mchakato mzima wa ngono.

**Mshiriki D**: neno hili katika wimbo huu unaweza pia kumaanisha kwamba hajui mahali ambapo nyundo itaingizwa, sehemu hasa palipo wazi.

**Mshiriki E**: katika wimbo maana ni ya ndani labda ina maana sawa na kufanya kwenyewe; kuingia kwa mwanaume sijui kama ninaeleweka.

**Mshiriki F**: neno hili kwangu linamaanisha kuweka mahali.

**Mshiriki A**: kulingana nami neno ita*uwa* linawasilisha dhana ya kuleta athari kwa nani hasa tukizingatia wimbo huu.

**Mshiriki B**: mimi naona uwa pia inaweza kumaanisha kiwango cha juu cha juu cha kitu Fulani kufurahisha.

**Mshiriki C**: *kuzusha* nayo ni kuzungumza kwa hasira ama ukali.

**Mshiriki E**: lakini hapa katika wimbo kuzusha inamaanisha kulalamika au kusisimkwa kwa sehemu nyeti tayari kwa tendo la mapenzi.

**Mshiriki D**: tukizungumzia neno *rusha* kwangu inarejelea hali ya kilele cha ngono kwa mwanaume.

**Mshiriki F**: ku*dunga* kando na maana ya kawaida katika wimbo inamaanisha kule kuvaa nguo ukapendeza.

**Mshiriki E**: kudunga kwangu inamaanisha kutiwa mimba

**Mshiriki C**: kulingana na wimbo huu neno hili kwangu naona linamaanisha ile hali ya ngono.

**Mshiriki A**: kulingana nami *kushikwa na joto* ni kule kuwa tayari kwa tendo la ndoa. kuwa na uchu yaani kusisimka.

**Mshiriki D**: *mtoto* ni msichana tena aliye mrembo wa kupendeza.

**Mshiriki B**: ndio habari ndio mtoto ni msichana anayependeza na kutamanisha. Halafu msumari na msumeno ni maneno yanayoashiria sehemu za siri za kike na kiume mtawalia wakati wa ngono.

**Mshiriki C**: kwa misingi kwamba taswira inayochorwa katika wimbo huu ni ya ngono, naona maneno mengi hapa yanarejelea tu hiyo shughuli alivyosema mwenzangu kwa

sababu hata *kupiga  randa* na *kusugua kitanda* ni semi zinazomaaanisha tu hali ya kufanya ngono.kwa kweli maneno haya ya kawaida yanaonekana yametumika kitaashira labda kuficha yanayoendelea na pengine kushabikiwa pasipofaa yaani na kikundi cha watu katika jamii ambao haitarajiwi wanjihusisha na mambo hayahasa tunapozingatia maadili ya jamii kwa jumla.

**Mshiriki F**: nakubaliana na mwenzangu kwa sababu hata *kiti* na *kabati* ni maneno yaliyotumiwa kumaanisha sehemu nyeti ya msichana.

**Mshiriki B**: naunga mkono yaliyosemwa na mwenzangu japo neno kabati kwangu linamaanisha makalio ya msichana nikizingatia wimbo husika.

2.Taja maana nyingine ya maneno zilizo tofauti na maana ya maneno haya katika nyimbo hizi.

**Mshiriki C**:eh ziko maana nyingine. Maneno haya hasa katika muktadha wa mtindo wa sheng' yana maana Zaidi.

**Mshiriki A**: kuna maana tu nyingi labda unajua kuna sehemu fulani makundi yanatumia maneno kumaanisha vitu tofauti. Neno moja kwetu linaweza kumaanisha kitu Fulani labda kwako likawa linarejelea kitu tofauti. tuseme kupiga nyundo. Yeye labda anamaanish akufanya tendo la ndoa ila kwetu kupiga nyundo kukawa kunamaanisha kumlaghai mtu tuesme nimekuambia uniletee kitu ninunue alafu nikose kukupa pesa. unaweza kusema nimekupiga nyundo. Kwa hivyo kuna maana nyingi tuseme tu si zile sanifu kabisa lakini zipo. Yaani ni maneno tu ambayo yana maana Zaidi ya moja katika muktadha wa nyimbo za kizazi kipya na maana nyingine pia katika miktadha mingine kando na muziki.

3. Bainisha maana zaidi ya maneno haya katika muktadha wa nyimbo hizi za kizazi kipya zinaweza kutumika katika mazungumzo ya kila siku katika jamii.

**Mshiriki B**: Inawezekana kulingana na hadhira. muktadha yaani kama mimi na mwenzangu hapa tukiongea tunakaa wa rika, moja ni kama zinatoshana tunaweza kutumia lugha hiyo lakini ukienda kama kuzungumza na watu wakubwa kama vile wahadhiri, hospitalini. Huwezi kutumia lugha hivi. Lakini mahali kama sokoni, kati ya wanarika tunaweza kutumia lugha hivi ili kupitisha ujumbe ama labda unataka kusema jambo na hutaki mwingine asikie.

**Mshiriki C**: inategemea unayezungumza naye kwa mfano kiwa ninazungumza na babangu siwezi kutumia neno 'kuiva'kurejelea kuchomeka au kuwa tayari kwa shughuli… hata elewa lakini ikiwa ninazungumza na kijana mwenzangu yeye ataelewa. hata wanafunzi unaowafunza huwezi kuzungumza vile kwa sababu huenda watatatanika.

**Mshiriki E**: kwa kweli ukitumia maana kama hii ya kuiva kwa mazingira ya wazungumzaji wa lugha walio wachanga huenda wakachukulia maan ilvyo ilhali huenda ulimaanisha kitu fiche kwa hiyo maana hizi zaidi ambazo zinaonekana pia kuwa fiche zitatumika kurejelea mazingira na kimsingi mtu ambaye atakuelewa kikamilfu unavyokusudia kama maana.

***Suala la kuvurugika kwa mawasiliano***

**Mshiriki A**: kwa kweli mawasiliano yanavurugika pakubwa kutokana na maana zaidi zinazoibuka katika mazingira mbalimbali ambamo maneno yanatumiwa.hii ni kwa sababu ya uwezekano wa watu kumaanisha vitu tofauti kwa neno moja.

**Mshiriki B**: kabisa mawasiliano yanaweza kuvunjika yakawa hayapo.hii ni kwa sababu tunahesabu kuwa mtu amewasiliana na mwenzake iwapo anayepokea ujumbe amemeelewa kilichomaanishwa. Sasa ikiwa yeye anapata maana nyingine ambayo si sawa na yule anayezungumza hapo tunachukulia kwamba mawasiliano hayajakamilika. maana zinazotokana na jinsi maneno yalivyotumiwa katika nyimbo hizi zitatatanisha hasa ikiwa watu ni wa umri tofauti kwa sababu kijana na mzee kwa mfano watatumia neno moja lakini wanamaanisha vitu tofauti katika mazungumzo yao hivyo hawataelewana.

**Mshiriki C**: Ni vile tuseme watu wa Kisumu tuna mtindo wetu labda wa sheng' na wale wa Nairobi pia wana mtindo wao kwa hivyo utapata mtu wa Nairobi akikuambia kitu kwa ule mtindo wao, wewe utachukulia anamaanisha unavyofahamu ambayo ni tofauti sana nay eye anavyofahamu maan ya neno hilo alilotumia.kwa hiyo utapata mnakosa kuelewana kwa sababu maana aliyokusudia sio maana ambayo mtu mwingine anakusudia.

4.Toeni maoni yenu kuhusiana na matumizi ya maneno na hivyo lugha katika nyimbo hizi teule za kizazi kipya.

**Mshiriki A**: kwangu mimi naona maneno mengine yanapotosha watu. Tuseme Watoto watakaposikia ngoma hizi yaani nyimbo hizi za juacali, Nonini na wengine amabzo zimejaa maneno haya yenye maana zaidi kulingana na nyimbo zenyewe watakuwa wanapotoka kwa sababu wakienda kule labda ninafunza wanafunzi kuandika insha kwa mfano; utapata mwanafunzi anaandika maneno akimaaanisha vingine vilivyo tofauti na maana halisi.Tuseme kwa mfano anasema buda alinituma sokoni nikamletee vocha….Sasa unajua kama mwalimu sitaelewa amemaanish anini kwa sababu huenda amemaanisha mzazi anapotumia neno buda lakini neno hili maana yake halisi katika lugha ya Kiswahili ni tofauti kwa hizyo itakuwa inakanganya sana mawasiliano katika Kiswahili sanifu na labda itakuwa tu inapotosha kwa jumla.

**Mshiriki B**: Mimi sasa sijui nitachangia kotekote kwa sababu; kwanza alivyosema itakuwa inapotosha wanafunzi lakini pia unajua ningependa niseme iwe inakuwa kwamba lugha ya Kiswahili inaponzwa kuwe na kufunzwa kwa mtindo wa sheng' na lugha ya kawaida zungumzi. Hii ni kwa sababu wakati tuko katika kizazi kingine na unajua ndio hizi nyimbo

zisikike na zienee watu wanataka kuelewa maana ya maneno yanavyotumiwa katika mazingira yao hivyo ili wimbo wako kama msanii ununuliwe na usikizwe na watu maneno hayo yanavyotumiwa inabidi yawasilishe maana unayokusudia .ndio sababu ninasema shuleni kama ni kufunzwa labda ile sehemu ya isimujamii waangazie maneno haya yenye maan Zaidi katika miktadha mbalimbali halafu kuwe na mtihani kando na lugha ya Kiswahili kutahiniwa inavyotahiniwa kawaida.

**Mshiriki C**: Mimi pia naona matumizi ya maneno hay katika nyimbo hizi za kizazi kipya yana mitazamo miwili.ni vizuri kutumia maneno hayo vile kwa sababu mtu ambaye hakulengwa akose kuelewa ni nini kinachosemwa. Kwa mfano hii ngoma imetokezea juzi ya mwanamuziki Khaligraph ya 'stick'; sasa vile anasema,'nitakuja kukupiga rungu' mwanafunzi hatajua anamaanisha nini lakini kama unaelewa inamaanisha nitakuja kujamiiana na wewe. Kitu kama hicho. sasa unajua kunai le maana fiche. Lakini ubaya wake ni vile inavyotupotosha, inapotosha wale wadogo kwa hivyo watakuwa wanatumia neno wakati mwingine bila kujua maana haswa. kwa hivyo watakuwa wanatumia maneno ambayowao wenyewe hawaelewi maana. Anajua ni Kiswahili kwa sababu kuna kitu kama dinda kwa mfano neno ambalo tunajua maana linamaanisha kukataa. Mara nyingi unajua neno hili linatumiwa katika muktdaha wa sheng' pia. Sasa unajua wakati uko kwenye mtihani unashindwa kuelewa kama ni sheng' am ani Kiswahili sanifu. hiyo ndiyo sasa shida.

**Mshiriki D**: Nafikiri pia katika kiwango hiki niseme matumizi ya lugha au jinsi ambavyo maneno haya yametumika yana mchango mseto; ule hasi na chanya. Mchango hasi ni kwamba tutaona zile itikadi za lugha ama usanifu wa lugha umekuwa kidogo na chandamoto kwa sababu hatujui sasa sanifu ni ipi na maan isiyo snaifu ni ipi kwa saabu ni wazi kwamba ikwa tutazingatia maana kimuktadha basi maana itakuwa si ya kamusi pekee. Kumaanisha kwamba maana itazuliwa kutoka kwa muktadha na pia matumizi ya maneno labda katika jamii ama kwa wakati Fulani.kwa msiingi hii basi tutakuwa tunagongagonga lugha kwa kiwango kingine lakini katika mtazamo chanya nikwamba maneno haya yanavyotumiwa huenda yanachangia katika kuwa lkwa lugha. Lugha ya Kiswahili inavyoendelea kugongwa na kupitia mapigo kama haya labda itazuka ikiwa na nguvu Zaidi kuliko awali. Tunaona kama kiingereza maneno yanaingizwa pale katika kamusi zile. Kuna maneno ya Kiswahili kama safari, bodaboda ambalo hata si neno la kiswahili ni neno la lugha mojawapo za lugha za kiafrika.na hivi karibuni neno bodaboda huenda litapata jina jingine kulingana na labda watu wanapotumia chombo hicho cha usafiri katika nchi zetu nyingine za kiafrika. Kwa hivyo ni mchango wenye mikondo miwili. Kwangu naona ipo pande zote mbili; kwamba lugha yaweza kuelekea kubomoka lakini tena huenda ikaibuka kuwa na nguvu zaidi.

**Mshiriki A**: Lakini iwejetuseme ibomoke zaidi na ijengekee kiasi? Labda iwe inajenga sana na ibomoa kiasi. Labda tunaweza kusema tuache hayo mapigo yawe na lugha ikue halafu huenda tukapoteza lugha katika ule muhula wa kuunda hivi.

**Mshiriki D**: kuna maoni tofautitofauti kuna wale wanaosema lugha huenda ikapotea kabisa huku wengine wakisema wacha lugha ipigwe hivyoitakua tu. Wajua nyimbo hizi ni fasihi na fasihi ni kioo cha jamii. Nyimbo hizi zinasawiri jamii ilivyo. msanii hawezi kutumia maneno katika ombwe; ni maneno ambayo ameyasikia watu wakitumia, hivyo ndiyo maana akatumia maneno yale katika nyimbo zake. Daima msanii huwa anasawiri tu jamii ilivyo. Ni ile tu sasa jinsi alivyotumia maneno hayo katika njia ya kiufundi sasa ndiyo tunazungumzia fasihi. Tukisema kwamba nyimbo hizi haizchangii basi itakuwaje zinazidi kusikizwa mpaka sas na wengine wanazidi kutunga wakitumia maneno kwa maana hizi zaidi. Wanaolamba lolo wanaendelea tu……. Na hatuwachi kucheza hii miziki tunaicheza kila siku.

5.Fafanua maana hizi zaidi za maneno ya Kiswahili katika nyimbo za kizazi kipya zinavyoathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili.

**Mshiriki A**: maneno haya yanaiathiri Kiswahili kwa sababu maana inabadilikana kuongezeka. Kuna wale labda wanaelewa sana, kuna wale labda wanapotoka. Wale ambao hawawezi tuseme kutenganisha maana za kisanii na maana sanifu. Kuna wale wanapotoka kuna wale watajua huyu amemaanisha hivi sababu ameimbia mahali hapa na amekuwa na watu hawa. Labda watajua huyu alitumia maneno haya kwa sababu Fulani na pale pengine labda angetumia kivipi kwa maana nyingine.

**Mshiriki B**: kwa kweli watu wanachanganyikiwa. Sasa mtu ambaye hajui mtindo wa lugha wa sheng' anaweza kukosa kuelewa mada ya wimbo huo pia.

**Mshiriki C**: inafanya pia watu wasahu ngeli; kama Kiswahili hata kuna ngeli.

**Mshiriki D**: sasa watu hawafuati zile sharia za lugha, wanatumia tu maneno kiholelaholela.

**Mshiriki A**: Na wengine wanatengeneza maana zao tu kutoka kwa maneno hayo kulingana na yalivyotumiwa.

**Mshiriki E**: mimi kwa mtazamo wangu, athari ipo pande mbili. kwanza lugha inakua tunapotumia maana hizi zaidi kwa misingi ya kuwepo kwa maana za maneno zilizopanuka. Kwa upande mwingine hata hivyo lugha inashuka kihadhi kwa sababu utakuwa na neno moja linaloashiria vitu vingi na mara nyingi maana hizi mpya huwa zaelekezewa makundi lugha Fulani.hivyo ikiwa uko nje ya kundi lugha hilo hutapata maana iliyokusudiwa.

Maana zaidi za maneno katika lugha zinajenga au kuboma ile lugha. jadili ikiwa lugha itakuwa inadidimia au kua.

**Mshirika A**: Kwa mtazamo wangu iwapo maana nyingi zitawafikia watu wengi na waweze kuelewa maana zile, inaweza kuwa inajenga kwa sababu watajua kuyatumia maneno yale katika miktadha tofautitofauti na vile watakuwa wanaelewana. Watakuwa na ule mfumo wa

kuwasiliana. saa hizi watakuwa wanawasiliana kwa ile lugha inayostahili wakitumia zile maana ambazo wamezitengeneza wenyewe. Itakuwa inajenga.

**Mshiriki B**: Eh hata mimi naona inajenga.kwa sababu wanazidi kutoa maana nyingine za maneno na kwa kawaida lugha haijafikia mwisho; bado inazidi kukua kwa hivyo wakizidi kuongeza na wanasarufi nao waingilie kati watazidi kutupa maana zaidi. Wataalamu watazidi kufanya ukarabati na kuonyesha kuunga mkoano au kupinga lakini kwa kawaida wataalamu mara nyingi wanaunga mkono masuala kama haya.

**Mshiriki C**: mimi kwangu inabomoa kwa upande wa lugha ya Kiswahili. Inabomoa kwa sababu inafanya mtu kwa mfano saa hizi unaweza kupata kuna ile maana halisi iliyowekwa kurejelea neno kwa mfano hii ya kujamiiana halafu mtu aje kusema kupiga rungu; wanatukanganganya kabisa sasa hujui maana ni gani sababu ile ikon a maelezo zaidi, hii ingine pia inakuja na maelezo yake. Sasa unaona kuna utata; hujui maana ni gani haswa. Sas unakuja unapata unaweza kuandika maana yoyote kwenye karatsai ukisema kwangu neno fulanilinamaanisha hivi kumbe kuna maana nyingine tofauti na hiyo, sasa unaona hatuna msimamo.

**Mshiriki B**: Unajua maneno ya Kiswahili hayako…... sasa waimbaji pia wanaweza kuja na maneno yao kumaanisha kitu kingine. kwa hivyo lugha ya Kiswahili inaweza kuchukua maneno yale katika maana hizo zilizozuliwa kutokana na matumizi ya maneno katika mzinginra mablimabli. Kwa hivyo mimi bado ninashikilia kuwa lugha inajengeka.

**Mshiriki C**: neno kama buda sasa kwa Kiswahili tunajua ni mzee ambaye hana meno halafu tunapata maana ya baba. Sasa itakuwa kwamba mahali palipotolewa maelezo ya maana ya baba pia pawe na kisawe kama buda na mahala pa neno buda kulikuwa na tu na maelezo. Kimsingi si unaona upo utata.

**Mshiriki D**: maana hizi zote ziwe ni Kiswahili lakini maana zaidi tunaona imeibuka .hivyo inajenga na kubomoa kiasi Fulani.Tuseme tu wataalamu wakiweza kufuata.kuna baadhi ya maneno yametumika sana, kuna mengine yametumika laikini si vile tuseme mjini Kisumu kuna neno juakali ambalo limetumika sana lakini kule kakamega neno hili halijasikika,Mombasa pia huenda linatumika kurejelea dhana tofautri kabisa.hata hivyo kuna neno ambalo labda mwimbaji amelitumia sana katika nyimbo zake kama vile mtoto; wataalamu wanaweza kuangalia maana hizi zaidi ikiwa zinweza kukubalika na kuidhinishwa kutumika katika jamii kirasmi.basi wanaweza kuhalalisha na kuingizwa katika lugha sanifu ya Kiswahili kwa vile yatakuwa yamezoewa na watu wanakuwa hivyo yatatumika jambo ambalo ni ni gumu pia. kwa hiyo sisemi kwamba maana zote za maneno ziwekwe katika lugha, kuna yale ambayo pia yanaweza kutengwa.

**Mshiriki C**: kumaanisha zitawekwa kwa upande wa misemo?

**Mshiriki B**: ni sawa hivyo.

**Mshiriki C**: sasa ikiwa ni upande wa misemo inamaanisha kuwa maneno haya yenye maana fiche yanatumiwa kuashiriwa kitu Fulani.

**Mshiriki B**: na maneno yenye maana sawa. yanaitwa visawe pia yatazingatiwa katika suala hili.

**Mshiriki D**: maana hizi nyini zinapozuka tunaishia kuwa na visawe na hata misemo kwa sababu maaana hizi za ziada hasa katika nyimbo hizi hazionekani moja kwa moja bali ni fiche.

**<u>Kundi 3</u>**

**Mtafiti**: naomba tutambue maneno ya kiswahili ambayo yanaonekana kumaanisha kitu tofauti na kinachojulikana kwamba ni maana zao katika wimbo huu.

**Mshirki A**: maneno yapo ninaanza kwa kukatika na ameng'ara.

**Mshiriki B**: kwangu kuna ameshiba na ameshona.

**Mshiriki C**: amebeba na tukipoa kwa maoni yangu.

**Mshiriki D**: kwangu mizigo na ngoma.

**Mshiriki E**: mimi pia nimeona umerogwa.

**Mshirki F**: na hii kuroga na wananiroga inapitisha ujumbe mmoja ama ni tofauti? kwa maoni yangu ni baadhi ya maneno ambayo yana maana nyingi katika mazingira sawa.

**Mtafiti**: hebu tusawiri mazingira yaliyo katika wimbo huu ili kuelewa muktadha.

**Mshiriki A**: Wimbo huu mimi nafikiri unahusu msichana wa Nairobi. Mwimbaji anazungumzia msichana wa nairobi kwa kumsifia na hata mahusiano naye yalivyo kwa jumla. Vilevile sifa hizi zinaonekana ni kama zinatolewa mahala pa raha, starehe na labda sherehe Fulani ambapo watu wanafurahia na kusherehekea.

**Mshiriki B**: sasa tunaangalia maneno. *kukatika* si ni kucheza tu yaani kufurahia wimbo.

**Mshiriki C**: kweli kukatika ni kudensi yaani kusonga kwa sehemu fulani za mwili mtu anaposikiliza wimbo.

**Mshiriki D**: kitu ime*kaza* mtu ni kitu labda imemshika mwilini lakini pia ku*kazia* ni kuzuia mtu kupata kitu.

**Mshiriki E**: kukazia ni kumyima mtu kitu.

**Mshiriki B**: Ukisema mtu *ameshona* ni kumaanisha tu yeye ni mnene lakini wakati mwingine inaweza pia kuwa inamaanisha kushiba au wingi wa kitu.

**Mshiriki A**: kushona ni kunenepa.

**Mshiriki D**: ndio ni hivyo. Kushona enyewe ni kuwa mkubwa kimaumbile.

**Mshiriki C**: *kuwika* nayo ni kukataa na kuonyesha pingamizi kwa jambo Fulani.

**Mshiriki E**: kulingana na mimi kuwika ni kuzungumza kwa nguvu.

**Mshiriki B**: *Poa* nayo inamaanisha kitu kizuri japo tusisahau kwamba neno hili linaweza pia kumaanisha kutulia tu kando na maana ya kawaida ya kitu kilichofanyika kuwa baridi.

**Mshiriki A**: ndio, poa ni nzuri tu. halafu mizigo hapa ni makalio yaani sehemu ya nyuma ya msichana.

**Mshiriki C**: Kwa hilo neno *mizigo* mimi naona inamaanisha mambo yanayomhusu anayezungumzia.

**Mshiriki B**: Mimi sasa hapa kwa mizigo nimepotea., kwa sababu mimi nilikuwa nafikiria mizigo ni vit utu vimebebwa.si maana nyingine tofauti.

**Mshiriki E**: *ngoma* hapa ni wimbo tu halafu roga ni kuimba tu kunakofurahisha yaani kuimba vizuri.

**Mshiriki C**: Kwani *roga* ina maana tofauti hapa?

**Mshiriki A**: Ndio.kama katika sentensi hii roga inamaanisha tu kuburudisha sana yaani kufurahisha kabisa.

**Mshiriki D**: Nakubaliana na mwenzangu; roga hapa hasa katika wimbo huuu n ahata mazungumzo ya kawaida inamaanisha kutekwa makini na kitu kinachofurahisha.

**<u>Kundi 4</u>**

**Mtafiti**: kwa kuangalia maneno ya wimbo huu je kuna maneno ambayo yanaonekana kuwa na maana tofauti na zile maana tunazojua kila siku, iwapo yako naomba tuyabainishe.

**Mshiriki A**: ngoma na atakudondoa.

**Mshiriki B**: kuna chota mtoto, mantiki ya fungu hili la maneno nje ya wimbo haipo ila kwenye wimbo ipo kabisa.

**Mshiriki C**: mimi nadhania hili fungu; atanipigia magoti nimbariki hata inaonyesha ufasihi kwa namna fulani.

**Mshiriki D**: nizame na utakatika kulingana na mimi.

**Mshiriki E**: kwa maoni yangu maneno tulia na ataruka yanajibu hilo swali.

**Mshiriki F**: mimi nyundo.

Eleza maana ya maneno hayo katika muktadha wa wimbo 'We kamu'

**Mshiriki A**: wanazungumzia uhusiano wa kimapenzi na hili neno linaashiria kwamba yuko tayari kwa kuja kwa mpenzi. katika muktadha huu *ngoma* haimaanishi muziki hata.

**Mshiriki B**: ngoma inamaanisha kitu spesheli.

**Mshiriki C**: ngoma ni sehemu nyeti katika hali ya kusubiri tendo la ngono.

**Mshiriki A**: kitu *poa* ni kitu kizuri, iko sawa au inapendeza

**Mshiriki D**: Neno *dondoa* nalo linamaanisha kushuka kutoka kwa gari

**Mshiriki E**: kwangu naona labda kumwonyesha mtu mahali fulani.

**Mshiriki A**: kulingana na mimi neno hili linamaanisha kumfanya mtu asahau.

**Mshiriki B**: neno hili kwangu kwa kurejelea wimbo huu wa nonini linamaanisha kumtoa mtu labda mahali.

**Mshiriki A**: Kuna *kuchota mtoto* hapa ambako kuna maana fiche. kuchota kunamaanisha kitu toafuti na kitendo cha kawaida tunachojua. katika wimbo huu nafikiri neno hili linaleta dhana ya kumteka mtu kihisia hasa kimapenzi.

**Mshiriki C**: mimi ninatofautiana na mwenzangu kidogo kwa sababu kuzingatia wimbo neno hili linaweza tu kumaanisha kumsisimua mtu na kumtayarisha kwa ajili ya tendo la ndoa labda kwa kumshika.

**Mshiriki B**: kumchota mtu wenzangu mimi nafikiria ni kumpapasa mtu na anayezungumziwa hapa ni binti mrembo.

**Mshiriki D**: mimi naona tu kumbusu msichana ukimchangamsha kwa ajili ya shughuli ya kufanya mapenzi.

**Mshiriki A**: *Atanipigia magoti nimbariki* wah! Huyu msichana leo atakipatapata.ni kama leo ni leo katika hali ya ngono

**Mshiriki B:** yaani inamaanisha atakuwa tayari kwa tendo la ndoa na kwamba ataonyesha ile hamu moja kwa moja.

**Mshiriki C**: usemi huu unarejelea ile hali ya kuonyesha raha na kutosheka kuhusiana na lile endo la kujamiiana.

**Mshiriki E**: huyu msanii anajaribu tu kusema kwamba yule msichana atahisi vizuri sana na kumradhi waendelee katika tendo la mapenzi.

**Mshiriki A**: *kuzama* nako ni ile tu hali ya ngono. katika wimbo huu taswira ni ya ngono tu.

**Mshiriki B**: mtu anaweza pia kusema nizame akawa anamaanisha astarehe na afurahie.

**Mshiriki C**: neno *katika* humaanisha kucheza au kuvunjika kwa kitu kulingana nami lakini wimboni humu ina maana tofauti na kucheza wenzangu, kwangu neno hili linamaanisha kuumizwa ama kusikia raha ya kilele wakati wa ngono.

**Mshiriki D**: mimi naona inamaanisha kutosheka na ngono.

**Mshiriki E**: *kuruka* katika wimbo huu pia ina maana fiche ambayo ni kule kusisimuka kwa uume kwa ajili ya ngono.

**Mshiriki B**: neno hili; kuruka katika wimbo huu pia unaweza kumaanisha kutungwa mimba.

**Mshiriki D**: kuruka hapa pia inaweza kumaanisha kuwepo kwa mimba yaani kupachikwa mimba katika muktadha wa wimbo huu.

**Mshiriki C**: *kibao* tulishasema ni wingi.ila tu napenda kuongezea kwamba kibao kwa maana ya kawaida huwa nomino lakini hapa katika muktadha wa wimbo neno hili limegeuka na kuwa kivumishi kinapoleta dhana ya wingi.

**Mshiriki A**: *nyundo* katika wimbo huu ni ngono.

**<u>Kundi 5</u>**

**Mtafiti**: Naomba tutambue maneno ya kiswahili ambayo yanaonekana kumaanisha kitu tofauti na kinachojulikana kwamba ni maana zao katika wimbo huu wa kiasi.

**Mshirki A**: kwangu inanibamba mbaya, sanasana hilo neno mbaya...halafu pia neno skia pia.

**Mshiriki B**: siku inanirarukia mbaya na kuituiliza

**Mshiriki C**: mimi naona maneno ngoma na ukatike kutokana na neno katika.

**Mshiriki D**: wanaungua na wamechanuka.

**Mshirki E**: kwangu mimi zitoke na wakiiva.

**Mshiriki A**:  neno tulia pia.

**Mshiriki F**: mimi pia nimeona chinjia na tunakuta vitu ambayo kimuundo nitachukulia kuwa nahau

**Mtafiti**: Eleza maana za maneno mliyobainisha katika muktadha wa wimbo ‘kiasi’

**Mshiriki A**: *Inanibamba mbaya*; Mimi ninafikiri maneno haya yanamaanisha tu msanii anayeimba an furaha yaani inamfurahisha kabisa au inamweka juu.

**Mshiriki B**: Mimi nimechanganyikiwa juu ninashindwa kama bamba ni neno la Kiswahili

**Mshiriki C**: mimi ninafikiri maneno hayo yana maana kwamba msanii amezidiwa. Anaingiwa sana na wimbo wenyewe unaoibua hisia kutokana na maneno na labda mapigo yake. kimsingi anafurahia wimbo.

**Mshiriki D**: mbaya ni kivumishi chenye maana ya kitu kisichopendeza.

**Mshiriki A**: mbaya ni neno la Kiswahili linalorejelea kisicho kizuri lakini katika muktadha wa wimbo neno ‘mbaya’ limebadilishwa maana na kurejelea kitu kizuri.

**Mshiriki E**: Mimi nilitaka kusema ‘mbaya’ bado ni kivumishi ila hapa inamaanisha mtu anafurahia kitu kiasi cha kutoweza kueleza. Neno hili linaleta dhana chanya tofauti na ile ya kawaida amabyo inajulikana.

**Mshiriki A**: Neno *kurarukia* kwa kweli maana yake si sawa na ile ya kawaida tunayojua. Naona dhana ya kinaya hapa. kwamba mabo yamepita kiasi.

**Mshiriki B**: kuraruka yenye tunajua ni kutawanyisha kwa hivyo msanii ni kama anasema maisha yake ni matamu lakini siku haienendi vizuri, anamaanisha kuwa anaona siku imemwanzia vibaya lakini maisha yake ya kila siku huwa sawa.kwa hivyo kurarukia hapa kwamaanisha tusiku haimwendei vizuri wala hahisi salama na jinsi siku ilivyomwanzia.

**Mshiriki C**: *ngoma* ni muziki tu ama kando na ile ala; maana ya kawaida.

**Mshiriki A**: kwangu mimi ngoma ni wimbo.

**Mshiriki B**: *Kukatika* si ni kucheza. maana halisi japo ni kutenga kwa kisu au pia kihusishi kwenye sentensi. wimboni humu ni kunengua tu. Halafu ku*shika* ni kule kufurahishwa au kuburudika kutokana na wimbo

**Mshiriki A**: nakubaliana naye

**Mshiriki C**: hata mimi naona hivyo halafu *zitoke* hapa mimi naona inamaanisha yaani watu wapate burudani pamoja.

**Mshiriki D**: mtazamo wangu wa neno zitoke ni kwamba inaashiria mwanzo wa burudani ama raha.

**Mshiriki E**: Mtu akisema zitoke naye kwangu mimi anamaanisha makini yake inaswe na kitu Fulani.kama kwamba amepandwa na jazba. msisimuko tu niseme.

**Mshiriki A**: *mbao* ni neno linalorejelea kinchotokana na mti lakini katika wimbo huu neno hili linarejelea sarafu yaani pesa.

**Mshiriki C**: mimi nina maoni tofauti kuhusiana na maana ya neno hili. kwangu mbao tukizinagatia muktadha ni kile kichapo wanachopata washukiwa hasa kule korokoroni.

**Mshiriki E**: *kuchanuka* ni kupevuka kimawazo ama tunaweza kusema kwamba kule kupata ujuzi ambao mwanzo haukuwepo.

**Mshiriki D**: mimi naona kuchanuka hapa ni kule ambako watu wana uwezo wa kuchagua yaani wana uelewa Fulani unaowaongoza kufanya mambo ambao haukuwepo awali.

**Mshiriki B**: *vitu* sasa hapa ni pombe ama; mimi nafikiria hivyo

**Mshiriki E**: kwangu vitu inarejelea maumbile ya binti Fulani.

**Mshiriki A**: vitu mimi inanichanganya juu sijui kama ni pesa, ngono au vileo.

**Mshiriki C**: *Kuiva* nayo inamaanisha kuwa tayari kwa kiasi fulani kwamba watu wako katika hali ya upeo wa kufanya kitu kama kusoma au hata ngono.

**Mshiriki B**: Ni kama kuchomeka. kwangu mimi nafikiri ni kuchomeka ambapo msanii analeta dhana ya kuchomeka kutoka kwa ile ya upishi.

*Jedwali linaloonyesha maana za maneno teule*

**MAHOJIANO**

**Mahojiano na msailiwa wa kwanza**

**Mtafiti**: Je, wasikilizaji wanatumia nini kuwawezesha kuzua maana nyingine ya maneno haya ya kawaida ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo hizi? Kwa mfano waka, washa, kibao.

**Msailiwa 1**: Bila shaka mwanzo ni kwamba wanatumia ujuzi wao wa lugha kama wasemaji wa lugha kisha wanatumia ujuzi wao wa miktadha mbalimbali ambamo lugha hutumiwa. Kwa hivyo wakisha kujua lugha yenyewe kuizungumza na pia kuelewa wanapozungumziwa au wanapolengwa wao na maneno Fulani.Kisha kujua neno limetumiwa katika miktadha gani, kwa kusudi gani kwa hivyo wanaeza kunyumbua maana kwa misingi kwamba ni wajuzi wa lugha na kisha miktadha ya matumizi ya lugha.

**Mtafiti**: Je, vipi kuna maana nyingine ya maneno haya ya kawaida katika nyimbo hizi, kwa mfano; rusha, kibao, chota n.k. Huku kuzuka ka maana hizi zaidi kunasababisha na nini haswa?

**Msailiwa**: mambo mengi. Ah unajua kila neno huwa na labda etimolojia yake ya kipekee kwa mfano neno waka. Ni kawaida kwa wanywaji wa pombe na hata kama si wanywaji kaika kuumia lugha katika muktadha wa kutumia vileo na nini. Mtu aliyelewa huambiwa kwamba amewaka kwa sababu gani? Pombe ndivyo ilivyo, humwasha mtu. Ikawa labda ni mwenye kuweza kufanya mambo ambayo kawaida hangefanya. Kwa hivyo, anaambiwa kwamba amewaka na pombe yenyewe namna inavyotengenezwa ni kwamba kuna kuchemshwa ushaona? Kwa viungo fulanifaulani na ule moto ndio huzusha nini, kutengezeka kwa pombe hivyo kwa sababu ya kutumia moto na mambo kama hayo sasa wanahusisha. Maanake na wewe umekuwa pombe ukishalewa umewaka. Moto uliotumika katika kuchemsha vile viungo kutengeneza pombe umekuingia wewe kwa hivyo umewaka nawe pia.

**Mtafiti**: Je, unafikiri nafasi ya muktadha ni ipi katika mchakato wa kufanyiza maana katika nyimbo hizi?

**Msailiwa**:Wajua semantiki hasa pragmatiki maana ni muktadha ushaona?Neno hupewa maana na muktadha.La sivyo wajua  maneno haya hayana maana.Hupewa maana na miktadha ,miktadha mbalimbali kwa neno moja litakuwa na maana hivi katika muktadha huu neno lilelile litakuwa na maana tofauti katika muktadha tofauti uashaona?Ukisema kwamba mtu huyu ni mchafu kiwanjani .Huu ni muktadha wa kiwanjani,michezoni ,ule uchafu si sio kwamba kapakwa tope ahaha ni tofauti.Mtu anaweza akawa mchafu kwamba

matendo yake si mazuri siyo,katika muktadha mabpo tunazungumzia tabia,muktadha uwe ni tabia.Muktadha ni mchezo kwa hivyo mtu mchafu ni kwamba yeye ni hodari sana katika ule mchezo .hivyo, muktadha ndio hutupa maana ya neno.Maneno yenyewe kama yalivyo hayana maana.

**Mtafiti**: Kwa hiyo waimbaji hawa haswa huzingatia sana lile suala la muktadha wanapotunga nyimbo zao kwa sababu wana maana wanavyokusudia.

**Msailiwa**: Eeh na waimbaji kama wasanii kwa sababu ya kwamba wanataka kuyarembesha mambo kuyafanya yawe yenye kuvutia n. k wao huvuta miktadha mbalimbali na maana mbalimbali ili kutekeleza lile jukumu la kuweza kluburudisha, kufunza au kuonya na mambo kama hayo. Huzingatia sana miktadha na kile ambacho wanajua kwamba wasikilizaji wanakijua. Wajua katika kuzungumza na hasa mawasiliano ni kwamba mwasilishi na mwasilishaji lazima wawe wana muoano fulani wa kufairi maana, ujumbe na kadhalika.

**Mtafiti**: Kwa misingi hii je kuna uwezekano wa kuvurugika kwa mawasiliano na kupotea kwa maana iliyokusudiwa na waimbaji katika mtazamo wa wasikilizaji wa nyimbo hizi, pamoja na kwamba kuna maana zaidi inayozuliwa kutoka kwa maneno haya ya Kiswahili yalivyotumiwa katika nyimbo

**Msailiwa**: Bila shaka.Kuvurugika kwa maana ni kwamba labda msikilizaji anayehusika eh si mmoja wa lile kundi- lugha ,sijui kama tunaelewana.Maanake hata tunapozungumza tuna makundi lugha mbalimbali kwa hivyo kama unasikiza muziki amabo labda ni wa umri Fulani ,wew e si mmoja wa lile kundi basi hutaelewa na hata katika mazungumzo ya kawaida,watu wanaweza wakawa wanazungumza na wewe kwa sababu si wa kundi- lugha hilo…you know you are lost.So huko ndiko kuvurugika sasa kwa mawasiliano au maana kwa sababu mwimbaji anapoimba anasikizwa na watu wengi; wale ambao wapo katika kundi-lugha lake na wale ambao labda hawapo.Kwa hivyo kuna tena labda ambaye haelewi ,lazima aulize,afunzwe au ajizoeshe.

**Mtafiti**: Sasa maana …wajua maneno haya ni maneno ya kawaida sasa yakitumika wasikilizaji wale wakitumia maneno haya labda katika mazingira mengine tofauti nje ya muziki, je watayavuruga mawasiliano?

**Msailiwa**: Inategemea, kama anazungumza na kundi lao au katika kundi lugha lao hakuna taabu maanake maneno yale wanyaotumia katika muziki kama unavyosema ni maneno ya kawaida lakini hupewa maana mbalimbali. Kama mtu yuko katika kundi lake la lugha hakuna taabu lakini na binadamu nao hujua. Akitaka kuzungumza na watu anaichuja ya kwamba hadhira yake ni ya kwake au tofauti na ndio kwa sababu watu hubadilisha lugha. Wanamuziki haohao si kwamba wanavyoimba ndivyo wanavyozungumza. Wana uwezo zaidi wa kunyumbua lugha kwenda kulia kushoto kutegemea na hadhira.

**Mtafiti**: Je, nyimbo hizi za kizazi kipya hasa za Nonini na Juacali zinaithiri vipi lugha ya Kiswahili?

**Msailiwa**: Usanii wowote ule ni kwamba huchangia lugha kwa kujenga au hata kubomoa na…. ndivyo mambo yalivyo kwamba lugha ipo kama fenomena moja kati ya wasemaji wa lugha kwamba hujengwa na kubomolewa vilevile. Ni kama elimu unaweza kuchangia kwa kujenga au kubomoa ni kama nyumba wewe labda unaweza kuacha nyumba ikawa chafu au ukaisafisha au hata ukaimarisha zaidi usafi wake. Na ndivyo lugha ilivyo. Ni fenomena ambayo hutumiwa kati ya binadamu kwa hivyo mchango unawezekana ni kotekote….

**Mtafiti**: Je, mustakabali (hali) wa Kiswahili ni upi hasa tukizingatia maana hizi zinazochipuka hasa katika nyimbo hizi?

**Msailiwa**: Kiswahili kama Kiswahili na kama lugha lazima kiwe na uwezo wa kustahimili mapigo ya namna hii. La sivyo haitakuwa lugha. Itaporomoka iwe si lugha tena na tunajua lugha zisokufa. Kama lugha haina uwezo wa kustahimili mapigo na mitindo ya kawaida katika maisha na katika matumizi yake eeh itakuwa ni lugha hafifu. Na mimi najua kwamba Kiswahili ni lugha ambayo ina nguvu, inaweza kustahimili, itakuwa tu inajimudu katika uwepo wake kama lugha inayotumiwa na watu wengi. Kuna wale ambao hata ikibomolewa huku wao husawazisha kama wewe unavyofanya utafiti. Utatuambia kama haya yanatupeleka wapi. tuone kama tutabadili mkondo au labda… Wakati mwingine katika kule ambako lugha i katika hatari fulani ndio huipa nguvu tena maanake inajikaza. kwa hivyo, kiwa Juacali, Nonini, zile bongo na nini kama zinapigapiga Kiswahili kwa namna fulani ambayo labda itawia kiswahili ugumu fulani kuna wale ambao wanarekebisha. Na ndio kazi hasa ya watafiti, walimu wa lugha kuonyesha labda tuna vilugha ushaona? Hakuna lugha kama Kiswahili, kuna viswahili kama katika nyimbo hizi za juacali, Nonini na wengine. Kuna Kiswahili rasmi ambayo tunajua lakini si cha pekee, kuna Kiswahili cha Congo, Burundi na ni Kiswahili. Kuna Kiswahili cha waingereza wanaotoka Ulaya ambao asili yao Uiingreza, Ujerumani wanazungumza Kiswahili na kile ni Kiswahili.Tusichukulie kwamba kuna lugha itakuwa ni moja kama kiingereza. Kiingereza kile cha ‘Ugo come’ ya Nigeria na kile cha London’Queen’s English ni rasmi.

**Mtafiti**: Kwa misingi kwamba kuna viswahili ulivyotaja mtu atachukulia kwamba sasa kuna mtazamo wa Kiswahili kupotoka au kutopotoka?

**Msailiwa**: Katika lugha ni vigumu kuzungumzia kupotoka. Maanake wanaotumia lugha moja ni wengi na wana lugha zao zinaathiri matumizi ya lugha ya pili, tatu n.k. Kisha baadaye lugha hizi zinaathiri hata lugha ya mwanzo kama lugha mame huathiriwa pia nyingine. Kwa hivyo utampata mtu mzaliwa wa kijaluo au dholuo akiwa sasa anaanza kuingizaingiza maneno ya kiingereza, Kiswahili katika dholuo. Mengine inaingia ikakaa katika Kiswahili, mengine yanatoka kwenda katika kiingereza. Kwa mfano kila mwaka Oxford wanazidisha maneno katika kamusi yao. Mara kwa mara maneno ya Kiswahili

yanaingia katika kamusi ile ya oxford kama maneno ya kutumiwa katika lugha ya kiingereza. Ndivyo lugha ilivyo. Wakati mwingine unapoona kwamba lugha ni kama inapotoka eeh sas ndio nguvu zake zinatokea pale kwenye kupotoka huko. Ikitoka kule ikija huku inapewa nguvu zaidi na mimi ni mmoja wa wale wanaosema kwamba tusizuie lugha kwamba isiende katika mkondo Fulani. Acha iende ikirudi tuiangalie.

**Mtafiti**: Kwa hiyo je ina maana hizi zaidi zinazozuka katika nyimbo hizi zinakubalika katika jamii ama ni kwa kuzingatia kundi-lugha tena?

**Msailiwa:** Kukubalika au kutokubalika …. hivyo si vigezo. Maneno hayo yanatumika na kwamba kuna kundi-lugha inayotumia lugha kama inavyotumia lugha. Lugha ni hai na lile kundi lugha likwa hai, lugha pi aitakuwa hai. Kiswahili ni hai kwa hivyo kitumiwe vivyo hivyo katika muziki. Acha watumie. Wacha watumie lugha iwe hai pale. The English language is such a powerful language kwa sababu wao wanakiacha kiingereza kienee. ikija uswahilini kiingereza kikapata neneo kikarudi nalo. Kule wanasema hii tuituie tajaze hii, tutumie hii. Hawachukui kila kitu lakini baadhi kama safari hii tuichukue. Maanake katika utamaduni wa muiingereza ni ajabu, wana journey, travel n.k. maneno hayo yalikuwa hayatoshi. Unapata neno kama 'safari' ambalo ndilo neno limetoka uarabuni likaingia katik …kwa hiyo lugha inakua.

**Mtafiti**: Kiswahili kiko vile?

**Msailiwa**: Kiswahili kiwe vile. Sisi wakati mwingine tunafuata ufasha mpaka kuna mambo ambayo tunapoteza.Huufasaha huowa akina Hassan Mwl Mbega kukosoa….sasa tunaizamisha .Wajapani wanasema msumari ndio unaogongwa.Sasa watu wasemaji,waalimu,waalimu wa Kiswahili wao kazi yao ni kugonga mpaka hata hujui kama kuna misumari wapi eeh.Kwa hivyo mimi huona kwamba kokote ambako lugha inakwenda kuna uwezekano wa lugha kujijenga kwa namna hiyo.Dholuo na luhya wakati mwingine hatujui neno ni la wapi but both languages are using it.both languages are very strong with words like 'Nyasaye'.They use it in churches and wherever. You can't mistake this for luhya or dholuo.

**Mahojiano na msailiwa wa pili**

**Mtafiti**: Je, wasikilizaji wantumia nini kuwawezesha kuzua maana nyingine ya maneno haya ya kawaida ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo hizi? Kwa mfano waka, washa, kibao.

**Msailiwa**: kwa mtazamo wangu nafikiria kwamba wasikilizaji wanapotafuta maana itabidi watafute dhana ya maneno yale minaarafu ya mikadha lakini la ziada ni kwamba maneno

hayo kwa sababu mengi si ya lugha sanifu ya Kiswahili yana utata na ni maneno ambayo ni vigumu kupata maana basi hawana budi kuzingatia muktadha wa wimbo husika.

**Mtafiti**: Kwa misingi ya maneno ambayo ni ya Kiswahili kama vile waka, washa, kibao n.k watatumia mbinu gani kuzua maana nyingine kwa sababu maneno haya yana maana kadiriinayopatikana labda kwenye kamusi?

**Msailiwa**: Tuchukulie kwamba, wimbo ni utanzu wa fasihi simulizi na pale mtunzi ana uhuru katika uteuzi wa maneno atakayotumia. Basi wao wanapoyatumia maneno yale kuna maana na ujumbe wanaotarajia kupitisha kwa hadhira. Basi sidhani kama kuna tatizo. Japo, wakati mwingine wale wasikilizaji hufurahia tu mapigo ya muziki lakii wanatoka bila kupata maana ya maneno halisi katika nyimbo hizi.

**Mtafiti**: Je, ni vipi kuna maana nyingine ya maneno haya ya kawaida katika nyimbo hizi kwa mafano rusha, kibao, chota n.k

**Msailiwa:** Maneno haya hupata maana zaidi ya moja kwa sababu ya kuzuka kwa kijilugha cha Sheng’ kinachonekana kutosheleza mahitaji ya vijana, kizazi ambacho hakijazidi miaka 30.wao hutilia maanani sana matumizi ya kijilugha hiki. Wanapotumia kijilugha hiki kinawaruhusu kubuni ama kutumia maneno ambayoyamo na kuyapa maana zaidi ya zile zinaojulikana. Basi wanapoimba nyimbo zao wanalazimika kufanya hivyo. Jambo la pili wakati mwingine wanakuwa na uhaba wa msamiati basi wanalazimika kutumia maneno kurahisisha mawasiliano ama kufidia uhaba wa msamiati katika mazungumzo yao katika kupitisha ujumbe.

**Mtafiti**: Je, unafikiri nafasi ya muktadha ni ipi katika mchakato wa kufanyiza maana katika nyimbo hizi?

**Msailiwa:** Msingi wa kuelewa kaiz yoyote iwe nyimbo au shairi ni muktadha basi kuelewa mazingira hayo ambayo mtunzi amezingatia itakuwa ni vigumu sana. Kuna baadhi ya nyimbo ambazo zimeimbwa na ikawa vigumu kwa watu wasikilizaji kupata maana kwa sababu ukikosa kupata muktadha a wimbo basi itakuwa vigumu wewe kuelewa yanayozungumziwa. Ama unaweza kupata maneno u ukakosa kupata kusudio la mtunzi katika utunzi wa wimbo wake.

**Mtafiti**: Je, kuna uwezekano wa kuvurugika kwa mawasiliano na kupotea kwa maana iliyokusudiwa na waimbaji katoika mtazamo wa wasikilizaji wa nyimbo hizi, pamoja ikizingatiwa kwamba kuna maana zaidi kutoka kwa maneno haya ya kiswahili yalivyotumiwa katika nyimbo teule.

**Msailiwa**: Kweli kwamba mara nyingi na sio wakati mmoja tu tuseme asilimia 30 ya watu wanaotumia maneno haya katika nyimbo hizo ndio hupata ujumbe lakini asilimia 70 ya watazamaji au wasikilizaji hupotoka yaani hawapati mantiki kabisa. kuna watu

watakaposikia neno kwa kurejelea misingi ya masomo wanaweza kulifasiri neno hilo kwa njia tofauti kabisa. Lakini kuna wale ambao labda kwa kukosa nafasi ya kwenda shule ama kiwango duni cha masomo wanaweza kupata maana tofauti basi neno moja linalotumika katika nyimbo linaweza kuzua maana nyingi tofauti tofauti.

**Mtafiti**: Je, nyimbo hizi za kizazi kipya hasa za Nonini na Juacali zinaithiri vipi lugha ya Kiswahili?

**Msailiwa**: Tukisema kwamba zina mchango hasi pekee tutakuwa tunakosea kwa sababu lengo la lugha ni mawasiliano na Kiswahili kama lugha nyingine pia bado ingali inakua basi wasanii wanapotumia lugha wanatusaidia kupata msamiati ambao baadaye unaweza kuruhusiwa na kutumika katika lugha. Pili, inaruhusu kutumia lugha iliyolegezwa kidogo na hivyo hufanya mawasiliano kuweza kukamilika. Vilevile inakuwa ni tatizo haswa kwa wale wanaokusudia kutumia lugha sanifu hasa wanafunzi na hivyo kufanya matokeo yao ya mtihani wa matumizi ya lugha kudidimia kabisa. Basi kwangu naona japo kuna mchango hasi muziki huu wa kizazi kipya pia unatusaidia kukuza lugha ya Kiswahili.

**Mtafiti**: Je mustakabali wa kiswahili (hali) wa Kiswahili ni upi hasa tukizingatia maana hizi zinazochipuka hasa katika nyimbo hizi.

**Msailiwa**: Tunapoelekea hauna budi kuendelea kuongeza msamiati kutokana na uvumbuzi wa sayansi na teknolojia. Kuna maneno yanayoongezwa katika lugha kila kuchao. Vilevile wanamuziki hao wanapotumia maneno haya, maneno haya yatakapofanyiwa utafiti utafika wakati ambapo maana hizo yataruhusiwa na kutumika katika lugha ya Kiswahili.

**Mtafiti**: Hivi unamaanisha kwamba maana hizi zitaishia kupata ukubalifu kwa kiwango fulani katika jamii?

**Msailiwa**: Bila shaka maana hizi za ziada zitaishia kukubalika na hata huenda zikatumika katika lugha.

**Mtafiti**: Je Kiswahili kinapotoka maneno haya ya kawaida, yanapopata maana zaidi hasa katika nyimbo hizi teule

**Msailiwa**: Hatuwezi kusema kwamba Kiswahili kinapotoka japo tukiangalia namna ambvyo lugha zinaendelea kukuzwa, Kiswahili kinapata changamoto kutoka kwa lugha nyingi na kuna wakati ambapo inabidi Kiswahili pia kifanyiwe bidii kuhakikisha kwamba kinapewa nafasi. kwangu naona maana hizi yanachangia ujenzi wa msamiati wa lugha na baada ya muda zitaruhusiwa tu kwahivyo sioni kama wanaozitumia wanapotoka. Halafu, katika utunzi wa nyimbo hizi ni vigumu kutumia maana sanifu za maneno haya kwani mara nyingi watunzi wanakusudia kupitisha tu ujumbe kwa hadhira lengwa kwa njia fiche. basi wanapotumia lugha kwa njia sanifu itakuwa vigumu kuweza kuficha siri haswa kwa kile kikundi ambacho si lengwa kwa hivyo wanalazimika kutumia maana hizi za maneno haya

japo ya kawaida. Kimsingi, maana hizi kabla ya kutumika katika lugha yafanyiwe utafiti, yakubaliwe na kupokelewa kama sehemu ya lugha ya Kiswahili.

**Mahojiano na msailiwa wa tatu**

**Mtafiti**: Je, wasikilizaji wantumia nini kuwawezesha kuzua maana nyingine ya maneno haya ya kawaida ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo hizi? Kwa mfano waka, washa, kibao.

**Msailiwa**: Wao huwa wanabuni upya maana ya manneno kulingana na miktadha mbalimbali na pia yale ambayo waimbaji wanataka wawasilishe kwa wasikilizaji kwa mfano rusha roho inaweza kuchukuliw akumaanisha wakati ambapo wasikilizaji wanasikia wimbo wanaweza kucheza na mara nyingi kucheza huko kukaandamana na miondoko. Sasa kurusha roho inatoa picha ya hali ya furaha isiyo ya kawaida. Neno kama kibao huleta dhana ya kiasi fulani lakini kwao viwango havipo, muziki kibao inamaanisha muziki wa kufaurahia bila kuthibitiwa.

**Mtafiti**: Kwa hiyo mbinu wanazotumia labda ni miktadha na ujuzi wa lugha au kusudi la kuwasilisha ujumbe…….

**Msailiwa**: Eeh ndio kusudi na pia kulingana na msisimko kwa waskilizaji.

**Mtafiti**: Je ni vipi kuna maana nyingine za maneno haya ya kawaida katika nyimbo hizi kwa mafno; rusha, kibao, chota n.k

**Msailiwa**: kulingana na wanamuziki wa kisasa huwa wamebobea kwa kijilugha cha Sheng'kwa hiyo unapata neno likitoka katika kiswahili sanifu na kuingia katika lugha hii ya vijana.waimbaji hutaka kujitambulisha n vijana na pia wanafanya utafiti wa yale yanayowafurahisha vijana .hivyo misemo kama rusha roho ipo kwa ajili ya kuwafikia na kuwafurahisha vijana.Wanaolengwa katika nyimbo hizi ni vijana na utapata kwamba wazee hata wakisikia nyimbo hizi hawafurahii wanasema ni mambo ya vijana.sasa ili wasanii wajitambulishe ana wawafikie vijana lazima watumie lugha ya vijana .hivyo maana hizi zaidi zitaibuka kutokana na mtazamo wa walengwa kaika nyimbo zenyewe.

**Mtafiti**: Je unafikiri nafasi ya muktadha ni ipi katika mchakato wa kufanyiza maana katika nyimbo hizi?

**Msailiwa**: Muktadha huwa na nafasi. Muktadha ulipo hapa ni wa mazungumzo ya vijana mabayo wazee hawapati. Mawasiliano hapa yamefanikishwa miongoni mwa vijana na kuwatenga wazee. Katika nyimbo hizi walengwa ambao ni vijana wanapata ujumbe kwani nyimbo inajikita katika miktadha yao

**Mtafiti**: Je, kuna uwezekano wa kuvurugika kwa mawasiliano na kupotea kwa maana iliyokusudiwa na waimbaji katika mtazamo wa wasikilizaji wa nyimbo hizi pamoja na kwamba kuna maana zaidi inayozuliwa kutoka kwa maneno haya ya Kiswahili yalivyotumiwa katika nyimbo teule.

**Msailiwa**: Ni kweli. Vijana hawa wanaishi katika maeneo tofautitofauti sasa unaweza ukapata maana ya neno katika eneo fulani ni tofauti na maana ya neno lenyewe katika eneo jingine. Watajifanya tu kwamba wamepata ujumbe ilhali fasiri yao ni tofauti kwa sababu mtindo huu wa lugha katika mauizki huwa si sanifu. Watu wa eneo fulani wanazua maana yao wengeine katika eneo jingine wakibuni yao. Sasa wakizua maana hivyo wanachukulia kwamba wamepata ujumbe lakini ni kieneo wala si fasiri ya jumla.

**Mtafiti**: Kwa hiyo kuna uwezekano wa kuvurugika kwa mawasiliano kunakosababishwa na zile tofauti za kimaeneo?

**Msailiwa**: Ndio tofauti za kimaeneo. Ni kweli.

**Mtafiti**: Je, nyimbo hizi za kizazi kipya hasa za Nonini na Juacali zinaithiri vipi lugha ya Kiswahili?

**Msailiwa**: Nyimbo hizi zinaithiri lugha ya Kiswahili kwa sababu huvurugika maana sanifu za maneno. Tuna maana za maneno tunazojua ni sanifu ama mantiki. Tunapata kwamba neno ambalo tuseme limeandikwa katika kamusi sasa wao watavuruga neno hilo hadi neno lenyewe liwe lina maana ambayo haikuwepo hapo awali. Sasa utapata hata wanafunzi wenyewe ambao wamekulia katika kizazi cha kisasa huwa hawapati maana hizi asilia hasa katika mtihani. Wanatumia maana zile katika muktadha wa kimuziki.

**Mtafiti**: Je mustakabali (hali) wa Kiswahili ni upi hasa tukizingatia maana hizi zinazochipuka hasa katika nyimbo hizi.

**Msailiwa**: Natumai kwamba kuchipuka kwa maana hizi kutokana na neno moja maana yake kuvurugika inafanya maenezi ya Kiswahili yanatingwa na maendeleo ya Kiswahili yanatingwa tunapata sasa Kiswahili kiankuwa ovyo tu, watu wanatumia lugha viovyo hawanuii maana kusudiwa na wale watunzi wa kamusi ambayo ndio inayochukuliwa kuwa asilia. Sasa neno limevurugwa hata hujui maana halisi ni ipi. Kiswahili basi kitaishia kuwa lugha ya watu ovyo amabo hawajajipanga, hapo panakuwa hata na utata katika upangaji wa lugha, maenezi yake na maendeleo yake.

**Mtafiti**: Je Kiswahili kinapotoka maneno haya ya kawaida, yanapopata maana zaidi hasa katika nyimbo hizi teule:

**Msailiwa**: Kiswahili chenyewe hakijapotoka watu ndio wanakipotosha. Unapata hata kama mttu amebuni Kiswahili bado ni sanifu lakini wao wenyewe wanayaingiza yale ambayo si yaliyonuiwa. Sasa wao wenyewe wanakipotosha Kiswahili. Wakati huu Kiswahili

kimevurugwa ni ovyo ovyo, shaghalabagala, huwezi kusema hata huwezi ukakienzi katika hali hii. Kiswahili tunakienzi kwa sababu ni lugha ya kiafrika sisi wenyewe ndio waasisi, asilia yake ni huku pwani ya afrika mashariki. Lakini sasa sisi wenyewe tumekivuruga mambo ya vijana, mtindo wa sheng'. Hata wengi wanaona anayezungumza kwa Kiswahili ni mtu mjanja kwa sababu ujanja fulani ulioingia ndani ya Kiswahili. Haya zaidi yanatinga maenenzi ya Kiswahili. mchango wa nyimbo hizi za kizazi kipya ni hasi na yaniathiri sana lugha ya Kiswahili.

**Mahojiano na msailiwa wa nne**

**Mtafiti**: Je, wasikilizaji wanatumia nini kuwawezesha kuzua maana nyingine ya maneno haya ya kawaida ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo hizi? Kwa mfano; waka, washa, kibao. (

**Msailiwa**: Yeah, haya ni maneno ya kawaida lakini fasiri yao inategemea ni umri upi wa wasikilizaji uanohusika. kama ni watu wa makamu, wazee basi maan ahizo zitakuwa vigumu sana kwao kupat lakini msamiati mwingi uanotumika na wanamuziki huwa ni msamiati wa kirika na huwa umebobea katika rika la vijana. Sasa wengi kwa sababu ni msimbo wanaotumia kila wakati wanaweza kupata maana hiyo lakini wengi ambao hawana tajriba hiyo huwa ni mpaka wapate maelekezo.

**Mtafiti**: Kwa hiyo ni matumizi ya …. yaani wanatumia tajriba yao ya lugha na kiutangamano?

**Msailiwa**: Wanatumia tajriba yao ya lugha na utangamano ni vipi wanaelewa jinsi lugha hiyo inavyotumiwa.

**Mtafiti**: Je ni vipi kuna maana nyingine ya maneno haya ya kawaida katika nyimbo hizi kwa mfano rusha, kibao, chota.

**Msailiwa:** Mwanzo maneno hayo kijuujuu unaweza kuchukulia ni maneno yametumika kikawaida tu. Haya ni maneno yanayotumika kawaida katika lugha lakini jinsi yanavyotumiwa katika nyimbo hizi huwa yana maana fiche. Huwa yanalenga kuzungumzia masuala yanayofanyika katika jamii lakini wanayatumia kama mafumbo. Unapata mara nyingi mambo wanayoyaimba wasanii hawa ni mabo yanayohusu mapenzi, hali za kutangamana kati ya mwanaume na mwanamke au wavulana na wasichana. Kwa hivyo utakuta kuna zaidi ya mambo yale wanayoyazungumzia.

**Mtafiti**: Je unafikiri nafasi ya muktadha ni ipi katika mchakato wa kufanyiza maana katika nyimbo hizi?

**Msailiwa**: Muktadha ni muhimu sana kwa sababu kikawaida maneno haya yanapotumiwa katika mazungumzo ya kawaida hamna fasiri nyingine ya ziada. Lakini hapa katika sajili ya muziki hasa unapozingatia hawa ni vijana wenzao. utapata kwamba muktadha wa kufasiri

maneno haya ni muhimu sana kwa sababu kikawaida hayawezi kutumika tu hivyohivyo. itabidi ujiweke katika muktadha wa kiburudani, muktadha wa kimawasiliano kwa hali ya kufundisha na pia kutumia mambo yanyofanyika katika jamii kupitia nyimbo hizo kwa hivyo muktadha huo ni muhimu sana katika fasiri hizo.

**Mtafiti**: Je kuna uwezekano wa kuvurugika kwa mawasiliano na kupotea kwa maana iliyokusudiwa na waimbaji katika mtazamo wa wasikilizaji wa nyimbo hizi, pamoja na kwamba kuna maana zaidi inayozuliwa kutoka kwa manneo haya ya kiswahili yalivyotumiwa katika nyimbo teule.

**Msailiwa**: Ni kweli  mawasiliano yanaweza kuvunjika na hata  kukuleta vita miongoni mwa wasikilizaji maanake kuna wakati nimemsikiza mzee fulani akihojiwa akiulizwa ,je muziki wa kisasa uanukadiria vipi? sasa yeye akawa anazungumzia mambo ya kupiga randa,kupiga nyundo  na juala.Yeye anachukulia maneno haya katika muktadha wa kawaida maanake kila mtu anajua karatasi ya kubeba bidhaa au vbitu kwenda sokoni.Sasa yeye anapoulizwa kwamba watu watumie juala ili wasipate taabu wanapobeba vitu vyao ama wanaposafiri na vitu vyao.Yeye fasiri ni tofauti sana na jinsi ilivyokuwa katika wimbo ule. sasa yeyekatika muktadha wa kawaida unaweza kumpata anazungumzia mambo haya ,hali inayomweka katika aibu maanke yeye fasiri anayotoa katika muktadha huu ni tofauti na jinsi mwimbaji alivyokusudia.Kwa hivyo unakuta kwamba hali kama hizi zinaweza kuzusha aibu au vilevile zizushe mtafaruku katika mawasiliano kiasi cha watu kukuona wewe pengine ni mpumbavu unayezungumzia vitu ovyoovyo katika jamii ama huna heshima katika lugha yako.Ingawa kwenye muziki unavyoimbwa na maneno yale yanapotamkwa watu huchangamkia lakini katika mazungumzo ya kawaida yanaweza kuleta matatizo.

**Mtafiti**: Je nyimbo hizi za kizazi kipya hasa za Nonini na Juacali zinaithiri vipi lugha ya Kiswahili?

**Msailiwa**: Tunavyojua lugha hukua kila siku na mambo mapya huibuliwa mengine yakachukuliwa na lugha, mengine yakapuuliziwa mbali. Tunapozingatia zaidi matumizi ya lugha jinsi watu wanvyotumia lugha katika jamii ndipo tunapoelekeza kipengele cha maana. Kwa hivyo unakuta kwamba baadhi ya maneno yaliyotumika na yakubalike kwa urahisi basi yataingizwa katika msamiati unaotumika na watu kwa kawaida. Tunavyojua ni kwamba lugha haijikiti katika kamusi kwamba maneno ya kamusi ndio yenye maana pekee yake katika matumizi. Watu huibua maana za maneno kulingana na jinsi yanavyotumika. kwa hivyo utakuta kwamba mchango wa muziki huu wa kisasa ni ule wa kupanua maana asilia ya maneno katika lugha. Hata hivyo, kuna athari kwamba msamiati huu ibuka unaweza pia kutatanisha matumizi sahili ya Kiswahili kiasi cha kupata upotovu wa maana na wale wanaojifunza hasa wakiwa ni wale vijana chipukizi, wanaweza kuwa na mwelekeo tofauti wa maana ya maneno eeh kama walivyoathiriwa na muziki wao.

**Mtafiti**: Je mustakabali (hali) wa Kiswahili ni upi hasa tukizingatia maana hizi zinazochipuka hasa katika nyimbo hizi.

**Msailiwa**: Kama nilivyosema haswa lugha yoyoteile hukua na Kiswahili ni lugha changa sana na utakuta kwamba lugha ya muziki ina upekee wake. Lugha yoyote ile hukua na Kiswahili ni lugha changa sana na utakuta kwamba lugha ya muziki ina upekee wake.Lugha hii kama kuboronga sarufi na usanifu wa lugha lakini kimatumizi hasa kwa lengo la kuwasiliana ni muhimu sana maanake ni lugha nzito.Utakuta kwamba msamiati ambao unatumika katika muziki huu ni msamiati wenye picha pana zaidi ya yale yanayozungumziwa.kwa mfano nyundo ni kifaa cha ujenzi tu lakini mpigo ule wa nyundo na zile ishara zinazoandamana na matumizi ya nyundo unapozipana kitaashira na kuzielekeza katika tendo la kimapenzi utapata ule mpigo wa hali ya juu zaidi ukilinganisha na jinsi msanii atakavyozungumzia kwa kawaida mambo ya kimapenzi n.k. kwa hivyo unakuta kwamba msamitai ule ni msamiati unaotumia…ninasema ni tamathali ya hali ya juu ya usemi. Ni msamiati wenye ishara kubwa na hujenga taswira/picha pana zaidi inayoweza kumpanulia na kumpa mtu maana halisi maana kimatumizi jinsi maneno hayo yanavyotumika.

**Mtafiti**: Je, Kiswahili kinapotoka maneno haya ya kawaida, yanapopata maana zaidi hasa katika nyimbo teule?

**Msailiwa**: Hakipotoki pengine watu wenye mtazamo wa kimapokeo ndio wanaweza kusema kwamba Kiswahili kinapotoka lakini tunavyojua kwamba mtu anapojifunza lugha hujifunza lugha kutokana na matumizi na ni lugha ya sajili Fulani na upotoshaji wa Kiswahili huja zaidi katika matumizi mabovu na hapa si matumizi mabovu bali ni matumizi ya kisanaa matumizi ya kisanaa kamwe hayawezi kuharibu lugha. Ni njia mojawapo za kuendeleza lugha hivyo katika nyanja za kimatumizi. Pengine useme vijana wale wanaojifunza lugha waanze kuiga matumizi hayo na kuyatumia katika usanifu wa lugha pasipo kujua kawamba hayo ni matumizi ya kisanaa. Pindi tu waenzi/wapenzi wa Kiswahili wanapojua kwamba lugha hii ni lugha ya kipekee katika muziki hakuna tatizo lolote unapoiambatanisha na lugha sanifu ya Kiswahili.Lugha ina mawanda yake kimatumizi na muziki ni uwanda mmoja tu wa kuonyesha ujuzi huu kwa hivyo zozote asi ambazo zinaweza kusemekana zinaiharibu laugha hiyo hapana.

**Mahojiano na msailiwa wa tano**

**Mtafiti**: Je wasikilizaji wanatumia nini kuwawezesha kuzua maana nyingine ya maneno haya ya kawaida ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo hizi? Kwa mfano waka, washa, kibao n.k

**Msailiwa**: Kinachotendeka ni kwamba wanamuziki pia wana sheria ambazo mara nyingi wanafuata, huwezi ukaweka mambo peupe tu moja kwa moja. Kwa hivyo mara nyingi wanatumia mbinu ya kufumba. Wanatumia maneno ya kawaida ndio, lakini wanajaribu kuyatumia kwa namna ambavyo msikilizaji hawezi akapta maana moja au akipata maana moja kwa moja na ile maana ambayo imefichwa ili mambo ya siri yasijitokeze tu moja kwa moja.

**Mtafiti**: Je, ni vipi kuna maana nyingine ya maneno haya ya kawaida katika nyimbo hizi kwa mfano rusha, kibao, chota n.k.

**Msailiwa**: Ndio sasa unajua maana inapokuwa zaidi ya moja inategemea na neno lilitumika vipi na kitu kinachoachangia hali ya kuwa na maana zaidi ya moja ni suala la muktadha/ mazingira ya matumizi kwa hivyo k.m. chota tunajua maana yake ya kawaida mabayo inapatikana katika kamusi lakini sasa inapotumika katika muktadha wa muziki na hasa muziki wa kizazi kipya inategemea.  wakati mwingine labda neno hili litaelekea kumaanisha rushwa lakini neno lenyewe linaweza kutumika jinsi unavyofikiria katika ile hali ya kimapenzi kwamba umepata msichana ukitaka kumwomba labda katika ile hali ya ngono huyo mvulana sasa anamwambia achote tofauti na ile 'chota' ya kawaida.

**Mtafiti**: Je unafikiri nafasi ya muktadha ni ipi katika mchakato wa kufanyiza maana katika nyimbo hizi?

**Msailiwa**: Muktadha ni jambo muhimu katika kutoa maana ya maneno na unapoangalia ile taaluma ya semantiki. Maana inaweza kuangaliwa kwa jinsi tofauti tofauti. Kuna ile maana ya kileksia na kimuktadha. Wale wanaotumia hiyo lugha na pia neno husika wataangalia huu muktadha; nikitumia neno hili basi maana itakuwa hii. Maana hii itakuwa tofauti pia wakielekea katika muktadha mwingine tofauti. Kimsingi hao vijana wanaoimba nyimbo hizi za kizazi kipya unajua kulingana na umri wao bado wana mazoea ya kuzungumzia masual ya kimapenzi n.k kwa hivyo unaweza kuchukua ule muktadha wa hali, naweza kusema ni hali yao ya maisha katika kiwango kulingana na umri wao.

**Mtafiti**: Je, kuna uwezekano wa kuvurugika kwa mawasiliano na kupotea kwa maana iliyokusudiwa na waimbaji katika mtazamo wa wasikilizaji wa nyimbo hizi, pamoja na kwamba kuna maana zaidi inayozuliwa kutoka kwa manneo haya ya kiswahili yaliyotumika katika nyimbo teule.

**Msailiwa**: Ni kweli kuna kuvurugika kwa mawasiliano na hali hii huotkea kwa sababu hizi nyimbo si lazima zisikizwe katika dancehall pekee. Nyimbo hizi zinaweza pia kusikizwa hata nyumbani vijana hao wanapokuwa wameketi na wazazi wao. Inaweza kuwa unasafiri ukakuta gari limebeba watu wenye umri wa makamu pekee hamna vijana. Sasa unajua nyimbo kama hizi zinapochezwa wanajaribu kusikiza wanaona neno Fulani limetumika kwa njia ambayo si ile ya kawaida kwa hivyo hapo tunaona kwamba kuna kuvurugika kwa mawsailiano. Hata hivyo vijana mahali popote wakiwa nyumbani, dancehall, wanaosoma au

hata wanaposafiri hizo nyimbo zinawaingia na wanaelewa kile ambacho kinamaanishwa moja kwa moja.

**Mtafiti**: Je nyimbo hizi za kizazi kipya hasa za Nonini na Juacali zinaithiri vipi lugha ya Kiswahili?

**Msailiwa**: Kwa kiwango kikubwa huathiri lugha ya Kiswahili na hii ni kutokana na hasa vijana wanaolengwa kama soko.nao vijana wenyewe wakati huu wanaenda shuleni si wazee. Sasa unajua wanapoenda shuleni wanachanganyikiwa kwa sababu wanapoingia darasani wanafunzwa hivi; neno hili lina maana hii, wanaposikiza muziki pia wanakuta kuan matumizi mengine. Kuna wale vijana ambao hawawezi kutofautisha ni gani fasaha na ni gani ambayo si fasaha. Hivyo utakuta kwamba hata wanapoandika maswali uatgundua maoja kwa moja anaweza kutumia neno kama lile akaingiza katika insha ama sarufi. Hali kama hiyo inapotokea tunaona kwamba inawaathiri.

**Mtafiti**: Je mustakabali(hali) wa Kiswahili ni upi hasa tukizingatia maana hizi zinazochipuka hasa katika nyimbo hizi.

**Msailiwa**: Tusipobainisha sisi kama wataalamu tujaribu kuwaelekeza wanafunzi kwamba matumizi ya maneno Fulani haya ya lugha ya Kiswahili katika dancehall, michezo n.k wasijaribu kuyaleta katika Kiswahili sanifu. La sivyo, matumizi ya lugha ya Kiswahili yatavurugika katika siku zijazo. Kwa hivyo ni lazima tuhakikishe kwamba kila wakati vijana hao wanatumia lugha sanifu.Hata hivyo kuna changamoto kwa sababu hatuwezi kuweka hali ya darasa kila wakati hata watoto wanapocheza uwanjani au kanisani au wamekwenda wapi; mazungumzo yao ya kawaida nyumbani.Hali kama hiyo inakuwa ni ngumu ndio sababu tunakuta katika matumizi ya lugha kuna kile tunachoita ‘ communicative language’ ambapo mtu anzungumza tu anavyotaka bora mwenzako amekuelewa lakini wakati ambapo tumeanza kuingatia kwamba Kiswahili sanifu kila wakati.It becomes very boring at times kwa sababu utakapozungumza na hao wanafunzi watakuambia it doesn’t work. Hivyo basi kuna shida kwani tunaona mukstakabali wa Kiswahili una shioda hapo mbele kwa hivyo ni lazima tujaribu kurekebisha japo ni kazi nyingi.

**Mtafit**i: Je Kiswahili kinapotoka maneno haya ya kawaida yanapopata maana zaidi hasa katika nyimbo hizi teule?

**Msailiwa**: Kimsingi Kiswahili kinapotoka. Hata hivyo inategeme kiwango cha elimu cha mtu. Unajua tunapozingatia masual ya labda matumizi ya lugha katika chuo kikuu. Watu wana fikra abazo tunasema kwamba yamepevuka kwa hivyo mtu anaweza kupewa naeno na atoe maana zaidi ya ile maana inayokubaliwa kwa hivyo nana juhuru w akufikiria. Vilevile ukianagalia taaluma ya sematiki tunakubaliwa, wanafunzi wanakubaliwa, wataalamu wanakubaliwa kwamba kutakuwa na maana ya kileksia na kiisimu ambayo inapatiokana katika kamusi yaani maana halisi ya neno lakini muktadha pia huweza kuchangia. Kitu ambacho nimegundua ni kwamba nikiangalia tahajia ya maneno ambayo yanatumiwa na

wanamuziki hawa wanajaribu kuwa tofauti na msingi wa tahajia wa kawaida wa Kiswahili.they add some things like in ushairi. They play around with words in a way. Hali kama hii huonyesha kuvurugika kwa tahajia na matamshi ya maneno.

Kwa misingi hii bila shaka Kiswahili kinapotoka na hatungefurahi tukiwapa akina Nonini na Juacali nafasi hiyo. Hata hivyo ukiwahoji watakuambia wanatafuta namna ya kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Wanamuziki wanakubaliwa 'you use language in the way you want kwa sababu wewe ni msanii. Kwa upande mmoja wanazingatia usanii wao kwani tungependa lugha ya Kiswahili ipande ngazi kwa jinsi inavyotakikana. Wao kwa upande wao wanaangalia watumie Kiswahili vipi ili ujumbe tunaowasilisha uwafikie walengwa.

**Mahojiano na msailiwa wa sita**

**Mtafiti:** Je wasikilizaji wanatumia nini kuwawezesha kuzua maana nyingine ya maneno haya ya Kiswahili yaliyotumika katika nyimbo hizi? Kwa mfano waka, washa, kibao nk.

**Msailiwa**: Naam, nafikiri wanatumia muktadha wa nyimbo. naamini pia kwamba baadhi ya maana wanazizua kutoka kwa yale wanayosikia kutoka kwa marafiki zao wakizungumza. Kwa hivyo inategemea marafiki uliyo nao na Ikiwa wao ni wapenzi wa nyimbo hizo. wanaweza kukuambia maana mbalimbali au kukuvuta kuamini kwamba baadhi ya maana za maneno Fulani.

**Mtafiti**: Je ni vipi kuna maana nyingine ya maneno haya ya kawaida katika nyimbo hizi kwa mfano; rusha, kibao, chota n.k

**Msailiwa**: Nafikiri inategemea kile anachoamini msikilizaji, ikiwa wanataka kuchukulia kwamba neno linamaanisha kitu Fulani katika mkondo wa fikira. Watu wengine huenda wakawa na maana zao ambapo huenda wakataka kuamini kwamba neno lina maana maalum kwa sababu hawajapata kutangamana na mtunzi au mwimbaji wa wimbo wenyewe kwa hivyo wanabakia kukisia tu.

**Mtafiti**: Je unafikiri nafasi ya muktadha ni ipi katika mchakato wa kufanyiza maana katika nyimbo hizi?

**Msailiwa**: Muktadha ni kila kitu hususan katika mchakato wa kufanyiza maana hasa pale ambapo maana halisi ya neno hilo hulijui; tunategemea muktadha ili kufahamu maana. hata hivyo muktadha pia huweza kupanua maana ya neno kutegemea maeneo kimuktadha unayolenga. Muktadha unaweza kuwa kitu kipana na ndio maana wakati mwingine kunazuka maana tofauti tofauti za neno moja.

**Mtafiti**: Je kuna uwezekano wa kuvurugika kwa mawasiliano na kupotea kwa maana iliyokusudiwa na waimbaji katika mtazamo wa wasikilizaji wa nyimbo hizi, pamoja na

kwamba kuna maana zaidi inayozuliwa zaidi inayozuliwa kutoka kwa maneno haya ya Kiswahili yaliyotumiwa katika nyimbo teule.

**Msailiwa**: Kuna uwezekano mkubwa kwamba maana inayokusudiwa na mzungumzaji unaweza kupotea.na ndio maana swali lako la kwanza lilikuwa likizungumzia watu kuwa na maana tofauti za maneno Fulani.kwa hivyo inamaanisha kwamba hitilafu katika mawasiliano ipo. Kumbuka kwamba mwimbaji huenda amemaanisha upendo au mapenzi ilhali wasikilizaji wawe wanapata maana ya ufisadi. Hivyo, maana kwa hakika itapotea wakati popote ambapo hatuna ilemaana iliyokusudiwa na mzungumzaji.ni wazi kwamba maana itapotea.

**Mtafiti**: Je nyimbo hizi za kizazi kipya hasa za Nonini na Juacali zinaithiri vipi lugha ya Kiswahili?

**Msailiwa**: Ninafikiri lugha ya Kiswahili inakua kwa vyovyote vile. Huenda ni maendeleo …. Huenda maneno mengine yana maana zaidi zilizozuliwa upya. kwa hiyo neno linaweza kuwa na maana tofauti na ile asilia.wakati huohuo huenda kuna athari mbaya kwa sababu wanaojifunza lugha hii ya Kiswahili huenda wakachanganyikiwa kuhusiana na maana ya manneo na tunapata mtu anaweza kutaka kutumia neno lakini akaishia kutumia neno vibaya bila kujua analitumia hilo neno viabaya kwa kukosa kujua maana.hii ni kwa sababu huenda neno hilo lina maana nyingine tofauti katika nyimbo hizi za kizazi kipya.kwa hiyo tuna vipengele hivi viwili kwamba lugha huenda ikawa na wakati huohuo ikawa hatarini hasa upande wa wanafunzi wachanga wa lugha hii.

Labda Kiswahili kinahitaji kukubali baadhi ya mabadiliko yanayotukia kwake. hata hivyo wakati huohuo lugha ya Kiswahili inastahili kuwa angalifu kwa sababu maana ya neno inapochukua maumbo mengi nadhani kuna haja ya udhibiti. Nafikiri sasa inabidi wasanii waanza kuelewa na kufahamu kwamba wanapotumia maneno kwa njia Fulani wanahitaji kuwasiliana kwa kutumia maneno hayo inavyo faa au kwa njia sanifu.la sivyo, Kiswahili kinaweza kutahatarishwa.

**Mtafiti**: Je mustakabali (hali) wa kiswahili ni upi hasa tukizingatia maana hizi zinazochipuka hasa katika nyimbo hizi.

**Msailiwa**: mustakabali wa Kiswahili nafikiri umethibitiwa kwa sababu lugha hii mwanzo hata inatumiwa katika nyimbo na hiyo ishara nzuri kwamba lugha hii haitakabiliwa na changamoto hasi. Hivyo, nafikiri Kiswahili kina siku nzuri za baadaye kinachohitaji kufanywa labda ni kuwa udhibiti wa jinsi maneno mengine yanavyotumiwa na nilivyosema hapo awali. Wasanii hasa wa nyimbo hizi za kizazi kipya ni lazima watajitokeza huku wanatambua kwamba wao ndio lazima waitunze lugha hii hivyo wanapotumia maneno huku watu wanapata maana tofauti tofauti tunahitaji kujali.kwa hiyo nafikiri hili litakuwa linatishia maendeleao ya Kiswahili.

**Mtafiti**: Je, Kiswahili kinapotoka maneno haya ya kawaida, yanapopata maana zaidi hasa katika nyimbo hizi teule?

**Msailiwa**: Hali hii tunaiita mchepuko au mkengeuko wa kimaana na tunajua tu kilichokengeuka chaweza kuwa kibaya. kiswahili kinaweza kupotoka hasa ikiwa maneno mengine yanatumiwa na yanapewa maana nyingi mpaka hatujui maana halisi na asilia ya neno ni ipi.kwa hiyo hicho kipengele cha kupotoka ni kweli katika maneno fulani siyo yote lakini hasa katika nyimbo hizi za kizazi kipya. kiswahili kinaweza kupotoka kwa hakika na hivyo kuwa hatari kwa lugha

**Kiambatisho 5**

## Ethical Review

MASENO UNIVERSITY ETHICS REVIEW COMMITTEE

Tel: +254 057 351 622 Ext: 3050
Fax: +254 057 351 221

Private Bag – 40105, Maseno, Kenya
Email: muerc-secretariate@maseno.ac.ke

**FROM**: Secretary - MUERC

**DATE**: 16th August, 2019

**TO**: Marolyne Jerujael Moses
PG/MA/FA/00022/2015
Department of Kiswahili and other African Languages
School of Arts and Social Sciences
Maseno University
P. O. Box, Private Bag, Maseno, Kenya

**REF**: MSU/DRPI/MUERC/00751/19

**RE: A Lexico Semantic Analysis of Kiswahili Words as Used in Juacali and Nonini's Selected Songs. Proposal Reference Number MSU/DRPI/MUERC/00751/19**

This is to inform you that the Maseno University Ethics Review Committee (MUERC) determined that the ethics issues were adequately addressed in the initial proposal. Consequently, the study is granted approval for implementation effective this 16th day of August, 2019 for a period of one (1) year. This is subject to getting approvals from NACOSTI and other relevant authorities.

Please note that authorization to conduct this study will automatically expire on 15th August, 2020. If you plan to continue with the study beyond this date, please submit an application for continuation approval to the MUERC Secretariat by 15th July, 2020.

Approval for continuation of the study will be subject to successful submission of an annual progress report that is to reach the MUERC Secretariat by 15th July, 2020.

Please note that any unanticipated problems resulting from the conduct of this study must be reported to MUERC. You are required to submit any proposed changes to this study to MUERC for review and approval prior to initiation. Please advice MUERC when the study is completed or discontinued.

Thank you.

MASENO UNIVERSITY SECRETARY 16 AUG 2019 ETHICS REVIEW COMMITTEE

Dr. Bernard Guyah
Ag. Secretary,
Maseno University Ethics Review Committee.

Cc: Chairman,
Maseno University Ethics Review Committee.

MASENO UNIVERSITY IS ISO 9001:2008 CERTIFIED

.